

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Kumi Na Moja – Tarehe 23 Juni, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. PINDI H. CHANA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA,  
SHERIA NA UTAWALA:**

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 99 (3), cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Mezani Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge Katiba, Sheria na Utawala, Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DAVID E. SILINDE (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI):**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Msemadi Mkuu wa Upinzani, naomba kuwasasilisha Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kuweka Mezani Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Taasisi zote zilizopo chini ya Ofisi yake, kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

## **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 106

### **Kero Kiwanda cha Mtibwa**

**MHE. AMOS G. MAKALLA** aliuliza:-

Uwepo wa kiwanda kimoja tu cha sukari (*Mtibwa*) unasababisha matatizo mengi kama vile kuchelewesha malipo ya wakulima, mafao na bei ndogo ya miwa:-

(a)Je, kwa nini Serikali isiwashawishi wawekezaji kujenga kiwanda kingine na vingine vidogo vyta sukari guru ili kuleta ushindani?

(b)Je, Serikali iko tayari kuwawezesha wazawa ki-mtaji endapo watajitokeza ili wajenge kiwanda?

**SPIKA:** Hii meza ya mbele hii ni ya wale watakaojibu maswali, sasa naona mnatokea huko mnakotokea; sijui wapi!

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, Mbunge wa Mvomero, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa kina uwezo wa kusindika kiasi cha tani 50,000 cha miwa kwa mwaka. Kwa sasa, uzalishaji wa miwa kwa kiwanda na wakulima wadogo ni wastani wa tani 38,135.875 kwa kipindi cha miaka 2000/2001 hadi 2009/2010. Vilevile, bado kiwanda kina uwezo wa kusindika miwa mingi sana. Kimsingi mpaka hapo uwezo wa kiwanda cha Mtibwa wa kusindika miwa utakapokuwa mdogo ikilinganishwa na wingi wa miwa inayolimwa katika eneo hilo, ndipo kiwanda kingine kinaweza kusajiliwa vinginevyo tutakuwa tunavunja Sheria na Kanuni za Sukari. Aidha, ili Mtibwa pasiwepo na upungufu wa miwa, kiwanda kingine kinaweza kujengwa umbali wa Km. 80 kutoka kiwanda cha sasa kilipo, kuwezesha wakulima wa miwa wanaouza miwa Mtibwa waendelee kuuza miwa Mtibwa walikosajiliwa na wakulima wapya. Na pia wale wengine wasajiliwe kuuzia kiwanda kipyta ili kila kiwanda kiweze kuwa na wakulima wake wanaolima miwa ya kutosha kukidhi mahitaji ya kiwanda husika.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali imeshajiondoa kabisa katika uendeshaji wa moja kwa moja wa biashara na kuiachia sekta binafsi ambayo ni injini ya maendeleo ikiendelea kufanya hivyo. Aidha, kufuatia mageuzi ya uchumi, Serikali iliruhusu mabenki na taasisi za fedha kuanzishwa nchini ili zitoe huduma kwa sekta binafsi wakati wa kuwekeza.

Wananchi wengi wanaowekeza kwenye kilimo wanawezeshwa na taasisi hizo za fedha. Endapo kuna wananchi wanaotaka na wangependa kujiunga kwa nia ya kujenga kiwanda cha sukari, hili ni jambo jema linalokubaliwa na kuungwa mkono na Serikali. Na katika kufanya hivyo mchanganuo wa mradi wa kiwanda utatoa picha kwa taasisi zinazokopesha fedha ili ziwapatie mkopo. Serikali kupitia taasisi zake za usimamizi itaratibu uanzishwaji wa kiwanda hicho kwa maslahi ya wadau wote.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ambayo hayajajitosheleza swali langu. Lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri alivyojibu si kweli kwamba kiwanda cha Mtibwa kimewahi kuzalisha sukari tani 50. Hizo ni takwimu za uwongo kwa hiyo, amejibu uwongo. Kwa sababu, takwimu nilizonazo...(Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hiyo sio lugha inayotumika humu ndani, unatakiwa useme hizo takwimu sio sahihi; neno uwongo, kasome ile Kanuni, itakwambia sivyo hivyo tunavyosema. Unaweza kuanza tena kuuliza swali lako.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Takwimu za ukweli tulizonazo ni kwamba mpaka mwaka jana, tangu kiwanda kibinafsishwe mwaka 1997, kiwanda kimezalisha tani 40,000 na sasa matarajio ya mwaka huu ni tani 47,000 kwa hiyo, hakijawahi kuzalisha tani 50,000. Kwa hiyo, ninayo orodha hapa na uzalishaji wa tani kwa kila mwaka mpaka mwaka jana?

(a)Mheshimiwa Spika, swali; kwa kuwa, Serikali inasema kwamba kwa kuanzisha kiwanda kingine tutakuwa tunakiuka sheria. Serikali haioni kwamba kwa kero zilizopo katika kiwanda cha Mtibwa, ndio kitaendelea kuwadidimiza wakulima? Kwa sababu, zipo kero za kuchelewesha mishahara, kulipa bei ndogo ya sukari?

(b)Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ipo haja sasa ya kuwawezesha watanzania wenye nia ya kuwekeza kiwanda kingine. Na kwa kuwa, lipo dirisha la wakulima kupitia benki ya *TIB* na fedha nyingine ziliwahi kuongezwa hata za *EPA*.

Je, Serikali sasa haioni kwamba ipo haja ya kuondoa monoksoni iliyopo kiwanda cha Mtibwa, ili kuwawezesha wazawa na wananchi wengine kuweza kuweka kiwanda kingine na kuondoa kero hizi nilizozitaja?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Makalla, kwa juhudi zake na

jitihada zake za kuwatetea wakulima wa miwa katika eneo hili la Mtibwa, kule kule Morogoro.

Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi ambalo nimelitoa Serikali imesema kwamba kiwanda hiki cha sukari kina kitu kinachojulikana kwa kitaalam *installed capacity* ya tani 50,000. Na hatujasema kwamba kinazalisha tani 50,000. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili Katika jibu la msingi tumesema, uzalishaji wa miwa uliopo katika hili eneo la Mtibwa, kwa wakulima wote wadogo wadogo ni tani 38,000. Kwa maeneo mengine uzalishaji wa miwa ni mdogo kuliko *installed capacity* na chini ya Kanuni za sukari zinazosimamiwa na Bodi ya Sukari, ni lazima kwanza kiwanda kilichoanzishwa kiweze kukidhiwa mahitaji ya kuwa na uzalishaji wa kutosha kabla ya kiwanda kingine hakijaruhusiwa. Utaratibu unaotumika kuruhusu uanzishwaji wa kiwanda kingine ni sharti kiwe umbali wa kilometra 80 kutoka kiwanda kilichopo cha kwanza. Lakini la pili, ni lazima mahitaji halisi ya kiwanda cha kwanza yawe yametimizwa na kuwe na uwezo kiukulima wa kuweza kutoa miwa yakutosha kwa ajili ya kiwanda cha pili.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, kwa kuendelea kuwahimiza wananchi wake, kuwa tayari kuanzisha kiwanda cha sukari, *TIB*, katika dirisha la kilimo. Serikali itaendelea kuwa tayari kuwasaidia na wakati muafaka wa ukulima huu utakapoongeza *capacity*, Serikali itawaunga mkono katika juhudi hizo. (*Makofii*)

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa, miongoni mwa matatizo yanayowakabili wakulima wa miwa wale wanaouzia viwanda vikubwa, yaani *out growers*, ni kodi nyingi tokea usafirishaji mpaka usindikaji. Je, Serikali ina mpango gani kusaidia upunguzaji wa kodi hizo ili kipato cha mkulima wa miwa kikue?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, chini ya utaratibu wa Serikali wa KILIMO KWANZA, Serikali inahuisha mfumo mzima wa Kodi ili kuweza kumsaidia mkulima kufanya ukulima wenye tija. Tunaangalia uzalishaji, tunaangalia uwezo wa kuwa na mbegu bora, tunaangalia mfumo mzima wa usafirishaji, ikiwa ni pamoja na juhudi za Serikali kuwekeza katika miundombinu ya vijiji ni kuwawezesha wakulima kupeleka bidhaa zao masokoni. Na kwa kufanya hivyo, tunaamini kabisa ukulima huu utakuwa na tija na utamsaidia mkulima.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa matatizo ya wakulima wa miwa katika kiwanda cha Mtibwa yanafanana kabisa na wakulima wa miwa wa kiwanda cha Kilombero; kwa matatizo ya wakulima kulima miwa na inapofika wakati wa kuza miwa imeshaiva na wamekopa *SACCOS*,

miwa hiyo wenyе kiwanda cha Kilombero wanakataa kuinunua na kuwaingizia hasara kubwa wakulima hao. Na wengine mpaka wamekufa kwa sababu ya mshtuko watalipa vipi.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kutazama kwa karibu matatizo ya wakulima wa miwa wa Kilombero katika haki zao za kimsingi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, hoja kwamba kuna miwa inalimwa lakini wazalishaji au wale wenyе viwanda wanakataa kwa makusudi kuinunua ni hoja nzito. Serikali italiangalia hilo suala na kulichukulia hatua kama kweli lipo. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa majibu mazuri. Nilitaka tu kuongezea kidogo kwamba wakulima hawa wa miwa katika mashamba yote yanayozunguka viwanda, wanalima kwa mikataba maalum (*Contract Farming*). Na katika mikataba yao wanayo makubaliano kati ya wakulima na wale wenyе viwanda.

Makubaliano hayo pia yanaonesha jinsi ya kutatua migogoro iliyopo. Sasa hatua ya kwanza ni kumpata mpatanishi kati ya wakulima na wenyе viwanda; wakashindana hapo, ndipo tunaingia hatua ya pili. Kwa hiyo, tumekuwa tunawashauri kwanza wafuate yale makubaliano, wampate yule mpatanishi waliyekubaliana katika makubaliano yao, halafu Serikali inaingilia kufuutilia kama wameshindana. (*Makofi*)

Na. 107

### Soko La Uhakika La Mahindi

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Wananchi wa Mbozi ni wakulima hodari wa zao la mahindi, lakini hawana soko la uhakika kwa ajili ya zao hilo:-

Je, ni lini sasa Serikali kupitia Wizara hii itawahakikishia wananchi hao, soko la uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Bisahara, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la ukosefu wa soko la mahindi la uhakika mara nyingi hutokea wakati wa mavuno hususan katika miaka ya mavuno mengi. Aidha jitihada za

Serikali, kupitia Mpango wa KILIMO KWANZA, zimeanza kuzaa matunda kwa kuongezeka kwa uzalishaji wa mahindi kote nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko la uzalishaji wa zao la mahindi, serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuwahakikishia wakulima wa mahindi hapa nchini, ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Mbozi, uhakika wa soko la mahindi kwa kufanya mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (*NFRA*) imeongeza uwezo wake wa kununua mahindi kutoka kwa wakulima kuanzia tani 140,000 hadi tani 350,000 za mahindi kwa mwaka. Bei inayotolewa na wakala ni ya kuridhisha kwani inazingatia gharama za uzalishaji na bei ya soko. Lengo la wakala ni kununua mahindi yote ya ziada yanayozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeanzisha Bodi ya Mazao Mchanganyiko, itakayoshughulikia mazao yote yasiyokuwa na Bodi. Moja ya kazi ya Bodi hiyo ni kununua mazao kutoka kwa wakulima kibiashara, ikiwa ni pamoja na zao la mahindi. Bodi hiyo, imeanzishwa na inatarajiwa kuanza kununua mahindi katika msimu wa mwaka 2011/2012. Aidha, uanzishwaji wa wa mfumo wa stakabadhi za maghala kwa mazao yote yanayohifadhika, unaonesha dalili nzuri kwa wakulima ikiwa ni pamoja na wakulima wa mahindi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, zaidi ya mikakati hiyo, Shirika la Kimataifa la *World Food Program (WFP)*, kuanzia mwaka 2009/2010 limeanza kununua mahindi kutoka moja kwa moja kwa wakulima, moja kwa moja chini ya mpango ujulikaonao kama *Purchase for Progress*. Uamuzi wa Shirika hilo kununua mahindi kutoka kwa wakulima, unazingatia vigezo vya ubora na umesaidia sana kuimarisha upatikanaji wa soko la uhakika kwa mazao kama mahindi.

Vile vile, Mradi wa *Southern Highlands' Foods Systems* unaotegemea kuanza msimu wa 2011/2012 unatarajia kusaidia kuimarisha soko la mazao ya wakulima kama mahindi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuwahakikishia wakulima na wafanyakibashara wa mahindi kote nchini, ikiwa ni pamoja na wakulima wa Jimbo la Mbozi Mashariki, kuwa kutokana na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali, kuna uhakika wa Mkulima kupata soko lake la mahindi na mazao mengine mchanganyiko.

Jambo la msingi ni kusaidiana kuhamasisha wakulima kuijunga katika vikundi au ushirika ili kuimarisha ubora na wingi wa mazao yanayozalishwa.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Lakini kabla sijafanya hivyo na kwa kuweka kumbukumbu sawa, jina langu naitwa Godfrey sio Geofrey, hayo ni majina mawili tofauti, sio Geofrey; la kwangu ni Godfrey.

Mheshimiwa Spika, baada ya masahihisho hayo nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katika majibu yake amesema bei inayotolewa na wakala ni ya kuridhisha, kwani inazingatia gharama za uzalishaji.

Sasa ninaomba Waziri atueleze, hiyo bei ya kuridhisha ni kiasi gani kwa kilo moja ya mahindi? Maana mwananchi hapo hatajua hiyo bei ya kuridhisha ni kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, swal la pili, mwaka jana kwenye soko la mahindi pale Vwawa karibu na Tazara kulikuwa na vunjo kwa ujumla katika uuzaji wa mahindi, sababu mojawapo ni kwamba Serikali ilikuwa inatoa fedha kidogo kwa ajili ya ununuzi wa mahindi, na wakulima walikuwa wanalahizimika kutoa rushwa sasa ili wapate nafasi ya kuuza mahindi yao.

Serikali inawaambia nini wananchi wa Mbozi mwaka huu na Watanzania wengine kwamba pesa zitatolewa za kutosha ili waweze kuuza mahindi yao vizuri na wapate fedha ya kuridhisha?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba nijibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Godfrey Zambi kama ifuatavyo.

Kwanza sisi Serikali inanunua mahindi kulingana na bei iliyopo sokoni, lakini tumekuwa tunajitahidi kwa miaka hii nyuma kama miwili mitatu huko nyuma kuhakikisha kwamba Serikali tunatoa bei ile ambayo inamvutia mkulima.

Wakala wa hifadhi ya chakula ndiye ambaye anakwenda kununua mahindi kule kwa wakulima na pale ambapo tunaona kwamba wakulima wawafanya biashara wanajitahidi kuyanunua kwa haraka sisi tunaweka bei nzuri ya kuwawutia ndiyo maana wakala ananunua mengi tena kwa haraka sana ila tunapokuwa tumezidisha tu tumeshafunga tumezidiwa ndiyo hapo basi wakala hawezitena kununua.

Kwa kweli msimu uliopita bei ilikuwa nzuri, kama kule kwao haikuwa nzuri sana mimi nashindwa kuelewa hali imekuwaje, maana yake wakala alijaza hifadhi yake vizuri sana. (*Makofî*)

Kuhusu bei kuongezeka, naomba niseme kwamba kwanza mwaka jana tumepitisha hapa ndani sheria namba 19 ambayo imeanzisha bodi ya nafaka na mazao mchanganyiko, bodi hiyo sasa imekwishaanza kazi na moja ya majukumu ni kuhakikisha kwamba inanunua mahindi hayo nayo itasaidia ku-regulate bei hizo, Kwa hiyo, nina hakika kabisa kwamba hii bodi itakapokuwa imefika kule Mbozi, wakulima wa Mbozi haya matatizo yataanza kupungua. (*Makofî*)

## **Kuanza Kwa Masomo ya Kidato cha Tano na Sita Sekondari ya Tandahimba**

**MHE. JUMA A. NJWAYO** aliuliza:-

Je, ni lini Masomo ya kidato cha Tano na Sita yataanza katika sekondari ya Tandahimba kufuatia kukamilika kwa vigezo vyote vinavyotakiwa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, shule ya sekondari ya Tandahimba imetimiza vigezo vyote muhimu vya kuanza masomo ya Kidato cha Tano katika michepuo ya *HKL*, na *HGL* kwa wasichana. Hata hivyo, taarifa ya ukaguzi wa shule hiyo iliyothibitishwa kukamilika kwa vigezo hivyo iliyasilishwa Wizarani, wakati zoezi la uchaguzi wa wanafunzi wa kujiunga na kidato cha tano kwa mwaka 2011 likiwa limekamilika. Kwa vile shule ya sekondari Tandahimba, haikuwemo katika orodha ya shule zenye kidato cha tano mwaka 2010 hakuna wanafunzi aliyechanguliwa kujiunga na shule hiyo kwenye Sel-Forms. Aidha, idadi ya wahitimu wasichana wa kidato cha Nne, mwaka 2010 walikuwa na sifa za kujiunga na Kidato cha Tano kwa michupuo ya *HKL* na *HGL* ilikuwa ndogo sana ikilinganishwa na nafasi nyingi zilizokuwepo.

Mheshimiwa Spika, kutopteka na sababu hizo shule ya sekondari Tandahimba haikuweza kupangiwa wanafunzi wa kujiunga na kidato cha tano mwaka 2011. Nachukua nafasi kumjulisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako tukufu kwamba, shule hiyo ya Tandahimba itapangiwa wanafunzi wa kidato cha tano mwaka 2012. (*Makofii*)

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza, awali ya yote naomba kumpongeza Naibu Waziri na Serikali kwa ujumla kwa kuamua kabisa sasa kupeleka shule ya Kidato cha Tano na cha Sita kwenye shule ya sekondari ya Tandahimba. Lakini nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wa Tandahimba wametimiza wajibu wao wa kuwekeza katika elimu kiasi cha kuchanga kujenga majengo ya kidato cha Tano na cha Sita. Je, Serikali inawahakikishiaje wananchi wa Tandahimba uhakika wa walimu wa kudumu pale ili isije ikafanana na shule zingine za kidato cha Tano na Sita ambazo kwa sasa zimefunguliwa lakini hazina walimu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali nyongeza la Mheshimiwa Abdallah Njwayo Mbunge wa Tandahimba kama ifuatavyo.

Kwanza nampongeza yeche binafsi pamoja na wananchi wa Tandahimba kwa kukamilisha vigezo ambavyo Wizara ya Elimu ilikuwa inataka ili shule yake iweze

kukamilika. Lakini Mheshimiwa Mbunge hapa anachoiomba Serikali kwa ujumla kupitia Wizara ya Elimu ni kumpa uhakika wa walimu wa kudumu katika shule hiyo ambayo itaanza masomo hayo mwaka 2012.

Nakuhakikishia Mheshimiwa kwamba Serikali imejipanga kuwa na walimu wengi na watahitimu masomo yao vyuoni na Serikali mwaka huu itapanga walimu wengi sana pamoja na wilaya hiyo ya Tandahimba. Kwa hiyo, nakuhakikishia Mheshimiwa kabisa kwamba utapata walimu wengi tena wa kudumu na shule hiyo itakuwa mstari wa mbele sana katika matokeo ya Kidato cha Sita.

**SPIKA:** Leo kuna shule inayofanana na hiyo, mnasimama kabla mkisimama baadaye siwapi nafasi, naomba uulize swali.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wilaya ya Bahi, mpaka mwaka jana ilikuwa haina hata shule moja ya Kidato cha Sita licha ya kuwa na sekondari za kawaida 20, lakini mwaka huu Serikali imekubali kufungua shule moja ya sekondari ya Kigwe lakini shule hiyo imeshaanza. Lakini naomba nitoe ombi rasmi na naomba anikubalie Mheshimiwa Waziri shule ile iko na hali mbaya na kama Serikali haitochukua juhudzi za kusaidia wanafunzi wale watasambaratika na ile shule itakufa na jina lake la sekondari itakufa.

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kwenda kutoa msaada katika sekondari hiyo?

**SPIKA:** Linafanana na lile la Tandahimba.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, swali hili lina majibu mafupi tu kwamba katika Wilaya ya Bahi, shule hiyo ya Kigwe nadhani mwezi ujao Serikali inapanga walimu sehemu mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja ya shule ya Kigwe sekondari. Kwa hiyo, tunahakika tutawapatia walimu ili shule iweze kuendelea. (*Makofii*)

Na. 109

#### **Ongezeko la Mifugo na Athari Zake**

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI** aliuliza:-

Mifugo ni shughuli yenye tija kiuchumi kwa wananchi wa mkoa wa Shinyanga, Mwanza, Mara na kadhalika. Lakini hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la mifugo kwenye maeneo mengi pasipo kuongezwa kwa maeneo ya malisho na kusababisha migogoro sugu baina ya wafugaji na wakulima; wafugaji kuchunga mifugo yao kwenye hifadhi ya taifa na kuzua matatizo makubwa.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wafugaji maeneo ya malisho ili kuondoa migogoro baina ya wafugaji na wakulima?

(b)Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatengea wafugaji maeneo ya pembezoni mwa hifadhi ya Taifa (*buffer zones*) ili waondokane na hali ya uvunjaji wa sheria kwa kuachilia mifugo kuchunga katika hifadhi na kusababisha usumbu na askari wa Wanyama Pori?

#### **WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, Mbunge wa Bukombe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine limewezesha kupanga mipango ya matumizi ya ardhi, vijiji yaani *village land use plans* kwa kuzingatia sheria ya matumizi ya Ardhi, Na. 6 ya mwaka 2007 na sheria ya maeneo ya malisho na rasilimali za vyakula vya mifugo Na. 13 ya mwaka 2010. Hadi sasa maeneo ya malisho yenye jumla hekta 2.3 milioni yametengwa katika vijiji 450 katika wilaya 49. Zoezi hili linaendelea chini ya uratibu wa Tume ya Taifa ya mipango ya matumizi ya ardhi.

(b) Mheshimiwa Spika, kulingana na sheria ya Wanyama Pori Na. 5 ya mwaka 2009 kipengele cha 21 hairuhisiwi eneo la nusu kilometra kutoka katika hifadhi yaani Buffer Zone kutumika kwa shughuli yoyote.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu kuuliza maswali mawili ya nyongeza, katika nchi nzima ya Tanzania katika miaka ya karibu kumetokea ongezeko la mifugo ambayo katika hali ya kawaida ni neema lakini ongezeko hili ni tatizo kubwa na namwuliza Waziri au tuseme Serikali. Je, inaonaje kama ingeunda jopo la wataalam ili wafanye utafiti na kuishauri Serikali kuhusu tatizo hili kwa sababu ni tatizo kubwa?

Je, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba zoezi la kuwatengea sehemu ya malisho wafugaji linaendelea, je, zoezi litafanyika katika jimbo la Bukombe?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Prof. Kulikoyela Kahigi, Mbunge wa Bukombe, kama ifuatavyo. Swal la kwanza alilouliza kusema kweli kuongeza kwa mifugo ni dalili nzuri na ni *opportunity* ambayo Watanzania tunatakiwa tuitumie ili mifugo hiyo iweze kuongeza pato la taifa na kubadilisha maisha ya wafugaji. Lakini kuhusu kuunda chombo ama jopo la wataalam kuchunguza kuongezeka kwa mifugo sidhani kwamba hii inahitaji kuundwa tume, kinachotakiwa ni kwamba wafugaji waelewe kwamba hii ni rasilimali yao ya kuwasaidia na waweze kujisaidia kuvuna mifugo hiyo ili isiweze kuharibu mazingira. Katika sheria yetu ya malisho na rasilimali za vyakula vya mifugo Na. 13 ya mwaka 2010 tunasisitiza kwamba wafugaji wafuge kutokana na eneo walilo nalo na tabia za kuhamama si nzuri na wala siyo suluhisho la kuweza kutatua matatizo ya ardhi tuliyonayo. Wafuge wanyama ambao wanalingana na

eneo lao. Serikali kuitia *DADPs* na program zingine itakuweka miundombinu kwa ajili ya mifugo yao.

**SPIKA:** Mfugaji mwagine Mheshimiwa Laizer Lekule.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mikoa ya Kaskazini, Arusha, Shinyanga, Mara na Kagera ni Mikoa ya wafugaji na wakulima, lakini hakuna migogoro kama huku Kusini. Je, Serikali haiwezi ikaangalia kwanini wafugaji walioko Kusini wanashindwa kukaa vizuri na wakulima kama wanavyokaa wafugaji wa Kaskazini na wakulima?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, asante kunipa nafasi hii nami nitoe mchango wangu. Kwa kifupi ni kwamba wale wa Kaskazini wana mazoea kuishi na mifugo hiyo, Kusini hawana mazoea wanahitaji kuelimishwa. Kwa hiyo, wale wanaohamia Kusini ni kwamba wanaleta *disturbance* kwa wale wakulima, na *solution* siyo kuhama, solution kila mmoja afuge mifugo inayotosha sehemu yake ya ardhi aliyyo nayo. Ofisi ya Makamu wa Rais tuna mpango wa kuendesha masomo ya kuvuna, mifugo hiyo tuvune *bio gas* ili watu waweze kupika chakula kwa kutumia *bio gas* ili wasikate miti hovyo.

Kwa hiyo nachoweza kusema ni kwamba Waheshimiwa Wabunge tuwaelimishe wananchi wafugaji naman ya kufuga vizuri kwa kisasa na mifugo inayozidi wauze wapate pesa wajenge nyumba za kudumu ili elimu hiyo ya *bio gas* itakapokuja iwakute wako tayari, ahsante sana.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, ahsante nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Tanzania tunaamini kwamba tuna rasilimali ya samaki wanaoweza kuliingizia pato kubwa taifa letu. Ndiyo maana tumekuwa tukilalamikia juu ya meli zinazokuja kuvua samaki hao bila utaratibu.

Je, Serikali tunazo meli ngapi zinazomilikiwa na Serikali aidha na wazalendo zinazovua katika bahari kubwa na kama hatuna tuna mpango gani juu ya hili? v Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamad nakushukuru sana kwa swali lako la nyongeza. Yaani ni nje, kabisa kabisa ya swaku la msingi. Kwa hiyo, tunaendelea. (*Makofî*)

Na. 110

### **Mifugo Iliyohamishiwa Rufiji toka Ihefu**

**MHE. KURUTHUMU J. MCHUCHULI** aliuliza:-

Mwaka 2005/2006 Serikali ilihamisha wafugaji kutoka Ihefu na kuwapeleka Rufiji kwenye maeneo maalum yaliyotengwa ya Mbilinganya, Lolondo, Chumbi, Siasa

na kadhalika na waliahidiwa kujengewa miundombinu kama shule, malambo na kadhalika, lakini hadi sasa hakuna chochote kilichofanyika.

(a) Je, kwanini Serikali hadi sasa haijatekeleza ahadi yake na kusababisha mwingiliano kati ya wakulima na wafugaji wa kuharibiana mazao na baadhi yao kupoteza maisha kwa kupigwa na wafugaji?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuwahamisha wafugaji waliozagaa maeneo mbalimbali na kuwapeleka kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili yao?

### **WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kwamba maeneo ya ufugaji hasa kule Rufiji maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge yanahitaji miundombinu ya mifugo, Serikali imetekeleza ahadi yake kwa kujenga majosho manne, katika vijiji vya Mbilinganya joshmoja, Chumbi joshmoja, Siasa moja na Nyamwage moja na imechimba lambo moja katika kijiji cha Lolondo.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji imekuwa ikiwhamasisha wafugaji kwenda kwenye vijiji 24 ambavyo vilivytenga jumla ya hekta 77,138.91 kwa ajili ya ufugaji.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri lakini kwanza napenda nimpe taarifa atambue hilo lambo analolizungumzai ambalo anasema lipo Lolondo lipo Kiwanga na halijakamilika hilo lambo moja. Pamoja na kutengeneza majosho manne, ambayo kwanza hayakidhi haja lakini tatizo la wafugaji wa Rufiji na uwepo wa malambo wa kunyweshea maji kwa mifugo yao na hivyo imewalazimu sasa wapeleke mifugo yao katika mto Rufiji.

Tatizo la pili ni uwepo ndorobo ambao wanabisha magonjwa ya hivyo inawalazimu sasa wafugaji hawa kuhamia katika vijiji vya Umwe, Mgomba na Rufiji Adekta ambako wanaharibu mazingira kwa kiasi kikubwa.

Je, Mheshimiwa Waziri anaeleza nini katika hili?

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, natumia Kanuni ya 68 (7).

**SPIKA:** Naomba uisome.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili

Spika atoe ufanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na Majibu ya Spika yataolewa papo hapo au baadaye kadri itakavyonekana inafaa.

Mheshimiwa Spika, jana wakati tupo kwenye kutunga sheria ile ya Muswada wa Fedha, Serikali ilitoa majibu mawili kwenye suala la faini za barabarani ambazo mimi nilishindwa kuelewa. Kwenye hotuba ya Waziri, yale makosa ya barabarani Serikali ilisema kwamba yataongezwa kutoka shilingi 20,000/= mpaka 30,000/=. Lakini kwenye Muswada wa mabadiliko au *amendment* iliyoletwa na Serikali ukiisoma inasema hivi na ninaomba niisome.

*In the proviso to paragraph B; by deleting the phrase 50,000/= but not exceeding 30,000/= and substituting for it the phrase 20,000/= but not exceeding 30,000/=.*

Sasa kwenye hii ndiyo mabadiliko yaliyoletwa na Serikali lakini ilisema kwamba faini hiyo itakuwa kati ya shilingi 20,000/= na 30,000/= lakini baadaye Waziri alipokuwa anajibu akasema kwamba faini hiyo ni shilingi 30,000/=. Sasa mimi naona kama ilituchanganya maana yake tuliyotegemea hapa ni mabadiliko yaliyoletwa na Serikali kwenye *amendment* lakini baadaye Serikali katika utaratibu amba mimi sikuujua ikatamka *figure* ya shilingi 30,000/=.

Mheshimiwa Spika, katika hali hiyo naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Nitautoa baadaye tukishaingia kwenye *Hansard* na kuona ni nini kilichokuwa kimesemwa. Kwa hiyo, nitakutolea baadaye mwongozo.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea!

## **KAULI ZA MAWAZIRI**

### **Kampuni ya Uingereza ya BAE System**

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:**  
Mheshimiwa Spika, kauli ya Serikali ya Tanzania dhidi ya Kampuni ya *BAE-Systems* ya Uingereza kutoa fedha za tozo ya rada kwa Asasi za Kiraia za Uingereza.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipatia nafasi kuwasilisha kauli ya Serikali Bungeni dhidi ya uamuzi wa *BAE Systems* ya Uingereza kwa kuamua kutoa fedha walizoamriwa na Mahakama *Pound* milioni 29.5 sawa na takribani bilioni 75 zinazotokana na tozo ya fidia ya mauzo ya Rada kwa wananchi wa Tanzania kupitia Asasi za Kiraia za Uingereza yaani *Charity Organisations* badala ya kuzirejesha fedha hizo kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tarehe 23 Novemba, 2010 kwenye Mahakama ya *West Minister*, Kampuni ya *BAE* inayotengeneza zana za kivita ambayo iliilangua Tanzania Rada kwa bei ya dola za Kimarekani karibu milioni 40 ilikiri kwamba imefanya kosa la

kutoweka kumbukumbu za fedha na hesabu katika mchakato wa mauzo ya Rada kwa Serikali ya Tanzania. Kampuni hiyo iliomba kukaa mezani na shirika la uchunguzi la Uingereza yaani SFO, kupata usuluhisho nje ya Mahakama.

Katika makubaliano hayo na SFO BAE ilionyesha utayari wa kulipa wananchi wa Tanzania kiasi cha pound milioni 30 ikijumuisha gharama za kesi ambazo zingeamuliwa na Mahakama ya mwisho. Kwa upande wake shirika la uchunguzi la Uingereza *SFO* ilikubali kusitisha uchunguzi wote dhidi ya *BAE* na kwamba haitachukua hatua nyingine yoyote dhidi ya mtu yeoyote kwenye kampuni ya BAE iwapo italipa tozo hizo. Makubaliano hayo yangetekelezwa baada ya kupata baraka za Mahakama ya juu yaani *Crown Court*.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha makubaliano hayo Mahakamani, *SFO* yaani Shirika la Uchunguzi la Uingereza, Serikali ya Uingereza na Serikali yetu zilijadiliana na kukubaliana kuwa ni vema fedha hizi za wananchi zikarejeshwa kuitia kwa Serikali ya Tanzania. Serikali hizi mbili zilikubaliana kuwa fedha hizo zitumike kwenye sekta ya elimu, mpango huo ulikuwa moja ya ushahidi muhimu uliotolewa Mahakamani kumshawishi jaji kutoa uamuvi wa kuridhia makubaliano kati ya *SFO* na *BAE*.

Katika mpango huo Serikali ilidhamiria kufanya mambo yafuatayo:-

- (i) Kununua vitabu milioni 4.4 kwa ajili ya wanafunzi wa shule za msingi nchini.
- (ii) Kununua vitabu 192,000 vya kufundishia kwa ajili ya Walimu wa Shule za Msingi.
- (iii) Kununua madawati 200,000 kwa ajili ya wanafunzi 16,000 wa Shule za Msingi.
- (iv) Kujenga nyumba 1,196 za Walimu wa Shule za Msingi Vijijini na kujenga Vyoo 200,000 kwenye Shule za Msingi nchini.

Mheshimiwa Spika, tarehe 21 Desemba, 2010 Jaji *Bien* wa Mahakama ya *South Work* ya *London Crown Court* kwa kwa kuzingatia ufanuzi huo alikazia makubaliano kati ya *SFO* na *BAE* yalyowasilishwa kwake kwa kuamuru kwamba kiasi cha pound *milioni* 29.5 kilipwe na *BAE* kwa wananchi wa Tanzania na kiasi cha *pound* 500,000 kilipwe kama gharama za Mahakama yaani *Court Fees*.

Mheshimiwa Spika, baada ya uamuvi huo wa Mahakama kutolewa, *BAE* haikuchukua hatua yoyote ya kuzirejesha fedha hizo Tanzania. Tarehe 15 Me, 2011 *BAE* ilieleza nia yake ya kurudisha fedha hizo kuitia Asasi za Kiraia yaani *Charity Organisations* za Uingereza na siyo kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kigezo kwamba sera ya kampuni hiyo zinaruhusu kutoa misaada kwa Asasi za Kiraia tu.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu ilishangazwa na uamuzi huu kwa sababu fedha hizi *pound million* 29.5 si za misaada kama BAE wanavyotaka kuaminisha ulimwengu. Fedha hizi ni tozo kwa hela zilizokwapuliwa na kampuni ya BAE kutoka kwa Serikali ya Tanzania. Aidha, Serikali yetu ilishangaa kwa sababu uamuzi huu unapishana na makubaliano yaliyofikiwa kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Uingereza na una lengo la makusudi ya kuonyesha sura ya kutoiamini dhamira ya Serikali ya Tanzania kutumia fedha hizo kwa kusudi lililotolewa. Kwa uamuzi huu BAE inataka umma wa Uingereza na wengine uamini kuwa Asasi za Uingereza zitatumia fedha hizo kwa umakini zaidi kuliko Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipinga uamuzi huo kwa sababu ni uamuzi wa kuidhalilisha Serikali yetu, Asasi za Kiraia zilizopo nchini kwetu na wananchi kwa ujumla. Ni uamuzi unaoiondolea heshima nchi yetu. Fedha milioni 29.5 za walipa kodi wa Tanzania hazina budi kurejeshwa kwao kupitia Serikali yao pamoja na kelele zote tulizozipiga tarehe 17 Juni, 2011 BAE sasa imeunda Bodi ya watu sita itakayoishauri BAE namna bora ya kuwafikishia Watanzania fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi chote hiki hadi sasa Serikali imechukua hatua zifuatazo.

Nimefanya mazungumzo na Mheshimiwa Henry Bellingam Waziri wa Uingereza anayeshughulikia masuala ya Afrika wakati wa ziara yake nchini Tanzania kati ya tarehe 24-27 Mei, 2011. Katika mazungumzo yetu Waziri huyo alisisitiza kuwa msimamo wa Serikali ya Uingereza haujabadiliya na kuwa wanaunga mkono fedha hizo kurejeshwa kwa Serikali ya Tanzania kwa matumizi yaliyoainishwa. Msimamo huo ulijidhihirisha tarehe 7 Juni, 2011 katika kipindi cha maswali na majibu kwenye Bunge la Uingereza ambapo Waziri wa Uhusiano wa Kimataifa Mheshimiwa Andrew Mshel, Mbunge alilieleza Bunge lao kuwa msimamo wa Serikali yao ni kutaka fedha hizi zirejeshwe kwa Serikali ya Tanzania. Alisisitiza kuwa katika miaka yote fedha za maendeleo kutoka Serikali ya Uingereza zimekuwa zikitolewa kwa wananchi wa Tanzania kupitia Serikali ya Tanzania na wamekuwa wakiridhika na jinsi fedha hizo zinavyotumika. (*Makofii*)

Taarifa ya mazungumzo hayo na Waziri wa Uingereza niliiwasilisha kwenye Kamati ya Bunge ya Nje, Ulinzi na Usalama wakati Wizara yangu ikiwasilisha mapendekezo ya Bajeti ya mwaka 2011/2012 tarehe 1 Juni, 2011. Kamati iliunga mkono nia ya Serikali yetu kutoa shinikizo kwa fedha hizo kutolewa kwa Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kufuatia ombi la Serikali, Bunge lako Tukufu kupitia kwako nimetuma timu ya Wabunge nchini Uingereza kukutana na kamati husika na kufanya mazungumzo na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Uingereza yaani *House of Commons*. Timu hiyo itakutana pia na viongozi wengine wenye ushawishi mkubwa nchini uingereza ili kuwashawishi kuishinikiza kampuni ya BAE System kutoa fedha hizo kwa Serikali ya Tanzania bila masharti yoyote. Napenda sasa kuitambua timu hiyo ya Bunge ambayo ipo Uingereza kama ifuatavyo:-

Mheshimwia Job Y. Ndugai - Mwenyekiti na Naibu Spika wa Bunge, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu - Makamu Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Bunge, Mheshimiwa Angella Jasmine Kairuki Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Mheshimiwa John M. Cheyo - Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*PAC*).

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *BAE* ina masikio lakini haitaki kusikia kilio cha wengi, imeonyesha dharau ya waziwazi dhidi ya Serikali yetu na watu wake. Bunge lako Tukufu litapenda kujua kuwa katika kesi inayofanana na ya kwetu kampuni hii imeilipa kampuni ya Serikali ya Marekani dola za Marekani milioni 400 mwaka 2010 hatukusikia kwamba wameunda Bodi wala kupitisha fedha hizo kwenye Asasi za *Kiraia* za Uingereza. Serikali yetu imetahadharisha kwamba haitaruhusu Asasi ya *Kiraia* yoyote ile ya Uingereza itakayonufaika na fedha hizi kuja kuendesha shughuli zake nchini Tanzania. Tanzania ni nchi maskini sana lakini haiko tayari kudharauliwa kiasi hicho kwa Serikali yake, Taasisi zake na Taasisi zake kutoaminiwa. Kuruhusu hilo kufanyika ni kuruhusu kuibiwa kwa mara ya pili. Tuwe tayari kupoteza fedha hizi kwa kulinda heshima ya taifa letu, tusiwe tayari kudhalilishwa na kuruhusu kampuni iliyotuobia iamue fedha zetu apatiwe nani huko Uingereza na zitumike vipi hapa nchini. Ni matumaini yangu kuwa Waheshimiwa Wabunge wote bila kujali itikadi na wananchi wote wazalendo tutakuwa pamoja katika hili ili kulinda heshima ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kutoa fursa kwa Serikali kuwasilisha kauli hii na pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kubariki kauli hii kutolewa Bungeni leo hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kauli hii ijadiliwe na Bunge liazimie.

**SPIKA:** Imeungwa mkono tutatoa wakati utakaofaa. (*Makofi*)

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

## HOJA ZA SERIKALI

### AZIMIO

**Azimio la Bunge la Kuridhia Kuongeza Muda wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma** (*The Consolidated Holding Corporation*)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Azimio la Kuongeza Muda wa Shirika Hodhi za Mali za Mashirika ya Umma (*The Consolidated*

*Holding Corporation (CHC)* kwa kipindi kingine cha miaka mitatu baada ya muda wake kufikia ukomo itakapofika tarehe 30 Juni, 2011.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu zangu za dhati kwa Kamati ya Fedha na Uchumi chini ya Mwenyekiti wake Dkt. Abdallah O. Kigoda, Mbunge wa Handeni kwa kujadili kwa kina mapendekezo ya Serikali kuhusu Azimio hili siku ya terehe 20 Juni, 2011. Aidha, napenda kuwathibitishia kwamba michango yenu imesaidia sana kuboresha azimio nitakalowasilisha hapa Bungeni hivi punde.

Mheshimiwa Spika, *Consolidated Holding Corporation* lilianzishwa kisheria chini ya sheria ya *The National Bank Of Commerce, Re-Organisation and Investing of Assets and Liabilities Act* sura ya 404 kwa lengo la kuuza mali, kukusanya madeni na kusimamia mashauri mbalimbali yaliyopo Mahakama ya iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biasara. *CHC* ilipewa uhai wa miaka mitano hadi Septemba, 2002 ili kutekeleza majukumu yaliyoainishwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutokamilika kwa majukumu yake, mnamo mwaka 2002 *CHC* iliongezwa muda mwingine wa miaka mitano kuanzia mwaka 2002 hadi 2007 kupitia Azimio la Bunge Namba 20 la mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, kupitia sheria namba 10 ya mwaka 2007 ya *The National Bank of Commerce and Re-Organisation Investing of Assets and Liabilities Amendment Act*, *CHC* iliongezwa muda kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2007 hadi 30 Juni, 2011. Ambapo pamoja na kuongezewa muda *CHC* ilipewa majukumu mengine kwa kukabidhiwa majukumu yaliyokuwa ya *LAAT, Air Tanzania Holding Cooperation, SIM 2000 Limited na PSRC* baada ya mashirika haya kufikia ukomo kisheria.

Mheshimiwa Spika, matakwa ya kifungu namba 5 ya kifungu cha Sheria iliyobainisha hapo juu yameweka bayana kwamba uhai wa Shirika la *CHC* unapaswa kuwa na muda maalum ambapo utafikia ukomo baada ya kuhitimisha majukumu yake yaliyobainishwa kupitia kifungu hiki cha sheria. Majukumu haya ni kukamilisha majukumu yaliyoachwa na iliyokuwa *LAAT, ARTICLE* na *SIM 2000* ifikapo tarehe 30 Juni, 2011.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukomo wa *CHC* kuwekwa kisheria, sheria hii imetoa nafasi kwa Serikali kuwasilisha mapendekezo Bungeni kuhusu kuongeza muda wa uhai wa *CHC* ambapo endapo Bunge litaridhia uhai wa *CHC* utaongezwa kwa utaratibu wa Azimio la Bunge.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inafanya majumuisho ya taarifa ya Kamati za Hesabu za Serikali na Taarifa ya Kamati ya Kamati ya Mashirika ya Umma katika mkutano wa tatu wa Bunge kikao cha pili kilichofanyika tarehe 6 Aprili, 2011 hapa Mjini Dodoma. Kamati husika ziliwasilisha taarifa na kutoa mapendekezo kadhaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma (*POAC*) iliwasilisha mapendekezo kuhusu kuongeza uhai wa *CHC* ambapo yalitolewa mapendekezo ya aina mbili.

- (i) Kuiongezea *CHC* uhai usio na ukomo ili kuwezesha *CHC* kukamilisha majukumu yake.
- (ii) Kuongeza uhai wa *CHC* kwa kipindi cha miaka mitano baada ya tarehe 30 Juni, 2011.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya mawili yalipokelewa na kukubaliwa na Serikali kupitia Waziri wa Fedha kwa maana ya kufanyiwa kazi kwa mujibu wa taratibu za Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya tathmini ya utendaji kazi wa *CHC* na pia kwa kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge kupitia kikao cha pilii cha mkutano wa tatu wa Bunge kilichofanyika tarehe 6 Aprili, 2011.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya utendaji kazi wa *CHC* imebaini kwamba ifikapo tarehe 30 Juni, 2011 baadhi ya shughuli na majukumu muhimu yanayofanywa na *CHC* yatakuwa bado hayajakamilika kama ifuatavyo:-

- (i) Urekebishaji yaani *reorganisation* ya *TRL* baada ya Kampuni ya *RITES* kuondoka.
- (ii) *Re-organisation* ya Kampuni ya *TTCL* baada ya hatua ya awali ya ubinafsishaji kushindikana na mwekezaji wa *Airtel* kuonyesha nia ya kutoka katika ubia katika kampuni hiyo.
- (iii) Kushughulikia uuzaaji wa hisa za Serikali katika *NBC Limited* na *Zain Tanzania Limited*.
- (iv) Uperembaji wa uhakiki yaani *monitoring and evaluation* kwa vitengo vya mashirika yaliyobinafsishwa.
- (v) Urekebishaji wa Mashirika 34 yaliyobaki na kukamilisha ufilisi wa Mashirika ya Umma 24 yaliyobaki.
- (vi) Ukusanyaji wa madeni ya iliyokuwa *NBC* yenyeye thamani ya shilingi bilioni 64.9 na madai ya ubinafsishaji yenyeye thamani ya shilingi bilioni 15.8 katika mwaka 2009 *CHC* walikusanya shilingi bilioni 2.6 ukilinganisha na shilingi bilioni 1.2 kwa mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, majukumu yaliyoanishwa hapa juu yanahitaji kuendelezwa, hivyo Serikali kwa kutambua umuhimu huo inapendekeza kuwepo kwa chombo cha kuendelea kuyatekeleza kwa lengo la kuzuia upotevu wa mali na fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mapendekezo haya, Ofisi ya Msajili wa Hazina itaendelea kuimariswa kwa kufanyiwa marekebisho ya kimuundo, kiuwezo na kisheria ili baadaye ofisi hii iweze kuchukua na kushughulikia majukumu ya *CHC* yatakayosalia mara baada ya kumalizika kwa muda unaopendekezwa. Hatua hii itatekelezwa baada ya Serikali kujiridhisha endapo Ofisi ya Msajili wa Hazina imeimarika vya kutosha kuweza kuchukua majukumu yatakayokuwa yamebakia.

Mheshimiwa Spika, katika kuiimarisha na kuijengea uwezo Ofisi ya Msajili wa Hazina, ofisi hii itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi yaliyokabidhiwa kwa mujibu wa Sheria ya Msajili wa Hazina, hususan kumiliki hisa kwa niaba ya Serikali katika Mashirika ambayo Serikali inahodhi hisa nyingi (*majority shares*) na Mashirika ambayo Serikali inahodhi hisa chache (*Minority Shares*)

Mheshimiwa Spika, wakati wa kipindi cha mpito cha miaka mitatu kinachopendekezwa *CHC* wataendelea na majukumu yao yaliyosalia na wakati huo huo Ofisi ya Msajili wa Hazina inaendelea kujiimarisha. Aidha, Serikali itawasilisha Bungeni kupitia Kamati husika taarifa za mara kwa mara kuhusu hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuimariswa Ofisi ya Msajili wa Hazina, ili kuiwezesha kupokea na kutekeleza majukumu yatakayosalia kutoka *CHC*.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua uwepo wa kumbukumbu na utaalam (*Institutional Capacity and Memory*) uliojengeka miongoni mwa watumishi wa *CHC* wakati utakapowadia kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina kupokea majukumua yatakayoachwa na *CHC* baada ya miaka mitatu, Serikali haitasita kuwahamishia baadhi ya wataalamu kutoka *CHC* kwenda Ofisi ya Msajili wa Hazina kama ilivyofanyika kwa watumishi waliohamishiwa *CHC* kutoka *LART, PSRC, PATCO* na *SIMU 2000*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzingatia tathimini iliyofanyika na Serikali pamoja na maelezo niliyoyabainisha hapo juu, Baraza la Mawaziri lilikutana hapa mjini Dodoma na kuamua kuongeza uhai wa *CHC* kwa kipindi cha mpito cha miaka mitatu kuanzia tarehe 1 Julai, 2011 baada ya muda wa uhai wa *CHC* kufikia ukomo wakati Serikali inaandaa kukamilisha utaratibu wa kuhamishia majukumu ya *CHC* kwa Ofisi ya Mjasili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kuwasilisha Azimio lenye kama ifuatavyo:

NA KWA KUWA Sheria ya Benki ya Taifa ya Biashara, upangaji na umilikishaji wa mali na madeni *The National Bank of Commerce (Re-organisation and Vesting of Liabilities) Act*, Sura ya 404 ilipitishwa na Bunge kwa ajili ya kuanzisha Shirika Hodhi la Mashirika ya Umma (*The Consolidated Holding Corporation*) ambalo zamani lilijulikana kama Shirika Hodhi la Benki ya Taifa ya Biashara (*NBC Holding Corporation*);

NA KWA KUWA kwa mujibu wa sheria hii Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma lilipewa jukumu la kukusanya madeni na kusimamia uuzaji kwa mali zote za

iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara, ambazo hazikugawanywa kwa Benki ya Taifa ya Biashara (*NBC 1997 Ltd*) na *NMB* pamoja na kusimamia kesi zote za madai na za jinai dhidi ya iliyokuwa *NBC*;

NA KWA KUWA kutokana na kutokamalika kwa majukumu yake mwaka 2002, Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma, liliongezwa muda wa miaka mingine mitano (2002 – 2007) kupitia Azimio la Bunge Na. 20/2002;

NA KWA KUWA kupitia Sheria ya Benki ya Taifa ya Biashara upangaji na umilikishaji wa mali na madeni, ilifanyiwa marekebisho kupitia Sheria Na. 10 ya mwaka 2007 na Sheria Na. 26 ya mwaka 2007, ili kuliongezea Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma muda wa kipindi kingine cha uhai kuanzia tarehe 1 mwezi Oktoba, mwaka 2007 hadi tarehe 30 mwezi Juni, mwaka 2011, na vilevile kuongezewa majukumu kufuatia mashirika ya *LART, Air Tanzania Holding Corporation, SIMU 2000 Ltd.* na *PSRC* kufikia ukomo kisheria;

NA KWA KUWA muda wa uhai wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (*The Consolidated Holding Corporation*) kwa mujibu wa sheria unamalizika tarehe 30 Juni, 2011 ambapo majukumu muhimu yaliyokabidhiwa chombo hiki yatakuwa hayajakamilika;

NA KWA KUWA Serikali inatambua umuhimu wa kuongeza muda wa mpito, wa Shirika na Serikali inaandaa na kukamilisha utaratibu wa kuhamisha majukumu ya Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma kwenye Ofisi ya Msajili wa Hazina.

NA KWA KUWA marekebisho yaliyofanywa na Sheria Na. 10 ya mwaka 2007 yanalipa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mamlaka kwa kupitia Azimio la Bunge kuongeza muda wa uhai wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma kabla ya kufikia ukomo wake tarehe 30 Juni, 2011.

KWA HIYO BASI, kwa madhumuni haya maalum Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Mkutano wa Nne, kwa mujibu wa kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Benki, linaazimia kuongeza muda wa uhai wa mpito wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe 1 Julai, 2011 hadi tarehe 30 Juni, 2014, ili kutoa fursa kwa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma kukamilisha taratibu za kiutendaji na kisheria za kuhamisha kazi zitakazokuwa zimebaki na kuzipeleka kwenye Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**SPIKA:** Ahsante. Azimio limeungwa mkono, sasa nitamwite Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia suala hili au Makamu wake, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI)** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la 2007 niweze kutoa maoni na ushauri kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi Kuhusu Azimio la Kuongeza Muda wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (*The Consolidated Holding Corporation-CHC*).

Mheshimiwa Spika, Shirika hili lilianzishwa kisheria chini ya Sheria ya *The National Bank of Commerce (Re-organisation and Vesting of Liabilities) Act*, SURA ya 404 kwa lengo la kuuza mali, kukusanya madeni na kusimamia mashauri mbalimbali yaliyopo Mahakamani ya iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara (*NBC*) na ilipewa uhai wa miaka mitano hadi Septemba, 2002 ili kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, historia inaonyesha kuwa kutokana na kutokukamilika kwa majukumu yake, Shirika hili limekuwa liliongezewa muda mara kwa mara, mnamo mwaka 2002 *CHC* liliongezewa muda wa miaka mingine mitano (2002-2007) na tarehe 1 Oktoba, 2007 hadi tarehe 30 Juni, 2011 liliongezewa muda mwengine wa miaka mitano, pamoja na kuongezewa majukumu mengine ya iliyokuwa *LART, Air Tanzania Holding Corporation (ATHCO), Simu 2000* na PSRC baada ya mashirika haya kufikia ukomo kisheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inakubaliana na Azimio hili la kuongeza Muda wa uhai wa mpito wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (*CHC*) kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe 1 Julai, 2011 hadi 30 Juni 2014; ili kutoa fursa kwa *CHC* kukamilisha taratibu za kiutendaji na kisheria za kuhamisha kazi zitakazokuwa zimebaki na kuzipeleka kwenye Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge la kuongeza muda wa uhai wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (*Consolidated Holding Corporation*). Kimsingi Kamati inaunga mkono Azimio la kuliongezea muda Shirika la *CHC* kama Serikali ilivyopendekeza.

Hii inatokana na kauli ya Serikali kuwa pamoja na muda wa uhai wa *CHC* kuisha tarehe 30 Juni, 2011 bado zipo shughuli zifuatazo ambazo bado hazijakamilika. Shughuli hizi ni pamoja na:

- (a) Urekebishaji (*re-organization*) ya *TRL* baada ya kampuni ya RITES kuondoka.
- (b) Urekebishaji wa kampuni ya *TTCL* baada ya hatua ya awali ya ubinafsishaji na

Mwekezaji wa Airtel kuonyesha nia ya kutoka katika ubia katika kampuni hii.

(c) Kushughulikia uuzaji wa hisa za Serikali katika *NBC (T) Ltd.*

(d) Uperembaji (*Monitoring*) na uhakiki wa vitengo na Mashirika yaliyobinafsishwa.

(e) Urekebishaji wa Mashirika 34 yaliyobaki na ufilisi wa Mashirika ya Umma 24 yaliyobaki.

(f) Ukusanyaji wa madeni ya iliyokuwa *NBC* yenyeye thamani ya shilingi bilioni 64.9 na wadaiwa wa ubinafsishaji yenyeye thamani ya shilingi bilioni 15.8 (katika mwaka 2009 *CHC* walikusanya shilingi bilioni 2.6 ukilinganisha na shilingi bilioni 1.2 kwa mwaka 2008).

Mheshimiwa Spika, Serikali imesema vile vile muda huu unaombwa wa kuliongezea muda *CHC*, utafsiriwe kama muda wa mpito unaosubiri kukamilika kwa kufanywa marekebisho ya kimundo na kisheria ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ambaye atakabidhiwa majukumu ya *CHC*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kukubaliana na pendekezo la Serikali imetoa angalizo na ushauri katika maeneo yafuatayo:-

(a) Mara kazi za *CHC* zikihamishiwa Ofisi ya Msajili wa Hazina (*TR*) ni vidi uhuru na uwajibikaji wa Ofisi hii utaendelezwa yaani '*Independence and Accountability*' hasa ikizingatiwa kuwa Muundo unaotarajiwa ni kuifanya Ofisi ya Msajili wa Hazina (*TR*) kuwa ni *Executive Agency* ambayo kazi yake itakuwa ni usimamizi wa utitiri wa Mashirika ya Umma. Msajili wa Hazina (*TR*) itawajibikaje? Na kwa nani? Hasa ikizingatiwa kuwa yeye ndiye msimamizi?

(b) Ofisi ya Msajili itaundwaje ili iweze kuchukua majukumu ya Shirika moja (*CHC*) kwa maana ya uwezo ambao umejengeka muda mrefu katika Shirika hilo (*capacity*).

(c) Ofisi ya Msajili wa Hazina kazi yake itakuwa ni kusimamia mashirika mengine (*oversight*).

Je, kumalizika kwa muda wa *CHC* kutatafsiriwa vidi?

Mheshimiwa Spika, moja ya eneo ambalo Kamati za Kudumu za Bunge zimeshindwa kuisimamia, kisheria, ni kuangalia maslahi ya Umma (*Managing Government Interest*) katika Kampuni na Mashirika ambayo Serikali ina hisa chini ya asilimia 50.

Kwa utaratibu huu, Bunge halipati fursa ya kupata taarifa za namna Maslahi ya Umma yanavyolindwa katika Makampuni hayo. Ni vyema sasa hoja hii iangaliwe na kujengwa kisheria ili kupunguza udhaifu huu. Kamati inashauri kuwa wakati huu *CHC*, ikielekea katika muda wa mpito yafanyike mabadiliko madogo katika Sheria zifutazo:-

(a) *Amendment of the NBC (Re-organization and Vesting of Assets and Liabilities) (Amendment) (No.2) Act No.26 of 2007*; na ile ya

(b) *Amendment of the Public Corporations Act Cap. 257* ili mapungufu yaliyooneshwa hapo juu yaondolewe.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali kuliongezea muda wa miaka mitatu Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (*CHC*) ni wa busara ukizingatia bado kuna mali ambazo *CHC* inazisimamia na kuna watu wengi wanadaiwa kutokana na kununua Mashirika ya Umma na Mali zake bila kulipia kikamilifu.

Kwa mujibu wa tathimini iliyofanywa na Shirika Hodhi la yaliyokuwa Mashirika ya Umma (*CHC*) hadi kufikia 30 Juni, 2009 kwa Mashirika 62 yaliyobinafsishwa ni Mashirika 12 tu ndiyo yalikuwa yanaendelea vizuri na uzalishaji, Mashirika 27 yalikuwa katika hali ya wastani kiutendaji na Mashirika 23 yalikuwa yamefunga shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Baada ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati, sasa napenda kuwatambua kwa majina wajumbe wa Kamati walioshughulikia Azimio hili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dkt. Abdallah O. Kigoda; Mwenyekiti, Mheshimiwa Josephine J.Genzabuke, Mheshimiwa Eustas O. Katagira, Mheshimiwa Maulidah Anna V. Komu, Mheshimiwa Dkt. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Devotha M. Likokola, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Christina L. Mughwai, Mheshimiwa Mwigulu L.N. Madelu, Mheshimiwa Abdul-Aziz M. Abood, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Dunstan L. Kitandula, Mheshimiwa Dkt. William A. Mgimwa, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Freeman A. Mbewe, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mheshimiwa Amour Amina Abdulla, Mheshimiwa Rostam A. Aziz, Mheshimiwa Alhaj. M. H. Missanga, Mheshimiwa Andrew J. Chenge na Mheshimiwa Luaga J. Mpina.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumshukuru, Waziri wa Fedha, Manaibu Waziri Fedha na Watendaji Wakuu wa Wizara pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuandaa na kukamilisha Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia miongozo na maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi kukamilisha taarifa ya Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio hili. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Sasa nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu suala hili, nafikiri kwa niaba ya Msemaji Mkuu, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS (K.n.y. MSEMADI MKUU WA UPINZANI - WIZARA YA FEDHA).** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Kuongeza Muda wa Uhai wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (*Consolidated Holding Corporation (CHC)*), yakiwasilishwa na mimi ambaye ni Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama hapa kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Wizara ya Fedha, Kabwe Zuberi Zitto, kuwasilisha Maoni na Mapendekezo ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Kuongeza Muda wa Uhai wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (*CHC*), kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 96 (6).

Mheshimiwa Spika, hoja mahsusisi iliyoletwa na Serikali mbele ya Bunge hili Tukufu inataka Bunge la Jamhuri ya Muungano, katika Mkutano huu wa Nne, kwa mujibu wa kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Benki, liazimie ifuatavyo, ninanukuu:-

“Kuongeza muda wa uhai wa mpito wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe 1 Julai, 2011 hadi Juni 30, 2014, ili kutoa fursa kwa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika kukamilisha taratibu za kiutendaji na kisheria za kuhamisha kazi zitakazokuwa zimebaki na kuzipeleka kwenye Ofisi ya Msajili wa Hazina”, mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunaona kuwa pendekezo hilo la serikali haliendani kabisa na hali halisi ya majukumu yaliyo mikononi mwa shirika hilo wala yale inayopaswa kuyabeba. Pia pendekezo hilo la serikali halionekani kwa kuzingatia vema historia ya shirika lenyewe, ambalo kwa sababu ya kupewa vipindi vifupi vifupi vyta utekelezaji wa majukumu yake, serikali imejikuta mara kwa mara ikilazimika kurudi Bungeni kuomba muda wa uhai wa shirika hilo uongezwe kama inavyofanya leo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa *Consolidated Holding Corporation (CHC)* ilianzishwa kisheria chini ya Sheria ya *The National Bank of Commerce (Re-organization and Vesting of Liabilities) Act*, Sura ya 404, kwa dhumuni la kuuza mali, kukusanya madeni na kusimamia mashauri mbalimbali yaliyopo mahakamani ya iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara (*NBC*). Wakati huo, *CHC* ilipewa uhai wa miaka mitano hadi Septemba, 2002 ili kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, izingatiwe kuwa hadi kufikia mwaka 2002, *CHC* ilikuwa bado haijakamilisha majukumu iliyokuwa imepangiwa. Kwa hiyo, Bunge lililazimika

kuiongezea muda mwagine wa miaka mitano kuanzia mwaka 2002 -2007, kupitia Azimio la Bunge Na. 20/2002.

Mheshimiwa Spika, itiliwe maanani kuwa mnamo mwaka 2007, kupitia Sheria Na. 10 ya Mwaka 2007 (*The National Bank of Commerce (Re-organization and Vesting of Assets and Liabilities) (Amendment) Act, CHC*, iliongezewa muda mwagine kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2007 hadi tarehe 30 Juni 2011. Pamoja na kuiongezewa muda, *CHC* pia iliongezewa majukumu kwa kukabidhiwa majukumu yaliyobaki ya iliyokuwa *LART, Air Tanzania Holding Corporation (ATHCO)*, *Simu 2000* na *PSRC*, baada ya mashirika haya kufikia kikomo kisheria.

Mheshimiwa Spika, ili kufanya maamuzi sahihi na yenyе maslahi kwa taifa kuhusiana na Shirika hili, Kambi ya Upinzani tunaona ni muhimu kwanza kuzingatia hali halisi ya matokeo ya tathmini ya utendaji wa *CHC*. Tathmini hiyo ya kiutendaji inaonesha kuwa, ifikapo tarehe 30 Juni, 2011 shughuli na majukumu mengi na muhimu ya Shirika hili bado yatakuwa hayajakamilika kama ifuatavyo:-

- Urekebishaji (*re-organization*) ya *TRL* baada ya Kampuni ya *RITES* kuondoka.
- *Re-organization* ya Kampuni ya *TTCL* baada ya hatua ya awali ya ubinafsishaji kushindikana na Mwekezaji wa *Airtel* kuonesha nia ya kutoka katika ubia katika kampuni hii.
- Kushughulikia uuzaaji wa hisa za Serikali katika *NBC (T) Ltd.*
- Uperembaji (*monitoring*) na uhakiki wa Vitengo na Mashirika yaliyobinafsishwa.
- Urekebishaji wa Mashirika 34 yaliyobaki na ufilisi wa Mashirika ya Umma 24 yaliyobaki.
- Ukusanyaji wa madeni ya iliyokuwa *NBC* yenyе thamani ya shilingi za Kitanzania bilioni 64.5 na wadaiwa wa ubinafsishaji yenyе thamani ya shilingi bilioni 15.8.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali na Bunge lako Tukufu, lizingatie kuwa, majukumu hayo ni makubwa na endelevu. Aidha, majukumu haya, mathalani yale majukumu ya kisheria na uperembaji na uhakiki wa vitengo na Mashirika yaliyobinafsishwa, yanahitaji uzoefu wa kutosha wa kitaasisi katika kuyatekeleza. Uzoefu ambao kimsingi hauwezi kupatikana popote pale, isipokuwa kwa *CHC* yenyewe, kwani tayari imeshafanya kazi hiyo kwa takriban miaka kumi sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kazi za *CHC* hazijakamilika, zinaendelea na zitabaki kuwa endelevu hasa kwenye masuala hayo ya kufanya *monitoring and evaluation* ya Taasisi za Serikali zilizouzwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma iliwasilisha Taarifa yake ya mwaka Bungeni mnamo tarehe 6 Aprili, 2011, ambapo mionganoni mwa mapendekezo yaliyotolewa na kukubaliwa na Bunge ilikuwa ni kuongeza muda wa kazi wa Shirika Hodhi la Mali za yaliyokuwa Mashirika ya Umma (*CHC*);

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bunge liliridhia mapendekezo hayo ya Kamati ambayo kimsingi yalitaka Shirika la *CHC* lipewe muda wa kudumu;

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumbukumbu rasmi za Bunge (*Hansard*) zinamnukuu Mheshimiwa Waziri wa Fedha siku hiyo hiyo ya tarehe 6 Aprili, 2011 akikubaliana na Mapendekezo ya Kamati na kuahidi kuwa Serikali itatekeleza mapendekezo ya Bunge asilimia mia kwa mia;

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda wa *CHC* unamalizika kisheria tarehe 30 Juni, 2011; na kwa kuwa unawasilisha Muswada wa Fedha wa Mwaka 2011 ambao umelenga kubadili Sheria mbalimbali zinazohusiana na ukusanyaji na usimamizi wa fedha za umma; hivyo basi, Kambi ya Upinzani kwa kuzingatia yote hayo, tunapendekeza kufanyike mabadiliko madogo katika sheria zifuatazo:-

- *Amendment of the National Bank of Commerce (Re-Organization and Vesting of Assets and Liabilities) (Amendment) (No.2) Act, No. 26 of 2007.*
- *Amendment of the Public Corporations Act, Cap.257.*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunapendekeza kwamba, *CHC* wapewe muda wa kutosha (*perpetual existence*) ili wafanye shughuli zao za kisheria kwa muda wa kutosha. Kwa hiyo, tunapinga pendekozo la azimio lililoletwa na Serikali na badala yake tunalitaka Bunge hili Tukufu kwa kuweka mbele maslahi ya Taifa lipitishe azimio linalosomeka kama ifuatavyo:-

“Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Nne, kwa mujibu wa kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Benki, linaazimia kuongeza muda wa uhai wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma, kuanzia tarehe 1 Julai 2011 mpaka hapo Bunge litakapoamua vinginevyo.”

Mheshimiwa Spika, pia Kambi ya Upinzani inapendekeza *CHC* wapewe jukumu la kuangalia Maslahi ya Umma (*managing government interest*) katika Kampuni na Mashirika ambayo Serikali ina Hisa chini ya asilimia 50 na kwa kupitia njia hiyo, Kamati za Bunge zitapata nafasi ya kufahamu namna Maslahi ya Umma yanavyolindwa katika Makampuni hayo kupitia *CHC*.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante kwa kuwasilisha vizuri, kwa hiyo, tuna wachangiaji wachache. Kwanza, tutaanza na Mheshimiwa Zitto Kabwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, sitawachukua wengi kwa sababu tuna kazi nyingine.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika hoja iliyopo mbele yetu. Hoja ya kuongeza muda wa Shirika Hodhi la Mashirika ya Umma (*Consolidated Holding Corporation*), ambapo Serikali imekuja kuomba kwa Bunge lako Tukufu kwamba, muda huu uongezwe kwa muda wa miaka mitatu tofauti kabisa na Azimio ambalo lilipitishwa na Bunge tarehe 6 Aprili, 2011 wakati Bunge likijadili taarifa ya Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma ambayo mimi ninaiongoza.

Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa kwamba, baadhi ya watu kwa mawazo yao na fikra zao, wakadhani kwamba, jambo hili ni la Kamati ya Mashirika ya Umma na kama wengine wanavyoita kimakosa, Kamati ya Zitto. Kamati ya Mashirika ya Umma, ina Wabunge wa pande zote katika Bunge hili na *majority* ya Wabunge kwenye Kamati ya Mashirika ya Umma ni Wabunge wa kutoka Chama Tawala, Chama cha Mapinduzi, sisi wengine tumepewa dhamana tu ya kuongoza. Dhamana ambayo leo inaweza ikawepo kesho isiwepo. Kwa hiyo, tunapojadili jambo hili kwa wale ambao wanaugua Ugonjwa wa Zitto *Phobia's* wajaribu kumtoa Zitto waweke nchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zitto, jadili hoja wenzi tukuelewe, hii nyingine hatukuelewi. Tunaomba utujadilie hoja tuweze kuelewa hoja yako ni nini, hii nyingine yote vijembe, vineno neno havimsaidii mtu. Tupe hoja.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa mwongozo wako, nilikuwa ninataka nianze hivyo ili jambo hili liweze kueleweka vizuri kwamba, tunajadili jambo la msingi sana ambalo tayari Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma ililijadili kulileta Bungeni, Bunge likapitisha na Waziri wa Fedha akakubaliana na mapendekezo na baadae limerudi kinyume na makubaliano ambayo Bunge lilipitisha.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, jambo hili lilijadiliwa kwenye Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi na katika Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi tulikubaliana tofauti na ambavyo leo Waziri wa Fedha amekuja kusoma Bungeni na kwa taarifa nilizonazo, hakuna kikao kingine cha Kamati ya Fedha na Uchumi kilichokaa kutengua yale maamuzi ambayo tulikubaliana katika Kamati ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, ukisoma Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi, utagundua kwamba ili maswali haya wanayoyaauliza yaweze kujibiwa vizuri ni lazima *CHC* iongezewe muda wa kutosha. Ninaomba kunukuu, Kamati ya Fedha na Uchumi inasema: "Mara kazi za *CHC* zikihamishiwa Ofisi ya Msajili wa Hazina (*TR*), ni vipi uhuru na uwajibikaji wa Ofisi hii utaendeshwa, yaani *independence and accountability* hasa ikizingatiwa kuwa muundo unaotarajiwa ni kuifanya Ofisi ya Msajili wa Hazina kuwa ni *Executive Agency* ambayo kazi yake itakuwa ni usimamizi wa utitiri wa Mashirika ya Umma (*Regulatory Function*)"?

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi inahoji hapa kwamba, *Regulator* ambaye anapaswa ku-regulate Mashirika yote ya Umma anawezaje leo akapewa kazi ya utendaji, yaani kama hivi leo tuichukue *EWURA* ambayo inasimamia bei ya umeme tuipe kazi ya kuuza umeme? Hili ndiyo jambo ambalo Serikali inalipendekeza. Jibu hili la Kamati ya Fedha na Uchumi likijibowi, pendekezo lote la Serikali linakuwa halina maana. Kamati ya Fedha na Uchumi, pia inasema Msajili wa Hazina atawajibika kwa nani, ikizingatiwa kuwa yeye ndiyo msimamizi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda nilikumbushe Bunge lako kwamba, tulipitisha sheria wakati wa kufanya mabadiliko haya ya mwisho mwaka 2007 na ninamshukuru Mwenyezi Mungu, nilikuwa sehemu ya Bunge hili tulifanya *amendment* ya Sheria ya *Public Corporation Act, Cap. 257*, ambayo ilimpa mamlaka Msajili wa Hazina kuwa sehemu ya *Consolidated Holdings*. Leo unapotaka kuichukua *Consolidated Holdings* ukaipeleka kwa Msajili wa Hazina unaua *the whole spirit* ambayo tulikuwa nayo mwaka 2007, kwa sababu kimsingi *Consolidated Holdings* inamilikiwa na Msajili wa Hazina kwa asilimia mia moja. Kwa hiyo, leo huwezi ukamchukua *Consolidated Holdings* ukampeleka kwa *TR*.

Baadhi ya Wabunge wanahoji kwamba, tunawezaje kuwa na taasisi mbili zinazoshughulikia suala moja? Ninapenda ifahamike wazi, Msajili wa Hazina ana kazi zake tofauti na *CHC* ina kazi zake tofauti. Leo niwaambie Waheshimiwa Wabunge, sasa hivi nchi yetu ina hisa ambazo inamiliki kwenye taasisi mbalimbali ambazo tulizibinafsisha na tumetoa taarifa hapa Bungeni, Msajili wa Hazina ambaye anazisimamia hisa hizi chini ya asilimia 50 sasa hivi baadhi ya hisa, wala hajui *certificate* ziko wapi.

Mheshimiwa Spika, kuna Mashirika 25 leo tunavyozungumza. Tuna mali ya umma, tuna fedha za walipa kodi mle, Msajili wa Hazina hajui hati ziko wapi! Kuna Mashirika hayalipi *dividend* kwa sababu ya uzito wa kazi ambazo Msajili wa Hazina anazo. Leo hii tunataka tuhamishe kila kitu *CHC*, tupeleke kwa Msajili wa Hazina. Wakati Bunge hili linaunda Kamati za Bunge, nilikabidhi majukumu ya kusimamia ubinafsishaji kwenye Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma, kwa mujibu wa ukurasa wa 131 wa Kanuni za Bunge. Majukumu ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma ni kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma. Kuna madudu mengi sana kwenye ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, tumeagiza leo *CHC* wafanye tathmini ya ubinafsishaji wote. Tathmini inaendelea, leo tunataka tuiue *CHC*. Kuna watu ambao wamebinafsishiwa hawajalipa, wanapenda *CHC* ife. Kuna watu wanadaiwa na *NBC* hawajalipa wana kesi, leo ukisema unawapa *CHC* miaka mitatu wataziendeleza zile kesi na ninafahamu Mahakama zetu zilivyo, miaka mitatu itakwisha zile kesi zitapotea na mali ya umma itapotea. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, ninawaomba japo kwa muda mfupi, mfumbue macho yenu mliangalie Taifa hili; msikubali maamuzi haya ya Baraza la Mawaziri, ni maamuzi

yanayotokana na *lobbyist* ambao wanatolea macho mali zetu, ambao wanataka wahakikishe mali hazisimamiwi vizuri, ambao wanataka waendelee kuinyonya nchi yetu. Hii ni *test* ya uzalendo, siyo suala la uchama, siyo suala la Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma peke yake, suala hili ni *test* ya uzalendo wa nchi yetu. Kuna watu wa Mbarali kule wanahangaika na mashamba, kuna watu wa Babati wanahangaika na mashamba.

Tumeiagiza *CHC* ifanye tathmini ilete kwenye Kamati yetu kwa ajili ya kuangalia ni namna gani ambavyo tunawaokoa wakulima wetu. Leo Baraza la Mawaziri la nchi hii ambalo limepigiwa kura na wakulima maskini wa nchi hii wanakwenda kutaka walieu Shirika hili.

### **MBUNGE FULANI:** Fisadi!!!!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, anakagua wote wawili; *TR* na *CHC*. *TR* anakaguliwa kama *Vote* yoyote ya Serikali au kama Wizara ya Ngeleja inavyokaguliwa *Vote 58* na kama Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inavyokaguliwa, Msajili wa Hazina hana *balance sheet*, mali na madeni hana. *Consolidated Holdings* ina mali na madeni, ina *balance sheet*. Tunaposema Kamati ya Mashirika ya Umma ilivyopendekeza kwamba, mali zetu ambazo zinamiliikiwa chini ya asilimia 50 zisimamiwe na *Consolidate Holdings*, lengo letu ni kutaka tuwe na jicho kwenye zile mali. Niliwaambia juzi hapa, tumeuza AIRTEL, hapakuwa na mawasiliano yoyote na Watu wa Tanzania na tunao *Board Members*, *TR* hakuangalia pale.

Mheshimiwa Spika, tuna hisa *TTC*, Sigara, *Kilombero Sugar* na kwenye Makampuni ambayo *you can't even imagine*, tunataka sasa tuwe na jicho hili, jicho hili litaangaliwa na *CHC* tu. Hakuna nchi duniani na ninaomba mtu mmoja aje kuni-*prove me wrong*, ambayo haina Shirika la *Consolidated Holdings*, *Holding Company* ambayo inasimamia hisa na wala hili halitaondoa majukumu ya *TR* kwa sababu *TR* anamiliki *CHC* asilimia mia moja. *CAG* akienda kukagua katika *balance sheet* yake ataangalia *investments* kwenye hisa ndogo ndogo. Watakuja kwenye Kamati ya Bunge wataleta pale kwenye Kamati ya Bunge tutahoji hisa zetu hapa zinafanya nini. Kazi hiyo haifanyiki hivi sasa na wewe ni shahidi yangu na Mhesimiwa Sitta toka nimekuwa Mwenyekiti wa Kamati hii ya Mashirika ya Umma, nimekuwa nikihangaika tufikie hisa hizi. Leo Mashirika yote yanafutwa kwa Baraza la Mawaziri kukaa na kupitisha jambo ambalo linakwenda kupoteza mali za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninaliomba Bunge hili lisikubali, ninawaomba Wabunge wa Vyama vyote tusikubali, tutoe muda wa kutosha kwa *CHC* tuazimie kuwaongezea majukumu wasimamie mali zetu ambazo ziko chini ya asilimia 50. Bunge hili Tukufu liwe na jicho na tusikubaliane na maamuzi ya Baraza la Mawaziri, ambayo yameletwa. Ninaamini kabisa, Baraza la Mawaziri halikupata *proper information*, halikuwa *well advised* na ndiyo maana kwenye Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi tukafikia makubaliano ya kwamba, aah tusubiri kwanza tathmini ifanyike, Wizara ya Fedha ikafanye utafiti baadae ndiyo ilete mapendekezo. Ninasikia Wizara ya Fedha imeamua *ku-go ahead with this*. Nimeamua kufanya *lobbying* kwenda *ku-mislead* Wabunge wa

Chama Tawala, kwenda kudanganya kwenye *caucus* ya Wabunge na mimi ninaamini Waheshimiwa Wabunge wa Chama Tawala ni Wazalendo, ambao hawawezi kukubaliana na jambo hili na ni lazima wakatae.

**MBUNGE FULANI:** Mafisadi!!!!

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika

**SPIKA:** Wote mnakaa. Hoja inaweza kujadiliwa kwa utulivu na wenzako wakafuata. Sasa mkianza nini danganya, fanya nini, watu tuko hapa tunataka kusikiliza uzito wa hoja zenu, siyo kelele za hoja zenu. Sasa ninaomba hii muelewane.

Kwanza, Waheshimiwa Wabunge, lazima niseme ifuatavyo: Azimio hili limeletwa sasa kwa sababu ya udharura wa kwamba, itakapofika tarehe 30 Juni hili Shirika litakuwa halina kazi, ndiyo udharura wake hii. Sasa ninavyoona ni kwamba, hoja mnazozingumza ni nzito, mimi ningependa kwanza muipe uhai hii *CHC* kwa maana ya Azimio hili halafu mazungumzo mengine haya hatuzuiliwi kuongea.

Ninaona ipo hatari ya kuchukua maeneo fulani mkaendelea kuyawekea nguvu wakati ukweli ukubwa wake wote hatujuangalia vizuri. Mimi ninapendekeza kwamba, kukubali liongezewe huo muda lakini tutengeneze hoja nyingine nzito kuhusu suala zima hili. Kwa sababu ninaona zipo hoja nzito, lakini tukichanganya sasa hivi hatutafika kwenye hii kitu. Tuipe uhai wa hii miaka yake mitatu wakati tunafanya kazi nzima ya kuangalia haya mnayoyasema sasa. Kwa hiyo, ninaomba tuendee.

## MWONGOZO WA SPIKA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ninarejea Ibara ya 64 ya Kanuni za Bunge. Wakati mchangiaji aliyekaa sasa hivi, Mheshimiwa Zitto Kabwe, alipokuwa anachangia amesema Azimio hili linaletwa hapa baada ya Baraza la Mawaziri kupitiwa na *lobbyist*. *Lobbyist* maana yake ni kwamba, Baraza la Mawaziri, sisi wote tumepitiwa na watu waliotushawishi tufanye maamuzi hayo. Kanuni zinasema: “*Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge; ninarejea vifungu viwili: (a) hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli. Kifungu (g) kinasema hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine.*”

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Baraza la Mawaziri, sijafikiwa na mtu na nina uhakika wapo Wabunge Mawaziri wengi watasema hivyo. Sasa ninaomba kama mtu anapinga kitu, aseme atoe hoja zake. Mheshimiwa Zitto Kabwe, umetudhalilisha

Waheshimiwa Wabunge wenzio kwamba tumeptiwa, tumerubuniwa na ma-lobbyist, katika hili ninaomba mwongozo wako na kama ana ushahidi awataje hao waliokuwa *lobbied* halafu wakaifikisha Serikali hapa tulipofika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimetolea uamuzi kabla nikasema, tunapojadili hapa tujadili uzito wa hoja; siyo lugha mbaya wala siyo mashambulizi yasiyokuwa na maana kwa sababu mwisho wake hayatufikishi sisi kufikia hotuba hii. Kwa hiyo, nimesema suala zima linalohusika na hatima ya *CHC*, kwanza kabisa, kwa sababu ya udharura wake, tukubali miaka mitatu, halafu shughuli nzima ya kuandaa nini kitakuwa hatma yake ndiyo tuanze kuifanyia kazi katika miaka hiyo mitatu. Sasa hilo ningependa tulijadili kwa msingi huo; vinginevyo, hili Shirika itabidi life tarehe 30. Kama mnaamua hivyo, litakufa tarehe 30. Ninaomba tuelewane hivyo.

Sasa namwita Mheshimiwa Zitto aendeleee.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa mwongozo wako, kwa sababu mambo ambayo nimeyasema nina uhakika nayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zitto, nimekutetea wewe unataka urudi huko!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, ninaomba wengine wakae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa anaendelea kuthibitisha, Kifungu cha 64

...

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Kifungu gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Tundu Lissu, wewe siyo Spika na ndiyo utaratibu wenyewe huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Zitto amehusisha jambo hili na mambo ambayo siyo ya kuaminika. Mzungumzaji wa nyuma ameomba atuthibitishie haya aliyoyasema. Ninasikitika kusema hata baada ya wewe kutoa *rulling*, anasema ana uhakika na anachokisema. Sasa hiyo ina-*justify* ukweli kwamba, tunaomba atuthibitishie hayo aliyoyasema.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Ninafanya uamuzi wa suala moja baada ya lingine; Mheshimiwa Wenje kaa. Mimi nilifikiri Zitto amenielewa, lakini kama yeze anafikiri ana uthibitisho basi atupe uthibitisho. Ninazungumza na Zitto na nilifikiri amenielewa niliposema. Tunapozungumza tujadili, lakini kama anafikiri yeze ana uthibitisho mimi ninaweza kumwambia anipe na kama una uthibitisho simama.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, mimi nimekuelewa kwamba, Azimio hili lirekebishwe tuongeze huu uhai kuelpuka udharura na tutoe tamko la kuangalia ni namna gani ambavyo tutaendelea kuhakikisha kwamba, mali zetu zinaangaliwa vizuri. Nimekuelewa na ninakuunga mkono kwa ushauri ambaa umeutoa.

**SPIKA:** Hiyo ya kusema Baraza limedanganya sijui? Tunaongea kwa utaratibu humu ndani, anasimama mtu mmoja anasema. Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kurejea maamuzi ya Baraza la Mawaziri ambayo yamewasilishwa hapa na Waziri wa Fedha ni matokeo ya ushawishi ni *lobbying*. Wala sitaki kufinyanga maneno, maamuzi haya ni maamuzi yanayotokana na *lobbying* na kama sivyo, Serikali ilete hapa mbele pendekezo la awali ambalo limetoka Wizara ya Fedha kwenda kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu, kwenda kwenye *Cabinet Secretariat*, kuhusiana na pendekezo la *CHC*. Ninaomba Serikali ilete hapa na ndipo Bunge litathibitisha ya kwamba, maamuzi ambayo Baraza la Mawaziri limeyafanya juzi ni matokeo ya *lobbying* na ninarejea ni matokeo ya *lobbying* na tusiruhusu Baraza la Mawaziri kuendeshwa na ma-*lobbyist*.

**SPIKA:** Serikali; Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kwa heshima zote, tumesikia yote yaliyosemwa, ninajua Mheshimiwa Zitto ana uchungu sana, anakerwa sana kama ni kweli. Sasa kwa sababu hajui Mfumo wa Serikali unavyofanya kazi, hivyo vyombo vyote alivyovitaja, *Cabinet Secretariat*, Kamati ya Makatibu Wakuu (*IMTC*), siyo vikao vya maamuzi ni vikao vya ushauri. Kikao cha juu cha uamuzi ndani ya Serikali ni Baraza la Mawaziri, pamoja na ushauri wote na Baraza la Mawaziri hukaa kumshauri Mheshimiwa Rais akubali au akatae. Huu ndiyo utaratibu, umeandikwa upo kisheria.

Sasa kwa sababu Mheshimiwa Zitto ameng'ang'ania kwamba, haya yametokana na ushawishi, Baraza la Mawaziri limerubuniwa, ninarudia msimamo wetu kwamba, Mheshimiwa Zitto aje athibitishe hapa ni akina nani wamerubuniwa; wamerubuniwa namna gani; na kwa vipi? Baraza la Mawaziri ni Kikao pekee kinachojitegemea, hakina mahusiano, hakishawishiwi, wala hakiamui kutokana na ushauri wa mtu mwengine; kile ni kikao cha uamuzi wa juu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Zitto athibitishe hapa. (*Makofii*)

## MWONGOZO WA SPIKA

**SPIKA:** Sasa mnakaa chini, mwongozo haupo, nipe taarifa Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako kwa jambo ambalo limetokea muda mfupi uliopita. Umemwelekeza Mheshimiwa Zitto Kabwe, athibitishe kauli aliyoitoa hapa Bungeni kwamba, Baraza la Mawaziri limeshawishiwa kufikia maamuzi ambayo yameletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, mwongozo ninaouomba unatokana na Kanuni ya 63(3) na (4):-

- (3) *Mbunge mwingine yeyote anaweza kusimama mahali pake na kumtaka “kuhusu utaratibu” na baada ya kuruhusiwa na Spika, kudai kwamba, Mbunge aliyeokuwa anasema kabla yake ametoa maelezo ya uwongo kuhusu jambo au suala alilokuwa analisema Bungeni.*
- (4) *Mbunge anayetoa madai kwa mujibu wa fasili ya (3) ya Kanuni hii atakuwa na wajibu wa kutoa na kuthibitisha ukweli kuhusu jambo au suala hilo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge.*
- (5) *Bila ya kuathili masharti ya fasili zilizotangulia za Kanuni hii, Spika au Mbunge mwingine yeyote, baada ya kutoa maelezo mafupi ya ushahidi unaotilia mashaka ya dhahiri kuhusu ukweli wa kauli au usemi au maelezo juu ya jambo au suala ambalo Mbunge amelisema Bungeni, anaweza kumdati Mbunge huyo atoe uthibitisho wa ukweli wa kauli au usemi au maelezo yake na kama atashindwa kufanya hivyo, afute kauli au usemi au maelezo yake hayo.*

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu, mtu wa kwanza mwenye wajibu wa kuthibitisha ni upande wa Serikali, Mheshimiwa Lukuvi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Lukuvi, akithibitisha kwamba, wao hawakushawishiwa, kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge, basi wajibu wa kuthibitisha unamrudia Mheshimiwa Zitto. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, yaani mnapenda kubadilisha mambo kwa ajili ya kufurahisha. Taratibu za kiserikali, Baraza la Mawaziri haliwijabiki kwa Bunge. Kinachowajibika kwa Bunge ni Hoja za Serikali zilizokuja hapa. Mliposema Baraza limerubuniwa, amesimama huyu akakwambia uthibitishe nani karubuniwa, kwa sababu sisi hatuna mtu yeyote aliyerubuniwa na wala siyo utaratibu wa kurubuniwa. Sasa huyu aliyetumia maneno ya kuudhi ya kurubuniwa ndiyo aseme maana anaweza kuwa anajua wapi walirubuniwa. Kwa hiyo, ninakupa mpaka siku ya tarere 29, Mheshimiwa Zitto, utataja nani alimrubuni mwenzie halafu tuweze kuona tunaendelea vipi.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, mimi nimeshatoa uthibitisho wangu, nimesema Serikali ilete.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zitto, ninaomba ukae chini. Tusibishane, nimeshawaambieni watu wanatuangalia, kwa sababu hatuchungi midomo yetu. Lengo letu ni hoja na siyo maneno ya kugombana hapa. Kwa hiyo, ninakupa mpaka tarehe 29 utathibitisha nani alimrubuni na ulikuwaje urubunishi huo mimi siufahamu. Baraza la Mawaziri haliwajibiki katika Bunge hili. Tunaendelea, tumemaliza taarifa na ninadhani Mheshimiwa Zitto umemaliza dakika zako.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, mimi nimemaliza hoja zangu.

**SPIKA:** Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, kama nilivyosema tujadili kwa maana ya kulikoa hili Shirika liweze kuendelea baada ya tarehe 30, habari zingine tutaandika utaratibu mwingine.

**MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii. Pili, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri, namna alivyowasilisha pamoja na Kamati yangu ya Fedha na Uchumi.

Kwanza kabisa, ninaomba *ku-declare interest* kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa hiyo, yale nitakayoyaongea kwa namna fulani, *yata-reflect* ambayo Naibu Mwenyekiti wetu ameshayasema kwa mwelekeo wa msingi ulivyotuelekeza.

Ninaomba uniruhusu niseme kiufupi kitu gani kinaniongoza kuyajadili haya mbele ya Bunge hili. La kwanza, sisi kama Kamati, tulizingatia kazi nzuri iliyofanywa na *CHC* na tukakubali kwamba, *CHC* mpaka sasa imefanya kazi yake vizuri. La pili, tulitambua kwamba, *CHC* kazi zile kwa mujibu wa Sheria iliyopo, Sheria iliweka ukomo wa uhai kama ilivyoelizwa ndani ya Sheria na kwamba tulikuwa tunakabiliwa na uamuzi wa namna inavyoweza ikaendelea kwa hali ambayo ipo ya kazi ambayo imeongezwa.

Vilevile tulitazama Sheria iliyoanzisha *CHC* na tukaona kwamba, tutazame Sheria ya *NBC* kama alivyoeliza Makamu Mwenyekiti wetu, pamoja na *Public Corporations Act* kama tulivyopendekeza kwamba itabidi kuwe na mabadiliko katika Sheria hizo. Kama ulivyosema; ni kweli na sisi kama Kamati tulitambua umuhimu wa *CHC* kuendelea kuwepo kwa mujibu wa *extension* ya kazi zao ili kazi zilizo mbele yao wamalize. Hii ilikuwa hoja ya msingi na tulikubali hivyo na kuogopa kwamba, tarehe 30 utakuwa ndiyo mwisho wa uhai wao.

La pili, tuliweka angalizo kwamba, hoja ya Serikali ya kuomba kuweka ukomo miaka mitatu na *ku-transfer* kazi hizo kwenda kwa *Treasury Registrar*, kama Kamati, kusema kweli tuliishauri Serikali tofauti na hilo lililoelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitaweka ufanuzi, tulikubaliana Bunge liweke *extension* ya *three years*, lakini angalizo lilikuwa la kwanza tunahitaji Serikali baada au kabla ya kuhuisha hiyo miaka mitatu, waangalie hiyo *capacity* ya *CHC* na umuhimu wa kuijengea *capacity* yoyote kama kutakuwa na umuhimu mbele ya safari wa *ku-hand over to another institution*; lakini kwanza wa-*establish required competencies* kwa ajili ya *capacity building*.

La pili, tulikubaliana wa-*define autonomy* au *independency* ambayo inatakiwa kuwepo ili *ku-avoid conflict of interest* ikiwa kutakuwa na umuhimu wa *ku-transfer* hii *role* kwenye chombo kingine zaidi ya *CHC*.

Tatu, tuliomba waangalie uwezekano wa kuwa na *effective structure* itakayohakikisha kwamba, hicho tunachosema *capacity building, accountability levels* pamoja na *autonomy* itakuweje ikiwa maoni ya Serikali ya kupeleka kwa *TR* yatabakia hivyo.

Wao wafanyie kazi hayo halafu baadae kabla ya mwisho wa miaka mitatu ambao tulikubaliana nao, tunaweza kufanya *extension* ili kazi hizo ziendelee kwa muda huo, wayafanyie kazi ili hayo yaje yatusaidie tutakapokuja kutathmini upya. Hofu yetu ilikuwa kwa sababu tunatambua kwamba, *TR* ni *Regulatory Authority*, wasije waka-*compromise* kazi ambazo ziko mbele yao ikiwa watachukua *role* za *CHC*.

Mheshimiwa Spika, kiujumla ni kwamba, Kamati yetu tulikubaliana na Serikali, hoja yao ya *ku-extend shughuli za CHC for three years subject to study hizi conditions* ambazo tumeziweka mbele yetu na kimsingi mapendekezo yetu yalikuwa ni kuunga mkono *extension to three years*, lakini siyo *ku-transfer automatically to TR*, kwa sababu *it was subject to fulfilment to these conditions* na yaletwe baadae sisi Wabunge tutazame hiyo *carrying structure* itakidhi kwa kiwango gani yale ambayo tunaona ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nimeona ni muhimu kueleza hali halisi iliyotawala katika mazungumzo ya Kamati yetu ya Fedha, kwa sababu hii itatujengea heshima ili tusiwe na ushabiki au tusiwe na mwelekeo wa mazungumzo yasiyo na *analysis*. Kwa hiyo, wenzenu tulitazama hivyo na tukapendekeza hivyo.

Mheshimiwa Spika, mtazamo wetu haukuwa unatazama *interest* za pande gani, *we were just looking on the viability of the position* iliyokuwa mbele yetu.

Ninawaomba Wabunge wenzangu, suala hili tulitazame hivyo, tusilete labda purukushani ya kwamba, sasa labda hapa pana mtazamo tofauti hapana! Tutaangalia mitazamo ya hoja *scientifically* na kuepusha usalama wa shirika lililopo na kazi zilizo mbele ya shirika ili uhai na usalama uendelee kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. (*Makofî*)

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Azimio hili la kutaka kuongeza muda kwa *CHC*.

Mheshimiwa Spika, pengine nianze na kumnuuu Waziri alipokuwa akiwasilisha Azimio hili hapa Bungeni. Nitamnukuu kwenye aya ya mwisho ya Azimio: “Kwa hiyo basi, kwa madhumuni haya maalum, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Mkutano wa Nne, kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1), Sheria ya Benki inaazimia kuongeza muda wa uhai wa mpito wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma, kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tahere 1 Julai, 2011 hadi tarehe 30 Juni, mwaka 2014, ili kutoa fursa kwa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika kukamilisha taratibu za kiutendaji na kisheria za kuhamisha kazi zitakazokuwa zimebaki na kuzipeleka kwenye Ofisi ya Msajili wa Hazina.”

Mheshimiwa Spika, mjadala ndani ya Azimio hili siyo tu kwamba ni kuongeza muda kwa *CHC* ndiyo iwe *concern* ya mjadala, ni pamoja na Wabunge kuwa na angalizo katika michango yao ya mawazo, ni kwa sababu gani na ni kwa namna gani Wizara kwa maana ya Serikali, inataku kuhamisha kazi za *CHC* kwenda *TR*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukiwa na *limit* kwamba, tunajadili tu muda wa *CHC*, tutakuwa hatujadili Azimio lililoletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, suala hapa siyo muda wa *CHC* kufanya kazi zake, suala hapa ni kuitazama *CHC* katika majukumu yake, ni kutazama pia ni kwa sababu gani Serikali sasa imeona ihamishe shughuli za *CHC* ziende *TR*. Lazima Wabunge tuwe na maangalizo kwa ajili ya kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge wa CCM na nipo kwenye Kamati hii ya *POAC*, lakini katika jambo hili ni lazima niwe na uchungu na maslahi na mali za Watanzania.

Mimi niliyepata bahati ya kukutana na mashirika haya, kuwahoji na kuangalia hesabu zao na ufanisi wa mashirika haya, inanipa picha ya kuona kwamba, mashirika ya umeme yanatafunwa na wajanja wachache katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, leo hii hainiingii akilini, mkubwa kabisa wa *TR* ambaye leo ndiyo tunataka tuchukue kazi za *CHC* tumpelekee, hajui ana mashirika mangapi ya umma anayoyasimamia na hana hata *certificate* za hisa ambazo anazishikilia kwa niaba ya Watanzania!

Mheshimiwa Spika, nchi hii imefika pabaya, sasa hivi ubinafsishaji katika nchi hii imekuwa ni sehemu ya unyonyaji wa walipa kodi. Hapo zamani tulikuwa na Shirika linaitwa SCOPO, baadaye tukaja na LART, SIMU 2000 LTD, baadaye ATHC, baadaye PSRC, majukumu haya yote yakaondolewa tena tukawa na chombo kingine cha *CHC*.

Mheshimiwa Spika, unapoodia mahali ambapo kila shirika likianzishwa baada ya muda mfupi linafungwa, linanyang'anya majukumu yake, leo tumekwenda *CHC* hawajamaliza kazi, tunawafunga, tunawanyang'anya majukumu yao, hapo ndipo ulipo wizi wa mali ya umma katika nchi hii; lazima tufike mahali tukatae. Tumekuwa tukilaumu makampuni ya simu kwamba ni kwa nini kwa muda mfupi wanabadilisha majina, tumekuwa tukisema ni kwa sababu wanakwepa kodi na ni kwa sababu wanataka kuinyonya nchi hii. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kutoa kazi za *CHC* katika muda huu ambao sasa Kamati yetu iliwashauri katika eneo la *monitoring and evaluation*, watuletee tathmini ni kwa kiasi gani mashirika yaliyobinafsishwa ni mangapi yalipouzwa yanaendelea kufanya kazi zile walizoyanunulia na ni wangapi ambao bado wanadaiwa. Leo kabla hawajakamilisha hiyo kazi ambayo ni kubwa na nyingi, tunasema kwamba, wapo kwenye mpito na katika mpito huu kazi zao ziende kwa *TR*; hii ni kupotosha *institutional memory*, kwa sababu kuna wizi unataka kufanyika ndani ya mashirika haya.

Mheshimiwa Spika, *CHC* kama ambavyo Waziri ameleta Azimio hapa, ametusomea majukumu mengi sana ambayo katika hali ya kawaida, hawawezi wakayafanya ndani ya miaka mitatu; ni majukumu mengi na ni nyeti, ambayo bado wanawahitaji *CHC* waendelee kuyafanyia kazi kwa muda mrefu na ndiyo sababu tulishauri katika Bunge hili kwamba, aidha, wapewe *perpetual existence* au wapewe miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Mahesabu ya Mashirika ya Umma, kutokana na jinsi tulivyokuwa tunawahoji hawa, tuliona kwamba ni vyema wanawenza wakawa wamesogea mahali ili kukamilisha kazi hizi. Tarehe 6 Aprili hata Waziri amekiri hapa kwamba, alikubaliana na hoja na lile lilipitishwa kama Azimio lakini tumefika mahali Maazimio ya Bunge yanapuuzwa na Serikali, yanadharauliwa na Serikali. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Wananchi ambao tunawawakilisha, sisi ndiyo tunaisimamia Serikali na kuisimamia Serikali kwa njia ya Maazimio. Sasa inapofikia Maazimio ya Wananchi yanapuuzwa; kwa kweli hatuwatendei haki Wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye tafsiri ya Mashirika ya Umma, sasa hivi kumekuwa na tafsiri mbaya; inaonekana haya yanaitwa Mashirika ya Serikali, haya ni Mashirika ya Umma. Mashirika ya Umma ni lazima tuwe na chombo ambacho kinashikilia hisa za Watanzania. *CHC* leo ninaamini tukiwaongezea muda, tena siyo muda wa kuwatia hofu, eti tunaandika hapa kwamba, kipindi cha mpito, huu ni muda wa kuwatia hofu, nina uhakika hata yale majukumu ambayo Waziri ameyasema hapa hawatayatekeleza, kwa sababu wapo kwenye mpito na mpito maana yake ni hofu.

Mheshimiwa Spika, kuna mashirika ambayo yanazalisha faida sana kama Sigara na makampuni mengine kama NMB. Kama hisa za Watanzania ambazo ziko chini ya asilimia 50 nazo tumewanyima fursa Wabunge kuititia Kamati za Bunge kwenda

kuchungulia kuna nini katika utendaji wa mashirika haya; mimi huwa najiuliza, kwa nini tunazuiwa tusijue kinachoendelea huko kuna nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata kama ni shilingi moja ya mlipa kodi ina thamani kubwa, Wananchi wanataka kujuu shilingi yao moja inafanya nini, imezalisha nini na tunapata nini kwa ajili ya huduma za Watanzania. Wakati umefika sasa katika Azimio hili, ninaishauri Serikali ibadilike na itukubalie Wabunge juu ya mambo mawili: Jambo la kwanza, kuondoa hofu juu ya Shirika hili la *CHC*, tuwape muda wa kutosha na ikibidi wawajengee uwezo ili *CHC* iwe ni ya kudumu, ifanye kazi sawa na mashirika mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, madeni yetu yatapotea bure, maana ninaona sasa ni kama kuna watu wanajiandaa namna gani madeni haya yasilipike. Kwa hiyo, hilo ni la kwanza la kuwaondoa hofu na kuwapa muda wa kutosha, wawepo wafanye kazi ya Mashirika haya.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninahoji katika utaratibu huu ambaa Serikali ina sababu zake, kwa nini *TR* wasichukue kazi za *PPF* na *NSSF*, lakini wanachukua kazi za *CHC*; kuna nini huko *CHC*?

Mheshimiwa Spika, ninawaomba Wabunge wenzangu, wale ambaa tumepata fursa ya kuchungulia kwenye Mashirika haya kuna nini, ninaomba mtuamini huko ndiko kuliko na uozo, kama mashirika yenyewe tu haya ambayo tunayasimamia ambayo yapo juu ya asilimia hamsini yana wizi, yana ubadhirifu; je, yale ambayo wanajua kwamba Wabunge hawaji kuchungulia yana hali gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge wenzangu kwa vile ni lazima nimtzame Spika, wakati ninazungumza ningeweza kugeuka kulia na kushoto kuwaombeni nyote tuungane juu ya jambo hili kwamba, *CHC* wapewe muda wa kutosha ili waweze kufanya kazi hizi, wanusuru Mashirika haya ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kuonesha juu ya athari ya kupeleka kazi za *CHC* kwa *TR*; ni hii *General Tyre* ambayo leo hii tunahaingaika kuchunguza dola milioni kumi za kimarekani walizochokua *NSSF* walizipeleka wapi ni kutokana na udhaifu wa *TR*. Sheria ya Mashirika ya Umma (*Public Corporations Act*), kifungu cha 40 kinasema kwamba, Shirika lolote ambalo lipo katika hatua za kutaka kuuzwa, lakini wanataka kufanya *restructuring of any investment*, hawawezi wakafanya hivyo bila kupata *sanction* ya *TR*. *General Tyre* walifanya *restructuring* hawakuwasiliana na *TR*. Tukamwuuliza *TR* kwa nini huku-supervise hii *restructuring* ili wapate *sanction* kutoka kwako; akasema ninyi kwani hamjui haya ndiyo mambo ya hapa Tanzania!

Mheshimiwa Spika, leo huko ndiko tunataka tuhamishe kazi za *CHC* ziende, zinakwenda katika eneo ambalo liko *loose* kiasi hiki! Watanzania tutawafikisha wapi?

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita msemaji wa mwisho, Mheshimiwa Felister Bura, kama hayupo nitamwita Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaomba idhihirike ndani ya Bunge hili kwamba, hakuna Mbunge yejote anayekataa *CHC* isiongezewe muda. Kwa hiyo, wasiwasi wako kwamba, tarehe 30 unamalizika Wabunge wote tunakubali kwamba, muda uongezwe. Tatizo lililopo na ni la msingi kabisa ni kwamba, bado hakuna *yardstick* katika mambo yetu.

Mheshimiwa Spika, jana wakati tunapitisha *Finance Bill* lilizuka suala zima la misamaha ya kodi; ukilitazama suala lenyewe zima ni kwamba, hakuna *yardstick* ya lile tunaloliamua. Kwa mfano, unaposema *EPZ* kiwanda cha samaki kipewe miaka kumi na kiwanda kinachozalisha chuma kipewe miaka kumi; je, kuna uwiano wowote? Mmoja amekopa dola laki moja na mwingine amekopa dola milioni kumi. Kwa hiyo, tatizo la msingi hapa hakuna *yardstick* na ndiyo tatizo hilo hilo tulilonalo kwa Msajili wa Hazina, ndiyo hilo hilo tunalo kwa *CHC* tunayoipitisha hivi sasa. Kwamba, hawa *CHC* tulipowapa muda kipindi kile hatukupima uwezo na utendaji wa kazi yao ilipo na ndiyo maana Serikali imekuwa inarudi Bungeni kila wakati kuongeza muda na hili ni tatizo la msingi.

Mhehsimiwa Spika, hivyo hivyo kwa Msajili, wewe ni shahidi, ukiwa Naibu Spika, *share* za *Williamson Diamond* ambazo ziliikuwa asilimia hamsini, za Serikali asilimia 25 ziliuzwa kwa dola 138. Msajili wa Hazina hana habari! Tukahoji katika Kamati ya *PAC* na tukataka Wizara ya Fedha i-strengthen Msajili ili iweze kudhibiti mali za Serikali. Hili tulishalisema miaka kumi iliyopita, bado halijafanyika.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ninaloomba, ninaiomba sana Serikali ikubali kwamba, kuna haja ya msingi kwanza ya kuwa na *yardstick* ya kazi hizi zitakazofanywa. Waziri umeziorodhesha tu hizi kazi, katika hali ya nadharia, haiwezekani miaka mitatu ikamalizika hata kidogo, *there is no way!*

Mheshimiwa Spika, kesi zilizopo mahakamani, *assets* ambazo bado zimesimamishwa bado hazijarudishwa wala hazijatumika kufanya tathmini yake na kurudi kutoa taarifa miaka mitatu ni ndoto. Baya zaidi mtu unapompa muda wa miaka mitatu kwa kazi nzito kama hii, maana yake atafanya vitu viwili; ama ataharakisha aondoke au atakuwa *slow* aache kazi ibaki *volume* kubwa ili hata utakapoishamisha upande wa pili isiweze kufanyika. Hili tulilizungumza ndani ya Kamati ya Fedha tukakubaliana kabisa kwamba, tukisha *specify* muda ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, tukamwambia Waziri sisi tunakubali kwanza wapewe huo muda, lakini huu muda uweze kurudi wakati wowote Bungeni kusema muda huu umetosha sasa tunaomba kuhamisha, ndivyo tulivyokubaliana. Kwa kuelewa *volume of*

*work* iliyopo katika *CHC* hivi sasa kwamba, haiwezi kabisa kumalizika katika kipindi cha miaka mitatu, wameshindwa miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, tulikubaliana kistaarabu, mimi nikafikiri hilo limekwisha, lakini leo tukimwuliza Waziri baada ya miaka kumi na nia ya Serikali kukabidhi *CHC* kwa Msajili atupe *yardstick* ya Msajili na kazi zilizofanywa na Msajili ya matayarisho kwa nini hakuyaleta? Kwamba, Msajili imetayarishwa kwa hiki na hiki ili waweze *ku-take over any time from now*, hamna! Tumeuliza kwenye Kamati, hapa ndani ya Bunge hayajaja, kwa hiyo, tunarudi nyuma.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana, ninakuhakikishia Wabunge wote watakubali muda uongezwe. Ningombaa Serikali ili-frame hili Azimio, iseme kwamba, tunaongeza huo muda lakini tutarudi tena Bungeni pale kazi itakapomalizika, mkimaliza mwaka mmoja sisi hatuna tatizo, mkimaliza miaka miwili hatuna tatizo, mkimaliza miaka mitatu hatuna tatizo, lakini mkishindwa katika kipindi hicho msije tena hapa Bungeni kutuomba. Matokeo yake itamalizika miaka mitatu mmeshindwa kazi mtarudi tena hapa na maswali yatakuwa ni haya haya.

Mheshimiwa Spika, lakini moja baya zaidi ni kwamba, wale Watendaji waliopo kwenye Shirika watakuwa hawana hakika juu ya maisha yao, hawatafanya kazi vizuri, tunawahakikishia kabisa sisi tunajua *bureaucracy* yetu ilivyo.

Mheshimiwa Spika, ninafikiri tuwe *wise enough* kukubaliana na ushauri uliotolewa na Kamati ya Fedha na Uchumi kwamba, hiki kipindi cha miaka mitatu kiondolewe, tuwape muda pale ambapo Serikali imeridhika na Bunge litaridhika kwamba, Msajili sasa anaweza kutunza rasilimali za nchi, irudi tena Bungeni. Kwa kuwa Sheria inakuruhusu Waziri, wala haina haja ya kuja Bungeni, Sheria inaruhusu pale atakapoona kazi imemalizika, ana haki ya kufuta. Sasa kwa nini mnaogopa hilo?

Mheshimiwa Spika, kama miaka miwili imemalizika Waziri unaruhusiwa, kama miaka mitatu imemalizika, sheria inakuruhusu wala huna haja ya kuja Bungeni. *It is empowered to you.* Kwa hiyo, toa hii *blanked* hii nafasi tumalize kazi tuendelee, mimi nina hakika Wabunge wote kwa hilo watakubali. Mimi ninafikiri ushauri wangu huu ni wa kiutuzima.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Bunge letu tunakaribia miaka 50 sasa ya uhuru wetu; tumekua kiasi cha kutosha, tumekomaa, tumejifunza mengi, ninaomba tuwe na uvumilivu na tuwe na lugha ambayo itatusaidia Watanzania kujifunza ndani ya Bunge. Nawaomba sana, kwa umri wangu niliokaa ndani ya Bunge ninasema ninaomba sana tunahitaji kuwafunza vijana wetu, Watanzania wetu na wengine wanaotuangalia kwamba, tunahitaji kutoka miaka 50 tupige hatua nyingine ya kuzidi kuwasomesha wenzetu kwamba, Tanzania ni nchi ya kistaarabu, ni nchi ya kuvumiliana, ni nchi ya kuthaminiana na ni nchi ya watu wenye umoja. (*Makofi*)

Mwisho kabisa, bahati nzuri mimi ninafahamu utaratibu huu kutenda kazi za Serikali, ukisoma Katiba hata Baraza la Mawaziri kazi yake ni kumshauri Rais. Rais ana

uwezo wa kuendesha Serikali bila kuwa na Baraza la Mawaziri kwa mujibu wa Katiba. Kwa hiyo, peke yake ndiyo unaweza kumshauri na akakubali ushauri wako. (*Makofi*)

Mimi ninakumbuka siku moja Mawaziri, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu, tulifanyiwa semina na Mwalimu. Mimi nikamwuliza Mwalimu hivi Mwalimu wewe unajiuzulu wakati gani kwa sababu Katiba inasema kazi yetu kukushauri wewe ndiyo mwenye maamuzi. Sasa kwa nini mimi ninakushauri ujiuzulu, usijiuzulu, wewe ndiyo unatakiwa ukubali ushauri wangu. Akasema hivi nitajiuzulu mara ngapi?

Kwa hiyo, lazima *tu-share* hili, kila ukifanya kosa ujiuzulu, mimi nitajiuzulu mara ngapi; maana *nikijiuzulu* maana yake hakuna Serikali. Kwa hiyo, lazima *u-take political responsibility*. Kwa hiyo, kazi yao ni *ku-take political responsibility*. Kazi hasa kubwa na dhamana ya Katiba ni ya Rais mwenyewe. Ndiyo maana tunambana hapa Rais kila wakati kwamba, wewe ndiyo mwenye kirungu cha mwisho, una hati ya kumchukulia hatua. Kwa hiyo, ninafikiri tuelewe hilo kwamba, majukumu ya Kikatiba ya Kiserikali ni ya Rais. Ndiyo mwenye *executive power* na ndiyo Baraza la Mawaziri, kazi yake kumshauri. Inawezekana ushauri wakati mwingine mbaya, wakati mwingine inawezekana mtu wala hakushauri vibaya, lakini *in good faith* bahati mbaya ukawa mbaya. Yote haya yametokea kwa sababu sote ni binadamu, hakuna aliye mkamilifu.

Ninachoomba mimi siamini kabisa kama kuna watu wana nia mbaya, Watanzania wote tuna nia nzuri tu. Makosa yanatokea, ninarudia usemi wangu wa juzi; kufanya kosa siyo kosa ni kosa kurudia kosa. Mashirika ya Umma umekuwa mtaji wa watu. Watu wametajirika na mashirika haya. Hayakusimamiwa vizuri, tunachoomba sasa Bunge lijitalihidi na Serikali ijitalihidi mashirika haya yasimamiwe vizuri.

Kwa utaratibu wa kusimamiwa vizuri ni kuwa *yardstick*, unatakiwa ufanye nini, umalize nini ili tupate *track record* ya kuweza kusema huyu amefanya vibaya, huyu amefanya vizuri. Hili linakosekana. Kwa hiyo, ninaomba tena Waheshimiwa Wabunge, tukubaliane na Azimio lakini Serikali ikubali kabisa, kwa sababu sheria inampa madaraka Waziri wakati wowote kulifuta *CHC*, Shelia tuliyopitisha hapa ndani ya Bunge, azingatie haya ambayo tunayasema.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilisema huyu ni msemajji wetu wa mwisho sasa nimwite mtoa hoja. Mtoa hoja anasimama hapa siyo huko.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninashukuru kwa michango mingi na mizuri iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge na hasa huku mwishoni mwishoni. Nitajibu kwa kifupi sana. Kwanza, niseme Shirika la *CHC* liliundwa kwa kazi maalum ya miaka mitano. Shelia inasema wazi, baada ya miaka mitano shirika lile lilikuwa linatakiwa limalize uhai wake. Serikali yenyewe ndiyo imeendelea kuliombea muda. Mwaka 2007 Bunge Tukufu halikukubali kuongeza miaka mitano, liliongeza miaka mitatu na miezi tisa na ni kwa sababu tu kwamba, wakati ule

*PSRC* ilikuwa imemaliza muda wake, majukumu yake yalikuwa yanahamishiwa kwenye *CHC*.

Kwa hiyo, ili kukabili pia majukumu ya *PSRC* ndiyo Bunge likakubali kwamba, tuongeze miaka mitatu na miezi tisa. Waheshimiwa Wabunge, waliokuwepo wakati huo, watakumbuka jinsi *debate* ilivyokuwa kama ya leo hii wakitaka *PSRC* isife. Serikali tukasema kazi yake imekwisha na *PSRC* likaruhusiwa kufa. *CHC* ikaongezewa miaka mitatu na miezi tisa; Shughuli hazijakwisha Serikali inasema tupeni muda wa miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, ninakubali turuhusiwe tupewe miaka mitatu. Pale tuliposema kwamba, kuna Msajili wa Hazina ni baada ya miaka mitatu kwamba, ndani ya miaka hii mitatu Serikali itafanya haya yote yaliyosemwa ndani ya Bunge hili, yaliyosemwa na Kamati ya Fedha, kutathmini hata kwenye Azimio langu nimesema, Msajili wa Hazina atakuwa anatathmini mara kwa mara na kutoa taarifa kwenye Kamati ya Fedha ya Bunge ili kuona kama ana uwezo na amefikia wapi.

Sasa ndani ya miaka hii mitatu, Serikali itafanya tathmini na kwa jinsi ilivyojitokeza leo, hiyo tathmini ambayo tulikuwa tuienze wakati Fulani, nitaiharakisha ili *CHC* yenyewe ifanyiwe tathmini kwanza, kuona kama kuna ya kuiongezea muda, lakini pia kazi zingine. Kusema kwamba, tukafanye kazi ambazo ni za watu wengine na ili tuipe *CHC*, hilo kidogo tusubiri mpaka tathmini hii itakapokuwa imefanyika tutakuja tena Bungeni na hapo ndiyo tutaona kama kuna haja ya kufuta sheria nyingine ambayo inampa madaraka mtu mwngine ili tumpe kazi hiyo *CHC*.

Mheshimiwa Spika, ninasema kwa niaba ya Serikali, sina haja ya kusema kwamba nijibu kila hoja. Mambo mengine umeshatoa maagizo, ninadhani yanatekelezwa kwa jinsi ambavyo umeyatoa. Mimi kwa niaba ya Serikali, tunaomba Azimio hili lipite, Shirika hili lipatiwe miaka mitatu. (*Makofî*)

Baada ya Azimio hili kupita, watakapoanza mwezi Julai, Serikali itafanya tathmini ya *CHC* na kazi zake na kwanza *performance* yao, *efficiency* yao, sidhani kama inaweza ikafika miaka mitatu kabla hatujaja Bungeni kuleta taarifa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe hoja kwamba, Serikali inaomba Shirika lipewe miaka mitatu lakini pia ninatamka kwa niaba ya Serikali kwamba, Shirika litafanyiwa tathmini ili kuona jinsi gani ya kushughulikia Shirika hili ndani ya miaka mitatu au baada ya miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**SPIKA:** Sawa hoja imeungwa mkono Azimio linasomeka namna gani; Mheshimiwa Waziri unawasilisha Azimio; si una Azimio lako, sasa hapo ndipo utakapoona kama maneno yale ya mwisho hujayaondoa, Azimio lako litakoma. (*Makofii*)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ile *paragraph* ya mwisho isomeke hivi: “Kwa hiyo basi, madhumni haya maalum ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Nne na kwa mujibu wa kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Benki ninaazimia kuongeza muda wa uhai wa mpito kwa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe 1 Julai mwaka 2011 hadi Juni 30, mwaka 2014 ili kutoa fursa kwa Shirika Hodhi la Mali la Mashirika ya Umma, kukamilisha taratibu za kiutendaji na kisheria. Serikali itafanya tathmini ya kazi za Shirika hili na itatoa taarifa Bungeni ya nini kifanyike baada ya hapo.”

**SPIKA:** Sasa soma Azimio lote kama ulivyowasilisha, ndiyo shughuli yenewe.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, Azimio lote linasomeka hivi:

KWA KUWA Sheria ya Benki ya Taifa ya Biashara Upangaji na Umlilikishaji wa Mali na Madeni, yaani *The National Bank of Commerce (Re-organisation and Vesting of Liabilities) Act*, Sura ya 404 ilipitishwa na Bunge kwa ajili ya kuanzisha Shirika Hodhi la Mali la Mashirika ya Umma, yaani *The Consolidated Holding Corporation*, ambalo zamani lilijulikana kama Shirika Hodhi la Benki ya Taifa ya Biashara, yaani *NBC Holding Corporation*;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa Sheria hii Shirika Hodhi la Mali la Mashirika ya Umma lilipewa jukumu la kukusanya madeni na kusimamia uuzaaji wa mali zote za iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara ambazo hazikugawanya kwa Benki ya Taifa ya Biashara (*NBC 1997 Limited*) na NMB pamoja na kusimamia kesi zote za madai na za jinai dhidi ya iliyokuwa NBC;

NA KWA KUWA kutokana na kutojamiliika kwa majukumu yake mwaka 2002 Shirika Hodhi la Mali ya Mashirika ya Umma liliongezewa muda wa miaka mingine mitano, yaani kuanzia mwaka 2002 hadi mwaka 2007 kupitia Azimio la Bunge Namba 20 la Mwaka 2002;

NA KWA KUWA kupitia Sheria ya Benki ya Taifa ya Biashara, Upangaji na Umlilikishaji wa Mali na Madeni, ilifanyiwamarekebisho kupitia Sheria Namba Kumi ya Mwaka 2007 na Sheria Namba 26 ya Mwaka 2007 ili kuliogezea Shirika Hodhi la Mali ya Mashirika ya Umma muda wa kipindi kingine cha uhai kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2007 hadi tarehe 30 Juni, 2011 na vilevile kuongezewa majukumu kufuatia Mashirika ya *LART, Air Tanzania Holding Corporation, SIMU 2000* na *PSRC*, kufikia kikomo kisheria;

NA KWA KUWA muda wa uhai wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma za *Consolidated Holding Corporation* kwa mujibu wa sheria unamalizika tarehe

30 Juni, 2011 ambapo majukumu muhimu yaliyokabidhiwa chombo hiki yatakuwa hayajamalizika;

NA KWA KUWA marekebisho yaliyofanywa na Sheria Namba Kumi ya Mwaka 2007 yanalipa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mamlaka kwa kupitia Azimio la Bunge, kuongeza muda kwa uhai wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika za Umma kabla ya kufikiwa ukomo wake tarehe 30 Juni, 2011;

KWA HIYO BASI kutokana kwa madhumuni haya maalum, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Nne kwa mujibu wa kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Benki, linaazimia kuongeza muda wa uhai wa mpito wa Shirika Hodhi la Mali ya Mashirika ya Umma kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe 1 Julai, 2011 hadi tarehe 30 Juni, 2014 ili kutoa fursa kwa Shirika Hodhi la Mali ya Mashirika ya Umma kukamilisha taratibu za kiutendaji na kisheria.

Mheshimiwa Spika, ninaomba maneno haya mengine yaliyobakia yafutwe na yaingizwe yale ambayo nilikuwa nimeyasema mwanzo kufuatana na *Hansard* ilivyonukuu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, unasoma hayo maneno uliyosema ndiyo tunakamilisha hili.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninasema ya kiutendaji kisheria tunaweka *full stop* pale. Halafu tunaongeza ndani ya muda huo, Serikali itafanya tathimini ya kazi za *CHC* ili kubaini kama liongezewe tena muda au kufanyiwa uamuzi mwingine.

**SPIKA:** Sasa omba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninapenda nimpongeze sana Waziri wa Fedha na Serikali, kwa kusikia maoni ya Waheshimiwa Wabunge na kufanya haya marekebisho ambayo yanatakiwa. Nilikuwa ninaomba kwamba, kwa mujibu wa kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Benki, kinaamizia kuongeza muda wa uhai wa Shirika Hodhi, yale maneno wa uhai wa mpito yanakuwa hayana maana tena kufuatia marekebisho ambayo yamekuja. Kwa hiyo, isomeke kwamba, ninaazimia kuongeza muda wa uhai wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma kwa kipindi cha miaka mitatu, kuanzia tarehe hiyo mpaka hiyo, pale ambapo Mheshimiwa Waziri wa Fedha amezungumza. Kwa hiyo, yale maneno mawili tu “wa mpito” yanapaswa yaondoke. Ninashukuru.

**SPIKA:** Ninadhani Serikali hakuna tatizo hapo. Kwa hiyo, nitawahoji muiamue hoja iliyotolewa.

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kazi kwenu, hayo mnayoyasema myatekeleze kwa vitendo. Tulichokuwa tunakataa kwamba, hatuwezi kuanzisha suala kubwa katika muda huu mfupi ambapo maandalizi yake hayakutosha. Kwa hiyo, ninyi wenyewe fanyeni kazi zinazostahili halafu baadaye tuweze kuona mfumo mzuri wa kuweza kuendesha mashirika yetu na mambo mengine yaliyobakia.

Waheshimiwa Wabunge, asubuhi ninaona tuliwahi sana, kwa hiyo, wanaotoa taarifa ya wageni tulionao walikuwa hawajajiandaa. Kwa hiyo, nina wanafunzi 50 na walimu 10 wa Shule ya Msingi Bunge kutoka Dar es Salaam; hawa ni majirani zetu wa Dar es Salaam; wasimame na walimu wao walipo. Ahsanteni sana Walimu. (*Makofi*)

Tuna wanafunzi 32 na walimu 30 wa Shule ya Sekondari ya Kitwiru Iringa; wako wapi na walimu wao? Ninaona wao watakuwa wamekosa nafasi humu ndani. Kuna wanafunzi 26 na walimu 6 wa Shule ya Msingi Sanduli iliyopo Bahi, Dodoma; wako wapi? Karibuni sana.

Kuna wanafunzi 75 na walimu 5 wa Shule ya Msingi Chazungwa kutoka Wilaya ya Mpwapwa; wako wapi na wap? Ahsante, karibuni sana walimu.

Halafu nina wageni kwenye nafasi ya Spika pale; yupo Bibi Anna Ernestina Mkuchika, Mke wa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI. Ahsante.

Yupo pia Meja Jenerali Mstaafu Said Kalembo, Mkuu wa Mkoa wa Tanga na mke wake. Kuna wengine hawakuleta majina; ninaomba niwakaribishe tu wote. Ahsanteni sana.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma huyu ni mwenyeji wetu, Mheshimiwa Dkt. James Msekela. Ahsante sana, karibu sana.

Waheshimiwa Wabunge, pia Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama, anaomba niwaambie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, saa saba watakuwa na kikao, Chumba Namba 219.

Baada ya kusema hayo, ninaomba nimwite mwenye Hati za Kuwasilisha Mezani; kuna Hati moja walikuwa wameiacha. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha ya Uchumi; Makamu wake.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya

99(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 37 - Uwezeshaji na Uwekezaji kwa Mwaka 2010/2011 na Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kwamba tumetumia muda mwingi tuliotaka Waziri Mkuu aanze kusoma hotuba yake, lakini naomba mturuhusu kwamba tutumie Kanuni ya 28(2) kusudi Waziri Mkuu aweze kuendelea mpaka amalize hotuba yake.

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa Mwaka 2011/2012**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, iliyochambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2010/2011 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2011/2012. Vilevile, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Taasisi zilizo chini yake pamoja na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, hili ni Bunge la kwanza la kujadili Bajeti ya Serikali baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010. Nitumie fursa hii kuwashukuru Watanzania kwa kuendelea kukichagua Chama cha Mapinduzi na hivyo kukiwezesha kushinda Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010 na kukipatia tena ridhaa ya kuunda Serikali na kuongoza nchi. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuiongoza Serikali ya Awamu ya Nne. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa na Rais kushika nyadhifa hizo muhimu. Nawahakikishia wananchi wote kwamba Serikali ya CCM ni sikivu na itawatumikia kwa nguvu na ari zaidi bila kujali itikadi zao za kisiasa.

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Job Yustino Ndugai kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kuwa Wawakilishi wa wananchi katika Bunge hili. Wote nawapa hongera sana. Jukumu lililo mbele yetu sote ni kuwatumikia wananchi walio tuchagua ili kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tangu tulipohitimisha Mkutano wa Bajeti wa Bunge hili mwaka jana, nchi yetu imekumbwa na majanga mbalimbali yaliyosababisha vifo na uharibifu wa mali. Nitumie fursa hii kutoa pole kwa wote waliofiwa na ndugu, jamaa na marafiki.

Mheshimiwa Spika, natoa pole kwako wewe kwa kufiwa na mama yako mzazi, Marehemu Emilia Tulakela Samnyuha, Mungu azilaze Roho za Marehemu mahali Pema Peponi. Amina.

Kwa wale walioumia na bado wanajiuguza, namwomba Mwenyezi Mungu awasaidie kupona haraka na kurejea katika shughuli za ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa takriban siku tano Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kujadili taarifa kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa katika Mwaka 2010 na Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012. Napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkullo - Waziri wa Fedha kwa hotuba nzuri na ufanuzi wa hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira kwa kuwasilisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Vilevile, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kujadili kwa kina hotuba hizo na hatimaye kupitisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012. Serikali itahakikisha kwamba ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge unazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge lako Tukufu kwa ushauri walioutoa wakati wa kupitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara za Serikali zinazojitegemea na mamlaka za Serikali za Mitaa. Kipekee, nitumie nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala inayoongozwa na Mheshimiwa Pindi Hazara Chana. Naishukuru pia Kamati ya Fedha na Uchumi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omar Kigoda. Kamati hizi zimetoa mchango mkubwa wakati wa uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Bunge. Maoni na ushauri wao umesaidia sana kuboresha makadirio hayo.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali ambayo imepitishwa na Bunge lako Tukufu ndiyo inatuanzishia mchakato wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010. Katika Ilani hiyo, zipo ahadi mbalimbali ambazo Serikali ya Chama cha Mapinduzi itazitekeleza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Bajeti hii imezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Malengo ya Maendeleo ya Milenia, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini na Maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akizindua Bunge la Kumi tarehe 18 Novemba, 2010. Tutaimarisha usimamizi ili tuweze kutekeleza mipango na ahadi hizo kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu tunaadhimisha miaka 50 ya Uhuru tulioupata tarehe 9 Desemba, 1961. Watanzania wote tuna mengi ya kujivunia licha ya changamoto zilizopo. Sote tumeshuhudia kuimarika kwa umoja, mshikamano, amani na utulivu. Aidha, Serikali imeendeleza na kupanua huduma mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Demokrasia na Utawala Bora pia vimeshamiri. Natoa wito kwa Watanzania wote kuenzi Uhuru wetu kwa kufanya kazi kwa bidii ili kudumisha mafanikio yaliyopatikana na nchi yetu izidi kusonge mbele.

Mheshimiwa Spika, hali ya kisiasa nchini ni ya kuridhisha. Vyama vya Siasa na wananchi wanaendelea kushiriki kwa uhuru katika shughuli za kisiasa. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imeendelea kukuza demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa nchini. Msajili alipokea maombi ya usajili wa muda wa Chama cha Kijamii – CCK na *Movement for Democracy and Economic Change Movement – MDEC*. Aidha, Chama cha Jamii – CCJ na *Peoples Democratic Movement – PAM* vilifutwa baada ya kushindwa kutimiza masharti ya usajili wa kudumu. Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilisimamia utekelezaji wa Sheria Mpya ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010 na kushughulikia malalamiko yaliyowasilishwa na Wagombea.

Mheshimiwa Spika, ili kudumisha demokrasia nchini, Serikali ilianzisha Baraza la Vyama vya Siasa baada ya kufanyika Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 7 ya mwaka 2009. Baraza hilo linaundwa na Vyama vyote vya Siasa vyenye Usajili wa Kudumu na lilizinduliwa rasmi mwezi Mei, 2010. Majukumu ya Baraza ni pamoja na kuishauri Serikali kuhusu mambo ya kitaifa yanayohusu hali ya kisiasa nchini na utekelezaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa.

Vilevile, Baraza lina jukumu la kuishauri kuhusu uendeshwaji na utatuzi wa migogoro itokanayo na Vyama vya Siasa. Natoa wito kwa Vyama vya Siasa nchini kukiona chombo hiki kuwa ni kiungo muhimu kati ya Serikali na Vyama vyote vya Siasa nchini katika kujenga Taifa letu. Aidha, kupitia Baraza hilo, Serikali itaweza kupata maoni ya Vyama na Wananchi kuhusu zoezi muhimu la kuandaa Katiba mpya ya nchi. Serikali kwa upande wake itajitahidi kuliwezesha Baraza kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa itaendelea kupokea na kuchambua marejesho ya gharama za uchaguzi kutoka Vyama vya Siasa. Aidha, itashughulikia maombi ya usajili wa vyama, kukagua uhai wa vyama, kutoa elimu kwa umma, kuhakikisha vyama vinatekeleza na kuheshimu Sheria ya Vyama vya Siasa na kuimarisha Ofisi za Kanda.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilianda na kusimamia Uchaguzi Mkuu wa Urais, Wabunge na Madiwani nchini kwa mafanikio makubwa. Uchaguzi ulihusisha Majimbo 239, Kata 3,335 na Vituo vya Kupigia Kura 53,039. Jumla ya watu 20,137,303 walijiandikisha kupiga kura, lakini waliojiteze walikuwa 8,626,303 sawa na asilimia 43 ya wapiga kura wote. Matokeo ya Uchaguzi ya Urais yalionesha kwamba CCM ilishinda kwa asilimia 61.17. Hivyo, Tume

ya Taifa ya Uchaguzi ilimtangaza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete wa CCM kuwa mshindi wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Matokeo ya Vyama vingine ni kama ifuatavyo: CHADEMA asilimia 26.34; *CUF* asilimia 8.06; *APPT* - Maendeleo asilimia 1.12; NCCR - Mageuzi asilimia 0.31; *TLP* asilimia 0.20; na *UPDP* asilimia 0.15. Kura zilizoharibika ni asilimia 2.65.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uchaguzi wa Wabunge wa Majimbo: CCM ilipata viti 186, *CUF* viti 24, CHADEMA viti 23, NCCR Mageuzi viti vinne na *TLP* na *UDP* kiti kimoja kimoja. Tume pia ilitangaza majina 102 ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum. Kati ya viti hivyo, CCM ilipata viti 67, CHADEMA viti 25 na *CUF* viti 10. Matokeo ya uchaguzi kwa Madiwani yalikuwa kama ifuatavyo:- CCM viti 2,803; CHADEMA viti 326, *CUF* viti 126, NCCR-Mageuzi viti 28, *UDP* viti 28, *TLP* viti 20, *APPT*- Maendeleo viti vitatu na *DP* kiti kimoja. Kwa upande wa Madiwani wa Viti Maalum, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitangaza jumla ya Madiwani 1,184 kwa mchanganuo ufuatao: CCM viti 972, CHADEMA viti 127, *CUF* viti 52, NCCR - Mageuzi viti 11, *TLP* viti 10, *UDP* viti 10, *DP* kiti kimoja na *APPT* - Maendeleo kiti kimoja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wananchi wote kwa kujitokeza kupiga kura kwa amani na utulivu. Vilevile, naipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na wananchi kwa kukubaliana kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa baada ya maridhiano baina ya Vyama vya CCM na *CUF*. Makubaliano hayo yaliwezesha kufanyika uchaguzi wa amani na utulivu Zanzibar. Hatua hii imethibitisha ukomavu wetu wa kisiasa na uwezo tulionao wa kutatua mambo yetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, tarehe 10 Juni, 2011, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilimkabidhi Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Taarifa ya Uchaguzi Mkuu yamwaka 2010. Katika mwaka 2011/2012, Tume itaendelea kufanya utafiti wa kina kubaini changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 ili kuzifanya kazi zisijitokeze tena katika chaguzi zijazo. Aidha, itaanza maandalizi ya kuboresha daftari la kudumu la Wapigakura.

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu umetimiza miaka 47 yenye maendeleo katika maeneo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Maendeleo haya yananufaisha wananchi kwa kuwapa fursa za kuishi kwa amani na kufanya shughuli zao katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vikao vya Makatibu Wakuu na Mawaziri wa Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar vilifanyika ili kujadili masuala mbalimbali ya Muungano. Katika mwaka 2011/2012, Serikali itaendelea kuratibu Vikao vya Kamati ya pamoja ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya kushughulikia masuala ya Muungano. Aidha, Serikali itatoa elimu kwa umma na kuratibu masuala yasiyo ya Muungano kwa kuhakikisha kwamba Sekta, Wizara na Asasi zisizo za Muungano zinakutana mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Bunge imeendelea kutekeleza mpango mkakati wake na Mpango wa Muda wa Kati wa mwaka 2009/2010 hadi 2012/2013. Katika mwaka

2010/2011, huduma muhimu ziliendelea kutolewa kwa Waheshimiwa Wabunge ili waweze kutekeleza majukumu yao. Aidha, Mikutano minne ya Bunge imefanyika, miundombinu ya Ofisi za Bunge imeboreshwa, mafunzo yametolewa kwa Wabunge na Wafanyakazi na Umma umeelimishwa kuhusu shughuli za Bunge. Ofisi ya Bunge itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi na kutoa mafunzo kwa Waheshimiwa Wabunge na Wafanyakazi. Aidha, huduma ya mawasiliano na Maktaba zitaimarishwa pamoja na kuongeza machapisho na majorida.

Mheshimiwa Spika, uchumi wetu umeendelea kuimari. Ukuaji wa Pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 6.0 mwaka 2009 hadi asilimia 7.0 mwaka 2010. Ukuaji huo unatokana na usimamizi mzuri wa Sera za Uchumi, ukuaji katika Sekta ya Mawasiliano na Kilimo. Pamoja na kuimari kwa viashiria vya uchumi jumla, bado tuna changamoto ya kuboresha maisha ya wananchi walio wengi amba wanaishi Vijijini na wanategemea kilimo.

Tayari Serikali imeanza kuchukua hatua za kukabiliana na changamoto hizo kwa kutekeleza programu na mikakati mbalimbali kama vile Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*), azma ya Kilimo Kwanza, mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo na mifugo, uanzishaji wa dirisha la kilimo katika Benki ya Rasilimali (TIB), kuanzisha programu kabambe ya maboresho ya ushirika, azma ya kuanzisha Benki ya Kilimo, uanzishaji wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko na Mpango wa Kuendeleza Kanda za Kilimo (*Agricultural Growth Corridors*) kwa mfano, Mpango wa Kukuza Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (*SAGCOT*).

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo, Serikali inatoa kipaumbele katika Sekta za Nishati, Viwanda, Miundombinu, Maji na Rasilimali Watu ambazo ni muhimu katika kuchochea ukuaji wa Sekta ya Kilimo. Hatua nyingine zilizochukuliwa na zitakazoendelea kuchukuliwa ili kuboresha maisha ya wananchi ni pamoja na:-

(i) Kuimari Sera za Mapato na Matumizi ya Serikali, kudhibiti mfumuko wa bei, kuimari Utawala Bora na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika huduma za jamii;

(ii) Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula ameongezewa uwezo wa kununua na kuhifadhi chakula kutoka kwa wakulima kwa ajili ya kusambaza kwa gharama nafuu katika maeneo yenyе upungufu wa chakula;

(iii) Serikali imesambaza jumla ya tani 24,731 za mahindi katika masoko ya Miji ya Dar es Salaam, Mtwara, Kibaha, Morogoro, Arusha, Moshi, Singida na Dodoma kuititia Wafanyakazi wenye mashine za kukoboa na kusaga mahindi kama hatua mojawapo ya kupunguza makali ya maisha ya wananchi yanayotokana na kupanda kwa bei za vyakula;

(iv) Serikali imepunguza bei ya mahindi yanayouzwa na Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula kutoka Sh. 38,000/= kwa gunia la kilo 100 hadi Sh. 30,000/=;

(v) Serikali imechuka hatua za kudhibiti bei ya sukari isipande sana. Mapema mwezi Februari, 2011 nilikutana na wadau wote wa bidhaa ya Sukari na kukubaliana kupunguza bei ya sukari; na

(vi) *EWURA* inaendelea kudhibiti bei ya mafuta ya dizeli, petroli na mafuta ya kulainisha mitambo isipande sana kwa kuweka bei elekezi ya mafuta nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kuwa jitihada hizo zitaboresha maisha ya wananchi. Hata hivyo, jitihada hizo za Serikali zinatakiwa ziende sambamba na kufanya kazi kwa bidii na kuongeza uzalishaji wenyewe tija. Wafanyabiashara waepuke kuongeza bei za bidhaa na huduma kiholela kwa kisingizio cha hali ngumu ya maisha na kutaka kupata faida kubwa kwa maslahi binafsi. Tuweke uzalendo mbele na kujali maslahi ya wananchi wengi.

Mheshimiwa Spika, Sekta Binafsi ni kichocheo kikubwa cha ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Uwekezaji utaongeza pato la Taifa na ajira kwa Watanzania wengi. Kwa kuzingatia manufaa hayo, Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara na uwekezaji kwa lengo la kuendeleza Sekta Binafsi kama mhimili wa uchumi wa Taifa. Sekta Binafsi ina mchango mkubwa kuwekeza kwenye miradi na huduma mbalimbali. Kwa kuwa kiwango cha uwekaji akiba kwa wananchi ni kidogo kukidhi uwekezaji unaotakiwa kukuza pato la Taifa, Serikali inahimiza uwekezaji kutoka nje ili kufidia pengo la ndani. Aidha, uwekezaji utaongeza mitaji, teknolojia na ajira. Kwa kutambua umuhimu huo, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alimteua Waziri Mwenye Dhamana ya Uwekezaji, Maendeleo ya Sekta Binafsi na Uwezeshaji katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia iliandaa na imeanza kutekeleza Mpango wa Maboresho ya Mazingira Wezeshi ya Uwekezaji na Biashara Nchini. Lengo la Mpango huo ni kuleta mabadiliko ya mfumo wa kisera, kisheria na kitaasisi ili kuondoa urasimu usio wa lazima unaotokana na taratibu za kiutawala. Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa Mpango huo ni pamoja na kurahisishwa kwa taratibu za kusajili biashara, kulipa kodi, kuhamisha milki ya mali za kudumu, usajili wa hati miliki za ardhi na kupunguza vizuizi barabarani.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Ubina baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya mwaka 2010. Kanuni za kutekeleza Sheria hiyo tayari zimeandaliwa na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali Na.165. Utekelezaji wa Sheria hii utasaidia kupunguza mzigo katika Bajeti ya Serikali kutokana na Sekta Binafsi kushirikishwa zaidi katika ujenzi, uendeshaji na usimamizi wa miradi na huduma za umma katika maeneo ambayo Sekta hiyo inaweza kushiriki kwa ufanisi. Aidha, utekelezaji wa Sheria hii ni fursa nzuri ya kukabiliana na changamoto zinazokwamisha uwekezaji hasa katika maeneo ya miundombinu na nishati. Hivyo, Sekta Binafsi ishiriki kikamilifu kuwekeza katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali itaendelea kuratibu na kutekeleza Sera na Sheria ya Ubina baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Aidha,

itaendelea kushirikiana na Sekta Binafsi katika ujenzi wa uchumi wetu na kuboresha mazingira ya uwekezaji. Kwa kuzingatia umuhimu wa Sekta Binafsi katika kukuza uchumi, natoa wito kwa Watanzania kubadilika kifikra na kuiona Sekta Binafsi kwa mtazamo chanya kwamba ni mbia muhimu katika maendeleo ya nchi yetu. Ni jukumu la kila Wizara, Mkoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi kuhakikisha kwamba zinachukua kila hatua kuondoa vikwazo vya uwekezaji hususan urasimu ili kuongeza ajira hapa nchini. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Uwekezaji Tanzania kimeendelea kuhamasisha na kuwawutia wawekezaji wa ndani na nje. Katika mwaka 2010, Kituo kilisajili miradi 509 yenye thamani ya shilingi trilioni 7.6 na fursa za ajira 43,640. Kati ya miradi hiyo, miradi 242 ni ya Watanzania, 160 ni ya wageni na miradi 107 ni ya ubia kati ya Watanzania na Wageni. Aidha, mitaji ya kigeni ya moja kwa moja iliyoingizwa nchini ilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 859.5 mwaka 2010 ikilinganishwa na shilingi bilioni 760 mwaka 2009. Ili kuongeza ufanisi zaidi katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, Serikali itafanya Mapitio ya Sera na Sheria zinazohusika ili huduma zote kwa wawekezaji zitolewe katika kituo kimoja (*One Stop Centre*). Aidha, Serikali inaangalia uwezekano wa kutoa tuzo kwa Wizara, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zitavutia wawekezaji wengi zaidi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Mikoa mingi imeitikia wito wa kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji, ardhi iliyotengwa na Mikoa hiyo kwa ajili ya uwekezaji ni hekta 1,604,825 ambapo jumla hekta 567,308 sawa na asilimia 35 imepimwa. Aidha, kituo cha uwekezaji kimesajili hekta 200,000 SUMA JKT na hekta 267,000 za ardhi ya watu binafsi kwa ajili ya uwekezaji. Hatua za kupima na kutoa hati kwa maeneo hayo zinaendelea. Nahimiza mikoa na mamlaka za Serikali za Mitaa, kuendelea kutenga, kupima na kusajili maeneo zaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuwawezesha wananchi kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kuongeza ajira kupitia sera, mikakati na programu mbalimbali. Kwa mfano, hadi kufikia Mei, 2011, Mfuko wa Uwezesaji Wananchi Kiuchumi ulikuwa umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 5.1 na kuwanufaisha Wajasiriamali 4,437 kupitia *SACCOS* kwa kuanzia na Mikoa ya Lindi, Mtwara, Singida, Manyara na Rukwa. Mchakato wa kuongeza maeneo mengine umeanza katika Mikoa ya Ruvuma, Dodoma, Tanga, Shinyanga na Pwani kwa kulenga maeneo yanayofaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Nazipongeza *SACCOS* kwa kurejesha mikopo yao kama ilivyopangwa ambapo kiwango cha urejeshaji ni asilimia 98. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mfuko wa ‘Mabilioni ya JK’, hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2010, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 47.14 ilikuwa imetolewa kwa kuwanufaisha Wajasiriamali 72,197. Mikopo iliyotolewa ilielekezwa kwa wananchi wa hali ya chini kabisa kama ilivyokusudiwa na Serikali. Hii imewasaidia kuongeza kipato na hivyo kukidhi mahitaji muhimu kama kununua pembejeo na zana za kilimo, kuwasomesha watoto, kujenga nyumba bora na kupata lishe bora. Aidha, Mpango huo umebadili tabia za Wajasiriamali wadogo kwa kuwajengea utamaduni wa kufungua

Akaunti Benki, kuweka akiba, kukopa na kurejesha kwa wakati. Kiwango cha urejeshaji kimefikia asilimia 76.8.

Mheshimiwa Spika, wananchi pia wamenufaika kupitia mifuko mingine. Maendeleo ya baadhi ya Mifuko hiyo hadi Desemba, 2010 ni kama ifuatavyo: Mfuko wa Wajasiriamali Wadogo (*NEDF*) umetoa Mikopo yenyeye thamani ya shilingi bilioni 24.93 ambapo zaidi ya asilimia 50 ya walionufaika ni wanawake hususan waishio Vijijini, na urejeshaji wa mikopo hiyo ni wastani wa asilimia 90. Mfuko wa Maendeleo ya Vijana umetoa mikopo yenyeye thamani ya shilingi bilioni 1.19 kwa *SACCOS* 238. Serikali pia imeongeza mtaji katika Mfuko wa Udhaminii wa Mikopo kwa Mauzo Nje kutoka shilingi bilioni 6.5 mwaka 2002/2003 hadi shilingi bilioni 20.3 mwaka 2010/2011. Vilevile, Mfuko wa Udhaminii Mikopo kwa Miradi Midogo Midogo umeongezewa mtaji kutoka shilingi milioni 500 mwaka 2005/2006 hadi shilingi bilioni 5.5 mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, mikopo iliyotolewa na Mfuko wa Uwezeshaji Wajasiriamali Wadogo (*SELF*) iliongezeka kutoka shilingi bilioni 5.6 mwaka 2005 hadi shilingi bilioni 25.1 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 348. Hatua nyingine ni pamoja na kuanzisha ruzuku za pembejeo za kilimo na mifugo, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (*TASAF*) na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (*Presidential Trust Fund*). Serikali pia imeimarisha Benki ya Rasilimali Tanzania kwa madhumuni ya kutoa mikopo ya muda mrefu kwa riba nafuu, ikiwa ni pamoja na kuweka dirisha maalum la mikopo ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua pia jitihada za mabenki, taasisi za fedha, madhehebu ya dini, makampuni ya Sekta Binafsi, Asasi Zisizo za Serikali na Asasi za Kijamii katika kujihusisha na shughuli mbalimbali za kuwawezesha wananchi na kuongeza Ajira. Nazipongeza Taasisi na Asasi hizo kwa kutoa mchango mkubwa katika shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi. Natoa wito kwa Taasisi na Asasi hizo kuboresha huduma zao ikiwa ni pamoja na kupunguza viwango vya riba ili wananchi wengi waweze kumudu. Serikali itaendelea kuwashirikisha wananchi wote kwa njia ya uwezeshaji ili waweze kuwa na maisha bora, kujenga uchumi imara na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, kilimo, mifugo, uvuvi na nyuki, ili kiwango cha ukuaji wa Uchumi wetu kiongezeke ni muhimu mapinduzi yanayofanyika katika Sekta ya Kilimo yaende sambamba na ukuaji wa Sekta ya Viwanda. Sekta ya Kilimo ndiyo inayoajiri Watanzania wengi, hivyo ukuaji wa uchumi uliojengwa juu ya Mapinduzi ya Kilimo utahusisha wananchi wengi na utakuwa wa gharama nafuu na kuleta matunda ya haraka zaidi. Tafiti zimeonesha kwamba ukuaji wa uchumi unaotokana na ukuaji wa Sekta ya Kilimo unapunguza umaskini kwa zaidi ya mara mbili kuliko ukuaji unaotokana na sekta nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa kujenga Viwanda tutatumia malighafi zetu wenye, kusindika mazao yetu na kupata fedha nyingi zaidi katika mauzo ya ndani na nje ya nchi na pia kuongeza ajira kwa vijana wetu. Hivyo, ili kuwa na mapinduzi ya kweli katika kilimo, ni vyema viongozi wote tusimamie kwa vitendo utekelezaji wa mipango ya

kilimo na tuwafikishie wakulima vijijini maarifa yanayohusu Kanuni za Kilimo Bora cha mazao wanayolima. Aidha, wapimiwe maeneo ya kilimo na mashamba yao ili kupunguza migogoro ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hali ya upatikanaji wa chakula nchini ni ya kuridhisha isipokuwa katika baadhi ya maeneo machache ya Wilaya 48 yaliyopatwa na ukame. Ili kukabiliana na hali hiyo, Serikali ilitoa jumla ya tani 36,970 za mahindi zenyе thamani ya shilingi bilioni 14 kwa walengwa. Aidha, ilitoa shilingi bilioni 2.1 kugharamia usafirishaji. Wakati huo huo, Serikali inaendelea kufuatilia hali ya upungufu wa chakula katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara, Manyara, Arusha na Kilimanjaro. Aidha, katika msimu wa mwaka 2010/2011, Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula imevunja rekodi kwa kununua jumla ya tani 181,738 kati ya lengo la Tani 200,000. Nahimiza wananchi kutumia akiba ya chakula walichonacho kwa uangalifu na Wafugaji kuuza sehemu ya mifugo ili kujipatia mahitaji yao ya chakula pamoja na kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya Tanzania ambapo Wakulima Wadogo hawana fursa ya kupata mikopo ya kilimo, Mpango wa Ruzuku ya Pembejeo za Kilimo ni muhimu sana katika kuwawezesha wakulima na wafugaji kupata mbegu bora, mbolea na madawa. Kutokana na hitilafu ambazo zimejitokeza katika kusimamia vocha za ruzuku, Serikali imeamua kufanya ukaguzi maalum ambaeo yake yatatumika kuboresha Mpango huo. Lengo ni kuhakikisha kuwa vocha za ruzuku ya pembejeo zinawafikia walengwa na zinatumika kwa madhumuni yaliyopangwa. Serikali imeanza kuchukua hatua kwa Mawakala, Watumishi na Wakulima waliobainika kufanya udanganyifu na kujinufaisha binafsi kinyume na taratibu. Aidha, itawachukulia hatua za kisheria watakaobainika kufanya ubadhirifu baada ya ukaguzi kukamilika. Nawataka wote waache tabia hiyo mara moja kwani inadhoofisha jitihada za Serikali kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inasitisiza umuhimu wa matumizi ya zana za kisasa za Kilimo. Katika mwaka 2010/2011, Mfuko wa Pembejeo ulitoa jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni tatu ikiwemo ya matrepta makubwa na madogo na zana za umwagiliaji. Mamlaka za Serikali za Mitaa zimenunua jumla ya Matrepta Madogo 870 yenye thamani ya shilingi bilioni sita na matrepta makubwa 113 yenye thamani ya shilingi bilioni 2.2. Serikali pia imeingiza nchini matrepta mkubwa yapatayo 1,860 kutoka India yaliyotolewa kama mkopo wa masharti nafuu na Serikali ya India. Matrepta hayo yanasantazwa nchini kuitia SUMA JKT na yanaendelea kuuzwa katika vituo mbalimbali Nchini. Natoa wito kwa wakulima wajunge katika ushirika na vikundi ili kuweza kununua matrepta hayo ambayo ni imara, bei zake ni nafuu na vipuri vyake vinapatikana hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko makubwa ya Tabianchi ni muhimu Taifa letu lijiimarishe zaidi katika kilimo cha umwagiliaji ambacho kinatoa uhakika wa kulima na kuvuna. Serikali pia imeimarisha miundombinu ya baadhi ya mashamba ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Magereza, ili kuendeleza kilimo cha umwagiliaji na uzalishaji wa mbegu bora. Katika mwaka 2010/2011, Jeshi la Magereza limelima Hekta

880 zenyewe uwezo wa kuzalisha tani 1,618 za mbegu. Kwa upande wa JKT, upo Mkataba na Wakala wa mbegu (ASA) wa kuzalisha mbegu bora za mazao mbalimbali katika eneo la Hekta 650. Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi itaendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji kwa wakulima wadogo na wa kati ili kuongeza uzalishaji na ufanisi wa matumizi ya maji.

Mheshimiwa Spika, moja ya mikakakati ambayo Serikali imebuni kuishirikisha sekta binafsi na wadau wengine katika kilimo kupitia dhana ya Kilimo Kwanza ni kuanzisha Mpango wa Kukuza Kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (*Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania - SAGCOT*). Mpango huo ambao utatekelezwa kwa miaka 20 ni nyenzo muhimu ya kuongeza uzalishaji na tija katika mtiririko wa kuongeza thamani ya mazao ya kilimo. Katika mwaka 2011/2012, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.5 na Wafadhili mbalimbali wameahidi kuchangia shilingi bilioni 26.3 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa Mpango huo. Mpango huo ambao ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*) unategemewa kuongeza uzalishaji wa mazao ya Kilimo kwa zaidi ya mara tatu, hususan kwa Wakulima Wadogo. Mpango kama huo utaandaliwa pia kwa Kanda nyingine za kilimo nchini.

Mheshimiwa Spika, programu ya miundombinu ya masoko na huduma za kifedha vijijini, mwezi Julai, 2011, Serikali kwa kushirikiana na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo, Benki ya Maendeleo ya Afrika na *Alliance for a Green Revolution in Africa* itaanza kutekeleza Programu ya Miundombinu ya Masoko na Huduma za Kifedha Vijijini (*Marketing Infrastructure, Value Addition and Rural Finance Support Programme - MIVARF*). Programu hiyo ni ya miaka saba na itatekelezwa katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar. Utekelezaji wa Programu hiyo unatokana na mafanikio mazuri yaliyopatikana kutokana na Programu za Uendelezaji wa Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo ambayo utekelezaji wake ulikamilika mwezi Juni, 2010, na ile ya huduma za kifedha Vijijini ambayo utekelezaji wake utakamilika tarehe 30 Juni, 2011.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Programu hiyo ni kupunguza umaskini Vijijini na kuharakisha ukuaji endelevu wa kiuchumi. Miundombinu ya Masoko Vijijini itakayojengwa ni pamoja na barabara, majengo ya masoko na maghala ya kuhifadhi mazao. Aidha, wakulima na wazalishaji wadogo, wafanyabiashara wadogo na wa kati na wasindikaji watawezeshwa ili kuongeza ushiriki wao katika Soko la Mazao ya Kilimo. Uongezaji thamani wa mazao utatiliwa mkazo ili kuongeza tija na kuvutia ushiriki wa wadau katika uzalishaji. Vilevile, programu hiyo itasaidia kuendeleza utoaji wa huduma za kifedha Vijijini. Juhudi zitaelekezwa katika kuendeleza upatikanaji wa mitaji kwa wazalishaji na wafanyabiashara wadogo na wa kati kwa kuziimarishe Taasisi za Fedha zisizo rasmi na kutoa mafunzo na ushauri kwa Vyama vya Akiba vya Kuweka na Kukopa. Aidha, itasaidia Taasisi za Kifedha kupanua huduma zao Vijijini kwa kutoa mafunzo na usaidizi wa kiufundi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inahamasisha na kusimamia ufugaji wa kisasa na Uvuvi endelevu. Ili kufikia azma hiyo, mpango wa kutoa ruzuku ya dawa ya kuogeshea

mifugo umeendelea kutekelezwa. Serikali imenunua dawa za kuogesha mifugo na kusambaza kwa wafugaji nchini. Aidha, imedhibiti magonjwa ya mifugo kama homa ya mapafu ya ng'ombe kwa kutoa dawa za chanjo. Katika mwaka 2011/2012, Serikali itaendelea kutoa ruzuku ya dawa za kuogeshea mifugo na kuhamasisha wadau kukarabati majosho na kujenga mapya. Serikali pia itaendelea kuimarishe mashamba ya kuzalisha mitamba na mbegu bora za uhamilishaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Uvuvi, Serikali imeimarisha Vikosi vya Doria ili kudhibiti Uvuvi haramu ambao umeshamiri katika maziwa, mito na bahari. Doria hizo ziliwezesha kukamatwa kwa zana haramu na watuhumiwa wamefikishwa Mahakamani. Juhudi hizo zimechangia kukuza uvunaji wa mazao mbalimbali ya uvuvi. Aidha, Serikali imehamasisha uzalishaji wa vifaranga vya samaki aina ya perege na kambale na kuvisambaza kwa wafugaji wa samaki. Katika mwaka 2011/2012, Serikali itaendeleza juhudzi za kudhibiti uvuvi haramu katika mabwawa, mito na bahari na kuwaelimisha wananchi kuhusu faida za kuendeleza uvuvi kwa kuchimba mabwawa ya kufugia Samaki.

Mheshimiwa Spika, Sekta ndogo ya Misitu na Nyuki inayo fursa ya kuchangia pato la Taifa na kuondoa umaskini. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali inaendelea kulinda na kuhifadhi rasilimali za misitu. Kwa upande wa Sekta ya Nyuki, Serikali inatekeleza Mpango wa Kuboresha Ufugaji Nyuki ambao unafanyika katika Wilaya 27 nchini. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2010/2011 ni pamoja na uzalishaji wa tani 9,380 za asali zenyetani ya shilingi bilioni 35.2 na tani 625 za nta zenyetani ya shilingi bilioni 4.5.

Mheshimiwa Spika, ufugaji nyuki ukiendelezwa, unaweza kuongeza ajira nyingi, kipato cha mwananchi mmoja mmoja na pato la Taifa. Aidha, ufugaji nyuki ni biashara rahisi na nyepesi kuwezesha wananchi kupata kipato kikubwa na cha haraka. Kwa sasa asali ina bei nzuri katika Soko la ndani ambapo inauzwa Sh. 8,000/= kwa lita na katika Soko la nje inauzwa wastani wa Sh. 5,550/= kwa lita. Kwa upande wa nta, bei yake ni wastani wa Sh. 6,750/= kwa kilo moja. Hivyo, natoa wito kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Halmashauri zetu kuwahamasisha wananchi kuwekeza katika biashara ya ufugaji nyuki.

Mheshimiwa Spika, ardhi ni rasilimali ya msingi katika uzalishaji, kuleta maendeleo na kujenga uchumi imara wa wananchi na Taifa. Hata hivyo, ardhi isiposimamiwa vizuri na kupangiwa matumizi bora inaweza kusababisha migongano na migogoro na inaweza kuwa chanzo cha maafa katika jamii yetu. Hadi sasa Serikali imepima Vijiji 11,242 kati ya 11,817. Kati ya hivyo, Vijiji 7,043 vimepatiwa Hati za Ardhi za Vijiji. Katika mwaka 2011/2012, Serikali itatayarisha Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi na kuendelea kutoa Hati za Ardhi za Vijiji nchini. Pia, itaongeza kasi ya kupima mashamba ya wananchi na kutoa Hatimiliki za Kimila katika Wilaya na Vijiji vyote vinavyotekeleza miradi ya majaribio. Halmashauri za Miji na Wilaya zitashirikishwa kutumia vyanzo vyao vya mapato, kupima mashamba na kutoa Hatimiliki za Kimila.

Mheshimiwa Spika, Serikali imehamasisha Mabenki na Vyombo vingine vya Fedha kutoa mikopo ya ujenzi wa nyumba ya muda mrefu na yenye riba nafuu kupitia Sheria ya Mikopo ya Nyumba Na. 17 ya mwaka 2008. Sheria hiyo, imewezesha baadhi ya Benki kutoa mikopo kwa ajili ya kununua na kujenga nyumba kwa masharti ya kurejesha mikopo hiyo ndani ya miaka 15. Benki hizo ni *Commercial Bank of Africa, International Commercial Bank, Azania Bancorp, Stanbic Bank na United Bank of Africa*. Aidha, Taasisi za Benki nchini zimeungana na kuanzisha Kampuni inayoitwa *Tanzania Mortgage Refinancing Company* itakayowezesha Benki za Biashara kutoa mikopo kwa wananchi. Nichukue nafasi hii kuwahimiza wananchi watumie fursa hii kumiliki nyumba bora.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianza Ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa utakaochangia kupunguza ghamra za Mawasiliano. Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano wenye urefu wa Kilometra 4,300 katika Mikoa 16 umekamilika na huduma za Mawasiliano zimeanza kutolewa. Aidha, Vituo sita vya kuunganisha Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa na Nchi Jirani zinazozunguka nchi yetu vimekamilika. Awamu ya Pili ya ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa iliyoanza kutekelezwa mwezi Agosti, 2010 ikihusisha takribani Kilometra 3,000 inaendelea. Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India imejenga Kituo cha Umahiri cha *TEHAMA (India - Tanzania Center of Excellence in Information and Communication Technology)* katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ambacho kitatumika kutoa huduma mbalimbali za mawasiliano nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia kwa kushirikiana na *International Telecommunication Union* inaratibu miradi ya maendeleo ya *TEHAMA* nchini hususan katika Sekta ya Elimu. Lengo ni kuunganisha Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo katika Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa. Kupitia mradi huu, Tanzania inatekeleza Malengo ya Kimataifa ya *World Summit on Information Society* ya kusaidia jamii kunufaika na matumizi ya *TEHAMA* katika kukuza na kuendeleza uchumi. Aidha, vifaa vya *TEHAMA* vyenye thamani ya shilingi milioni 170 vimefungwa katika Shule mbalimbali nchini. Katika mwaka 2011/2012, Serikali itakamilisha ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa na kufanya mabadiliko ya Mfumo wa Mawasiliano, Habari na Utangazaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza Mkakati Unganishi kwa Maendeleo ya Viwanda (*Intergrated Industrial Development Strategy*) unaolenga kuongeza thamani ya malighafi mbalimbali nchini. Chini ya mkakati huo, Serikali imeainisha viwanda vya kipaumbele vya kukuza uchumi na kuleta maendeleo endelevu nchini. Miiononi mwa viwanda hivyo ni vile vitakavyozalisha mbolea, chuma, nishati, saruji, madawa na Viwanda vya Usindikaji mazao ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Asali.

Mheshimiwa Spika, juhudzi za kutafuta na kupata Wawekezaji watakaojenga viwanda hivyo zimeanza ambapo mwezi Januari, 2011, Serikali ilipata mwekezaji katika miradi ya makaa ya mawe ya mchuchuma na chuma cha Liganga. Miradi hiyo itakapokamilika itakuwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa MW 600 na chuma ghafi tani 1,000,000.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imehamasisha uanzishwaji na uendelezaji wa Maeneo ya Uzalishaji kwa Soko la Nje (*EPZ*) na Maeneo Maalum ya Kiuchumi (*SEZ*). Maeneo yasiyopungua hekta 2,000 kwa kila Mkoa yamebainishwa kwa ajili ya *EPZ* na *SEZ* katika Mikoa ya Pwani, Tanga, Tabora, Mtwara, Arusha, Ruvuma, Rukwa, Mara, Mwanza, Kigoma, Mbeya, Kilimanjaro, Kagera, Morogoro, Lindi, Shinyanga, Singida na Iringa. Makampuni 44 yamepewa usajili na yanazalisha chini ya masharti ya *EPZ*. Katika kipindi cha mwaka 2007 hadi mwezi Mei, 2011, Makampuni hayo yamewekeza mtaji wa shilingi trilioni moja na yameuza nje bidhaa zenyet thamani ya shilingi bilioni 525 na wafanyakazi 12,600 wameajiriwa. Aidha, eneo la *SEZ* la Bagamoyo lenye ukubwa wa hekta 9,081 limepewa kipaumbele katika Mpango Mkakati wa uendelezaji wa maeneo yaliyotengwa. Nahimiza Mikoa iliyobakia kubainisha maeneo kwa ajili ya maeneo ya uzalishaji kwa Soko la Nje na maeneo maalumu ya kiuchumi kwa kuwa yana fursa kubwa za kuvutia mitaji na kuongeza aira.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo – *SIDO* imeendelea kutoa huduma za kuendeleza viwanda vidogo nchini kwa kukuza teknolojia ili kuwawezesha Wajasiriamali kuzalisha bidhaa bora na zinazohimili ushindani. Katika mwaka 2010/2011, wajasiriamali 18,964 walipata mafunzo mbalimbali na huduma za ushauri wa ugani. Aidha, *SIDO* imesaini Mkataba wa Ushirikiano wa kukuza viwanda vidogo na Shirika la Taifa la Viwanda Vidogo la India.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano huo utasaidia wajasiriamali na wenyewe viwanda vidogo nchini kupata teknolojia mpya itakayoongeza ufanisi katika uzalishaji wa bidhaa za viwanda vidogo nchini. Serikali itaendelea kuliwezesha Shirika la Viwanda Vidogo – *SIDO* kutoa huduma na kuimarisha miundombinu ili kukuza Viwanda Vidogo nchini. Aidha, itatoa Mikopo kwa wajasiriamali wapya kupitia Mfuko wa Wajasiriamali Wadogo (*National Enterpreneurship Development Fund*).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali itaendelea kutekeleza Mkakati Uganishi na Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Viwanda. Aidha, itaendelea kuvutia Wawekezaji kuwekeza katika viwanda vinavyoongeza thamani ya mazao ya kilimo na kutoa mafunzo ya ujasiriamali kupitia *SIDO*. Pia, itashirikiana na Sekta Binafsi kujenga miundombinu na viwanda katika maeneo ya uzalishaji kwa Soko la Nje na maeneo maalumu ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ni kuboresha mtandao wa barabara nchini ili zipitike kwa kipindi chote cha mwaka na ziwe kichocheo cha kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Katika mwaka 2010/2011, barabara mpya zenyet urefu wa kilometra 204 zimejengwa kwa kiwango cha lami na madaraja 1,388 ya barabara kuu yamefanyiwa matengenezo ya kuzuia uharibifu. Aidha, hadi kufikia Machi, 2011, Serikali imefanya ukarabati mkubwa wa Kilometra 154.8 za barabara kuu kwa kiwango cha lami na kilometra 78.8 zimekarabatiwa kwa kiwango cha changarawe. Vilevile, jumla ya kilometra 18,366 zimefanyiwa matengenezo ya aina mbalimbali. Kwa upande wa barabara za Mikoa, jumla ya kilometra 31.6 zimejengwa upya kwa kiwango cha lami, madaraja 539 yamefanyiwa matengenezo na kilometra 778 zimekarabatiwa kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na dhamira nzuri ya Serikali ya kuongeza kasi ya ujenzi wa barabara nchini, miradi mingi ya ujenzi wa barabara inahitaji fedha nyingi ikilinganishwa na uwezo wa Serikali. Ili kuondokana na tatizo hilo, Serikali inakusudia kuanzisha Mfuko mahsus wa ujenzi wa barabara nchini. Aidha, Serikali itashirikiana na Sekta Binafsi katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara chini ya Mfumo wa Utaratibu wa Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi. Natoa wito kwa wakandarasi kujenga barabara kwa kuzingatia viwango vya kitaalam na vyenye ubora na kuzikamilisha kwa wakati. Vilevile, Mamlaka husika kwa kushirikiana na wananchi, zisimamie kikamilifu utunzaji wa barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu katika Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara pamoja na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kuhudumia meli na mizigo. Aidha, Serikali imeshirikisha Sekta Binafsi katika ujenzi wa maeneo ya kuhifadhi mizigo nje ya bandari.

Vilevile, ujenzi wa gati katika Bandari ya Mafia unaendelea na unatarajiwu kukamilika mwezi Desemba, 2011. Katika mwaka 2011/2012, Serikali itaanza kufanya upanuzi wa Gati Na. 1 hadi Na. 7 katika Bandari ya Dar es Salaam na kuongeza kina cha lango la Bandari hiyo ili kuongeza ufanisi. Aidha, itakamilisha ukarabati wa magati sita ulioanza mwaka jana katika Bandari ndogo za Kasanga, Lagosa, Kalya na Kibirizi (Kigoma) na Kirando na Karema (Rukwa/Katavi) katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Kampuni ya Reli Nchini (*TRL*) iliboresha miundombinu ya Reli ya Kati kwa kuweka mataruma kwenye umbali wa kilometra 47 kati ya Stesheni ya Dodoma na Tabora. Aidha, Serikali ilitoa shilingi bilioni 10.02 kwa ajili ya kuimarisha tuta la reli lililoharibiwa vibaya na mafuriko kati ya Stesheni ya Kilosa na Gulwe. Katika mwaka 2011/2012, Serikali itaendelea na kazi ya ukarabati wa kilometra 150 katika reli ya kati eneo kati ya Stesheni ya Dodoma na Tabora. Aidha, kazi ya usanifu kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kuunganisha Tanzania na Rwanda na Burundi itaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania na Zambia zimechukua hatua mbalimbali za kuimarisha reli ya *TAZARA* kutokana na changamoto mbalimbali za kiundeshaji na miundombinu. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Serikali za Tanzania na Zambia zimefanikiwa kupata mkopo wenye masharti nafuu kutoka China wa shilingi bilioni 59 ambaa utatumika kununua injini mpya sita, mabehewa mapya 90 na ununuzi wa vipuri vya kukarabati injini tisa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Serikali ilitekeleza Mpango wake wa Kuboresha na Kupanua Miundombinu ya Viwanja Mbalimbali vya Ndege Nchini. Chini ya Mpango huo, ujenzi wa jengo la watu mashuhuri katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere umekamilika. Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mpanda unaendelea na unatarajiwu kukamilika mwezi Septemba, 2011. Uwanja utakapokamilika, utawezesha Mbuga ya Hifadhi ya Katavi kuvutia watalii wengi zaidi. Katika mwaka 2011/2012, Serikali itaanza ujenzi wa njia ya kurukia na kutua ndege kwa

kiwango cha lami katika kiwanja cha Mafia na kukarabati viwanja vya ndege vya Bukoba, Arusha, Tabora na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kupanua wigo wa utalii na kuutangaza katika masoko mbalimbali duniani. Jitihada za kukuza Utalii nchini zimeweza idadi ya watalii kuongezeka kutoka 714,367 mwaka 2009 hadi 782,699 mwaka 2010 na mapato kuongezeka kutoka shilingi trillioni 1.74 hadi shilingi trillioni 1.9 katika kipindi hicho. Katika mwaka 2011/2012, Serikali itaimarisha mfumo wa ukusanyaji maduhuli pamoja na kuendelea kutumia teknolojia ya kisasa katika kutangaza utalii wetu kwa kutumia Wakala na Ofisi za Ubalozi Nje ya Nchi. Natoa wito kwa wadau wote wa utalii kuendelea kutangaza fursa za utalii zilizopo nchini ili Tanzania iendelee kuwa kivutio kikubwa cha utalii.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa nishati ya uhakika bado ni changamoto kubwa tunayoendelea kukabiliana nayo. Jitihada zinazoendelea kufanyika kukabiliana na tatizo hilo zitatoa matokeo ya kudumu katika miaka michache ijayo. Hii ni kutokana na miradi ya umeme kuhitaji utaalamu na uwekezaji mkubwa na hivyo kuchukua muda mrefu kukamilika. Sekta Binafsi kuruhusiwa kuwekeza kwenye miradi ya umeme kutawezesha miradi mingi zaidi kuanzishwa na hivyo kuongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini. Pamoja na changamoto hizo, katika mwaka 2010/2011, Serikali ilikamilisha kazi ya kufunga jenereta za kuzalisha umeme katika Wilaya za Kibondo na Kasulu. Aidha, mradi wa umeme ujulikanao kama *Way Leave Electrification Project* uliopo katika Wilaya za Kilwa na Rufiji umekamilika. Mradi huo umelenga kuvipatia umeme Vijiji vilivyopitiwa na bomba la gesi ya Songsongo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Wakala wa Umeme Vijijini ilikamilisha miradi saba ya kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya ya Kilindi, Vijiji vya Tungamalenga (Iringa), na Kibinda na Mkunguni Wilayani Pangani. Vilevile utekelezaji wa miradi 41 ya umeme Vijijini kwenye Mikoa 16 ulianza na upo katika hatua mbalimbali. Katika mwaka 2011/2012, Serikali itaongeza kasi ya upelekaji umeme Vijijini kuitia Wakala wa Umeme Vijijini. Serikali pia itaongeza ushiriki wa Sekta Binafsi katika uwekezaji wa kuzalisha nishati mbadala zitokanazo na juu, upepo, *biogas* na vyanzo vingine ili kuongeza upatikanaji wa umeme kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari hadi Mei, 2011, tumeshuhudia ongezeko la bei ya mafuta ya petroli ambayo imefikia dola za Kimarekani 120 kwa pipa moja la mafuta ghafi. Hili ni tatizo ambalo limetokea duniani kote kutokana na kuongezeka kwa bei ya bidhaa hiyo katika Soko la Dunia kulikosababishwa na vuguvugu za kisasa zinazoendelea katika baadhi ya nchi za kiarabu. Serikali imeendelea kutoa bei elekezi ili kuhakikisha kwamba hazipandishwi kiholela na Wafanyabiashara. Aidha, hatua za kisheria zimechukuliwa kwa wafanyabiashara wasio waaminifu wanaochakachua mafuta kwa tamaa ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, Mwezi Aprili, 2010 Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria mpya ya Madini ambayo inatoa wigo mkubwa zaidi wa ushiriki wa Watanzania kwenye shughuli za Madini. Sheria hiyo imekuwa kichocheo cha uwekezaji wa ndani katika

Sekta ya Madini na kutoa mchango mkubwa zaidi kwenye Pato la Taifa. Ili kuongeza mapato yatokanayo na madini, Serikali imekuwa ikishauriana na Kampuni za Uchimbaji wa Madini zenye Mikataba ya zamani kuanza kulipa mrabaha kwa kufuata viwango vipyta na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. Vilevile, Wakala wa Ukaguzi wa Madini unafanya ukaguzi wa kina ili kubaini kiasi cha madini kinachouzwa na Makampuni Makubwa. Juhudi hizo zimeanza kuleta mafanikio ambapo Kampuni zilizokaguliwa zimeanza kulipa kiasi kikubwa cha kodi ikilinganishwa na awali. Ukaguzi wa Makampuni mengine unaendelea na Serikali inatarajia kupata mapato mengi kutokana na rasilimali hiyo.

Mheshimwa Spika, kumekuwepo na migogoro katika maeneo mbalimbali ya uchimbaji madini nchini ambayo inadumaza shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini. Migogoro hiyo mara nyingi imekuwa kati ya wawekezaji wakubwa na wachimbaji wadogo, wawekezaji na wananchi na wakati mwингine baina ya wachimbaji wadogo wenyewe wakigombea maeneo ya kuchimba madini. Migogoro hiyo imesababisha ukosefu wa amani, kupoteza mali na maisha ya watu na pia kushuka kwa uzalishaji. Ili kudhibiti hali hiyo, Serikali itaimarisha usimamizi wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia uchimbaji na uwekezaji katika Sekta ya Madini. Serikali itaendelea kutoa Elimu Juu ya Sera na Sheria Mpya ya Madini na kuwatengea wachimbaji wadogo maeneo ambayo hayaingiliani na yale ya utafutaji na uchimbaji mkubwa. Vilevile, itawahamasisha wachimbaji wadogo kujunga katika vikundi ili kumiliki hisa katika uchimbaji mkubwa na hivyo kufaidika na rasilimali ya madini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali itaendelea kutenga maeneo kwa wachimbaji wadogo na kuwawezesha kupata vifaa vya uchimbaji. Aidha, italiimarisha Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*) ili liweze kuwa Mbia thabiti katika kuendeleza Sekta ya Madini. Serikali pia itaendelea kuhamasisha uwekezaji, utafutaji, uchimbaji na uongezaji thamani katika madini ili kukuza mchango wake katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Programu ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini umewezesha kuongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma ya maji safi na salama karibu na makazi yao kutoka asilimia 57.1 mwaka 2007 hadi asilimia 58.7 Desemba, 2010. Katika mwaka 2010/2011, Serikali imeboresha huduma za maji Mijini kwa kujenga na kukarabati Mifumo ya Maji katika Miji Mikuu 19 ya Mikoa ambapo kiwango cha upatikanaji wa Maji kwa Wakazi wa Miji hiyo kimeongezeka kutoka asilimia 78 mwaka 2005 hadi aAsilimia 86 mwaka 2010. Katika Jiji la Dar es Salaam kwa sasa, upatikanaji wa huduma ya maji ni wastani wa asilimia 55. Upatikanaji wa Maji katika Jiji la Dar es Salaam na Pwani utaimarika zaidi baada ya Serikali ya India kukubali kuipatia Tanzania Mkopo wenyewe masharti nafuu wa shilingi bilioni 270.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali itakarabati na kujenga miradi ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ikiwa ni pamoja na kujenga mabwawa kwa matumizi mbalimbali hususan katika maeneo kame. Vilevile, itahamasisha uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia teknolojia nyepesi na rahisi ya kukinga na kutunza maji. Pia

itaimarisha uwezo wa Mamlaka za Maji, Bodi za Mabonde ya Maji na kuishirikisha Sekta Binafsi katika utoaji wa huduma za maji.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya utekelezaji wa Awamu ya Kwanza na ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (*MMEM*) yamewezesha Tanzania kutambulika katika Jumuiya ya Kimataifa kuwa ni moja ya nchi za Bara la Afrika ambayo imefanya vizuri katika utekelezaji wa baadhi ya Malengo ya Maendeleo ya Milenia. Hii imejidhihirisha wazi kutokana na kiwango cha wanafunzi wa rika lengwa la Elimu ya Msingi walioko shulen i kufikia asilimia 95.4 mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa iliyopo mbele yetu ni kuimarisha mafanikio yaliyopatikana na kuongeza ubora wa elimu kwa kuhakikisha upatikanaji wa Walimu, vitabu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na ujenzi wa nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekondari, utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Elimu ya Sekondari (*MMES-II*) unaendelea vizuri. Kazi kubwa iliyofanyika mwaka 2010/2011 ni kupanua na kuimarisha miundombinu ya Elimu ya Sekondari hasa ujenzi wa madarasa, maabara, nyumba za Walimu, vyoo na hosteli za wanafunzi. Hadi mwezi Machi, 2011, Halmashauri zilikuwa zimejenga madarasa 870, nyumba za Walimu 410 na madawati 11,908 yametengenezwa.

Vilevile, wananchi walihamasishwa kujenga madarasa ya Kidato cha Tano na Sita ili kutekeleza azma ya kuwa na Shule moja ya Sekondari ya Kidato cha Tano na Sita kwa kila Tarafa. Kutokana na jitihada hizo, idadi ya wanafunzi waliojiunga na Kidato cha Kwanza kwa Shule za Sekondari iliongezeka kutoka wanafunzi 438,827 mwaka 2010 hadi wanafunzi 477,661 mwaka 2011 sawa na ongezeko la asilimia 8.8. Aidha, idadi ya wanafunzi waliochaguliwa kuingia Kidato cha Tano katika Shule za Serikali iliongezeka kutoka 26,065 mwaka 2010 hadi 37,721 mwaka 2011 sawa na ongezeko la asilimia 44.7.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zilizopo, changamoto zinazokabili Sekta ya Elimu nchini ni pamoja na upungufu wa Walimu, maabara, nyumba za Walimu, madarasa, madawati na upungufu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, changamoto nyingine ni ufaulu mdogo katika masomo ya Hisabati, Sayansi na Kiingereza katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu. Ili kukabiliana na changamoto hizo katika mwaka 2010/2011, Serikali iliajiri Walimu 21,891 katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu kuanzia mwezi Julai, 2010 hadi Aprili, 2011. Kati ya Idadi hiyo, Walimu walipangwa kufundishia katika Shule za Msingi ni 12,665 na Walimu 9,226 wamepangwa kufundishia Shule za Sekondari na Vyuo vya Ualimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali itaandaa Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (*MMEM III*) 2012 – 2014 na kuendelea kutekeleza Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (*MMES II*) 2010 – 2014. Jitihada zaidi zitawekwa katika kuimarisha na kuongeza kiwango cha ubora wa Elimu ya Msingi na Sekondari kwa kuongeza idadi ya Walimu, ununuzi na usambazaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Napenda kuwakumbusha na kuwahimiza

wananchi kuchangia chakula cha mchana kwa wanafunzi. Mpango huu utaongeza uwezo wa wanafunzi kufuatilia masomo na hivyo kuongeza uelewa na ufaulu wao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Serikali imeendelea na utekelezaji wa Mpango wa kupanua na kukarabati miundombinu muhimu ya Vyuo vya Elimu ya Juu kwa awamu ili kuboresha mazingira ya kusoma katika Vyuo hivyo. Kutokana na jitihada hizo, idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa katika Vyuo vya Elimu ya Juu imeongezeka kutoka 95,525 mwaka 2008/2009 hadi Wanafunzi 118,951 mwaka 2009/2010. Aidha, hadi mwezi Aprili, 2011, Serikali imetua mikopo ya shilingi bilioni 185 kwa wanafunzi 96,328 wa Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu. Maeneo yatakayopewa kipaumbele ni kutafuta njia mbadala ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu na kuimarisha urejeshaji wa mikopo hiyo. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza mpango wa kupanua na kuimarisha miundombinu ya Vyuo Vikuu na Vyuo vingine vya Elimu ya Juu ili viweze kuhimili ongezeko kubwa la wanafunzi wanaomaliza Elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na maendeleo mazuri ya Sekta ya Afya hasa katika viashiria vya kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia ambayo Tanzania imeridhia. Idadi ya Vifo vya Watoto chini ya Umri wa Mwaka Mmoja imepungua kutoka Vifo 58 mwaka 2007/2008 hadi vifo 51 mwaka 2009/2010 kwa kila watoto 1,000 wanaozaliwa hai. Vilevile, kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano, vifo vimepungua kutoka 91 mwaka 2007/2008 hadi 81 mwaka 2009/2010 kwa kila watoto 1,000 wanaozaliwa hai. Mwenendo huu ni mzuri na unaashiria kufikiwa kwa Malengo ya Maendeleo ya Milenia.

Mheshimiwa Spika, kiashiria kingine ni kupungua kwa vifo vya wanawake vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 578 mwaka 2007/2008 hadi vifo 454 mwaka 2009/2010 kwa kila wanawake wajawazito 100,000. Lengo la Maendeleo ya Milenia katika kiashiria hiki ni kufikia vifo visivyozidi 265 kwa wanawake wajawazito 100,000 ifikapo mwaka 2015. Aidha, kutokana na juhudzi za Serikali za usambazaji wa vyandarua kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano na wanawake wajawazito pamoja na matumizi ya Dawa Mseto, kiwango cha maambukizi ya Malaria kimepungua kwa asilimia 20. Utoaji wa chanjo mbalimbali pia umeendelea kuongezeka kwa wastani wa asilimia 85 hadi 95.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (*MMAM*) amba moja ya vipaumbele vyake ni upatikanaji wa watu wenye ujuzi katika Sekta ya Afya. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Serikali iliajiri jumla ya Watumishi 5,256 amba wamepangiwa vituo vya kazi kwenye Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri za Manispaa, Miji na Wilaya. Aidha, Serikali ilitoa vibali vya kufanya kazi katika Sekta ya Afya nchini kwa Wataalam 109 kutoka nje ya nchi. Serikali pia iliongeza idadi ya wanafunzi tarajali katika Vyuo vya Afya na wanafunzi wa Shahada ya Uzamili ili kuboresha huduma za afya za rufaa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali itaendelea kuboresha huduma za kinga na tiba zinazolenga kupunguza vifo vya watoto na wanawake vinavyotokana na uzazi. Aidha, itaendelea kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa katika Vyuo vya Afya na kuajiri watumishi wote wa kada za afya wanaohitimu na kufaulu masomo yao.

Mheshimiwa Spika, suala la lishe bora kwa watoto wa umri chini ya miaka mitano na akina mama walio kwenye umri wa uzazi ni muhimu katika kujenga Taifa lenye watu wenyе afya bora. Hata hivyo, taarifa ya hali ya afya nchini ya mwaka 2010 imeonesha kwamba asilimia 16 ya watoto wa umri chini ya miaka mitano wana uzito pungufu ikilinganishwa na umri wao na asilimia 42 wamedumaa. Kwa upande wa wanawake, asilimia 53 ya wanawake wajawazito wana upungufu wa damu na asilimia 3.5 tu ndiyo wanaotumia kikamilifu madini ya chuma ya nyongeza (*Iron Supplements*). Hali hii siyo nzuri kwa ustawi wa Taifa letu. Serikali imekuwa ikitilia mkazo suala la kujitosheleza kwa chakula katika ngazi ya Kaya na Taifa bila kuweka mkazo unaostahili katika suala la lishe bora.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua changamoto hiyo na kwamba suala hili ni mtambuka, Serikali imeandaa Mkakati wa Lishe Bora ambao utatekelezwa na wadau mbalimbali. Aidha, itaaniszisha kifungu maalumu cha Bajeti kinachohusu masuala ya lishe bora na kuunda Kamati ya kitaifa na kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa zitakazosimamia utekelezaji wa Programu ya Lishe Bora. Serikali imeazimia kutekeleza lengo la Kimataifa la kuboresha lishe (*Scaling Up Nutrition*) ambalo linasisitiza kuwepo umuhimu wa juu wa lishe bora katika kipindi cha siku 1,000 (*One Thousand Days Partnership*). Kipindi hiki ambacho ni kati ya kutunga mimba hadi mtoto anapofikisha miaka miwili ni muhimu sana kwa mama na mtoto kupata lishe bora.

Mheshimiwa Spika, kutoptana na juhudhi hizo za Serikali, nchi za Marekani na *Ireland* pamoja na Mashirika mengine ya Umoja wa Mataifa hususan *UNICEF* wamekubali kusaidiana na Serikali kutatua tatizo hili la lishe. Nazishukuru sana Serikali za Marekani na *Ireland* kwa kukubali kutenga Dola za Kimarekani milioni 8.7, sawa na shilingi bilioni 13.1 kuunga mkono juhudhi hizi za Serikali katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Tunavyo vyakula vya kutosha na vyenye viinilishe bora. Jukumu letu Waheshimiwa Wabunge na Wadau wengine ni kuwaelimisha wananchi umuhimu wa lishe bora ambayo inapatikana hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Serikali imeliwezesha Jeshi la Wananchi kutekeleza majukumu yake ya ulinzi na usalama wa nchi yetu. Kwa ujumla, mipaka ya nchi imeendelea kuwa shwari. Ili kutekeleza majukumu yake, Jeshi limepatiwa vifaa na vitendeakazi mbalimbali na kupatiwa mafunzo na mazoezi ya kuijiandaa kivita. Vilevile, Wanajeshi wetu wameshiriki kwa ufanisi katika majukumu ya kulinda amani katika nchi zenye migogoro. Katika mwaka 2011/2012, Serikali itaweka mazingira bora ya kufanya kazi kwa Wanajeshi ikiwemo ukarabati wa nyumba za kuishi na majengo mengine muhimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na jukumu lake la kusimamia usalama wa raia na mali zao kwa kushirikisha wananchi kuitia dhana ya ulinzi shirikishi. Kuitia dhana hiyo, wananchi wameongeza uhusiano na Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa ambazo zimesaidia kudhibiti vitendo vya uhalifu. Aidha, hatua za kukabiliana na msongamano kwenye Magereza zimechukuliwa kwa kupanua na kukarabati Magereza na kutoa vifungo vya nje. Majeshi ya Polisi na Magereza yameimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi ili kuyawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, ajali za barabarani zinaongezeka kwa kasi na zimeendelea kusababisha ulemavu, vifo na uharibifu wa mali za watu. Takwimu zinaonyesha kwamba idadi ya ajali imeongezeka kutoka ajali 22,019 mwaka 2009 hadi ajali 24,926 mwaka 2010. Ongezeko hilo limesababishwa na mwendo kasi, ulevi, uzembe wa madereva, ubovu wa magari na uegeshaji ovyo wa magari barabarani. Serikali imeazimia kukabiliana na hali hiyo kwa kuendelea kutoa elimu ya matumizi ya barabara kuitia Vyombo vya Habari na shulenii, kukagua na kubadilisha leseni za udereva na kufanya operesheni za mara kwa mara za kukagua magari. Serikali pia itasimamia kikamilifu utekelezaji wa Sera na Sheria za Usalama Barabarani pamoja na kutumia mfumo wa *TEHAMA* kudhibiti mwendo wa magari.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010/2011, Serikali ilitangaza nia ya kuanzisha maeneo mapya ya utawala ikiwemo Mikoa minne ya Simiyu, Katavi, Njombe na Geita pamoja na Wilaya 21 na Tarafa 34. Hatua iliyofikiwa ni kuhakiki mipaka ya maeneo mapya yanayopendekezwa kuanzishwa kwa mujibu wa sheria na taratibu, ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wananchi wa maeneo hayo. Aidha, kwa upande wa Wilaya, Serikali imeona Wilaya za Kahama isigawanywe na badala yake zitaanzishwa Halmashauri mpya za Msalala, Ushetu na Halmashauri ya Mji wa Kahama. Aidha, Wilaya ya Ulyankulu nayo haitaanzishwa hivi sasa badala yake itaanizishwa Wilaya ya Kaliua. Wilaya hizi mbili zitaangaliwa siku za baadaye baada ya kutatua vikwazo vilivyopo hivi sasa. Hivyo, Wilaya mpya zitakazoanzishwa ni 19 badala ya 21. Mchakato wa kuanzisha maeneo hayo utakamilika baada ya kupata maoni ya mwisho ya wananchi na taratibu za kisheria kukamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 31 Desemba, 2010, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete wakati akitoa salaam za mwaka mpya alieleza dhamira ya Serikali kuanzisha mchakato wa kutunga Katiba Mpya ya nchi. Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba dhamira hiyo inatekelezwa ili nchi yetu iwe na Katiba Mpya kabla ya mwaka 2015. Mchakato wa maandalizi ya Muswada wa Sheria wa Kuunda Tume ya Kuratibu ukusanyaji wa maoni hayo toka kwa Watanzania kuhusu Katiba mpya unaendelea. Napenda kutumia fursa hii kuwaomba wananchi washiriki kikamilifu katika kutoa maoni yao kuhusu Katiba Mpya. Aidha, nawaomba Wabunge wenzangu na viongozi wengine tusiingie katika mtego wa kuwapotosha wananchi kwa manufaa yetu binafsi kuitia mchakato wa kuandaa Katiba Mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya kuanzisha Mfuko wa Mahakama. Kuanzishwa kwa Mfuko huo kutaongeza uwezo wa kiutendaji na kuleta ufanisi katika Mahakama zetu nchini. Mfuko huo

utasimamiwa na Mahakama yenyewe kama ilivyo kwa mhimili wa Bunge. Sambamba na hatua hiyo, Serikali inaendelea kutekeleza Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria yenyе lengo la kuleta ufanisi katika utoaji wa haki na kuimarisha utawala bora nchini. Ni imani yangu kuwa kutohana na juhudи hizi za Serikali, Mahakama itaboresha utendaji wake na kutoa huduma bora kwa wananchi hasa kupunguza mlundikano wa kesi zilizopo Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu – Dodoma ilifanya Mapitio ya Mpango Kabambe wa kuendeleza Mji Mkuu Dodoma na kutayarisha Mipango ya kina ya matumizi ya ardhi. Aidha, Mamlaka iliandaa ramani za Mipango Miji; upimaji viwanja vipy 7,481 na kukamilisha upimaji wa viwanja vya zamani 460, katika jitihada za uendelezaji wa Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma. Katika mwaka 2011/2012, mamlaka itakamilisha zoezi la kusanifu mipango ya makazi ya uendelezaji wa Miji (*satelite towns*) katika maeneo ya Ihumwa, Hombolo na Veyula. Aidha, itapima viwanja 1,000 katika maeneo ya Msalato, Mbwenzelo, Nzuguni, Mkonze na kukamilisha upimaji wa viwanja vya zamani 2,038 katika maeneo ya Ipagala, Nkhuhungu na Kisasa. Kazi nyingine zitakazofanyika ni kuandaa Hati Miliki za ardhi zipatazo 2,000 na kuendelea na ujenzi wa barabara kwenye maeneo mapya ya uendelezaji wa Mji.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza malalamiko ya wananchi kuhusu ardhi Dodoma Mjini, Serikali imeanzisha utaratibu shirikishi kati ya Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu, Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma pamoja na Serikali za Mitaa ili kufanya tathmini, kupima na kugawa viwanja na kulipa fidia.

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa huduma bora kwa wananchi. Hata hivyo, jukumu hilo haliwezi kutekelezeka kama Halmashauri zetu hazitaweza kuongeza mapato na kuwa na nidhamu katika matumizi. Serikali Kuu inaelekeza Fedha nyingi katika Halmashauri ili kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Pamoja na hatua hizo, bado usimamizi wa raslimali hizo hauridhishi na pia ukusanyaji wa mapato ni mdogo. Kutohana na hali hiyo, Serikali itaimarisha usimamizi wa Mapato na Matumizi. Hivyo, Watumishi wanao wajibu wa kuhakikisha kuwa sheria, kanuni na taratibu za fedha za Serikali za Mitaa zinazingatiwa. Aidha, nazitaka Halmashauri kuongeza uwazi wa Mapato na Matumizi ili wananchi waweze kushiriki kupanga, kufuutilia na kutekeleza mipango yao kulingana na vipaumbele vyao.

Mheshimiwa Spika, masuala mtambuka, Jinsia, katika mwaka 2010/2011, Serikali imewawezesha Wanawake kupata nafasi katika ngazi mbalimbali za uongozi na maamuzi Nchini ili kuleta uwiano wa kijinsia. Hili limedhihirika wazi katika matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 ambapo Bunge lako Tukufu lina Wabunge Wanawake 126 sawa na asilimia 36 ya Wabunge wote. Aidha, idadi ya Mawaziri wanawake ni asilimia 27 ya Mawaziri wote. Bunge letu pia kwa mara ya kwanza linaongozwa na mwanamke. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Anne Makinda kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Kwanza Mwanamke katika historia ya Taifa letu. Hongera Sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendeleza jitihada za kuwawezesha Wanawake kiuchumi kupitia Mifuko mbalimbali ya Uwezesaji na Benki ya Wanawake. Benki ya Wanawake imepata mafanikio tangu ianzishwe mwaka 2009. Hadi mwezi Aprili 2011, Mtaji wa Benki hiyo ulikuwa Shilingi Bilioni 4.8 ikilinganishwa na Shilingi Bilioni 2.8 Benki hiyo ilipoanzishwa. Aidha, Akaunti 15,125 zenye thamani ya Shilingi Bilioni 13.8 zilifunguliwa na wakopaji 4,822 walipatiwa mikopo ya thamani ya Shilingi Bilioni 8.5. Vilevile, Benki hii hutoa mafunzo kwa Wateja wake watarajiwa ambapo hadi Aprili 2011, Wanawake Wajasiriamali 5,668 wamepata mafunzo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Serikali imetekeleza Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti Rushwa kwa kutoa mafunzo kwa Kamati za Uadilifu katika Wizara na Taasisi za Umma. Watumishi wa Umma 472 kutoka Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar walipata mafunzo ya Utawala Bora na Uadilifu. Aidha, tuhuma za Rushwa 2,258 zilifanyiwa uchunguzi ambapo tuhuma 598 uchunguzi wake ulikamilika, 399 ziliendeshwa Mahakamani na tuhuma 1,261 uchunguzi wake unaendelea. Jumla ya kesi 13 za Wagombea wa nafasi mbalimbali waliotuhumiwa kujihusisha na vitendo vya rushwa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 zilifikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU) itachunguza tuhuma 2,456 zilizopo na tuhuma mpya zitakazopokelewa na kuendesha Kesi 425 zilizopo Mahakamani. Aidha, itafanya uchunguzi maalum wa Vocha za Pembejeo za Kilimo baada ya kupokea malalamiko mengi ya wananchi yanayohusiana na Sekta ya Kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, dunia sasa inakabiliwa na changamoto kubwa ya mabadiliko ya Tabianchi. Ili kukabiliana na hali hiyo, Serikali iliendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Mazingira, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Mkakati wa Hifadhi ya Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Serikali ilianzisha Mashindano ya Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji, Kupanda na Kutunza Miti kwa lengo la kuhamasisha wananchi kuhifadhi na kutunza mazingira. Aidha, Serikali imeendelea kuhamasisha utekelezaji wa Kampeni ya Upandaji Miti Nchini.

Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kwa kuanzisha Mpango wa Kupanda Miti Zaidi ya 1,000 kila mmoja kwa mwaka katika majimbo yao. Natoa changamoto kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wananchi kwa ujumla kuiga mfano huo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali itaimarisha Elimu kwa Umma na kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi ili kuongeza ushiriki wa jamii katika kuhifadhi mazingira. Vilevile, Serikali itatoa mafunzo juu ya tathmini ya mazingira kimkakati na kuzijengea uwezo Serikali za Mitaa kutekeleza mikakati yao ya kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, nchi yetu imekumbwa na maafa mbalimbali yakiwemo ukame uliosababisha upungufu wa chakula katika baadhi ya

maeneo nchini, mafuriko, upopo mkali ulioambatana na mvua kubwa na milipuko ya magonjwa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 17 Februari, 2011, kulitokea ajali ya Milipuko wa Mabomu katika Kambi ya Jeshi ya Gongo la Mboto, Dar es Salaam. Katika tukio hilo, yalitokea madhara makubwa na kusababisha watu 30 kupoteza maisha. Watu 623 walijeruhiwa, kaya 1,577 ziliathirika, nyumba 71 zilibomoka kabisa na nyumba 1,689 ziliharibiwa kwa viwango tofauti. Serikali ilichukua hatua za haraka kurejesha hali ya kawaida katika eneo hilo ikiwa ni pamoja na kuwapatia waathirika misaada ya chakula, mahema na vifaa vya nyumbani. Aidha, baada ya tathmini kufanyika, zoezi la kutoa fidia na kujenga nyumba zilizobomoka kabisa kupertia SUMA JKT limeanza. Nitumie fursa hii tena kuwashukuru wote waliota misaada ya hali na mali katika kuwasaidia walioathirika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, baadhi ya maeneo nchini yamekumbwa na mafuriko na upopo mkali ulioambatana na mvua nyingi. Katika Wilaya ya Muleba, waathirika wamepatiwa tani 2,076 za mahindi na kiasi cha shilingi milioni 31, kukarabati madarasa tisa ya Shule za Msingi na madarasa mawili ya Sekondari yaliyoezuliwa.

Katika Wilaya ya Kilombero mafuriko yameharibu miundombinu na wananchi wengi kuharibiwa mazao yao. Serikali imetoa tani 239 za mahindi kwa waathirika hao. Aidha, Serikali imetoa shilingi milioni 210 kwa ajili ya matengenezo ya madaraja sita na shilingi milioni 340 kutengeneza barabara zilizoharibika. Serikali inakusudia kuanzisha Mamlaka inayojitegemea ya Kuratibu masuala ya Maafa Nchini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tunaanza kuona dalili za kutia moyo zinazoonesha kuongezeka kwa mwamko wa jamii yetu katika mapambano dhidi ya UKIMWI kutokana na juhudi kubwa za kutoa elimu ya UKIMWI mashulenii kuanzia Darasa la Tano na kwa jamii. Sasa UKIMWI umazungumzwa kwa uwazi na katika ngazi zote za jamii yetu. Sekta zote za Umma na zisizo za Umma zina mipango ya kudhibiti UKIMWI. Mipango hiyo inalenga katika maeneo makuu matatu: kuzuia maambukizo mapya ya virusi vya UKIMWI, huduma na matibabu kwa viashiria vya Virusi vya UKIMWI na kusaidia yatima na familia zilizoathiriwa na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Serikali imesogeza huduma za uratibu wa UKIMWI kwa kuajiri Waratibu wa UKIMWI katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Waratibu hao wanatakiwa kufanya kazi kwa karibu na Waratibu wa Wilaya katika kuboresha mipango ya UKIMWI ya Mikoa na Wilaya kulingana na vipaumbele vya Taifa. Serikali kwa kushirikiana na Wadau, imefanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI ya mwaka 2001. Aidha, imeandaa mfumo wa uratibu wa Asasi za Kiraia na Taasisi za Dini na kulijengea uwezo Baraza la Watu Wanaoishi na VVU ambao wameanzisha Konga kwenvye Halmashauri. Vilevile, Serikali inakamilisha mchakato wa kuanzisha Mfuko wa Kudhibiti UKIMWI Nchini. Mfuko huu utachangiwa na Serikali pamoja na wadau wengine.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali itaendeleza juhudhi za kudhibiti UKIMWI Nchini kwa kuweka taratibu endelevu za kukusanya raslimali za kudhibiti UKIMWI. Aidha, Serikali kwa kushirikisha wadau, itakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI ya mwaka 2001, na itatayarisha Mkakati wa Sekta zote wa kukabiliana na UKIMWI kwa kipindi cha mwaka 2013 - 2017.

Mheshimiwa Spika, biashara haramu ya Dawa za Kulevya ni tatizo kubwa kwa nchi yetu. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kukabiliana na tatizo hilo kwa kufuutilia na kubaini mitandao ya dawa hizo ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na Shirika la Polisi la Kimataifa. Aidha, Serikali imeunda Kikosi Kazi cha kuwabaini wanaojishughulisha na Dawa za Kulevya. Taarifa za kiintelijensia zinatumika kufuutilia biashara hiyo ili kudhibiti uingizaji na usafirishaji kupitia viwanja vya Ndege na Vituo vya mipakani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Serikali imeteketeza jumla ya ekari 310 za mashamba ya Bangi. Jumla ya watuhumiwa 7,221 walikamatwa na kilo 143,813 za bangi pamoja na kilo 3,978 za mirungi.

Katika kipindi hiki pia, jumla ya kilo 368.4 za *heroin* zilikamatwa zikiwahusisha watuhumiwa 23. Aidha, Kilo 148 za *Cocaine* zilikamatwa zikiwahusisha watuhumiwa 16. Ukamataji wa dawa za kulevya aina ya *Heroin* na *Cocaine* kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 ni kikubwa zaidi ya mara kumi ya jumla ya kiwango kilichokamatwa kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita (2000 - 2010). Hali hii inazidi kudhihirisha kuwa katika miaka ya karibuni kiwango kikubwa cha *Heroin* na *Cocaine* kimeanza kupitishwa hapa nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali itaendelea kuelimisha umma juu ya madhara ya matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevya. Aidha, itaendesha operesheni za ukamataji wa dawa za kulevya na uteketezaji wa mashamba ya bangi, na kuwezesha upatikanaji wa huduma za tiba na urekebishaji tabia kwa waathirika wa dawa za kulevya.

Natoa wito kwa wananchi wote kushirikiana na vyombo vya dola kuwafichua wanaojihusisha na biashara haramu ya dawa za kulevya, kwani tusipofanya hivyo, tutapoteza sehemu kubwa ya nguvukazi ya Taifa letu. Serikali imeamua kuanzisha chombo kimoja chenye nguvu na uwezo zaidi kitakachodhibiti dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Nimeelezea kwa muhtasari baadhi ya shughuli ambazo Serikali imetekeleza kwa kipindi kilichopita. Aidha, nimetoa mwelekeo wa kazi zitakazofanyika mwaka 2011/2012. Kwa kuhitimisha, napenda kusisitiza mambo yafuatayo:-

(a) Pamoja na changamoto tunazokabiliana nazo katika kuleta maendeleo na kuondoa umaskini na baadhi yetu kuendelea kubeza maendeleo tuliyoyapata tangu tupate uhuru, lakini bado nchi yetu inaendelea kukubalika Kimataifa. Aidha, imekuwa mfano wa kuigwa katika nyanja mbalimbali za Ushirikiano wa Kimataifa na Kikanda. Ukuaji

wa Uchumi wetu ambao ni wastani wa asilimia saba tangu mwaka 2001 hadi 2010, umeifanya Tanzania kuwa mionganoni mwa nchi 20 Duniani ambazo uchumi wake unakua kwa kasi kubwa. Vilevile, kulingana na uchambuzi uliofanywa na Shirika la Fedha Duniani (*IMF*), Tanzania ni moja ya nchi nne katika Bara la Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara ambayo uchumi wake utakua kwa kasi katika miaka ijayo. Kadhalika, Chuo cha *McKinsey Global Institute* katika chapisho lake la Juni 2010 linaloitwa “*Lions on the Move: The Progress and Potential of African Economics*” kimeeleza kuwa Tanzania ni mionganoni mwa nchi ambazo zimethibitika kuwa uchumi wake unakua kwa haraka na hivyo kuelekea kwenye uchumi wa kati. Mwandishi *Steven Radelet* katika Kitabu kinachoitwa *Emerging Africa 2010*, pia ameielezea Tanzania kuwa moja ya nchi 17 za Afrika chini ya Jangwa la Sahara ambazo zinaongoza katika kukua kwa uchumi, kupunguza umaskini na kuzingatia utawala bora na uwajibikaji. (*Makofi*)

Kutokana na ukuaji huo mzuri pamoja na uzingatiaji wa utawala bora na uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Marekani imeichagua Tanzania kuwa mionganoni mwa nchi nne Duniani, mbili kati ya hizo kutoka Afrika, kushiriki Mpango wa Ubua wa Kukiza Uchumi (*Partnership for Growth*). Mpango huo utatoa fursa nyingine ya kukua kwa uchumi wa Tanzania na kuimarisha ushirikiano baina ya Tanzania na nchi mbalimbali Duniani. Mifano yote hii ni ushahidi tosha kwamba Tanzania imefanya vizuri katika kujenga misingi ya uchumi imara na siyo sahihi kubeza mafanikio hayo. Vilevile, tathmini hizo siyo sababu ya kubweteka kwa kuwa zipo changamoto mbele yetu, bali ni hamasa ya kusonga mbele kwa kasi zaidi.

(b) Ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki umekuwa wa manufaa tofauti na hofu ya baadhi ya wananchi. Thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki iliongezekwa kutoka Dola za Kimarekani Milioni 263.9 mwaka 2009 hadi Dola Milioni 450 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 70.6. Naomba niwahimize Watanzania wote kuchangamkia fursa ya ukuaji wa Soko hilo la Afrika Mashariki na Kanda nyingine.

(c) Tunatimiza miaka 50 ya Uhuru tukiwa tumejjengea misingi imara ya amani na utulivu na sote tumeona manufaa yake. Hata hivyo, kuna dalili ya baadhi yetu kuanza kutaka kubomoa misingi hiyo. Naamini tunaweza kudai haki zetu bila kusababisha uvunjifu wa amani au vurugu ya aina yoyote. Tukumbuke kwamba sisi sote ni Watanzania. Nawasihi Watanzania wenzangu, tuendelee na tabia yetu ya kuishi na kufanya kazi kwa Amani, Umoja na Uzalendo kwa kutanguliza maslahi ya Taifa letu mbele. Vilevile, tukumbuke kwamba kutokana na amani tuliyonayo, nchi yetu imekuwa Msuluhishi wa Migogoro katika Nchi za Maziwa Makuu na Bara zima la Afrika. Hii ni sifa na heshima kubwa kwa Taifa yetu. (*Makofi*)

(d) Tumeanza kuona mafanikio ya utekelezaji wa azma ya Kilimo Kwanza. Ongezeko la matumizi ya pembejeo, zana bora za kilimo na kuzingatia kanuni bora za kilimo, kumeongeza uzalishaji na tija. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi, imeanza kutekeleza Mpango wa Kilimo katika Ukanda wa Kilimo wa Nyanda za Kusini ambaao una lengo la kuongeza uzalishaji na tija, uhakika wa chakula na kuongeza thamani

mazao ya kilimo. Mpango huo utahakikisha kuwepo kwa matumizi bora ya ardhi na kulinda ardhi ya wakulima wadogo.

(e) Ili kujilettea maendeleo endelevu kwa haraka, ni vyema wote tuwajibike kwa vitendo na kufanya kazi kwa bidii, ubunifu, ufanisi na umakini ili kufikia malengo tuliyojiwekea. Tunazo fursa nyingi za kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Tujitahidi kuongeza tija na thamani katika bidhaa na mazao yetu ili kuwa na uchumi wa kisasa unaohimili ushindani katika masoko ya kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu, nimwombe Mheshimiwa Kapt. (Mstaafu) George Huruma Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naye atoe maelezo ya mapitio ya kazi zilizofanyika katika mwaka 2010/2011 na mwelekeo wa kazi za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka 2011/2012. Ni matumaini yangu kwamba maelezo hayo yatawezesha Waheshimiwa Wabunge na wananchi kufahamu kwa upana shughuli zinazotekelzwa na Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, karibu! Nilishaomba dakika 30 zaidi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kutoa maelezo kuhusu shughuli za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, mapitio ya mwaka wa fedha 2010/2011 na mwelekeo wa kazi kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa siku hii ya leo. Naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Hotuba nzuri iliyotoa mwelekeo na malengo ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2011/2012. Vilevile, nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Waziri wa Fedha, kwa hotuba yake kuhusu Hali ya Uchumi na Mapendekezo ya Serikali ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2011/2012. Ni hotuba ambazo zimeonesha mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, kwa vile hii ni hotuba yangu ya kwanza ya bajeti baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka jana, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Uchaguzi la Newala kwa kunichagua tena kwa kura nyingi kuendelea kuwawakilisha hapa Bungeni. Napenda pia kumshukuru Rais, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani kubwa aliyionesha kwangu na kunitfea kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI) nikishirikiana na Mheshimiwa Aggrey Mwanri Mbunge wa Siha, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) na Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mbunge wa Ruangwa anayeshughulikia Elimu - TAMISEMI. Ahadi yangu kwa Mheshimiwa Rais na wapiga kura wangu wa Jimbo la Newala na kwa Watanzania

wote ni kufanya kazi kwa juhudini, uadilifu na maarifa bila upendeleo wala woga.  
*(Makofit)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuteuliwa na kupidishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nachukua nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge letu Tukufu ukiwa mwanamke wa kwanza katika historia ya nchi yetu. Nawapongeza Wabunge wenzangu wote waliochaguliwa kuingia katika Bunge hili. Kwa pamoja tunalo jukumu la kuiendeleza nchi yetu, hivyo sisi sote hatuna budi kushirikiana kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba niwasilishe maelezo ya kiutendaji ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 na mwelekeo wa kazi kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya OWM-TAMISEMI ni pamoja na kuratibu ugatuaji wa madaraka kwa umma; usimamizi wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Vijijini na Mijini; kuratibu utekelezaji wa majukumu ya Tawala za Mikoa; kuratibu uendeshaji wa elimu ya msingi na sekondari; kusimamia na kuendeleza rasilimali watu; kusimamia Mashirika, Programu na Miradi iliyo chini ya OWM-TAMISEMI na kusimamia Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya Mko, majukumu ya msingi ni pamoja na kujenga uwezo wa kitaalamu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, kudumisha amani na utulivu, kuratibu miradi na programu mbalimbali chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuhakikisha kwamba utawala bora unazingatiwa wakati wote.

Mheshimiwa Spika, mamlaka za Serikali za Mitaa ndizo watekelezaji wa Sera zote za Serikali ili kuhakikisha huduma bora zinatolewa kwa wananchi katika sekta zote. Dhana kubwa iliyopo ni ushirikishwaji wa wananchi katika kupanga, kufuatilia na kutekeleza mipango na bajeti kwa maendeleo yao wenyewe. Aidha, katika ngazi hizi za msingi, uko umuhimu mkubwa wa kuendeleza demokrasia na utawala bora kwa vile ndipo walipo Watanzania walio wengi. Kwa mantiki hiyo, upo umuhimu wa kuwajengea uwezo wa kiutendaji Watendaji na viongozi katika ngazi hizi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Majukumu kwa mwaka 2010/2011 na Mwelekeo kwa mwaka 2011/2012. Katika Ibara ya 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mamlaka za Serikali za Mitaa ndizo zenye jukumu la kufanya maamuzi mbalimbali yanayohusu utoaji wa huduma kwa wananchi. Aidha, Mamlaka hizo zina wajibu kuhakikisha kwamba wananchi wanashirikishwa katika mambo yanayowahusu kwa ajili ya maendeleo yao. Hata hivyo, uhuru huo wa Kikatiba hauna budi kutekelezwa kwa kuzingatia Sheria, Taratibu na Kanuni zilizopo hasa kwa wakati huu ambapo Serikali inatekeleza Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa yenye lengo la kupeleka madaraka kwa wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio ya kila mmoja wetu kwamba kupitia uboreshaji huo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaendelea kuimarika ili ziendelee kusimamia vema na kuratibu shughuli za kijamii na kimaendeleo sambamba na kuhakikisha kuwa huduma bora zinatolewa kwa wananchi katika nyanja zote. Aidha, yako matarajio kwamba Wizara za Kisekta nazo zitaendelea kuainisha majukumu yao wakati huu wa kuboresha mfumo huo katika mahusiano mapya kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Serikali Kuu inabaki na kazi ya kuboresha mazingira wezeshaji ya kisera, kisheria na Kitaasisi.

Mheshimiwa Spika, ili kufuatilia matumizi ya fedha za maendeleo zinazopelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Mfumo wa ugawaji wa ruzuku ya maendeleo, Kamati ya Ufundu ya Mfumo huo ilitembelea Mikoa ya Tanga mwezi Novemba 2010 na Singida mwezi Machi 2011. Wajumbe wa Kamati walitoka katika Wizara za Kisekta, Wizara ya Fedha, OWM-TAMISEMI, Wabia wa Maendeleo, Benki ya Dunia, Viongozi wa Mikoa ya Tanga na Singida na Viongozi wa Halmashauri zote za Mikoa iliyohusika. Baadhi ya mambo yaliyojitokeza katika ziara hiyo ni kuchelewa kutumika kwa fedha kulingana na ratiba ya kazi hususan fedha za miradi ya maji; uwezo mdogo wa utunzaji wa fedha na manunuvi katika ngazi za Serikali za Mitaa; kutotumika kikamilifu kwa mfumo wa usimamizi wa fedha na utekelezaji usioridhisha kwa baadhi ya miradi iliyotembelewa.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa wito kwa Mamlaka zote za Serikali za Mitaa kutekeleza miradi kwa wakati na hususan zinapokuwa zimeishapokea fedha. Aidha, zinatakiwa kutoa taarifa kwa ukamilifu kwa sababu mafunzo yameshatolewa kwa Waweka Hazina wote na Wahasibu wasiopungua wawili kwa kila Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na utaratibu wa kuzipima Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuona ni kwa jinsi gani zinazingatia vigezo vya utawala bora. Zoezi hilo liliifanyika mwezi Februari na Machi 2011 ambapo kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa 132, Mamlaka (4) zimeshindwa kufuzu vigezo. Matokeo haya pamoja na taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali yatatumika katika kugawa ruzuku ya maendeleo kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianza zoezi la kuwajengea uwezo Waweka Hazina na Wakaguzi wa Ndani wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika mwaka wa fedha 2009/2010 kwa kuwapatia mafunzo ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma. (*International Public Sector Accounting System (IPSAS)*). Wakaguzi wa Ndani 133, Waweka Hazina 133 na watumishi 399 wa kada mbalimbali kutoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa walipatiwa mafunzo hayo. Aidha, Wahasibu 266 na waweka Hazina 133 katika Mamlaka hizo wamepatiwa mafunzo ya Mfumo wa Usimamizi wa Fedha (*IFMS*). Pia, Serikali imeimarisha vitendea kazi kwa kununua kompyuta 133 na ‘printers’ zake na mchakato wa kununua magari 75 kwa ajili ya Wakaguzi wa Ndani unaendelea. Hatua hii itawezesha kufuatilia kwa karibu matumizi ya fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, OWM-TAMISEMI iliandaa viashiria vya upimaji wa utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa. Zoezi la ukusanyaji takwimu za msingi limefanyika katika Halmashauri 15 za Manispaa za Sumbawanga, Iringa, Temeke, Singida, Tabora, Lindi, Halmashauri ya Mji wa Korogwe na Halmashauri za Wilaya za Bahi, Mbarali, Mvomero, Liwale, Masasi, Rufiji, Sikonge na Biharamulo. Uchambuzi wa takwimu hizi utawezesha kuandaa vigezo vya kupima utekelezaji wa upelekaji madaraka kwa Umma.

Mheshimiwa Spika, suala la upungufu wa watumishi katika ngazi za Serikali za Mitaa liimeendelea kujitokeza. Aidha, ili kujenga uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa OWM-TAMISEMI, imetoa vibali vya kuhamisha watumishi 164 kutoka Halmashauri moja kwenda Halmashauri nyingine katika Mikoa mbalimbali ili kuboresha utendaji. Vilevile, Watumishi 1,995 waliomba uhamisho wenyewe na baada ya kufanya uchambuzi maombi 1,837 yalioneckana kukidhi vigezo na hivyo kupata kibali cha kuhamza na maombi 158 hayakukidhi vigezo kutokana na upungufu mbalimbali. Kada zilizoongoza kuomba kuhamza ni Ualimu kwa asilimia 81.5, Afya asilimia 8.17, Maendeleo ya Jamii asilimia 1.7, Kilimo na Mifugo asilimia 1.6, Fedha asilimia 1.3 na kada zilizobaki asilimia 5.73. Sababu za msingi za watumishi kuomba uhamisho ni pamoja na kutaka kuwa karibu na wenza wao, kuugua, kuwa karibu na wazazi ili kuwashudumia, kuwa karibu na hospitali za rufaa na kwa ajili ya kufanya maandalizi ya kustaafu.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia masuala ya nidhamu katika Utumishi wa Serikali za Mitaa, Wakurugenzi wa Halmashauri 16 walichukuliwa hatua za nidhamu. Makosa makubwa yalikuwa ni ukiukwaji wa Kanuni, Taratibu na Sheria za Utumishi wa Umma. Uchunguzi wa awali wa mashauri ya Wakurugenzi 11 umekamilika na mchakato wa hatua za nidhamu kwa mujibu wa Sheria za Utumishi unaendelea. Aidha, kwa waliobaki uchunguzi unaendelea.

Mheshimiwa Spika, maeneo mapya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Serikali imeridhia upandishwaji hadhi ya Mji wa Lindi kuwa Manispaa na kuanzishwa kwa Halmashauri za Mji ya Tunduma, Nzega, Makambako, Kasulu, Kahama, Handeni na Masasi. Aidha, imeridhia kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Nanyamba katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Kujenga uwezo katika Sekretarieti za Mikoa, Ofisi imeendelea kujenga uwezo kwa watumishi wa Sekretarieti za Mikoa ili waweze kuzisimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa mwaka 2010/2011, Ofisi imetoa mafunzo ya awali kwa Makatibu Tawala sita (6) walioteuliwa na Makatibu Tawala hao ni wa Mikoa ya Singida, Morogoro, Tanga, Arusha, Tabora na Kagera. Aidha, kilifanyika kikao cha Makatibu Tawala Wasaidizi 21 wanaoshughulikia masuala ya Serikali za Mitaa kutoka Mikoa 21 kwa lengo la kuboresha usimamizi na ufuutiliaji pamoja na utoaji taarifa kutoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Wakati wa kikao hicho maazimio mbalimbali yalifikiwa ili kuwezesha ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Sekretarieti za Mikoa. Aidha, mafunzo ya kutunza mazingira na kuzingatia mazingira kwenye

mipango na bajeti yalitolewa kwa Halmashauri zote za Mikoa ya Kagera, Rukwa, Iringa, Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Ruvuma, Manyara, Lindi na Morogoro. Mafunzo haya yataendelea katika Mikoa mingine katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, ujenzi na Ukarabati wa Hospitali za Mikoa. Ili kuboresha utoaji wa huduma katika hospitali za Mikoa, kuanzia mwaka wa fedha 2007/2008 Serikali imekuwa ikitoa fedha kwa awamu kwa ajili ya kukarabati Hospitali za Mikoa na kujenga hospitali mpya kwa baadhi ya Mikoa. Kwa mwaka 2010/2011 Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 12.3 kuendelea na kazi hizo. Mikoa ambayo inajenga hospitali mpya ni Mkoa wa Singida ambao ilitengewa shilingi bilioni mbili na hadi kufikia mwezi Aprili 2011 shilingi bilioni mbili zimepokelewa na ujenzi wa jengo la ghorofa moja la wodi za tiba unaendelea. Mkoa wa Mbeya ilitengewa shilingi milioni 708.9 kwa mwaka 2010/2011. Hadi mwezi Aprili 2011, Mkoa umepokea shilingi milioni 325 na fedha hizo zimetumika kujenga mifumo ya maji machafu na ununuzi wa nyaya za umeme kwenye chumba cha kufulia nguo za wagonjwa. Kazi nyingine iliyofanyika ni ujenzi wa minara kwa ajili ya kuweka matanki ya maji na kuandaa michoro kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wodi ya watoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mkoa mwengine ni wa Manyara ambao umeanza kutekeleza awamu ya pili ya ujenzi wa Hospitali ya Mkoa ambayo inahusisha ujenzi wa chumba cha maiti; chumba cha kuchomea taka; kuweka mfumo wa kuvuna maji ya mvua na hadi kufikia mwezi Aprili 2011 Mkoa umeshapokea shilingi bilioni 1.6. Ukarabati wa hospitali nyingine zote za Mikoa uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Serikali itaendelea kuzifanyia ukarabati hospitali za Mikoa na kuhakikisha zinapata vifaa vya kutosha kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana kwa lengo la kuzifanya kuwa Hospitali za Rufaa za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, barabara za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Gharama za matengenezo ya barabara za Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na uangalizi wake zimeendelea kutegemea mgao wa asilimia 30 ya fedha kutoka kwenye Bodi ya Mfuko wa Barabara baada ya mradi wa Usafirishaji na Uchukuzi (*LGTP*) uliokuwa unafadhiliwa na Wahisani mbalimbali kufikia mwisho. Hadi kufikia mwezi Mei 2011, jumla ya shilingi bilioni 78.5 zimepokelewa na kupelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara. Matengenezo hayo yalihusisha matengenezo ya kawaida, matengenezo ya muda maalum na matengenezo ya dharura katika sehemu korofi, matengenezo ya madaraja, makalvati pamoja na shughuli za usimamizi na ufuatiliaji wa matengenezo hayo. Hadi kufikia Machi 2011 jumla ya kilomita 8,059 zilifanyiwa matengenezo mbalimbali kati ya kilomita 21,636 zilizokuwa zimepangwa kwa mwaka wa fedha 2010/2011 katika maeneo hayo na kazi zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Mfuko wa Barabara utaendelea kuzifanyia matengenezo barabara za Halmashauri kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ili ziweze kuitika. Kiasi cha shilingi bilioni 94.02 kinategemewa kutoka kwenye Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka vyanzo vyake vya ndani kwa miaka mitatu iliyopita unaonesha kuwa makisio na makusanyo ya mapato siyo ya kuridhisha. Katika mwaka 2008/2009 makisio yalikuwa shilingi bilioni 109.8 na makusanyo halisi yalikuwa shilingi bilioni 100.1 sawa na 91%. Aidha kwa mwaka 2009/2010 makisio yalikuwa shilingi bilioni 138 na makusanyo halisi shilingi bilioni 117.8 ambayo ni 8% ya makadirio. Mwaka wa fedha 2010/2011 hadi kufikia Machi 31, 2011, jumla ya shilingi bilioni 115.1 zimekusanya sawa na 67% ya makadirio ambayo ni shilingi bilioni 172.5. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa ukusanyaji wa mapato siyo wa kuridhisha na hali hii imeendelea kuwa changamoto kwa Halmashauri. Natoa wito kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuongeza juhudzi za ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuongeza uwezo wa kutekeleza shughuli za maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinakadiria kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 350 kutokana na vyanzo vya ndani. Kiasi hiki ni ongezeko la makadirio ya asilimia 103 ukilinganisha na makadirio ya mwaka 2010/2011. Ongezeko hilo limetokana na uamuzi wa Serikali wa kurudisha baadhi ya vyanzo vya mapato vilivyofutwa. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kukusanya mapato na kutoa taarifa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hali ya usimamizi na utunzaji wa vitabu vya hesabu za fedha kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa imeshuka ikilinganishwa na ile ya mwaka 2008/2009. Kwa mwaka 2008/2009 Halmashauri zilizopata Hati inayoridhisha zilikuwa 77 kati ya 133 na mwaka 2009/2010 zilikuwa 65 kati ya 133. Huu ni upungufu wa 9% ukilinganisha na mwaka 2008/2009. Halmashauri moja ilipata Hati Chafu mwaka 2008/2009 na Halmashauri nne zimepata Hati Chafu kwa mwaka 2009/2010. Nachukua fursa hii kuzipongeza Halmashauri zote zilizopata Hati inayoridhisha na kuhimiza Halmashauri zilizopata Hati Chafu kuchukua hatua za dhati kutunza hesabu zao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Fedha. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa 64 zimepata hati yenye mashaka kwa mwaka 2009/2010 ukilinganisha na Mamlaka za Serikali za Mitaa 55 kwa mwaka, 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Mikoa 18 ilipata hati safi ikilinganishwa na hati safi 12 kwa mwaka 2009/2010. Kwa mwaka 2009/2010, Mikoa iliyopata hati zenyeshaka imeongezeka kufikia saba ikilinganishwa na Mikoa miwili kwa mwaka 2008/2009. Aidha, Mkoaa mmoja umepata Hati Chafu (*Adverse Opinion*).

Mheshimiwa Spika, sababu za kushuka kwa kiwango cha utendaji wa Halmashauri kwenye hesabu za mwaka 2009/2010 ni pamoja na kuwasilisha taarifa za fedha kwa ajili ya ukaguzi zilizo chini ya kiwango kinachotakiwa kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu wa Sekta ya Umma (IPSAs). Vilevile, Halmashauri kutokusimamia na kutokufutilia kwa karibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo ilitekelezwa katika ngazi za Kata na Vijiji na Mitaa lakini pia kutozingatia uimarishaji wa Mfumo wa udhibiti wa ndani. Udhaifu huu ni changamoto ya kufanya kazi ili kuelewa kuna tatizo gani na ukubwa wake katika ngazi ya Mkoaa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kutafuta ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, taarifa sahihi zinasaidia kutoa maamuzi yaliyo sahihi. Ili kuwa na taarifa sahihi ni lazima uanze na takwimu sahihi. Moja ya mikakati ya OWM-TAMISEMI ni kuhakikisha upatikanaji wa takwimu zilizo sahihi na kwa wakati katika ngazi zote. Katika kufanikisha kazi hii, OWM-TAMISEMI ilianda kikao cha Watakwimu wa Mikoa yote na Watakwimu wote kutoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kujadili mikakati ya utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Takwimu. Mikakati hiyo ni pamoja na kuhakikisha kuwa takwimu zinapatikana kwa kutumia mifumo ya takwimu iliyowekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mfano Regista ya Kijiji na Mitaa.

Mheshimiwa Spika, OWM-TAMISEMI kwa sasa inatumia Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa katika kuboresha mawasiliano ya “*Internet*”. Mkongo huu unaendelezwa kupitia zoezi linalofanyika la kuziunganisha Mamlaka za Serikali za Mitaa 106 katika Mikoa 16, kazi ambayo inatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Agosti 2011. Aidha, Ofisi imefunga mitambo ya mawasiliano katika Ofisi za Dodoma na Dar es Salaam inayoiwezesha kufanya mikutano kwa utaratibu wa “*Video Conferencing*”. Kufungwa kwa mitambo hii kumesaidia Ofisi kupunguza ghamama za Viongozi kusafiri kwa ajili ya kukutana katika vikao vya dharura wengine wanapokuwa Dar es salaam kikazi. Matumizi haya ya teknolojia za kisasa yataongeza ufanisi wa kazi katika ngazi zote za OWM TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, tovuti ya OWM - TAMISEMI kwa sasa inao uwezo wa kuweka taarifa mbalimbali zikiwemo taarifa za fedha za Halmashauri zote. Ofisi yangu inaendelea kushirikiana na wataalam wa TEHAMA katika Sekretarieti za Mikoa ili kuhakikisha kuwa tovuti za Mikoa zinafanya kazi. Kwa kuona umuhimu wa TEHAMA muundo wa Sekretarieti za Mikoa umefanyiwa mabadiliko na kuanzisha kitengo kinachojitegemea na kusimamia uendelezaji wa TEHAMA katika Mkoa. Muundo wa Mkoa umepitishwa na unaanza kufanya kazi mwezi Julai 2011. Aidha, Kitengo cha Takwimu kimeanzishwa na kinaunganisha Mamlaka za Serikali za Mitaa zote katika kuhifadhi takwimu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi ilianza kutekelezwa mwaka 2007 na itamalizika mwaka 2011. Malengo makuu saba katika mpango huu ni pamoja na kuongeza uandikishaji wa wanafunzi wanaojiunga na Elimu ya Msingi; kuongeza uwezo wa utendaji kwa kujenga uwezo; kushughulikia masuala mtambuka; uboreshaji wa Mifumo na Taasisi; kufanya tafiti za masuala ya elimu; kuongeza ubora wa elimu na kufanya tathmini ya elimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, ruzuku ya uendeshaji (*Capitation*) iliyotengwa kwa Elimu ya Msingi ni shilingi bilioni 80. Fedha hizo ni kwa ajili ya uendeshaji na ununuzi wa vitabu vya kufundishia na kujifunzia. Aidha, kazi zilizofanyika katika kipindi hicho ni pamoja na kuandaa takwimu za tange za Maafisa Elimu wa Elimu ya msingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; kuandaa takwimu za wanafunzi waliomaliza Darasa la Saba mwaka 2010 na waliochaguliwa kuijunga na Sekondari kwa mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madeni ya Walimu taarifa zinaonesha kwamba yamelipwa mpaka mwaka 2008. Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wameelekezwa kutozalisha madeni mapya katika fedha za uhamisho na likizo kwa sababu fedha hizo zinatengwa katika bajeti zao. Aidha, kwa mara ya kwanza michezo ya Umoja wa Michezo na Taaluma Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) ilifanyika mwezi Desemba 2010 katika Shirika la Elimu Kibaha na ilihuisha Mikoa 11 kwa kuanzia. Wanamichezo 600 walishiriki wakiwemo wenye ulemavu. Kwa mwaka 2011/2012, Mikoa yote inategemewa kushiriki katika mashindano hayo.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2011/2012 ni pamoja na kuwezesha Watumishi wa Idara ya Elimu kutekeleza majukumu ya uhamisho wa Walimu wa shule za Msingi, uendeshaji wa UMITASHUMTA, kushiriki maandalizi ya mitaala, miongozo na usambazaji, kufuutilia utekelezaji wa Elimu ya Msingi, kuratibu mahitaji ya Walimu wa Shule za Msingi na ajira mpya.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (*MMES*) umekuwa ukitekelezwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kwa kipindi cha miaka mitano (5) ya Awamu ya Kwanza kuanzia mwaka 2004 hadi mwaka 2009. Awamu ya Pili ya Mpango huu inatekelezwa kuanzia mwaka 2010 hadi 2014. Lengo la programu ni kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza kwa kutatua changamoto zinazoikabili elimu ya sekondari kwa kuboresha utoaji wa vitabu na vifaa vya kufundishia na kuboresha kiwango cha elimu inayotolewa. Programu ina maeneo manne muhimu ambayo ni kuongeza uandikishaji wa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza, kuboresha kiwango cha elimu inayotolewa, kuleta usawa wa kijinsia kwa wanafunzi wanaojiunga na elimu ya sekondari na kusimamia maboresho ya usimamizi na mfumo wa shule. Katika kipindi hiki, Ofisi ya OWM - TAMISEMI inahusika katika uratibu, usimamizi na uendeshaji wa Programu.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekeliza katika mwaka 2010/2011 ni kuanda moduli za mafunzo ya Bodi za Shule na mafunzo yataanza Mwezi Julai 2011. Maafisa Elimu 21 katika Mikoa 21 na Maafisa Elimu wa Sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 132 na Wakuu wa Shule za Sekondari 903 walipatiwa mafunzo juu ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari. Walimu 52 wa Shule za Sekondari wamepatiwa mafunzo ya michezo yaliyoendeshwa na mtaalam wa michezo wa Shirika la Elimu Kibaha. Umoja wa Wakuu wa Shule za Sekondari ulifanya Mkutano Mkuu Mkoani Kilimanjaro. Vilevile, takwimu za watumishi, mali, vifaa na miundombinu ya shule ziliandaliwa.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizotekeliza ni kusimamia uendeshaji wa mitihani ya kuhitimu Elimu ya Sekondari katika ngazi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kushiriki katika kuratibu uendeshaji wa mashindano ya Umoja wa Michezo ya Shule za Sekondari Tanzania (UMISETA), kuratibu shughuli za Umoja wa Wakuu wa Shule za Sekondari, kuratibu uendeshaji wa Shule za Sekondari za Binafsi na Mashirika na Taasisi za Dini. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, ofisi yangu itaendelea kuratibu utekelezaji wa shughuli za *MMES* kulingana na malengo yaliyoainishwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Serikali ilitoa shilingi bilioni 2.1 kwa ajili ya ukarabati wa shule za sekondari 42 ambazo ni kongwe kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 38. Aidha, kwa mwaka 2010/2011 hadi mwezi Aprili zimetolewa shilingi bilioni 3.0 kwa ajili ya ukarabati wa shule za sekondari 60 ambazo ni kongwe. Fedha hizo zimegawiwa katika shule husika kulingana na hali halisi ya miundombinu iliyoko na baada ya kupata taarifa ya matumizi ya fedha zilizopokelewa awali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 jumla ya shilingi bilioni 23 zilitengwa kwa ajili ya uendeshaji kwa shule za sekondari. Hadi mwezi Aprili 2011 jumla ya shilingi bilioni 11.9 zimetolewa na kupelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya matumizi ya shule ikiwa ni pamoja na uendeshaji na ununuzi wa vitabu, kemikali za maabara na vifaa vya michezo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Wabia wa Maendeleo kutoka nchi mbalimbali na Benki ya Dunia imekuwa ikitoa fedha kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Mfumo wa Ruzuku isiyo ya Masharti (*LGDG*) kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo katika maeneo yao. Kupitia Mfumo huu, tathmini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa hufanyika kila mwaka na Ruzuku ya Maendeleo hupelekwa kwenye Mamlaka hizo kulingana na jinsi zilivyofuzu vigezo vilivyowekwa. Pia, inatolewa Ruzuku ya Kujenga Uwezo kwa ajili ya maeneo ambayo Mamlaka za Serikali za Mitaa zitakuwa zimebaini kuwa na upungufu. Mfumo huu ulianza rasmi mwezi Januari, 2005.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2010/2011 hadi kufikia mwezi Aprili 2011, jumla ya shilingi bilioni 91.7 zimepelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Mfumo huo. Aidha, zipo sekta tatu zilizojiunga kwenye Mfumo huo ambazo ni kilimo kwa ajili ya Ruzuku ya Maendeleo ya Kilimo ambapo hadi mwezi Aprili 2011 zimepelekwa jumla ya shilingi bilioni 43.7. Sekta ya Afya kwa ajili ya Ruzuku ya Maendeleo ya Afya, imepeleka jumla ya shilingi bilioni 17.4 na maji kwa ajili ya Ruzuku ya Maendeleo ya Maji Vijijini ilipanga kupeleka shilingi bilioni 63.2 lakini hadi sasa hazijatolewa.

Mheshimiwa Spika, vigezo vya tathmini, kiwango cha ruzuku na namna ya kupata ruzuku ya maendeleo na ya kujenga uwezo vimefanyiwa mapitio. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 tathmini ilifanyika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kutambua Halmashauri zinazozingatia vigezo vilivyowekwa pamoja na kuja kiasi ambacho kila Mamlaka itastahili kupata kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Tathmini hiyo imeonesha kuwa Halmashauri 110 zitapata asilimia 100 ya stahili yake ya ruzuku, Halmashauri mbili zitapata asilimia 80 ya ruzuku yake. Aidha, Halmashauri 16 zitapata asilimia 50 ya ruzuku yake na nne zitapata asilimia 25 ya ruzuku yake. Kupitia Mfumo huo, jumla ya shilingi bilioni 423.67 zimepangwa kupelekwa kwenye Halmashauri. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 208.3 ni ruzuku ya maendeleo isiyo na masharti, shilingi bilioni 42.1 ni ruzuku ya kilimo, shilingi bilioni 142.5 ni ruzuku ya kwa ajili ya sekta ya maji na shilingi bilioni 30.7 ni ruzuku kwa ajili ya afya.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kuzisaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa ulianza rasmi mwaka 2004/2005 na unaendelea kutekelezwa hapa nchini. Kazi zilizofanyika katika mwaka 2010/2011 ni pamoja na ukarabati wa ofisi ya mradi na kuboresha miundombinu ya Miji; kutoa mafunzo kwa watumishi 174 wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zinatekeleza mradi ambayo yalihusu usimamizi wa fedha katika kituo cha mafunzo cha Afrika Mashariki na Kusini - Arusha (ESAMI); Maafisa 24 walifundishwa kuhusu kuhamisha fedha na uandaaji wa taarifa za fedha; Maafisa 53 walipata mafunzo kuhusu taratibu za manunuzi na Maafisa 15 walipata mafunzo katika eneo la usimamizi na maendeleo ya watumishi. Mafunzo mengine ya usimamizi wa kandarasi yalitolewa kwa Maafisa 30; usimamizi wa mazingira ya jamii yalitolewa kwa Maafisa 22 na mafunzo ya ufuatiliaji na tathmini yalitolewa kwa Maafisa 30 na wote wako katika Halmashauri zinazotekeliza mradi.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu katika Miji Tanzania ni matokeo ya makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania, Benki ya Dunia na Serikali ya Denmark. Mradi huu umepangwa kufanyika kuanzia mwaka wa fedha 2010/2011 hadi 2014/2015. Madhumuni ya mradi ni kuziwezesha Mamlaka nane zinazohusika na utekelezaji wa mradi huu kuboresha miundombinu na utoaji huduma za jamii katika Miji. Mamlaka hizi ni Jiji la Mwanza, Tanga na Mbeya; Manispaa za Arusha; Dodoma; Kigoma Ujiji; Mtwara/Mikindani na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma. Mradi ulizinduliwa rasmi mwezi Oktoba 2010.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi 2011, jumla ya shilingi bilioni 5.4 zimepelekwa kwenye Mamlaka zinazotekeliza mradi kwa mchanganuo ufuatao; kiasi cha shilingi bilioni 2.1 ni kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi watakaoathirika kutokana na utekelezaji wa mradi na hadi kufikia mwezi Aprili 2011 jumla ya shilingi bilioni 1.8 zimetumika kulipa fidia sawa na asilimia 88 ya fedha iliyotolewa. Shilingi bilioni 3.3 zimetengwa kwa ajili ya kujenga uwezo wa Mamlaka hizo. Utekelezaji uko katika hatua mbalimbali za kupata Wazabuni kujenga miundombinu pamoja na ununuzi wa vitendea kazi na kutoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi. Kupitia mradi huu maandalizi pia yameanza kwa ajili ya kuanzisha mradi mpya wa kuboresha miundombinu ya Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Programu ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya kuendeleza usimamizi shirikishi wa misitu katika Halmashauri za Morogoro Vijijini, Mvomero, Kilosa na Kilombero Mkoani Morogoro; Iringa Vijijini, Kilolo, Mufindi, Njombe na Ludewa Mkoani Iringa; Mbeya Vijijini, Mbozi, Chunya Mbarali na Ileje Mkoani Mbeya na Lindi Vijijini, Liwale, Ruangwa na Nachingwea Mkoani Lindi. Hadi mwezi Aprili, 2011 kiasi cha shilingi milioni 633.8 zilikuwa zimetolewa. Aidha, kazi zilizofanyika ni kuratibu utoaji wa elimu kwa jamii kuhusu usimamizi shirikishi wa misitu; kuainisha miradi ya wajasiriamali ya hifadhi ya misitu shirikishi kwa mfano ufugaji wa nyuki, samaki na uoteshaji wa uyoga. Wajasiriamali 43,827 walipata elimu ya ujasiriamali wa hifadhi ya misitu na Miti 15,607,095 ilioteshwu katika maeneo ya mradi. Hekta 2,850 za misitu ya wananchi imehifadhiwa (*Community Based Forest Management*) katika

Halmashauri za Mbeya Vijijini, Ileje na Mufindi. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 kazi zitakazotekelawa ni pamoja na kuendelea kusimamia kazi za kuhifadhi maeneo ya misitu jamii, kuratibu na kuwezesha wananchi wajasiriamali kutambua miradi inayoendana na hifadhi ya misitu, kuotesha miti na kufanya ufuatiliaji na tathmini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Programu Shirikishi ya Usimamizi wa Ardhi Oevu ilipata shilingi milioni 435.3. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 127 ni kwa ajili ya uratibu na shilingi 208.3 zimepelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazotekeliza mradi. Mradi unatekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa za Longido na Ngorongoro katika Mkoa wa Arusha; Iringa Vijijini, Kilolo, Mufindi, Makete, Njombe na Ludewa katika Mkoa wa Iringa; Mbarali, Chunya, Mbozi na Mbeya Vijijini katika Mkoa wa Mbeya. Kazi zilizotekelawa katika Mamlaka hizo ni pamoja na kufanya mapitio katika mwongozo wa usimamizi wa fedha na utekelezaji wa programu na kuandaa mafunzo kuhusu mwongozo kwa watendaji wa Mamlaka. Katika mwaka 2011/2012 programu hii itaendelea kutekelezwa katika Mikoa ya Arusha, Mbeya na Iringa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilitengewa jumla ya shilingi bilioni 104 kwa ajili ya utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Hadi mwezi Machi, 2011 Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepokea jumla ya shilingi bilioni 44 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya mazao, mifugo na uvuvi na shilingi bilioni 31 kwa ajili ya Mfuko maalum wa uendelezaji kilimo cha umwagiliaji wilayani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetengewa jumla ya shilingi bilioni 109.17 kwa ajili ya utekelezaji wa Mipango ya Kilimo ya Wilaya. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 65.3 ni kwa ajili ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na jumla ya shilingi bilioni 43.8 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta ya Ngozi na Viwanda vya Ngozi ulibuniwa na wadau wa sekta ya ngozi kwa kushirikiana na Serikali. Lengo ni kufufua na kuendeleza sekta ya ngozi na viwanda vya ngozi ili zipatikane ngozi zenye ubora kwa ajili ya viwanda kutengeneza ngozi na bidhaa zake. Mkakati unatekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 65 katika Mikoa 17.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, shilingi bilioni 1.2 zimepelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 65 na kila moja imepata shilingi milioni 19.8. Aidha, shilingi milioni 51 zimepelekwa katika Sekretarieti za Mikoa 17 kwa ajili ya kazi za uratibu na kila Mkoa umepata shilingi milioni tatu. Kazi zilizofanyika ni pamoja na uhamasishaji kwa wafugaji 6,433; wachinjaji na wachunaji 2,225; wawambaji na wachambuzi wa madaraja ya ngozi 1,229; wasindikaji 313; wafanyabiashara 1,067; Maafisa Ugani 1,772; na Madiwani na viongozi wengine 1,816. Uhamasishaji uliofanyika ulilenga kuleta ufahamu juu ya umuhimu wa zao la ngozi na umechangia katika ongezeko la ubora na biashara ya zao la ngozi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka miwili (2008/2009-2009/2010), Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi umeweza kupeleka kiasi cha shilingi bilioni 58 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zinatumika katika ujenzi wa majengo mapya katika hospitali sita (6) za Wilaya na kufanya kazi mbalimbali za ukarabati katika Hospitali 44 za Wilaya. Pia vituo vya afya 183 vimefanyiwa ukarabati na 41 vipya vinajengwa. Aidha, jumla ya zahanati 574 zimekarabatiwa na 282 zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Ili kuhakikisha kuwa watumishi wa Afya wanapata makazi bora, kupitia Mpango huo nyumba za watumishi wa afya 341 zimefanyiwa ukarabati na kuanza ujenzi wa nyumba mpya 492.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, kiasi cha shilingi bilioni 30.3 zilitengwa na hadi kufikia mwezi Aprili 2011 kiasi cha shilingi bilioni 17.4 zimetolewa na kupelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kugharamia kazi mbalimbali za ujenzi, ukarabati na upanuzi wa vituo vya kutolea huduma za afya. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 zimetengwa fedha kiasi cha shilingi bilioni 30.7 kwa ajili ya kuendelea kutekeleza kazi za ujenzi na ukarabati kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI. Chuo cha Serikali za Mitaa – Hombolo kilianzishwa kwa Sheria ya Bunge, Sura 396 ya mwaka 1994 iliyorejewa mwaka 2002. Madhumuni ya kuanzishwa kwake ni pamoja na kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ya taaluma, ujuzi, stadi kazi na mbinu za uendeshaji wa Serikali za Mitaa kwa Viongozi na Watumishi walioko katika ngazi mbalimbali za Serikali za Mitaa; kutoa mafunzo juu ya mabadiliko yanayohusu Serikali za Mitaa kulingana na Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, idadi ya wanachuo wanaotoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mpango wa mafunzo ya muda mrefu imeongezeka kutoka wanafunzi 41 mwaka 2007/2008 na kufikia wanafunzi 172 mwaka 2010/2011. Hata hivyo, uwiano wao ni mdogo (wastani wa asilimia 18 kila mwaka) ukilinganisha na idadi ya wanafunzi wote wanaojiunga na Chuo amba ni 1,389. Ni mategemeo ya Serikali kwamba Halmashauri zitaendelea kuwapeleka watumishi wake waliyo katika ngazi za msingi kwenda Chuo cha Serikali za Mitaa kuijendeleza katika stadi za kazi ili kuongeza tija katika nafasi walizo nazo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa masomo 2011/2012, Chuo kimepanga kudahili wanafunzi wapya 700. Idadi hiyo itafanya wanafunzi katika Chuo kufikia 1,800 kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada kwa fani za Utawala, Usimamizi wa Fedha, Ustawi wa Jamii na Usimamizi wa raslimali watu. Vilevile, Chuo kitaendelea na uandaaji wa fani nyingine mbalimbali zinazohusiana na Serikali za Mitaa kwa ngazi za Astashahada, stashahada na Shahada.

Mheshimiwa Spika, Chuo kimetoa mafunzo mafupi yanayohusiana na masuala ya kiutumishi kwa watumishi wa Halmashauri ya Misenyi, mafunzo ya uongozi ya Wenyeviti wa Vijiji 100 vya Halmashauri ya Mbinga na mafunzo ya taratibu za manunuzi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Maafisa Elimu 49 wa Shule za Msingi na Sekondari kutoka Halmashauri mbalimbali za Tanzania. Mafunzo ya aina hiyo

yataendelea kutolewa kwa Watendaji ngazi ya Vijiji, Mitaa, Kata, Madiwani, Maafisa Tarafa na Watendaji mbalimbali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mafunzo yatakayofundishwa yatazingatia mahitaji ya kila kada na kwa ngazi inayohusika. Napenda kutoa agizo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zote nchini kuweka gharama za mafunzo ya aina hiyo katika bajeti zao kila mwaka ili watumishi waweze kupata mafunzo kwa faida ya Mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ikama ya watumishi, Chuo kina watumishi wanataluma 25 na waendeshaji 44, idadi inayofanya watumishi wote kuwa 69 katika mwaka 2010/2011. Idadi hii ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji halisi ya watumishi kutokana na kukua kwa Chuo. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 kazi za kufanya tafiti kuhusu vyanzo vya mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaendelea. Aidha, Chuo kimepanga kuendelea na mipango ya kuboresha miundombinu ya Chuo kwa kutunza majengo yaliyokamilika, kuanzisha mchakato wa ujenzi wa kituo cha afya, nyumba za watumishi, kumbi za semina na makongamano, kuweka samani katika majengo mapya na kufidia sehemu ya eneo jipya la Chuo lenye ukubwa wa ekari 750.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa una majukumu makuu matatu kama yalivyoainishwa katika Sheria Na. 9 ya mwaka 2006. Majukumu hayo ni pamoja na kuandikisha na kukusanya michango toka kwa waajiri na wanachama; kutunza michango ya wanachama katika hali ya usalama na kuiwekeza katika vitega uchumi mbalimbali na kuwalipa wanachama mafao na kuzingatia taratibu bora za ulipaji wa mafao hayo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa ulipanga kuandikisha wanachama 6,029 ili kufikisha jumla ya wanachama 78,931 ifikapo Juni 2011. Hadi kufikia mwezi Machi 2011 Mfuko umeweza kuandikisha wanachama 5,319 ikiwa ni asilimia 88. Vilevile, Mfuko umekusanya shilingi bilioni 50.7 kutokana na michango ya wanachama sawa na asilimia 78 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 66. Kwa upande wa uwekezaji, Mfuko umewekeza jumla ya shilingi bilioni 116.5 sawa na asilimia 74 ya lengo la kuwekeza shilingi bilioni 157.0 kwa mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi 2011 Mfuko ulikuwa umepata kiasi cha shilingi bilioni 16.2 sawa na asilimia 61 ya lengo la kupata shilingi bilioni 26.6. Aidha, katika kipindi hicho Mfuko umeongeza mafao mapya mawili ya uzazi na msaada wa mazishi hivyo kufanya jumla ya mafao yanayotolewa na Mfuko kufikia sita. Hadi kufikia mwezi Juni 30, 2011 Mfuko unatarajia kutumia shilingi bilioni 24 kulipa mafao kwa wanachama wake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Mfuko utaendelea kuimarisha ofisi ndogo zilizofunguliwa katika Mikoa mbalimbali nchini. Mfuko utaanza malipo ya mafao mapya katika ofisi za kanda na inategemewa kuwa idadi ya wanachama itaongezeka kwa asilimia 13 kutoka wanachama 78,931 ifikapo mwezi Juni 2011 hadi 89,126 ifikapo mwezi Juni 2012. Aidha, Mfuko unategemea kuongeza michango ya wanachama kwa

asilimia 28 kutoka shilingi bilioni 66 mpaka shilingi bilioni 84.9 ifikapo mwezi Juni 2012.

Mheshimiwa Spika, Mfuko unayo sehemu ya uwekezaji ambapo inategemewa kwamba mapato yatokanayo na uwekezaji yataongezeka kwa asilimia 31 kutoka shilingi bilioni 26.6 mpaka shilingi bilioni 34.8 kufikia mwezi Juni 2012. Miradi ya ubia ya ujenzi wa kituo cha kisasa cha mabasi eneo la Msamvu katika Manispaa ya Morogoro, ujenzi wa kitega uchumi cha mabasi cha kisasa katika Jiji la Mwanza na kituo cha kuegesha malori eneo la Mbezi Luis katika Manispaa ya Kinondoni itaendelezwa.

Mheshimiwa Spika, Mfuko unatarajia kuanza ujenzi wa jengo la Makao Makuu yake hapa mjini Dodoma. Jengo hilo litakuwa pia kitega uchumi chenye ofisi zikiwemo za Wizara mbalimbali Serikalini. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Mfuko pia umepanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 205 kutoka katika vyanzo vyake vyaa mapato na kutumia kiasi hicho katika shughuli mbalimbali za Mfuko.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Elimu Kibaha lina jukumu kubwa la kupambana na maadui wa maendeleo ambao ni Ujinga, Umashini na Maradhi. Katika kupambana na adui Ujinga kwa mwaka 2010/2011 wanafunzi 2,761 walipatiwa elimu ya malezi bora na huduma ya maktaba na mtandao ilitolewa kwa wadau 47,210. Aidha, wanafunzi 806 walihitim masomo yao katika Asasi za Shirika. Shule za Shirika zimekuwa zikifanya vizuri katika mitihani ya kitaifa mwaka hadi mwaka. Kwa mfano mwaka 2011 Shule ya Sekondari Kibaha imekuwa ya nne kitaifa katika matokeo ya kidato cha sita na kuwa na mwanafunzi wa kwanza bora kitaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kupambana na adui umaskini katika kipindi hicho yametolewa mafunzo katika fani mbalimbali, kuitia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha. Fani hizo ni pamoja na kilimo na mifugo, ujenzi na useremala, umeme na magari, upishi na ushonaji, uungaji na uundaji vyuma pamoja na udereva ambapo wanachuo 234 walipatiwa mafunzo hayo. Pia ilitolewa elimu ya nadharia na vitendo juu ya ufugaji bora wa kuku. Shirika liliwauzia wananchi vifaranga wa nyama 62,655 na vifaranga wa mayai 27,696. Aidha, wataalamu wa ugani wa Shirika waliwatembalea wafugaji 85 ili kutoa ushauri juu ya ufugaji bora wa kuku. Kwa upande wa shamba la ng'ombe wa maziwa pamoja na kuwauzia wananchi maziwa kwa ajili ya lishe bora, yalitolewa mafunzo ya nadharia na vitendo kuhusu ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa kwa wakulima wadogowadogo. Aidha, katika uboreshaji wa ng'ombe wa kienyeji, Shirika liliendelea kusimamia na kutoa elimu ya ufugaji wa ng'ombe bora wa maziwa katika Mitaa ya jirani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa adui maradhi, wagonjwa 285,000 wamehudumiwa katika kipindi hicho. Shirika lilikuwa na lengo la kutoa elimu ya utabibu kwa wanachuo 120 ambapo wanachuo 115 walipatiwa mafunzo hayo na 40 kati yao walifanikiwa kuhitim. Pia, Shirika liliweza kuhudumia wahanga 1,673 wa ajali za barabarani katika Hospitali ya Tumbi. Katika upanuzi wa hospitali ya Tumbi, ujenzi wa awamu ya kwanza unaendelea na umefikia asilimia 99. Utunzaji wa mazingira uliendelea kutekelezwa ikiwa ni pamoja na upandaji wa miti na jumla ya miti 4,684

ilipandwa na kutunzwa. Kwa mwaka 2011/2012, Shirika limepanga kuendelea na utekelezaji wa Mpango kabambe wa matumizi ya ardhi ya Shirika 2006 – 2026 ili kuongeza vyanzo vya mapato ya ndani. Vilevile, kuendelea na upanuzi wa Hospitali ya Tumbi na malengo mengine makuu ya Shirika.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ambayo ilianzishwa kwa madhumuni ya kutoa mikopo yenyenye masharti nafuu kwenye Halmashauri, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuelekeza nguvu zaidi katika kukusanya Michango ya Akiba na kufuatilia marejesho ya mikopo kama njia mojawapo ya kuongeza uwezo wa Bodi kifedha. Hivyo, hadi tarehe 30 Aprili, 2011, Bodi imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 1.1 kati ya shilingi bilioni 1.4 zilizokadiriwa kukusanya kutoka kwenye Halmashauri sawa na asilimia 77.1 ya lengo. Michango yote imefikia jumla ya shilingi bilioni 4.49 kati ya shilingi bilioni 5.54 zinazopaswa kuchangwa na Halmashauri. Kwa upande wa marejesho ya mikopo pamoja na riba, jumla ya shilingi milioni 545 zimerejeshwa kati ya shilingi milioni 660 zilizokadiriwa kurejeshwa katika mwaka 2010/2011 sawa na asilimia 82.6 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, mikopo inayotolewa inalenga kuongeza mapato ya Halmashauri, kuchocha shughuli za kiuchumi na kuongeza ajira. Katika kipindi hicho, Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero ilipata mkopo kwa ajili ya upimaji wa viwanja 850 na kati ya hivyo viwanja 600 vimeuzwa kwa wananchi kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara/Mikindani ilipata mkopo kwa ajili ya ujenzi wa Soko la Samaki. Ujenzi unaendelea na umefikia hatua ya kupaua. Aidha, ujenzi wa Hostel ya Kituo cha Mikutano cha Benjamin Mkapa cha Jiji la Mbeya unaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imepanga kuendeleza shughuli za utoaji mikopo kwenye Halmashauri. Lengo ni kuhakikisha kuwa mtaji wa kuendeshea huduma ya mikopo unaongezeka na Halmashauri nyingi zaidi zinanufaika na huduma hii. Mtazamo kwa sasa ni kuwa na taasisi ya fedha iliyoboreshwa ili kuongeza ufanisi katika huduma ya utoaji mikopo.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usafiri wa Haraka Dar es Salaam (*DART*) umejikita katika utekelezaji wa malengo makuu matatu ambayo ni kusimamia utekelezaji na uendeshaji wa Mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es salaam; kuweka mpangilio makini wa matumizi ya barabara kuu na ndogo kwa watumiaji wote ili kupunguza msongamano; na kuhakikisha kuwepo kwa menejimenti ya Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka yenyenye kuleta tija na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka ni sehemu ya mkakati wa muda mrefu na utatumia mabasi makubwa kwenye njia maalum kutoka pembezoni na kuingia katikati ya Jiji la Dar es Salaam na hii itasaidia watu kutokwenda na magari yao binafsi kwa sababu takwimu zinaonesha watu wanatumia magari yao binafsi bila kubeba watu wengine na hivyo kila siku katika Jiji la Dar es Salaam kuna viti 700,000 ambavyo vinakuwa *empty*, kwenye magari binafsi. Hadi sasa usanifu wa kina wa mradi Awamu ya Kwanza utakaowezesha kujengwa kwa miundombinu inayokidhi watumiaji wote wa barabara na matumizi ya mabasi yenyenye ujazo mkubwa umekamilika.

Mheshimiwa Spika, gharama za ujenzi wa Mfumo huu Awamu ya Kwanza ni dola za Kimarekeni 169.7. Benki ya Dunia itatoa dola za Kimarekani milioni 143.7 na Sekta Binafsi (*Public Private Partnership*) itahusika na ununuzi wa mabasi, uendeshaji, ukusanyaji wa nauli na menejimenti ya fedha. Aidha, Awamu ya Kwanza itahusisha ujenzi wa barabara zenyenjia maalum za mabasi, njia za baiskeli na za waenda kwa miguu zenyenjia jumla ya urefu wa kilometra 20.9 zikijumuisha vituo vya mabasi ishirini na tisa (29) na vituo vikuu vya mabasi vitano (5), karakana za mabasi mbili (2) na vituo mlishe (*feeder stations*) sita (6).

Mheshimiwa Spika, uzinduzi wa ujenzi wa miundombinu ya Awamu ya Kwanza ilioainishwa hapo juu ulifanywa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 10 Agosti 2010 katika kituo cha Mabasi Kivukoni. Hadi kufikia mwezi Aprili 2011, kazi za ujenzi wa Mfumo wa *DART* zilikwishaanza katika kituo kikuu cha mabasi Kivukoni. Kazi ya uhamishaji wa nguzo za umeme, ujenzi wa vituo mlishe katika maeneo ya Mwinyijuma, Shekilango, Kinondoni A na Magomeni pia imeanza. Hata hivyo, bado ipo changamoto ya migogoro ya upatikanaji wa baadhi ya maeneo ili ujenzi uanze.

Mheshimiwa Spika, taratibu za upatikanaji wa mkopo wa Benki ya Dunia wa dola za Kimarekani milioni 197.1 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu kuitia Awamu ya Pili ya mradi wa *Central Transport Corridor* (CTCP2), zimekamilika. Katika mwaka 2011/2012 Wakala utaendelea kutekeleza kazi zake na kuhakikisha kuwa mradi unatekelezwa kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Naibu Waziri Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, anayeshughulikia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Majaliwa Kasimu Majaliwa, anayeshughulikia Elimu chini ya OWM-TAMISEMI, Katibu Mkuu, OWM -TAMISEMI Bw. Hussein Athuman Kattanga, Naibu Makatibu wakuu Bw. Eliakim Chacha Maswi na Bw. Jumanne Abdallah Sagini na Wakurugenzi wa OWM – TAMISEMI.

Vilevile, napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru Wakuu wa Mikoa wote, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wote wa Mikoa na Wilaya, Wakurugezi wa Halmashauri na Waheshimiwa Madiwani wote katika nchi ambao tunashirikiana kufanya nao kazi kwa ufanisi. Nawapa pole Waheshimiwa Madiwani kwa kuambiwa kwamba wao eti ni mbumbumbu. Nadhani gazeti lililoandika hivyo linapaswa kuwaomba radhi Madiwani kwa sababu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI ni mwanasiasa mkongwe, mtu makini, hata akiwa usingizini hawezo akawaita Madiwani mbumbumbu. Kwa hiyo, napenda kuwapa pole Madiwani kwa usumbufu walioupata, tulichosema tunaanda mafunzo kwa Waheshimiwa Madiwani ya muda wa siku saba kuwaimarisha ili waweze kusimamia vizuri fedha za Serikali za Mitaa. Ndugu zanguni, ukienda kwenye mafunzo sio kwamba wewe ni mbumbumbu. Mawaziri wa Jakaya Mrisho Kikwete karibu wote wana Digrii lakini tumekaa hapa muda wa siku saba tunasoma, ndicho tunachotaka tufanye kwa Waheshimiwa Madiwani. Kwa hiyo, naomba hilo lieleweke hivyo.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru watumishi wote waliopo katika Halmashauri ambao wanafanya kazi katika Wizara yetu, tunafanya kazi nao kwa ushirikiano. Napenda kuwashukuru kwa ushirikiano waliouonyesha kwangu tangu nimeteuliwa kushika nafasi hii kwani wamefanya majukumu yangu kuwa mepesi na sisi katika TAMISEMI tunaahidi kwamba tumeamua kufanya kazi kwa juhudhi na maarifa kwa maendeleo ya Watanzania wote na tutafanya kazi kwa ujasiri bila upendeleo, woga, wala ubaguzi wa aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya kipekee kabisa, napenda nimshukuru mke wangu mpandwa Anna Ernestina Mkuchika, nashukuru leo umempungeza hapa. Niwashukuru watoto wangu watano na wajukuu wangu Evelyne na Ethan kwa uvumilivu mkubwa wa kukaa peke yao hawamuoni baba, hawamuoni babu, hata muda wa kucheza na wajukuu unapungua, lakini nimewaelimisha na wameelewa kwamba nchi imenituma nifanye kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu unatakiwa uhitimishe hotuba yako kwa kuomba fedha.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii sasa kuwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri, kwa ushirikiano walionipa tangu wateuliwe. Aidha, nawashukuru Wafanyakazi wote wa Serikali na Taasisi zake chini ya Uongozi wa Katibu Mkuu Kiongozi, Bwana Phillemon Lutangilo Luhanjo kwa kukamilisha Bajeti ya Serikali ya mwaka 2011/2012 lakini nawashukuru sana Watanzania wote kwa ushirikiano katika ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kuwashukuru Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Mbunge wa Ismani, Waziri wa Nchi (Sera, Uratibu na Bunge); Mheshimiwa Dr. Mary Michael Nagu, Mbunge wa Hanang, Waziri wa Nchi (Uwezeshaji na Uwekezaji); Mheshimiwa Kapt. (Mstaafu) George Huruma Mkuchika, Mbunge wa Newala, Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Mheshimiwa Aggrey Joshua Mwanri, Mbunge wa Siha, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mbunge wa Ruangwa, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Elimu), kwa msaada mkubwa na ushirikiano walionipa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Shukrani za pekee kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa jitihada walizoonesha katika kipindi hiki. Nawashukuru vilevile Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, chini ya Uongozi wa Makatibu Wakuu, Bwana Peniel Moses Lyimo na Bwana Hussein Athuman Kattanga na Naibu Makatibu Wakuu, Bwana Charles Amos Pallangyo, Bwana Jumanne Abdallah Sagini na Bwana Eliakim Chacha Maswi, kwa ushauri wao wa kitaalam ambao wamenipa mimi na Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi katika kipindi hiki.

Nawashukuru kwa kukamilisha maandalizi yote ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, nchi yetu imepata misaada na mikopo kutoka kwa Wahisani wetu mbalimbali. Misaada na mikopo hiyo imetoka kwa nchi rafiki, nchi fadhili, Taasisi za Fedha Duniani, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Mifuko Mbalimbali ya Fedha Duniani, Madhehebu ya Dini na Mashirika Yasiyo ya Serikali. Misaada na mikopo hiyo imechangia sana katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Napenda kuwashukuru wote kwa dhati na kuwahakikisha kuwa Watanzania tunathamini misaada na mikopo walijotupatia na tutaendelea kushirikiana nao katika harakati za kuleta maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wapiga Kura wangu wa Jimbo la Katavi kwa imani na heshima kubwa walijonipa ya kunikubali na kunichagua kuwa Mbunge wao kwa vipindi vitatu vyta uchaguzi mfululizo na kukataa hadaa nyingine ambazo zimejitokeza kutoka kwa wale wasionitakia mema. Aidha, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani kubwa kwangu na hivyo kunitfea tena kuwa Waziri Mkuu kwa kipindi kingine. Nawashukuru sana nyinyi Waheshimiwa Wabunge wote mliokubali na kuthibitisha Uteuzi huo wa Rais ambao umeniwezesha kuwatumikia Watanzania katika wadhifa huu. Nawashukuru Viongozi wenzangu wote wa Kitaifa na wa ngazi nyingine zote, kwa ushirikiano mkubwa naoupati kutoka kwao ambao umeniwezesha kutekeleza jukumu hili kubwa la kusimamia utendaji wa Serikali katika sekta zote na kuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Kwenu nyinyi wote nasema ahsanteni sana! (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Bunge kwa Mwaka 2011/2012. Kwa mwaka 2011/2012, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 197,166,606,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 65,790,646,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 131,375,960,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2011/2012, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Asasi zake inaombewa jumla ya Shilingi 112,228,084,000. Kati ya hizo, Shilingi 42,735,411,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 69,492,673,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinaombewa jumla ya Shilingi 158,902,057,000. Kati ya hizo, Shilingi 123,956,300,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 34,945,757,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Aidha, Halmashauri zote zinaombewa jumla ya Shilingi 2,937,902,541,000. Kati ya hizo Shilingi 2,198,076,492,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 739,826,049,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano inaombewa jumla ya Shilingi 80,798,694,000 kwa ajili ya Mfuko wa Bunge ambapo Shilingi 77,798,694,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 3,000,000,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, kwa muhtasari naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2011/2012, yenye jumla ya Shilingi 80,798,694,000 kwa ajili ya Mfuko wa Bunge na jumla ya Shilingi 3,406,199,288,000 kwa ajili ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Halmashauri ikiwa ni Matumizi ya Kawaida na Fedha za Maendeleo za Ndani na Nje kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa kina Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, nimekumbushwa hapa kwamba ni vizuri vilevile kuwashukuru sana Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala, nawashukuruni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**SPIKA:** Wakati nawatambulisha wageni asubuhi kulikuwa na Wanafunzi 32 na Walimu 30 wa Shule ya Sekondari ya Kitwiru, Iringa. Naomba Walimu na Wanafunzi wasimame hapo walipo wawapungie mkono Waheshimiwa, ahsante sana. Tunawashukuru sana Wanyalukolo, karibuni na msome vizuri. (*Makofi*)

Halafu nafikiri wageni wetu wengine tutawatambulisha vizuri jioni kwa sababu sasa hivi mimi sina majina yao, lakini wako hapo, najua ni Wakuu wa Mikoa mbalimbali waliokuja kusikiliza hotuba ya Wizara yao. Tutawatambulisha jioni.

Tuna tangazo lingine hapa kutoka kwa Bunge *Sport Club* kwamba Kamati Tendaji ya Bunge *Sports Club* ikutane mara baada ya kuahirisha kikao cha Bunge mchana huu, ilikuwa 7.00 nadhani ni sasa katika ukumbi wa Msekwa C, kwa hiyo mnaweza kwenda kule.

Tukiingia jioni, nitawaita Wenyeviti wa Kamati zilizohusika na hotuba hii ya Waziri Mkuu. Yuko Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Fedha. Hawa kila mmoja atatumia nusu saa watakuja Kambi ya Upinzani wao kwa sababu anayewakilisha ni mmoja basi atatumia saa moja kwa maana hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuru kwa kukubali kuongeza muda huu, sasa nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa 11.00.

(*Saa 7.48 Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, habari za jioni. Tunaendelea na Kikao chetu kwa jioni ya leo, naomba nikae ili nimwite Katibu aweze kutuongoza, Katibu!

#### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Serikali kwa Mwaka 2011/2012 - Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea Hotuba ya Bajeti kutoka kwa Waziri Mkuu na Ofisi zake, sasa nitawaita Wenyeverti wa Kamati waliofanyakazi ya kuchambua mapendekezo hayo na nianza na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana.

**MHE. PINDI H. CHANA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2010/2011 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni 99 (7) na 114 (11), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Utekelezaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012, kwa Fungu 25 – Waziri Mkuu, Fungu 27 – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 42 – Mfuko wa Bunge, Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Fungu 91 – Tume ya Kuratibu Udhhibit wa Dawa za Kulevyta na Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawasilisha maoni ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, kwa Fungu 56 – Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na Mafungu 70 – 89 na 95 kwa ajili ya Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuilettea Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kazi ya kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012, tarehe 27/5/2011, Kamati ilikutana Dar es Salaam na kupokea

taarifa ya utekelezaji ya mwaka 2010/2011 pamoja na maelezo ya bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge.

Kimsingi Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge na Taasisi zake yaliwasilishwa mbele ya Kamati na Waziri wa Nchi, Mheshimiwa William Lukuvi, Pamoja na mambo mengine, Kamati ilielezwa kuhusu makusanyo ya maduhuli hadi kufikia mwezi Aprili, 2011 na matumizi ya kawaida na Maendeleo kwa Mafungu yote. Aidha, Kamati ilielezwa changamoto zilizoikabili Ofisi hii na Taasisi zake katika utekelezaji wa majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuchambua Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka 2010/2011, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ya utekelezaji na utendaji kazi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ushauri wa Kamati ulizingatiwa na kufanyiwa kazi kama ifuatavyo:-

(i) Uhamiaji Makao Makuu Dodoma. Serikali imetoa ahadi kuwa kuanzia Mwaka 2011, majengo mapya ya Wizara za Serikali yajengwe Dodoma badala ya Dar es Salaam. Aidha, Serikali imetengeneza eneo jipya (*Master Plan*) ambapo yatajengwa majengo ya Wizara, Ofisi za Mabalozi na taasisi nyingie litakalojulikana kama Mji wa Serikali. Vilevile, Sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (*CDA*) tayari imepitiwa upya na mchakato wa majadiliano na wadau mbambali kuhusu marekebisho ya sheria hiyo kupitia ofisi ya Waziri Mkuu unaendelea. (*Makofit*)

(ii) Idara ya Maafa kuwa Taasisi ya Umma au Mamlaka inayojitegemea. Kamati imejulishwa kuwa Serikali imeendelea na mchakato wa kuibadilisha Idara hii kuwa Taasisi inayojitegemea na Waraka husika umeandaliwa kujadiliwa na Baraza la Mawaziri.

(iii) Serikali kutoa maelekezo kwa Taasisi za Umma ili zilazimike kupeleka kazi kwa Mpigachapa Mkuu wa Serikali. Kamati imefahamishwa kuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu ametoa maelekezo kwa Maafisa Masuuli wote waanze kutumia Idara hiyo kuanzia tarehe 1 Julai, 2011 hasa baada ya kupata mitambo ya kisasa.

(iv) Msajili wa Vyama vya Siasa kusimamia utoaji wa elimu kwa wadau kuhusu Sheria ya Gharama za Uchaguzi na kuitafsiri kwa Kiswahili na kusambazwa kwa wananchi. Kuhusu suala hili, Kamati imefahamishwa kuwa Ofisi ya Msajili kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, imeendesha mafunzo kwa wadau mbalimbali na kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutafsiri Sheria hiyo.

(v) Ofisi ya Bunge kutekeleza Mpango Mkakati wa mwaka wa fedha 2009 hatua kwa hatua na kuimarisha vitendea kazi, TEKNOHAMA na miundombinu ya kiutendaji. Kamati imejulishwa kuwa Ofisi ya Bunge imetekeliza Mpango huo kuimarisha uwezo wa Sekretarieti kuhudumia Wabunge ipasavyo, kuwajengea uwezo

Wabunge na kuwezesha mawasiliano kati ya Bunge na wadau kwa kutumia semina, nyaraka, redio na televisheni (*Deepening Democracy*).

(vi) Tume ya Taifa ya Uchaguzi kujipanga vizuri katika kusimamia uchaguzi ili uwe wa haki, huru, amani na utulivu na changamoto zilitojitokeza wakati wa Uchaguzi Mkuu 2005 zifanyiwe kazi. Kamati imepokea taarifa kuwa Tume imeendesha Uchaguzi Mkuu 2010 kwa ufanisi kwa kutumia teknolojia ya kisasa na kwa mafanikio yaliyotarajiwa. Aidha, Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lilipelekwa siku nne kabla ya siku ya uchaguzi na Sheria ya Uchaguzi ilifanyiwa marekebisho ili kuondoa matatizo yaliyojitokeza kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005.

(vii) Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevyta iongeze kasi katika utaratibu wake wa kutoa elimu kuhusu athari za madawa ya kulevyta na iongezewe bajeti ili kutekeleza majukumu yake. Kamati imejulishwa kuwa Tume imetoea elimu kuitia vyombo vya habari kama vile redio na televisheni na kuandaa mpango wa kufikia watumiaji wa dawa za kulevyta (*Outreach Programme*). Aidha, Tume imeongezewa bajeti kutoka Sh.892,510,000/= hadi Sh.1,000,000,000/= na Sh.1,439,597,320/= kama fedha za maendeleo.

(viii) Tume ya Kudhibiti UKIMWI kutengewa fedha za kutosha ili kukabiliana na kukua kwa athari ya virusi vya UKIMWI na mtiririko wa fedha kutoka Hazina kwenda Tume uende kama ulivyokusudiwa. Kamati imepokea taarifa kuwa Serikali itaanzisha Mfuko wa UKIMWI kama njia mojawapo ya kukusanya rasilimali endelevu. Aidha, utaratibu wa kufuutilia rasilimali zilizopo umeimarishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na utekelezaji mzuri wa majukumu yake kwa kujielekeza kwenye vipaumbele kwa mwaka 2010/2011, Ofisi ya Waziri Mkuu inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na:-

(i) Mwitikio mdogo wa Wapiga Kura katika kuhakiki majina yao na Vituo walivyopangiwa kupiga Kura pamoja na kutojitokeza siku ya kupiga kura;

(ii) Kuongezeka kwa athari za dawa za kulevyta na mabadiliko ya mbinu zinazotumiwa na wahalifu wa biashara haramu ya dawa za kulevyta;

(iii) Uhaba na kuchelewa kupatikana kwa fedha za kuendesha Mikutano ya Bunge na shughuli mbalimbali za Ofisi ambako kumeathiri utekelezaji wa majukumu na kupunguza ufanisi wa kazi; na

(iv) Uelewa mdogo wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Na.6 ya mwaka 2010 kwa wagombea, wananchi pamoja na Vyama vya Siasa kutozingatia maadili ya uchaguzi licha ya kuweka saini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati na kwa kuzingatia dhima, azima ya Serikali na majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Kamati inatoa maoni na ushauri kwa Ofisi hii na Taasisi zake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 25 - Waziri Mkuu na Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu, Kamati inapendekeza yafuatayo:-

(i) Kamati inapenda kueleza masikitiko yake kuhusu ucheleweshwaji wa Vitabu vya Bajeti uliojitokeza na hivyo kushauri kwamba utaratibu uzingatiwe ili vitabu hivyo viwasilishwe Ofisi ya Bunge kwa wakati na kwa mujibu wa Kanuni ya 96(1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajumbe wa Kamati mbalimbali za Kudumu watakubaliana nami jinsi vitabu hivyo vilivyochelewa na kuwanyima haki ya msingi wawakilishi wa wananchi kupata fursa ya kutosha kuitia bajeti za Wizara kwa kina ili kuishauri Serikali. Pamoja na uvumilivu na busara zilizooneshwa na Kamati, Kamati yangu inashauri kuwa kitendo hiki kisirudiwe tena na kama kuna tatizo la msingi ambalo lipo nje ya uwezo wa Serikali, Kamati inashauri kuwa ni vema Ofisi ya Bunge ijulishwe mapema kwani kwa kutofanya hivyo kunavuruga hata ratiba za Kamati. (*Makofi*)

(ii) Watendaji wa ngazi za Mikoa na Wilaya watekeleze majukumu yao kwa ufanisi ili kupunguza safari nyingi za viongozi wa ngazi za juu hasa Waziri Mkuu kwenda kufuatilia utekelezaji wa shughuli mbalimbali ambazo zingeweza kutekelezwa na Viongozi wa ngazi husika. Mfano, Waziri Mkuu anapokwenda kwenye ziara hizi huwa anapokea malalamiko mengi sana ambayo yangeweza kupatiwa ufumbuzi na Viongozi wa maeneo hayo, kama vile matatizo ya ardhi, madaraja, afya na miundombinu. Hili likitekelezwa litamfanya Waziri Mkuu kwenda Mikoani kwa shughuli nyingine za maendeleo na kupunguza gharama kwa Taifa.

(iii) Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi duniani kote (*climatic change*) kama vile kuongezeka kwa joto duniani (*global warming*) ambapo majanga kama matetemeko ya ardhi, njaa na vimbunga mbalimbali, Kamati inashauri kuwa ni vyema Serikali ikajiandaa vya kutosha kukabiliana na majanga hayo. Ikumbukwe kwamba Tanzania sio Kisiwa kwani majanga haya yanetoka Japani, Marekani, Australia na China, hivyo hata kwetu yanaweza kutokea. Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kuwa tarehe 10 Juni, 2011, tukiwa hapa Bungeni, kulijitokeza tetemiko dogo la ardhi Jijini Dar es Salaam lililochukua takribani sekunde 15 na kutikisa maghorofa marefu hali ambayo iliwatia hofu wananchi.

(iv) Juhudi zaidi zifanyike katika kufikisha chakula cha msaada kwenye maeneo yanayohitaji msaada huo mara taarifa zitakapowafikia kwani kumekuwepo na malalamiko mengi ya ucheleweshwaji.

(v) Mpigachapa wa Serikali ongezewe uwezo ili kumudu jukumu kubwa la uchapaji wa nyaraka za Serikali na hivyo kuondokana na tatizo la siri za Serikali kuvuja

ambalo linasababishwa na nyaraka nyingi kuchapishwa bila kufuata utaratibu na pia kuwezesha nyaraka hizo kupatikana haraka pale zinapohitajika.

(vi) Manispaa ya Dodoma inakadiriwa kuwa na idadi ya wakazi wapatao 324,347 kwa sensa ya mwaka 2002. Idadi hiyo inakadiriwa kuongezeka karibu mara mbili kutokana na ongezeko la idadi kubwa ya wakazi wa Manispaa hiyo ambayo imesababishwa na kuanzishwa kwa Vyuo Vikuu mfano Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Mtakatifu John, Chuo cha Mipango, Chuo cha Biashara Dodoma na Chuo cha Madini. Ni vyema Serikali ikafikiria suala la kuongeza na kupanua miundombinu ya maji na barabara ili kukidhi haja kwani hivi sasa Mji huu amba ni Makao Makuu ya Nchi unakabiliwa na misongamano ya magari, uhaba wa maji na upungufu wa miundombinu mingine muhimu. Ni vizuri tuiangalie Dodoma kwa miaka mingi ijayo na kuipanga vizuri kwani ndiyo Makao Makuu ya nchi yetu. (*Makofi*)

(vii) Kwa vile nyumba za Idara/Wizara za Serikali na viongozi mbalimbali wa Serikali kwa wakati mmoja zinajengwa sehemu mbili, kwa maana ya Dodoma na Dar es Salaam, Kamati inashauri kuwa ni wakati muafaka sasa Serikali iache kujenga nyumba hizo Dar es Salaam na badala yake nyumba hizo na ofisi za Serikali zijengwe Dodoma ili kutimiza lengo la Serikali la kuhamia Dodoma. Kamati inazidi kusisitiza kwamba hivi sasa Serikali itimize dhima yake na kuondoa kigugumizi cha kuhamia Dodoma. (*Makofi*)

(viii) Kamati imebaini kwamba Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zimekuwa na matumizi makubwa katika kulisipia gharama za DSTV, magazeti na samani. Kamati inashauri kwamba ni vema suala hili likatazamwa upya ili kupunguza gharama hizo kwani ni mzigo kwa Serikali na haziendani na hali halisi. Aidha, Kamati inashauri kuwa Idara na Taasisi zote za Serikali kununua samani zake kutoka Tanzania ili kuinua uchumi wa wananchi wetu hasa ukizingatia ndizo samani zenye ubora zaidi kuliko hizo za nje.

(ix) Kamati imepata wasaa wa kupitia bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kifungu kwa Kifungu na kubaini kwamba fedha nyingi zimetengwa kwenye utengenezaji wa magari ya Serikali. Ili kuipunguzia mzigo Serikali, Kamati inadhani kuwa umefika wakati sasa wa kurudisha ule utaratibu wa zamani wa kuwa na gereji za Serikali ili magari yote ya Serikali yaweze kutengenezwa huko na kuwepo na usimamizi wa karibu na wa kutosha. Kamati imebaini kwamba katika mwaka ujao wa fedha (2011/2012) matengenezo ya magari katika Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi/Idara zilizo chini yake tu yanafikia kiasi cha shilingi 16,556,142,821/=, ambacho ni kikubwa sana kulinganisha na uwezo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 27 - Msajili wa Vyama vya Siasa. Baada ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010 kusainiwa na kuanza kutumika, pamoja na nia nzuri ya sheria hiyo, imejidhihirisha wazi hasa wakati wa Uchaguzi kwamba wananchi wengi na Vyama vya Siasa bado hawana uelewa wa kutosha kuhusiana na sheria hiyo. Kamati inashauri kuwa ni vema Serikali iendelee kutoa elimu ya Sheria hiyo ikiwa ni pamoja na kuangalia upungufu wake ili kupunguza matatizo ya rushwa ambayo bado yameendelea kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 42 - Mfuko wa Bunge, Kamati inapendekeza yafuatayo:-

(i) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuhamishia ujenzi wa ofisi za Wabunge kutoka Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, (TAMISEMI) kuja Ofisi ya Bunge. Hata hivyo, Kamati inapendekeza kuwa mikataba ya ujenzi wa Ofisi hizo iangaliwe kwa makini na ikiwezekana taasisi muhimu na ambazo zimeonesha ufanisi mkubwa kama JKT na Magereza zipewe kazi hizo. Aidha, Kamati inasisisitiza kwamba ni vema Ofisi hizo zikajengwa na kukamilishwa mapema ili kutatua tatizo lililopo hivi sasa kwa Waheshimiwa Wabunge. (*Makofii*)

(ii) Kwa vile wakati wa Kamati za Bunge Dar es Salaam imeonekana kuna tatizo kubwa la maegesho ya magari pamoja na upungufu wa kumbi za mikutano, ni vema Bunge kwa kushirikiana na Serikali wafikirie kupanua Ofisi iliyopo au kupata eneo lingine ili kukidhi mahitaji ya sasa kwa Wabunge, Watumishi, Maafisa wengine wa Serikali na wageni wanaokuja kwa shughuli za kiofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la kumbi limekuwa kero ambayo ufumbuzi pekee ni kuwa na jengo moja litakalokuwa na kumbi zitakazowezesha Kamati zote kupata huduma katika eneo moja kuliko hali iliyopo sasa ambayo inaleta usumbufu mkubwa kwa Kamati. Hii ni pamoja na kuongeza kumbi katika Ofisi ya Bunge Dodoma ili kukidhi ongezeko la Wabunge na Maafisa wanaokuja kwenye Kamati.

(iii) Wakati umefika sasa kwa Ofisi ya Bunge kuimarisha Kitengo cha Utafiti na ikiwezekana ianzishe Idara Maalum itakayo julikana kama Idara ya Utafiti wa Uendeshaji wa Bunge na Kamati (*Department of Committee and Table Research*). Kamati inapendekeza kuwa Idara kama hii iwe na wataalamu ambao kazi yao kubwa ni kutafiti wakati wote masuala ya Kamati na uendeshaji wa Bunge ambapo kutakuwa na jopo la wataalamu walibobe (analysts) ambao wanaweza kumshauri Spika haraka Bungeni kwa masuala ya uendeshaji wa Bunge na kuzishauri Kamati haraka kulingana na fani zao na mahitaji ya Kamati.

(iv) Kamati inashauri utafiti ufanyike ili kuwezesha urushaji wa vipindi vyta Bunge kwenye televisheni na radio ufanyike kwa kuchangia gharama kati ya Ofisi ya Bunge na vituo husika tofauti na iliyvo sasa ambapo Serikali inalipa fedha nyingi kulipia matangazo hayo. Jambo hili si geni kwani linafanyaika hata kwenye nchi nyingine kama India.

(v) Kwa vile hivi sasa huduma za afya kwa Waheshimiwa Wabunge zinatolewa kwa gharama kubwa, ni vyema Ofisi ikafikiria kuanzisha utaratibu wa Bima ya Afya kwa Wabunge ili waweze kutibiwa hadi kwenye hospitali binafsi kwa kutumia bima zao na sio utaratibu wa sasa ambapo wanatibiwa kwenye Hospitali za Serikali tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi; Kamati inapendekeza yafuatayo:-

(i) Tume ya Taifa ya Uchaguzi ishirikiane na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) kutoa elimu kwa Mpiga Kura hasa kwa wananchi wa Zanzibar kwa kuzingatia kuwa wana Madaftari mawili yaani la Zanzibar na la Bara. Wengi wao wanadhani kuwa wakishajiandikisha lile la Bara basi wana haki ya kupiga kura Zanzibar na hivyo kusababisha fujo wanapoambiwa hawaruhusiwi kupiga kura kwa vile hawajajiandikisha.

(ii) Kwa vile mpaka sasa Tume iko kwenye ofisi za kukodisha na pia hukodi maghala kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vyake, Serikali iiwezeshe Tume hii kwa kuiongezea bajeti ili iweze kujenga ofisi na maghala yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 91 - Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevy; Kamati ilipata muda wa kutembelea Tume hii na kujionea hali halisi katika kukabiliana na athari za matumizi ya dawa za kulevy, Kamati ina ushauri ufuatao:-

(i) Kwa vile Tume inakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo ukosefu wa mafunzo ya mara kwa mara kwa watendaji, upungufu wa rasilimali watu wenye taaluma katika ukaguzi wa dawa, utambuzi na uchunguzi pamoja na upungufu wa vitendea kazi kama magari, pikipiki, boti, mbwa wa kunusa, kompyuta, televisheni na *test kits*, Kamati inapendekeza kuwa Serikali iongeze bajeti ya Tume ili iweze kufanikisha majukumu yake na kufikia malengo yanayotarajiwa.

(ii) Kamati inapendekeza kuwa Serikali itoe ulinzi wa kutosha kwa Kamishna wa Tume hii kwani anafanya kazi kwenye mazingira magumu na yenye hatari ni pamoja na kuwawekea bima wafanyakazi wa Tume hii. Vile vile, ni vema pale wafanyakazi wanapofanikisha ukamataji wa dawa hizi za kulevy, itolewe motisha maalum ili kuongeza juhudzi za utendaji kazi ikiwa ni pamoja na kupunguza au kuondoa vishawishi vya rushwa kutoka kwa watuhumiwa wa dawa hizi za kulevy.

(iii) Kamati inapendekeza kuwepo na sera na sheria madhubuti za kupambana na tatizo la dawa za kulevy kwa kuboresha zaidi Sheria za Udhibiti wa Dawa za Kulevy (*The Drugs and Prevention of Illicity Traffic in Drugs Act, No.9 of 1995*) ili Tume iwe na Mkemia wake atakayeshirikiana na Mkemia wa Serikali pale inapohitajika kufanya uchunguzi au kuthibitisha dawa za kulevy zilizokamatwa. Sambamba na hilo, Kamati inapendekeza kuwa huduma ya matibabu kwa waathirika wa dawa za kulevy ipatikane katika Hospitali za Mikoa kote nchini kwani tatizo hili limeenea nchi nzima tofauti na ilivyo sasa hivi ambapo huduma hiyo inapatikana katika Hospitali za Mirembe na Muhimbili tu.

(iv) Tume inashauriwa kujipanga ili kutoa elimu kwa umma kuhusu tatizo la dawa za kulevy, ukubwa wake ulivyo na zinavyoingia nchini kwani hivi sasa limekuwa janga la Kitaifa.

(v) Tume iwe na matawi mpaka Mikoani na wakati huu wa mpito iweke Maafisa Maalum katika kila Halmashauri watakaokuwa wanashughulika na suala hili la dawa za kulevy ili kurahisisha upelekaji na ufuatiliaji wa taarifa.

(vi) Kamati imepokea kwa masikitiko taarifa kupitia vyombo veya habari kwamba kuna uwezekano mkubwa kuwa hata baadhi ya Viongozi wa Dini wanajihuisha na biashara hii haramu ya madawa ya kulevyo, Kamati inalaani kwa nguvu zote Viongozi wa Dini wa aina hiyo na kuiomba Serikali ilichukulie jambo hili kwa uzito mkubwa kwa kufanya uchunguzi wa kina na kuweza kuwabaini Viongozi hao kisha kuwafikisha kwenye vyombo veya sheria ili wachukuliwe hatua zipasazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 92 - Tume ya Kudhibiti UKIMWI; Kamati inapendekeza yafuatayo:-

(i) UKIMWI ni janga la Taifa baada ya Malaria na wananchi wengi wanakuwa kutokana na ugonjwa huu, Kamati inapendekeza kuwa vituo veya kudumu veya kutoa ushauri nasaha na elimu vijengwe kwenye maeneo mbalimbali hasa yenye mkusanyiko mkubwa wa watu ili hata wale walio tayari kwenda kupima basi wapate huduma hiyo kwa karibu.

(ii) Ili kukabiliana na maambukizi mapya ya ugonjwa huu, inapendekezwa kuwa vifaa veya kinga (*condoms*) vipatikane kwa wingi mpaka vijijini, ikiwezekana kuwe na mashine maalum za kutoa kinga hizo bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), baada ya kueleza Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu-Sera, Uratibu na Bunge, sasa naomba kuelezea bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 3 Juni, 2011, Kamati ilikutana Dar es Salaam ili kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Katika kikao hicho, Kamati ilipokea maelezo ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii kwa Mwaka 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2011/2012. Maelezo hayo yaliwasilishwa na Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa akisaidiwa na Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri, Naibu Waziri wa Ofisi hiyo. Napenda kushukua nafasi hii kuwashukuru sana Mawaziri hawa kwa ushirikiano wao wa karibu na wa dhati pamoja na Kamati ya Katiba Sheria na Utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, Kamati pia ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu kwa Mwaka 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Fungu 56 – Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Mikoa kwa Mwaka 2011/2012 kwa Mafungu 70 – 89 na Fungu 95, yaliyowasilishwa na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa. Aidha, Waziri alieleza kuhusu mpango mkakati wa Wizara, Dira na Dhima, mapato na matumizi na majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na kuratibu usimamizi na uendeshaji wa Shule za Msingi na Sekondari na kusimamia Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha, Mheshimiwa Waziri alifafanua kuhusu kazi ziliyofanyika kwa kipindi cha Julai 2010 hadi Machi, 2011 na changamoto zilizojitokeza

katika kipindi cha utekelezaji wa Mipango ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Halmashauri nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa mwaka 2010/2011. Wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii na Mikoa kwa Mwaka 2010/2011, kama ilivyo ada, Kamati ilitoa maoni na ushauri Mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba tena kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia ushauri uliotolewa. Pamoja na hayo, yapo maeneo mengine yanahitaji kuboreshwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia dhima, majukumu na mipango ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Kamati ilipokutana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ilipata taarifa kwamba watu waliokuwa wakimbizi siku zilizopita wapatao 162,256 toka Kambi mbalimbali za Wakimbizi baada ya kukaa nchini kwa muda mrefu, Serikali imeamua kuwapatia uraia. Aidha, Kamati imebaini kwamba hivi sasa Serikali inafanya mipango ya kuwatawanya watu hao kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu kwa makundi ili kuwapatia makazi ya kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kupata taarifa sahihi za jambo hili, kwani pamoja na nia nzuri ya Serikali hasa kwa kuzingatia kwamba hawa ni binadamu wenzetu ambao tumeishi nao kwa muda mrefu, inabidi kuchukua tahadhari na upo umuhimu wa kufanya utafiti wa kutosha ili kujiridhisha kwamba hakutatokea madhara ya kijamii, kiuchumi, kiusalama na kisiasa huko watakapelekwa. Kamati inahofia mipango yoyote ya haraka ya kufanikisha jambo hili inaweza kuwa ni chanzo cha tatizo lingine katika jamii hizo.

(ii) Kamati inashauri kuwa Kanuni zinazoongoza Vikao vya Baraza la Madiwani zifuatwe ili taarifa ziwafikie wajumbe siku saba kabla ya kikao kama Kanuni inavyotaka na hivyo waweze kupata muda mzuri wa kuzisoma hatimaye kuweza kuzijadili vizuri. Pia Kamati inashauri kuwa wakati wa kupanga ratiba ni vema Wabunge wakashirikishwa ili kuondoa tatizo la ratiba za vikao vya Baraza la Madiwani kugongana na vikao vya Bunge.

(iii) Kamati inapendekeza kuwa, vigezo vya kugawa Wilaya vifahamike na elimu juu ya vigezo hivyo itolewe.

(iv) Kwa kuwa migogoro ya ardhi inashughulikiwa kwa ngazi ya chini na Mabaraza ya Vijiji na Kata ambapo Mabaraza haya pia hushughulikia migogoro mingine na kwa kuwa Wajumbe na Wenyevitti wake hawana taaluma ya sheria wakati wakishughulikia masuala ya kisheria, na kwa kuwa Mabaraza haya yanashughulikiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Katiba na Sheria, Kamati inashauri kuwa ni vema migogoro ya ardhi ishughulikiwe kwa mfumo wa Kimakahama ili migogoro ya kisheria itatuliwe kwa mfumo mmoja. Vile vile Kamati

inahoji Bajeti ya kuendesha Mabaraza haya kwani Bajeti hiyo haipo, si Wizara ya Katiba na Sheria wala Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Aidha, Kamati inashauri elimu kwa Wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi Vijijini na Mabaraza ya Usuluhishi itolewe mara kwa mara ili kuwajengea uwezo wa kumudu majukumu yao.

(v) Kamati inapongeza Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kwa uamuzi wake wa kununua vitabu nya Ziada na Kiada badala ya utaratibu wa awali ambapo Maafisa Elimu walikuwa wanavinunua na kufanya vitabu hivyo kununuliwa kwa bei ya juu na wakati mwingine kutonunuliwa kabisa.

Kamati inashauri kuwa Wizara sasa ishughulikie tatizo la upangaji wa Walimu kwa vile hauzingatii uwiano kwani sehemu nyingine zina Walimu wengi na nyingine hazina kabisa. Mfano mmojawapo, ni tofauti iliyopo kati ya Mijini na Vijijini, Wilaya na Wilaya au Mkoa na Mkoa. Kamati inashauri kuwa suala hili liangaliwe kwa umakini kwa vile linadidimiza maendeleo ya elimu katika sehemu zenye upungufu na kuishauri Wizara kutoa posho maalum kwa Walimu wanaokwenda kwenye Mikoa ya pembezoni au yenye mazingira magumu. (*Makofi*)

Kamati inashauri kuwa, Serikali izisimamie Halmashauri zote nchini kutumia fedha za ukarabati (*capitation grants*) kama zilivyokusudiwa kwa shule husika ili shule zetu ziweze kukarabatiwa kwa wakati na kuongeza mioundombinu mipya ili kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefurahishwa na baadhi ya Halmashauri kutenga fedha kwa ajili ya kuwasomesha na kuwaendeleza watoto yatima, maskini na waishio kwenye mazingira magumu. Kwa vile suala hili hivi sasa ni changamoto kwa jamii zote nchini, Kamati inazishauri Halmashauri zote nchini zibuni vyanzo nya mapato mbalimbali na hivyo kupata fedha zitakazosaidia kuwaendeleza watoto waishio kwenye mazingira magumu, yatima na maskini.

(vi) Kamati imefuatilia kwa karibu maslahi wanayopata Madiwani ambayo kimsingi ni madogo sana ukilinganisha na uzito wa majukumu waliyonayo kwa jamii. Kamati haioni sababu ni kwa nini Madiwani hawa wasilipwe mishahara badala ya posho wanazopewa kwani utumishi wao unaeleweka. Kwa kuwa stahili za Madiwani hawa ni za kisheria, Kamati inaona sasa ni wakati muafaka sheria hizi zikafanyiwa maboresho ili kuwezesha Madiwani kupewa mishahara au haki zao ziongezwe kulingana na gharama za maisha.

Vilevile, Kamati inashauri kwamba, mafunzo ya mara kwa mara kwa Madiwani yaimarishwe ili kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria.

(vii) Kamati imebaini kwamba suala la kupandishwa vyeo limekuwa ni tatizo kubwa kwa watumishi waliopo Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Mfano, Walimu wamekuwa wakipandishwa vyeo lakini hawapewi mshahara unaostahili kulingana na vyeo vyao na pia tatizo la kutolipwa malimbikizo yao. Hata hivyo, Kamati imesikitishwa na taarifa za Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa

Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2010, kwamba amegundua watumishi wengi wa Halmashauri wanalipwa chini ya theluthi moja ya mishahara yao na wengine hawapati mishahara kabisa kutokana na fedha zao kukatwa na taasisi mbalimbali za fedha ambazo zimewakopesha. Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali imetolea mfano wa Manispaa ya Dodoma ambapo kati ya wafanyakazi 198 waliofanyiwa uchunguzi, wafanyakazi 45 sawa na 23% hawalipwi chochote kabisa mwisho wa mwezi kinyume na Waraka wa Utumishi Na. *CCE.45/271/01/87* wa tarehe 19/03/2009 unaoagiza kuwa makato ya mshahara wa mtumishi yejote yasizidi theluthi mbili ya mshahara halisi. Pamoja na kwamba lengo la mikopo ni kuinua hali za Wafanyakazi, Kamati inapinga utaratibu huu kufanywa kiholela kwani unashusha kiwango cha utekelezaji wa majukumu kwa Watendaji hawa.

(viii) Kuhusu suala la wananchi wa Gerezani - Kariakoo na maeneo mengine, ambao wanatakiwa kupisha ujenzi wa miundombinu ya *DART*, Kamati inashauri kuwa Serikali ifanye jitihada za kukaa nao na kumaliza tatizo hili la kupisha miundombinu ya *DART* kwani wengi wao walikuwepo siku nyingi kabla ya mradi kuanza.

(ix) Kwa vile mapato ya Halmashauri ni madogo na Halmashauri nyingi nchini hazijui vyanzo vyao vya mapato kwa mfano, hakuna taarifa sahihi za majengo ambayo yanatakiwa kulipa Kodi ya Majengo, Kamati inashauri kuwa ni vema akatafutwa Mshauri Mwelekezo atakayebainisha vyanzo vyote vya mapato ya Halmashauri ili ziweze kujitegemea kwa kiasi kikubwa kuliko kutegemea Serikali Kuu.

(x) Kamati imebaini kwamba baada ya Kamati za Kudumu za Kisekta za Halmashauri kuondolewa katika ukaguzi wa miradi ya Halmashauri na kazi hiyo kuachiwa Kamati ya Fedha peke yake ni miradi michache tu ndiyo imekuwa ikikaguliwa. Kamati inashauri kuwa utaratibu wa Kamati za Kudumu za Kisekta za Halmashauri kukagua miradi iliyo chini ya sekta husika uendelee na miradi yote iweze kukaguliwa.

(xi) Kwa kuwa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali mara kwa mara imekuwa ikionesa matumizi mabaya ya fedha kwenye Halmashauri ambayo yamekuwa yakididimiza maendeleo ya Halmashauri husika, Kamati inashauri kuwa Serikali iwachukulie hatua wale wote ambao wamezisababishia hasara Halmashauri.

(xii) Wakati Kamati inapitia vifungu vya bajeti za Mikoa, iligundua kwamba kwenye Fungu 72, Mkoa wa Dodoma, Kasma 6338 ambapo ni ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, jumla ya Tsh.2,000,000,000/- zimetengwa kwa ajili ya ujenzi huo. Hata hivyo, Kamati ilifuatilia na kuelezwu kwamba hiyo ni sehemu tu ya fedha zipatazo Sh. 8,000,000,000/= zinazohitajika kwa ajili ya ujenzi wa ofisi hiyo ambayo wote tunafahamu kwamba iliungua kwa moto tarehe 29/08/2010 na hivyo kwa sasa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wanatumia Ofisi ya kuazima ambayo ni ndogo ukilinganisha na majukumu ya Ofisi hiyo, ikiwa ni pamoja na Watumishi wa Ofisi hiyo kufanya kazi kwenye mazingira magumu. Kamati inaiomba Serikali kuongeza fedha zaidi ili kukamilisha ujenzi wa Ofisi hii hasa ikitiliwa maanani kwamba ni Mkoa ambao ndiyo Makao Makuu ya Nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha zoezi la kutangaza Mikoa na Wilaya Mpya kwenye Gazeti la Serikali ili Mikoa na Wilaya hizo ziweze kuanza kazi rasmi sambamba na kupatiwa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo maoni na ushauri ambao Kamati yangu iliutoa iliposhughulikia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Napenda nilieleze Bunge lako Tukufu kuwa baada ya ufanuzi uliotolewa na Ofisi hiyo, hatimaye Kamati yangu iliyapitisha makadirio ya Ofisi hiyo na kuiruhusu yawasilishwe Bungeni kwa hatua inayofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu kuwasilisha maoni ya Kamati. Kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, napenda nitumie nafasi hii pia kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge hili ambalo lina changamoto nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kumshukuru Mungu kusimama leo hii hapa kama Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala na vile vile nichukue nafasi hii kuishukuru sana familia yangu pamoja na wale wote ambao walinipa kura na wale wote ambao wamekuwa wakinombea na kuniwezesha kuwa Mbunge katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwanza, kwa jinsi anavyosimamia na kufuatilia kwa karibu shughuli mbalimbali zinazotekelawa na Wizara zote na pili kwa kuwa msikivu na kuwa tayari kuyashughulikia matatizo ya Kamati za Bunge wakati zinapotekelawa majukumu yake kwa niaba ya Bunge. Uongozi wake umesaidia kufikia muafaka kuhusu mambo mbalimbali yaliyojitekeza katika Kamati kadhaa. Tatu, namshukuru kwa ushirikiano wake mkubwa kwa Kamati yangu wakati wa uchambuzi wa Bajeti uliotuwezesha kufikia hapa tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge na Mheshimiwa George Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri na Mheshimiwa Majaliwa K. Majaliwa, Naibu Mawaziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Taasisi, Idara na vitengo pamoja na Maafisa wake, kwa maelezo na ufanuzi wa kina walioutoa kwa Kamati na kwa ushirikiano mkubwa waliouonyesha wakati wote Kamati iliposhughulikia kazi ya kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio haya. Lakini kikubwa zaidi niwashukuru sana kwa busara na hekima walizoonesha na kuwa wavumilivu hasa pale walipopata vitabu

kwa muda mfupi. Umahiri na uzoefu wa muda mrefu katika masuala ya sheria, utawala na sekta nydingine mbalimbali ndio uliofanikisha kazi hii. Kwa heshima kubwa, naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Angella J. Kairuki, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mjumbe; Mheshimiwa John Paulo Lwanji, Mjumbe; Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mjumbe; Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mjumbe; Mheshimiwa Fakharia K. Shomar, Mjumbe; Mheshimiwa Zahra A. Hamadi, Mjumbe; Mheshimiwa Mussa H. Kombo, Mjumbe; Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mjumbe; Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mjumbe; Mheshimiwa Azza H. Hamad, Mjumbe; Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, Mjumbe; Mheshimiwa Jaddy S. Jaddy, Mjumbe; Mheshimiwa Tundu A. Mughwai Lissu, Mjumbe; Mheshimiwa Deogratias A. Ntukamazina, Mjumbe na Mheshimiwa Jason S. Rweikiza, Mjumbe. Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dokta Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru Ndugu Charles Mloka, Mkurugenzi wa Kamati za Bunge, Ndugu Peter Magati, Asia Minja na Grace Bidya, Makatibu wa Kamati hii kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zake kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana kwa niaba ya Wajumbe wote wa Kamati kwa taarifa yake.

Waheshimiwa Wabunge, hotuba ya Waziri Mkuu pia inahu Wizara inayoshughulikia masuala ya uwezeshaji na Uwekezaji, kwa hiyo, naomba sasa nimwite msemaji wa Kamati ya Fedha na Uchumi ili aweze kutoa maoni ya Kamati hiyo na baada ya hapo tutampa nafasi Msemaji wa Kambi ya Upinzani ili aweze kuendelea. Mheshimiwa Devotha Likokola kwa niaba ya Kamati ya Fedha na Uchumi.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe Maoni ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 37-Uwezeshaji na Uwekezaji kwa Mwaka 2010/2011 na Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba niwasilishe maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi, kuhusu

utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 37 - Uwezeshaji na Uwekezaji kwa Mwaka 2010/2011 na Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana tarehe 31 Mei, 2011 na kupokea maelezo ya muhtasari wa Bajeti ya Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Uwekezaji na Uwezeshaji kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012. Aidha, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa majukumu kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Hapo awali kabla ya kubadilika kwa Kanuni za Bunge, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na Uwezeshaji ilikuwa ikiwajibika chini ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala. Hata hivyo, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na Uwezeshaji kwa kutekeleza vyema malengo yake ambayo yalikuwa yamelengwa kwa mwaka uliotangulia ikiwa ni pamoja na mipango mizuri iliyowekwa kwa mwaka huo wa Fedha. Kamati inaipongeza Ofisi hii kwa umakini mkubwa iliyouchukua katika kuendesha na kusimamia miradi mbalimbali ya maendeleo ya sekta binafsi, uwekezaji na uwezeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeendelea kutoa michango, ushauri na maelekezo ambayo yamelenga kuimarisha sera na mifumo mizuri ya kufanya biashara, uwekezaji na uwezeshaji wa wananchi hasa wale wenye kipato cha chini ambao utachochea ukuaji wa uchumi jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Pamoja na changamoto katika kutekeleza Mpango wa Bajeti ya mwaka wa fedha wa 2011/2012. Masuala ya Sekta ya Uwekezaji na Uwezeshaji yana changamoto kubwa hasa ukizingatia kwamba masuala haya ndiyo yanagusa moja kwa moja kuimarisha na kukuza uchumi wa nchi na kuondoa umaskini wa kipato ambapo unakwenda sambamba na ugumu wa maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha mwaka 2010/2011, bado Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na Uwezeshaji inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinabidi kuzingatiwa katika kipindi cha 2011/2012. Baada ya kupitia hali halisi ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2010, Kamati inashauri kwamba ili kuwawezesha wananchi walio wengi lazima rasilimali za Taifa zielekezwe kwenye maeneo ambayo yanawagusa wananchi wengi katika shughuli zao za kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta zinazokua kiuchumi kama Ujenzi, Mawasiliano na zile zinazotoa huduma zinagusa idadi chache ya watu katika Taifa na vile vile hazongezei sana ukuaji wa uchumi unaowagusa wengi ikilinganishwa na sekta ya Kilimo, Uvuvi na Ufugaji, sekta hizi ndizo ambazo zinaweza kuajiri wananchi wengi zaidi. Hali hii inaashiria kuwa, Serikali ina changamoto kubwa ya kuendeleza sekta hizi kupitia hatua mbalimbali za makusudi, kusimamia na kuelekeza maelekezo na maendeleo binafsi ya uwekezaji na uwezeshaji kwa walengwa husika waliokusudiwa katika sekta ya kilimo, uvuvi na ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutoa misamaha ya kodi kwa wawekezaji limekuwa likipigiwa kelele na wadau mbalimbali. Misamaha ya kodi kwa makundi mbalimbali imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka na hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa mapato ya Serikali yatokanayo na kodi. Takwimu zinaonyesha kuwa Kituo cha Uwekezaji cha Taifa (*TIC*) ndilo kundi linalochukua sehemu kubwa ya misamaha ya kodi takriban asilimia 39 ya misamaha yote ya kodi. Kamati inasisitiza kuwa Serikali ifanye utafiti wa kina (*cost-benefit analysis*) kuhusu faida na hasara inayopatikana kuhusiana na misamaha hiyo ya kodi inayotolewa kupitia Kituo cha Uwekezaji cha Taifa. Aidha, Serikali iangalie misamaha yote ya kodi iliyopo sasa na itathmini gharama yake inavyoshabihiana na Pato la Taifa, iangalie faida na hasara za misamaha hiyo yote kwenye uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la uwekezaji, pamoja na jitihada nzuri ambazo Serikali imefanya bado msukumo wa uwekezaji haujakuwa wa kutosha (*Investment Drive*). Serikali imejitahidi kuweka mikakati ya kupunguza urasimu, kupunguza rushwa na ucheleweshaji wa maamuzi, jitihada za kuboresha mazingira ya uwekezaji, Programu za *BEST*, kuanzishwa kwa Baraza la Uwezeshaji la Kiuchumi wa mkakati wa utekelezaji wa sera ya Ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (*PPP*). Bado mazingira yetu ya uwekezaji hayajaboreshwa vya kutosha hasa eneo la miundombinu kwa maana ya barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege, umeme, maji na kadhalika. Bado tunahitaji kuendeleza umakini katika eneo hili pamoja na kupunguza gharama ya kufanya biashara (*Cost of Doing Business*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikijitahidi kuandaa programu na mikakati mbalimbali ya kuwawezesa wananchi kiuchumi kama vile Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Mpango wa Uwezeshaji wa Wananchi, Kuongeza Ajira, Mfuko wa Wafanyabiashara Wadogo Wadogo wa Wananchi (*NEDF*), Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Uwezeshaji wa Wajasiriamali Wadogo (*SELF*) na mingine mingi. Yote hii ina lengo bora la kusaidia na kuwawezesa wananchi walio wengi wenye kipato cha chini kuwakwamua kiuchumi, hata hivyo, malengo ya Mifuko hiyo mbalimbali hayatimizwi ipasavyo kwa kuwa haiwalengi wananchi waliokusudiwa na imekuwa ikifaidisha wananchi wachache. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha Mifuko hii inawafikia walengwa walio wengi na kuwanufaisha wananchi na kuongeza wigo wa kukuza uchumi kwa wananchi walio wengi hususan vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*), Sura ya 148 ili kuhamasisha uwekezaji na kuboresha uzalishaji katika sekta ya Kilimo, Mifugo, Uvubi, Viwanda, Biashara na Utalii. Hali hii itasaidia wawekezaji wa kigeni na wale wa ndani kuchangia Pato la Taifa kuitia sekta zilizotajwa hapo juu. Aidha, mwelekeo huu, pamoja na uimarishaji mikakati ya Kilimo Kwanza, utasaidia sekta ya kilimo kufanya kazi vizuri na italeta mazingira bora na hatimaye kuongeza vipato vya wakulima. Kamati inasisitiza uwekezaji mkubwa katika kilimo cha umwagiliaji, ufugaji wa kuku, uvubi na uwekezaji katika viwanda vya usindikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Bunge lilipitisha Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya Mwaka 2010 (*Public Private Partnership Act, 2010*) na kanuni zake zimeshakamilika. Kupitia Sheria hii Sekta ya Umma kwa kushirikiana na Sekta Binafsi zitapata fursa za kujenga, kuendesha na kuwekeza katika miradi muhimu ambayo itasaidia kutoa huduma za kijamii na kiuchumi na kuawezesha wananchi kupata ajira na kuongeza kipato kupitia miradi hiyo ya ubia. Hata hivyo, Kamati inasisitiza Serikali kusimamia ipasavyo utekelezaji wa Sera na Sheria hii ya Ubia ili kufikia lengo lilokusudiwa na kuepusha migogoro ya utekelezaji wa miradi ya utaratibu wa ubia kama ilivyojitokeza katika Shirika la Reli Tanzania, Shirika la Ndege Tanzania, *TANESCO*, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro na mingine mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tumepitisha Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kuanzia Mwaka 2011/12 hadi 2015/16, ambapo lengo la Mpango huu ni “Kufungua fursa za ukuaji uchumi Tanzania”. Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwezeshaji na Uwekezaji kuhakikisha kuwa inasimamia ipasavyo miongozo yote iliyotolewa na Tume ya Mipango, kwa Ofisi hii, ili kuhakikisha inatimiza malengo yake iliyojiwekea na kuhakikisha kwamba inakuza uchumi na kupunguza umaskini kupitia vipaumbele vyta miradi vyta uwekezaji na uwezeshaji kama itakavyoelekezwa na Tume hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza kuwa Serikali ifanye jitihada kubwa kuhakikisha kuwa inaongeza Benki ya Ardhi na zinatambuliwa na wananchi na kutofautishwa na ardhi za vijiji. Hii itasaidia kuhakikisha kwamba shughuli mbalimbali za uwekezaji zinafanyika pasipokuwa na migogoro na wananchi wa maeneo husika ya ardhi. Aidha, matumizi ya ardhi katika maeneo hayo yaainishwe kwa utaratibu unaofaa ili kurahisisha mchakato wa uwekezaji wa ndani na wa nje kuwekeza katika shughuli za uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo moja ambalo linachangia ughali wa maisha kwa wananchi pamoja na kuongeza gharama za uzalishaji viwandani ni bei kubwa ya nishati ya petroli na dizeli. Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa jitihada zake za kupunguza bei za mafuta pamoja na kukamilisha zoezi la kuweka Kanuni za Kisheria juu ya uendeshaji wa taratibu za *Bulk Procurement*. Hatua hii itasaidia kupunguza gharama ya uzalishaji na kuvutia wawekezaji katika sekta ya viwanda vyta uzalishaji, sekta za usafirishaji pamoja na uendeshaji wa mitambo mbalimbali inayotumika katika shughuli za uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa Serikali katika mwaka 2010/2011, imetoa mikopo yenye masharti nafuu kupitia Mifuko mbalimbali, imehamasisha uanzishwaji wa Vyama vyta Ushirika (*SACCOS*) na *VICOBA* kama njia bora ya kupata mitaji na mikopo yenye masharti nafuu. Hata hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada hizo za kuongeza mikopo yenye masharti nafuu ili kuongeza kipato, ajira na kupunguza umaskini, bado kuna changamoto kubwa ya elimu inahitajika kwa wananchi walio wengi ili waelewe na kushiriki kikamilifu katika ujasiriamali, uwekaji wa akiba,

uwekezaji na kuhamasisha uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika kwa maana ya *SACCOS* na *VICOBA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kuwa wananchi wengi wanawezeshwa kiuchumi, Serikali inatakiwa kuhakikisha inasimamia vizuri Sera, Programu na Mifuko mbalimbali ilioanzishwa kwa nia ya kuwajengea uwezo wananchi kushiriki kikamilifu katika uendeshaji, usimamiaji na umiliki wa uchumi. Juhudi hizi zinalenga kuinua uwezo wa wananchi kupata mitaji, teknolojia na masoko ili waweze kutumia ipasavyo fursa za uwekezaji zilizopo na hivyo kufanikisha upatikanaji wa maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, Kamati inapenda kumshukuru sana Waziri wa Nchi, Uwekezaji na Uwezeshaji, Dokta Mary Michael Nagu, Katibu Mkuu, pamoja na wataalam wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuwa tayari kutoa ufanuzi na kupokea maoni na ushauri kwa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Ni matarajio ya Kamati kuwa ushirikiano huu utaendelea katika mwaka ujao wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa sana, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi ambao wameweza kutoa maoni na michango ya mawazo yao katika kuboresha makadirio haya ili hatimaye yaweze kuleta mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba sasa niwatambue Wajumbe wote kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dokta Abdallah Omari Kigoda, Mwenyekiti; Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mjumbe; Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mjumbe; Mheshimiwa Maulidah Anna Valerian Komu, Mjumbe; Mheshimiwa Dokta Binilith Satano Mahenge, Mjumbe; Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mjumbe; Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mjumbe; Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, Mjumbe; Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mjumbe; Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mjumbe;

Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mjumbe; Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mjumbe; Mheshimiwa Dokta William A. Mgimwa, Mjumbe; Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mjumbe; Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mjumbe; Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mjumbe; Mheshimiwa Freeman Aikael Mbewe, Mjumbe; Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mjumbe; Mheshimiwa Amour Amina Abdulla, Mjumbe; Mheshimiwa Rostam A. Aziz, Mjumbe; Mheshimiwa Alhaji Mohamed Hamisi Missanga, Mjumbe; Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mjumbe; Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mjumbe na Devotha Mkuwa Likokola, Mjumbe. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe kama Mwenyekiti wa Bunge na Wenyeviti wengine wa Bunge, naomba pia nimshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika kwa kutupatia maelekezo mbalimbali katika Kamati yetu. Lakini pia napenda niwashukuru Katibu wa Bunge Dokta Thomas D. Kashilillah kwa kusaidia shughuli zetu za Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi. Napenda pia

kumshukuru ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa nafasi ya pekee sana nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa baraka amazonijalia katika kuendeleza majukumu ambayo wanawake wa Mkoa wa Ruvuma wamenikabidhi na naomba kuwahakikishia wanawake wa Mkoa wa Ruvuma, nitaendelea kuwatumikia kwa umakini mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya yote, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 37-Uwekezaji na Uvezeshaji, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Devota Mkuwa Likokola, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Ruvuma kwa niaba ya Kamati kwa kuwasilisha vizuri maoni hayo.

Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu, naomba kwa heshima na taadhima kwanza nitambue wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu waliohudhuria katika kikao chetu cha Bajeti kwa siku hii ya leo. Baada ya kundi la kwanza wengine wote nitawataja kwa makundi yao. Wa kwanza kabisa ni ndugu Peniel Lyimo, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu; Bwana Hussein Katanga, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI; Bwana Charles Palangyo, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu; Bwana Eliakim Maswi, Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI; Bwana Jumanne Sajin, Naibu Katibu Mkuu, TAMISEMI Elimu; Bwana Rajabu Kiravu, Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Mheshimiwa John Tendwa, Msajili wa Vyama vya Siasa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge wengine sasa kwa makundi yao kwanza kabisa ni Wakuu wa Mikoa yote Tanzania Bara, ningeomba wote msimame, ahsante. Kundi linalofuata ni Makatibu Tawala wa Mikoa yote Tanzania Bara, ahsante sana, tunawashukuru kwa kujumuika nasi siku ya leo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge na kundi la mwisho, ningeomba niwatambue Wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ningeomba wote kwa umoja wenu msimame. Nashukuru sana, basi baada ya kuwatambua wageni hao wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa kanuni, naomba nimwite Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbwe ambaye pia ni Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mbwe kabla hujaanza samahani sana Waheshimiwa Wabunge naomba tu niwataje, wachangiaji wawili wa mwanzo, kusudi kama hawamo ndani ya Ukumbi waweze kurejea, kwa sababu mara baada ya Mheshimiwa Mbwe tutaanza na mchango wa jumla, ilikuwa leo aanze Mheshimiwa Edward Lowassa lakini ameomba udhuru na ilikuwa afuatiwe na Mheshimiwa Jenister Mhagama nadhani na yeje pia ana

udhuru yuko Mezani. Kwa maana hiyo, tutaanza na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer na atafuatia Mheshimiwa Amos Gabriel Makala.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE - KIONGOZI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI.** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kwa niaba ya Kambi ya Upinzani ninayoiongoza kuwasilisha maoni yetu kuhusu Hotuba ya Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Uratibu na Bunge, Uwezesaji na Uwekezaji pamoja na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2011/2012, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 99 (7), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa mahali hapa. Aidha, nimshukuru sana kwa ulinzi wake kwangu kwani nyumba asiyoilinda Mwenyezi Mungu, wote wailindao wafanya kazi bure. Namwomba aendelee kuniongoza na zaidi kunipa hekima, busara na uvumilivu ili kazi hii ninayoiongoza ikapate baraka na kibali chake popote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na kukupongeza kwa dhati wewe binafsi kwa jitihada unazofanya kuhimili mikiki-mikiki mingi ya kidemokrasia inayojitokeza hapa Bungeni. Mimi na Kambi yote ya Upinzani tunaahidi kuendelea kukupa ushirikiano wote unaostahili katika kuliwezesha Bunge letu kutimiza wajibu wake kikamilifu kwa manufaa ya Taifa letu. Nasi tunatarajia utaendelea kufanya kazi kwa kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni pamoja na mila na desturi bora za Kibunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuwashukuru makamanda wote wa chama chetu, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kwa kujitolea kwa uzalendo wa hali ya juu katika kuendesha harakati zetu za kulikomboa Taifa dhidi ya umaskini, ujinga, maradhi na ufisadi na woga, ambavyo vimetamalaki kwa miaka mingi. Nasema ahsanteni sana makamanda wote wa CHADEMA nchi nzima, ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natoa shukrani kwa Watanzania wote wanaotunga mkono, wasio wanachama wa CHADEMA. Nawaahidi Watanzania wote kuwa tutapigania kwa nguvu zote ndani na nje ya Bunge, yote yale yenye maslahi na yenye kutoa haki kwa Watanzania wote bila kujali dini, kabilia, itikadi na hata jinsia. Hatutawaangusha na hakuna kulala mpaka kieleweke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani zangu za kipekee ziwafikie wananchi wote wa Wilaya na Jimbo langu la Hai kwa imani kubwa sana waliyonayo kwangu. Kwa niaba yangu na viongozi wenzangu wote, naahidi kuwa tutatimiza yale yote tuliyokubaliana na tutaendelea kupambana na vikwazo vyote vinavyojitokeza kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyotujalia nguvu, uwezo na zaidi uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijawatendea haki kama sitatambua ushirikiano wa Wabunge wenzangu wa Kambi ya Upinzani. Ushauri wao, ushirikiano wao umekuwa wa tija kubwa kwangu. Kipekee zaidi niwashukuru Wabunge wote wa

CHADEMA kwa kazi kubwa wanayoifanya. Nawatambua Mawaziri wasaidizi wangu katika ofisi ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mheshimiwa Raya Ibrahim, Mheshimiwa Vicent Nyerere na bila kumsahau Mheshimiwa Esther Matiko. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini kwa umuhimu mkubwa ni kwa mke wangu mpendwa, Lillian, watoto wetu Dudley, Nicole na Dennis pamoja na ndugu na jamaa wote ambao wamenivumilia sana kutokana na misukosuko mbalimbali ya kisiasa ninayokutana nayo. Nashukuru sana na napenda kuwatia moyo kwa kunukuu maneno ya Martin Luther King Junior aliyesema: “*Every step towards the goal of justice requires sacrifice, suffering and struggle. It requires tireless exertions and passionate concern of dedicated individual.*” Mwisho wa kunukuu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uongozi bora na utawala wa sheria, pamoja na uwajibikaji wa viongozi na watumishi wa umma, ni nguzo ya msingi katika kukuza uchumi wa Taifa lolote duniani. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2010/2011, ukiukwaji wa misingi ya utawala bora umeendelea kuathiri kwa kiasi kikubwa uwajibikaji wa utawala kwa umma, licha ya Serikali kutamba kuchukua hatua madhubuti katika kusimamia uadilifu na uwajibikaji wa viongozi na watumishi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanafalsafa mashuhuri aliwahi kusema “*A politician thinks of the next election. A statesman thinks of the next generation*”. Hivyo ni rai yangu kwa Waheshimiwa Wabunge wote, wa Vyama vyote kutumia fursa ya kuwepo mahali hapa kutafakari kila maamuzi anayoyafanya kama yanamweka katika kundi lipi kati ya haya mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) iliendelea kuonyesha udhaifu mkubwa katika kukabiliana na tatizo la rushwa. Upembizi uliofanywa na Kambi ya Upinzani kupitia ripoti mbalimbali za utafiti kama “Ripoti ya Haki za Binadamu ya mwaka 2010” ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), umebaini kuwa, TAKUKURU iliweza kuchunguza malalamiko 2,497 yahusuyo rushwa sawa na asilimia 17.3 tu ya malalamiko yote 14,426 ya rushwa yaliyopokelewa na taasisi hiyo kati ya mwaka 2008 na 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na jumla ya kesi 101 tu zilizopatikana na hatia sawa na asilimia 22.2 ya kesi zote 424 zilizofunguliwa Mahakamani kati ya mwaka 2008 na mwaka 2010. Takwimu zote hizi zinaonyesha kuwa bado TAKUKURU ina uwezo mdogo wa kuchunguza na kufungua mashtaka ya rushwa, licha ya Serikali kusema mara kwa mara kuwa imeongezewa meno kupitia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya udhaifu huo wa TAKUKURU, rushwa imezidi kuota mizizi katika taasisi nyeti za utawala wa umma kama ilivyoonyeshwa na matokeo ya utafiti wa ‘*East Africa Bribery Index*’. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huo,

Jeshi la Polisi lilishika nafasi ya kwanza nchini na ya tano katika ukanda wa nchi za Afrika Mashariki likiwa limepewa asilimia 65.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi nyingine za Kiserikali zinazofuatia kwa rushwa kwa mujibu wa utafiti huo ni Mahakama iliyopewa asilimia 56.4, Msajili wa Vizazi na Vifo asilimia 46.7, Idara ya Magereza asilimia 43.2, Mamlaka ya Bandari asilimia 40.8, Mamlaka ya Mapato (*TRA*) asilimia 37.8, Uhamiaji asilimia 37.2 na Wizara ya Ardhi ambapo tatizo la rushwa lilionekana kuwa ni kubwa kwa asilimia 32.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini yetu ya jumla inaonyesha kuwa TAKUKURU imekuwa ikiacha kazi yake ya msingi ya kuzuia na kupambana na rushwa na kubaki ikifanya zaidi kazi za Idara ya Polisi ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai (*CID*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuwa rushwa sasa ni ugonjwa mkubwa ambao unalitafuna Taifa letu na kwa kuwa imekuwa vigumu sana kwa Serikali kulikabili tatizo hili kikamilifu sababu kubwa ikiwa wapokeaji wakubwa wa rushwa wako katika Serikali hii hii, Kambi ya Upinzani inashauri kwa sasa kuundwe Kamati ya Kudumu ya Bunge Inayosimamia Vita Dhidi ya Rushwa. Baadaye, katika Katiba mpya inayokusudiwa uangaliwe kwa umakini uwezekano wa kuifanya taasisi hii kuwa idara inayojitegemea na isiyo moja kwa moja chini ya Ofisi ya Rais. Badiliko hili litaiwezesha taasisi hii kuwa na uhuru zaidi wa kufanya kazi, kwani kwa hali ilivyo sasa, washirika wa taasisi hii ni wale wale wa kutoka chama kile kile chenye kukabiliwa na tatizo sugu la rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapendekeza kwamba, Kamati hii kama zilivyo *oversight Committees* za masuala ya fedha zinazoongozwa na Wenyeviti toka Kambi ya Upinzani, nayo ifuate mfumo huo huo. Lengo la kuanzishwa kwa Kamati hii, ni ili kusaidiana kukabiliana na janga hili linaloathiri kwa kiasi kikubwa ustawi na zaidi haki katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Viongozi wa umma wanapaswa kusimamia uwajibikaji na uwazi katika kupambana na rushwa. Sheria inayosimamia maadili na mwenendo wa watumishi wa umma ya mwaka 1995 inamtaka kila mtumishi wa umma kuwa tayari kutangaza mali zake au za mwenzi wake anapotakiwa kufanya hivyo. Aidha, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma chini ya Ofisi ya Rais, imepewa madaraka ya kufuutilia viongozi wa umma na matumizi mabaya ya madaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inaona kuwa tatizo kubwa lipo kwenye uwezo wa Tume hii katika kuhakiki taarifa ambazo zinaandikwa kwenye fomu hizi na viongozi mbalimbali wa umma. Hii ni kutokana na ukweli kuwa Tume hii ina watumishi wachache na pia ipo Dar es Salaam tu ilihali ina jukumu la kuhakiki taarifa za viongozi mpaka ngazi ya Kata kitu ambacho kwa uhalisia wake hakiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hitaji la kurejesha kwa wakati, ukweli kuhusu taarifa zilizojazwa katika fomu, ni muhimu sasa uwekwe utaratibu mahsus wa kuratibu ukweli wa taarifa za viongozi zilizojazwa katika fomu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii inawataka Madiwani na wao wajaze fomu hizo za kutangaza mali zao. Nchi hii ina Kata 4060. Fomu zote hizi pamoja na nyingine nyingi zinarejeshwa kwa Sekretarieti ya maadili ya viongozi Makao Makuu Dar es Salaam na kama kuna tatizo, wanawajibika kuitwa Dar es Salaam kukutana na Sekreatrieti. Pamoja na nia njema iliyokusudiwa, jambo hili linaweza kuwa la usumbufu mkubwa kwa wale waishio mbali na Dar es Salaam na zaidi wale ambao utumishi wao wa umma hauna kipato kikubwa cha kuwawezesha kujitegemea kuja Dar es Salaam kuonana na Sekreatrieti wanapohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema sasa ukawekwa utaratibu wa mpito utakaopunguza mzigo huu kwa Sekretarieti Makao Makuu, ili kuiwezesha kushughulika na viongozi katika ngazi ya Taifa na wale wote walio katika nafasi nyeti. Mamlaka ya ukusanyaji, uhakiki na uratibu wa viongozi katika ngazi ya Kata, Tarafa na Wilaya ufanywe katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa chini ya uratibu wa Sekreatrieti ya Taifa. Kutokana na unyeti wake, Katiba mpya inayokusudiwa iliangalie kwa kina jambo hili na kuliwekeea mfumo madhubuti utakaosaidia utekelezaji na ufanisi wake kwa mujibu wa mfumo wa utawala utakavyokuwa kwenye Katiba mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri pia, kuwa sheria hii inasisitiza viongozi katika ngazi za utawala (*senior public servants*) katika utumishi wa umma na sio wote, lakini hali halisi inaonyesha kuwa kuna watumishi wa umma ambao sheria haiwataki kupeleka taarifa zao kwenye tume lakini ukweli ni kuwa watumishi hawa mionganii mwao wapo ambao wanamiliki mali ambazo hazielezeki wamezipataje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili wananchi waone kuwa sekretarieti hii ya maadili ya viongozi wa umma ina maana kwa wananchi na nchi kwa ujumla, wananchi wawe na uwezo wa kuelewa viongozi wao wameorodhesha mali kiasi gani na ziko wapi, kwani wananchi wanaelewa vema kama wamesema uongo au wamesema ukweli. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inashauri sheria hii ifanyiwe utaratibu wa kuondoa kifungu kinachotaka mtu anayetaka kuelewa mali za kiongozi wake kulipia na pia sharti la kutokuchapisha au kutoa taarifa hiyo popote pale kwani hawa ni viongozi wa umma na hivyo wote wanawajibika kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi mabaya ya fedha za umma katika Halmashauri yameendelea kuwa kikwazo kikubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya wananchi. Uchambuzi wetu juu ya ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu hesabu za Halmashauri 133 zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2009/2010 pekee, umebaini takriban jumla ya Shilingi bilioni 233.4 zilitumika vibaya, sawa na asilimia 10 ya fedha zote zilizotumiwa na Halmashauri hizo ambazo jumla yake ilikuwa takriban Shilingi trilioni 2.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano ya fedha zilizopotea au kutumiwa vibaya katika Halmashauri kwa mwaka huo wa fedha wa 2009/2010, ni matumizi yasiyokuwa na hati za malipo ya jumla ya Shilingi bilioni 2.8, malipo yenye nyaraka pungufu ya jumla ya Shilingi bilioni 5.5, mishahara isiyolipwa ambayo haikurejeshwa Hazina ya jumla ya Shilingi bilioni 1.1, mishahara iliyolipwa kwa watumishi waliostaafu, kuachishwa kazi na watoro ya jumla ya Shilingi milioni 583, 221, 297 na maduhuli ambayo hayakurejeshwa na mawakala wa kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi bilioni 2.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha nyingine zilizotumiwa vibaya ni za wadaiwa wasiolipa za jumla ya Shilingi bilioni 44, wadai wasiolipwa za jumla ya Shilingi bilioni 52. Utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka iliyopita jumla ya Shilingi bilioni 122, vifaa ambavyo havikuingizwa katika vitabu jumla ya Shilingi milioni 577.5 na fedha za mikataba na miradi yenye nyaraka na kumbukumbu pungufu ya jumla ya Shilingi bilioni 1.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa matumizi yote mabaya ya fedha za umma yaliyofanywa katika Halmashauri zote zilizokaguliwa kwa mwaka huo wa fedha wa 2009/2010, ambayo jumla yake ni takribani Shilingi trilioni 2.3 umo katika viambatanisho vya hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, upotevu huu na matumizi mabaya ya fedha za umma katika Halmashauri umekuwa ukisababishwa pamoja na mambo mengine, yafuatayo:-

- (i) Kutofuatwa kikamilifu kwa viwango vya Kimataifa vya uhasibu katika sekta ya umma (*IPSAS*).
- (ii) Kutofuatwa kikamilifu kwa misingi ya uhasibu na matakwa ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa mwaka 2000) na *Memoranda* ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1997.
- (iii) Kutofuatwa kikamilifu kwa Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005.
- (iv) Kutotekelawa kwa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa na *CAG* ya miaka ya fedha iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo huu wa upotevu mkubwa wa fedha za umma hauvumiliki hasa ikitiliwa maanani kuwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kila mwaka amekuwa akitoa mapendekezo ya kudhibiti hali hii, lakini mapendekezo mengi yamekuwa yakipuuzwa au kutozingatiwa kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchoro hapo chini unaonyesha jinsi ambavyo upotevu wa fedha za umma ulifanyika kwenye Halmashauri zetu mbalimbali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010 kama ilivyoripotiwa na katika ripoti ya *CAG*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ubadhirifu katika manunuzi ya bidhaa na huduma Serikalini. Kabla sijaanza kusoma hotuba yangu sehemu hii, naomba kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Serikali maneno aliyoyasema Waziri Mkuu wa zamani wa Uingereza, Tony Blair akihitubia Mkutano Mkuu wa Chama chake cha *Labour* ambacho ni rafiki wa Chama cha Mapinduzi: “*The Radical decision is usually the right one. The right decision is usually the hardest one; the hardest decisions are often the least popular at the time. We are at our best when we are at our boldest*”. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri nyepesi na isiyo rasmi ya nukuu hii ni kuwa, kufanya maamuzi magumu ya kijasiri pamoja na ugumu wake hususan mwanzoni ndiyo njia sahihi ya kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ndicho chombo kikuu kinachoongoza kwa matumizi na kwa mujibu wa sheria zetu, matumizi haya hufanywa na kuhalalishwa na mfumo wa kutumia zabuni . Asilimia 70 ya matumizi ya Serikali hufanywa kuititia sheria ya manunuzi ya Umma ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza sheria hii, baadhi ya watumishi wa umma wasio waaminifu kwa kushirikiana na wafanyabiashara, hutekeleza azma yao ya wizi wa kitaasisi ambapo taratibu zote za kisheria zinafuatwa na hivyo kumfanya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kushindwa kugundua wizi huu. Hali hii, huwafanya wazabuni wasio waaminifu kwa kushirikiana na watendaji Serikalini kuiuzia Serikali bidhaa na huduma kwa bei ya juu ambayo katika mazingira mengine hufikia hadi 200% ya bei halisi katika soko. Aidha, hali hii huchochewa kwa kiwango kikubwa kwa utaratibu uliopo wa kuchagua wazabuni maalum kwa kipindi maalum kutoa huduma mbalimbali Serikalini na hivyo kuwapa fursa ya kujenga mahusiano yasiyo na nia njema na watumishi wa umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi mwengine amba ni wa kitaasisi ni ule amba kila kunapotokea tukio lolote la Kitaifa, makongamano, semina, warsha, kampeni maalum kama za UKIMWI, malaria na kadhalika. Taasisi na Idara za Serikali huandaa vitu vya uhamasishaji visivyo vya lazima kama vile kofia, *t-shirts*, mabegi ya kubebea nyaraka na kadhalika na kuvigawa bure. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kila mwisho wa mwaka au wakati wa sikukuu mbalimbali, umekuwa ni utamaduni kwa taasisi za umma, Serikali na Idara zake kushindana kutengeneza *diary*, kalenda na kadi za salaam na kuzisambaza bure. Aidha, kumekuwepo na utamaduni mbaya wa taasisi za umma kutumia gharama kubwa kupongezana kuititia vyombo mbalimbali vya habari na katika hili, natangaza maslahi kwani nina mahusiano ya karibu na baadhi ya vyombo vya habari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wa vitu hivi, ni dhahiri haviwezi kuwa vipaumbele katika matumizi ya umma hususan katika Taifa maskini. Aidha, tunaamini kila kiongozi au mtumishi wa umma na ninarudia Mheshimiwa Mwenyekiti,

aidha, ninaamini na Kambi nzima ya Upinzani naamini kwa kila kiongozi au mtumishi wa umma, mwenye kujua matumizi ya *diary*, hawezi kusubiri kugawiwa *dairy* za bure kwani huwa tayari ana *diary* ya mwaka unaofuata kuanzia mwezi wa kumi wa mwaka unaomalizika. Ni vyema kuikumbusha Serikali vilevile kuwa kila simu ya mkononi ina *diary* na kalenda na tunaamini kila kiongozi na mtumishi wa umma ana simu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni nyingi zinazopewa zabuni hizi ukiangalia zina mahusiano ya karibu na watendaji wa Taasisi au Idara husika na kutokana na ukaribu wao huo huwa bei ya bidhaa wanazouza zinakuwa ni zaidi ya bei halisi ya soko na hivyo kufanya Serikali kuingia hasara kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi huu wa kitaasisi umeendelea kuliumiza Taifa. Kwa kasi hii ya matumizi, inatia shaka kama kweli kuna dhamira ya kweli na utashi wa kisiasa kwa Serikali kukabiliana na umaskini wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali sasa kupiga marufuku utengenezaji na usambazaji wa bure wa *diaries*, kalenda, *t-shirts*, kofia, mabegi, kadi na vitu vingine kadhaa visivyo na tija na kuelekeza fedha hiso kwenye matumizi mengine ya lazima ya kupunguza umaskini wa Taifa hili. Tunashauri vilevile uboreshaji wa Sheria ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma uzingatie kuthibiti wizi huu wa kitaasisi. Aidha, kuna ulazima sasa wa kuiuhisha upya Sheria Namba Tisa ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 pamoja na marekebisho yake kadhaa iweze kuendana na mazingira ya sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitumia gharama kubwa kwa ajili ya kununua na kuhudumia magari aina ya shangingi wanayopewa viongozi na watumishi mbalimbali wa umma. Magari haya mara nyingi yamekuwa yakibadilishwa mara kwa mara *model* inapobadilika na kupelekea yale ya zamani kuuzwa katika utaratibu na bei zilizo tofauti sana na soko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mzigo mkubwa usio wa lazima kwa Watanzania na ni hakika siyo kipaumbele katika kutumia kwa busara rasilimali kidogo za Taifa letu. Magari haya yamekuwa mojawapo ya chanzo kikubwa cha chuki na narudia, magari haya yamekuwa mojawapo ya chanzo kikubwa cha chuki kati ya viongozi, watumishi wa umma na wananchi ambao hawaoni umuhimu wa magari haya ya gharama kwa kila kiongozi au mtumishi wa kada ya juu katika Taifa lao. (*Makofi*)

Kambi ya Upinzani baada ya kuliangalia kwa undani suala hili na kutafakari kauli ya Serikali kuwa inakusudia kuweka utaratibu maalum wa ununuzi wa magari haya siku za usoni na kwa kuwa tayari magari haya yako mengi sana kwa maelfu nchini, tunapendekeza kuyauza kwa mnada magari haya aina ya shangingi yanayotumiwa na viongozi hawa katika kipindi kisichozidi miezi sita ili kuipa Serikali muda wa kutosha kutengeneza utaratibu sahihi wa kutekeleza azma au ushauri huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ushauri wa Kambi ya Upinzani kwa Serikali, wananchi wanasilika, ili kutokuwakwaza viongozi na watumishi wa umma, Serikali

iwakopeshe magari ya chaguo lao watendaji wake kutokana na utaratibu huo utakaowekwa. Serikali iwe na magari machache kwenye *pool* yatakayotumiwa na watumishi na viongozi wake wanapokuwa kwenye safari za kikazi nje ya mizunguko ya kawaida ya kazi zao. Magari haya ya Serikali yawe ya gharama nafuu isipokuwa yale yatakayokuwa ya kazi maalum. Aidha, magari ya misafara ya viongozi wakuu nayo yawekewe utaratibu wa idadi na aina ambapo utajali na kukidhi hali halisi ya umaskini wa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu utakuwa na faida kadhaa zikiwemo zifuatazo kwa Taifa na viongozi au watumishi wa umma, kwanza, Taifa litaokoa fedha nyingi zitokanazo na ununuzi huu wa mashangingi, pili, Taifa litaokoa fedha nyingi zinazotumika katika kuyahudumia mashangingi haya na tatu, viongozi na watumishi wa umma watakuwa na magari wakati wa kumaliza uongozi wao au wakati wa kustaafuli, mikataba au ajira zao za kazi kwani watakuwa na magari tangu wanapokuwa watumishi na kuyatunza yale magari, wakistaafu wataondoka nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nidhamu ya utunzaji magari itakuwepo, kwani kila mtu atatunza gari lake kikamilifu. Ni ushuhuda usiopingika kwamba magari haya ya gharama kubwa hupakiwa mizigo mingine iliyozidi hata uzito unaostahili. Kwa sababu hakuna uchungu wa magari haya. Madereva au na mabosi wao vilevile wanaweza wakapakia mkaa, wakapakia mchanga, kwa sababu ni gari la umma halina uchungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa rahisi kwa Serikali yetu kudhibiti magari machache yaliyoko kwenye *pool* kuliko ilivyo sasa ambako nina hakika kuna magari mengi na hata uwezo wa Serikali yote unakuwa ni tatizo kidogo. Utaratibu huu siyo mgeni kwa nchi yetu kwani taasisi ya umma kama Benki Kuu ya Tanzania inautumia tayari. Nchi jirani kama Rwanda nayo inafuata utaratibu huu huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utaratibu wa viongozi wa Serikali wanaposafiri nje ya nchi, wanasafiri kwa daraja la kwanza na daraja la pili (*business class*) tu bila kujali kuwa maafisa wanaombatana na misafara hiyo wako daraja gani la utumishi wa umma na hili linaifanya Serikali kutumia fedha nyingi bila sababu za msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narejea, Kambi ya Upinzani tunapendekeza kuwa ili kuondokana na upotevu huu wa fedha za umma kwa ajili ya gharama za safari, Serikali itoe Waraka kuhakikisha kuwa ni viongozi wakuu na wenzi wao tu ndiyo waruhusiwe kwa kutumia daraja la kwanza yaani *first class*.

Pili, wanaposafiri kwenda nje ya nchi kwenye majukumu yenyе maslahi kwa Taifa na viongozi hao watajwe kuwa ni Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jaji Mkuu, pamoja na viongozi wastaafu wa nafasi hizo, wasaidizi wa viongozi hawa wasafiri daraja la *economy*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waraka huo pia utaje kuwa Mawaziri wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama pamoja na Wakuu wa Taasisi nyeti katika Taifa watasafiri kwa kutumia daraja la pili yaani *business class* pale wanaposafiri safari za Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wengine wote wa umma na watumishi wa umma wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wasafiri kwa kutumia daraja la kawaida yaani *economy class*. (*Makofi*)

Pia misafara ya viongozi wakuu ipunguzwe ili kupunguza gharama za kuhudumia misafara hiyo pindi wanaposafiri nje ya nchi sambamba na kuepuka gharama kubwa ya mahoteli nje ya nchi ambayo misafara ya viongozi wa nchi yetu hufikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwajibikaji wa viongozi na watumishi wa umma, kwa sababu ya mfumo mbaya wa utawala, utafiti wa hivi karibuni uliofanywa na Benki ya Dunia unaonyesha kuwa Tanzania ni mionganoni mwa nchi zilizokumbwa na tatizo la kile kinachoitwa rushwa ya kimya yaani *silent corruption*. Hii ni rushwa ambayo watendaji wa umma hawakai maofisini na muda mwangi wa kazi wanautumia kwa kazi za binafsi badala ya kutoa huduma kwa wananchi. Aidha, wengi wao wawapo kazini, bado hawatekelezi wajibu wao ipasavyo. Muda mwangi wa kazi usio wa mapumziko hutumika kusoma magazeti, kunywa chai na vitafunio mbalimbali vikiwemo vitumbua, chapati, mayai ndani ya ofisi, sambamba na kugeuza ofisi na sehemu nyingine za kazi kuwa vijiwe vya kujadili mambo mbalimbali yasiyohusiana moja kwa moja na kazi zao, kama michezo na kadhalika. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbewe, hivyo vitafunio havijaandikwa. Kwa hiyo, iambie *Hansard* inukuu na hivyo vitafunio unavyovitaja. (*Kicheko*)

**MHE. FREEMAN A. MBOWE - KIONGOZI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI:** Nimekusikia Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wenzetu wa upande wa Serikali wakieleza kuwa hali ngumu ya maisha imesababishwa na msukosuko wa uchumi wa dunia, uchambuzi wa kina tuliofanya Kambi ya Upinzani umegundua uwajibikaji wa viongozi na watumishi wa umma umekuwa sababu kuu ya hali mbaya ya kiuchumi inayowakabili Watanzania. Mazingira haya yamesababishwa pamoja na mambo mengine haya yafuatayo, watumishi wa umma kuwa na morali mdogo wa kazi na kukosa uzalendo, hali inayosababisha pia utendaji dhaifu na vitendo vya ubadhirifu wa mali ya umma na ufisadi. (*Makofi*)

Pia kukithiri kwa vitendo vya ufisadi ambavyo vimehusisha na vinaendelea kuhusisha ajira za upendeleo bila sifa katika Serikali na taasisi za umma kwa upande mmoja na viongozi wa kisiasa, jamaa na marafiki zao kwa upande mwingine na kukosekana uzalendo, uadilifu, umakini na upeo mionganoni mwa viongozi wa kisiasa kunakosababishwa na kukosekana mfumo imara wa kutambua, kupika na kutathmini utendaji wa viongozi wa umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa uthibiti makini wa nidhamu katika Serikali na taasisi zake na ajira za watumishi wengi wa umma kutokuwa na maelekezo rasmi yanayopimika ya wajibu wa kila siku, kila wiki na hatimaye kwa mwezi (*specific and measurable daily, weekly and monthly job description*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri Serikali iweke utaratibu mzuri utakaowajibisha na utakaoweza kuwapima kiutendaji viongozi na watumishi wa umma, ili pale wanapoonekana kushindwa kutekeleza majukumu yao, waweze kuondolewa mara moja na hivyo kutokuendelea kuwa mzigo kwa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kukosekana kwa ufanisi katika utendaji Serikalini na kwenye taasisi za umma ni ukweli ulio wazi yaani *open secret* na madhara yake yana athari kubwa katika utoaji huduma kwa wateja na hatimaye kuathiri kwa kiwango kikubwa kutokutimia kwa malengo ya Serikali, ni vyema sasa Serikali ikawa na mkakati maalum wa kuboresha na kuhuisha mazingira ya kazi katika ofisi na taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugatuaji wa madaraka kwa Serikali za Mitaa, mnamo mwaka 1996, Serikali ilikuja na Dira ya Maboresho ya Serikali za Mitaa iliyolenga kufanikisha mambo makuu matatu:-

Kwanza kuunda mfumo wa Serikali za Mitaa utakaojikita katika ugatuizi wa maamuzi na kuhamisha majukumu na rasilimali kwenda ngazi za msingi ndani ya mfumo mmoja wa Serikali (*political devolution and decentralization of functions and finance within the framework of a unitary state*). Pili, Serikali za Mitaa ziwe jumuishi (*holistic*) kwa idara na nyanja zote zikiwa na misingi na kutambulika kisheria (*corporate body operating on the basis of discretionary but general powers*).

Tatu, kujenga Serikali za Mitaa zenyе mamlaka, zenyе nguvu pana, zinazojitegemea, zinazoendeshwa kidemokrasia na kupata uhalali wake kutokana na huduma zake kwa jamii (*autonomous institutions, democratically governed and deriving their legitimacy from the services they provide to the people*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza dira hiyo, Serikali ilijiwekea malengo yafuatayo ili kuboresha Serikali za Mitaa:-

Kwanza kuimarisha ushiriki wa moja kwa moja wa jamii katika kuendesha Serikali zao na kuchagua madiwani, pili, kuweka huduma za jamii chini ya usimamizi wa jamii kuititia Halmashauri zao, tatu, Halmashauri kuwa na nguvu za kisiasa na maamuzi juu ya mambo yote ndani ya maeneo yao na nne, kuimarisha uwazi na uwajibikaji wa fedha, rasilimali na maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, kukusanya rasilimali na fedha kwa huduma za jamii, sita, kujenga utawala utakaowajibika kwa jamii na kupunguza muingiliano wa watendaji wa Serikali za Mitaa toka kwa Wizara mama na saba, kuweka mfumo mpya wa mahusiano kati ya Serikali za Mitaa na Serikali kuu unaozingatia Sheria, Kanuni na majadiliano na sio amri na maagizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kuhakikisha kuwa Halimashauri zinakuwa na uwezo wa kuajiri watumishi wake haswa watendaji wa vijiji, Kata, madereva na wengineo bila kuomba kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi kwani hili ni kinyume na falsafa ya ugatuaji wa madaraka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine, Dira ya Maboresho ya Serikali za Mitaa ililenga kupunguza urasimu wa kiutawala na kurahisisha utekelezaji wa shughuli zote zinazolenga kumletea mwananchi maendeleo ya haraka. Hata hivyo, leo ikiwa ni miaka mitano imepita tangu kuanza kwa mfumo huu, bado malengo mengi hayajatekelezeka kikamilifu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya Malengo ya Dira ya Maboresho ya Serikali za Mitaa na dhana ya ugatuaji wa madaraka ni kutaka Halmashauri ziwe na uwezo wa kutosha wa kujitegemea kirasilimali zikiwemo rasilimali fedha, ili ziwe na uhuru wa moja kwa moja wa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa manufaa ya wananchi wa maeneo husika na wakati huo huo zikipaswa kuchangia mapato ya kutosha katika Bajeti Kuu ya Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mpango wa Maboresho ya Serikali za Mitaa ukiwa ulilenga hivyo takriban miaka mitano iliyopita, bado mpaka sasa Halmashauri nyingi zinategemea Serikali Kuu kwa kiasi kikubwa na cha kutisha. Kwa wastani, Bajeti za Halmashauri zimekuwa zikitegemea ruzuku kutoka kwa Serikali Kuu kwa wastani wa kati ya asilimia 82 hadi asilimia 96. Hata katika mwaka huu wa fedha wa 2011/2012, mchango wa Halmashauri zote kwa Bajeti ya Serikali umeonekana kuwa ni asilimia tatu tu ya Bajeti yote. Huu ni mchango mdogo sana na mazingira haya yanatisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ndizo zinazopaswa kuwa chanzo kikuu cha mapato yote ya Serikali kwani zipo karibu na fursa zote za kiuchumi. Hata hivyo, badala ya Halmashauri kuwa chachu ya ongezeko la mapato ya Serikali, zenyewe ndio zimekuwa zikisubiria kutafuna kile kinachookotewa na kuelekezwa kwake na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madaraka nusu nusu yaliyotolewa kwa Halmashauri zetu pamoja na uwezo mdogo wa Halmashauri zenyewe katika kuvuna na kuzigeuza rasilimali na fursa zilizopo kuwa mapato ya kiuchumi, ndio unaosababisha Bajeti ya Serikali Kuu iwe ndogo, hivyo nchi kubaki ikitegemea misaada ya nje na wahisani kila mwaka. Hali hii ndiyo pia inayokwamisha au kusababisha utekelezaji wa mipango mingi ya maendeleo ya Kitaifa kusuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwa na mgongano mkubwa baina ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa dhana ya ugatuaji madaraka. Mfumo wa Bajeti unaotumiwa na Halmashauri katika kutengeneza mipango na Bajeti yaani Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (*O&OD*) huzingatia zaidi kuibua mipango kutoka kwa jamii za vijiji na mitaa. Hata hivyo, utekelezaji wa mfumo huu wa Kibajeti umekuwa ukigongana moja kwa moja na mfumo wa Serikali na Wizara zake katika uandaaji wa Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiashiria kingine cha kutotekelezeka kwa dhana ya ugatuaji wa madaraka, ni Halmashauri kutopewa mamlaka ya moja kwa moja ya kuajiri watumishi kulingana na mahitaji yake. Badala yake, kabla ya kuajiri zimekuwa zikilazimika kuomba kibali cha kuajiri kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi (Serikali Kuu). Kwa hali hii, ni dhahiri kuwa tuko nyuma katika utekelezaji wa falsafa hii ya kiutawala, kwani bado madaraka yanayopaswa kuwa katika Halmashauri, yapo mikononi mwa Serikali kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mikoa na Wilaya ikiendelea kutumia bila kuzalisha, Serikali inajikita katika kuongeza idadi ya Mikoa na Wilaya na hii ni kuongeza gharama za utawala na ndio maana Bajeti ya uendeshaji wa Serikali kwa ujumla wake ni kubwa kuliko Bajeti ya Maendeleo na hii inatokana na ukweli kuwa mfumo uliopo ni wa kutumia zaidi badala ya kuzalisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa pamoja na mipango kadhaa iliyopo na inayoendelea, mgawanyo wa madaraka kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ni jambo litakalojadiliwa kwa kina katika mchakato unaokusudiwa wa uandikaji wa Katiba mpya ya nchi yetu. Hata hivyo, ni vyema dhana ya kujenga misingi ya fikra za kujitegemea zikaanza kujengeka katika Halmashauri zetu sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri mambo yafuatayo yazingatiwe ili kuanza kutekeleza azma ya kujitegemea na hatimaye kuweka misingi ya kutekeleza kikamilifu dhana ya ugatuaji wa madaraka kwa maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuzipa nguvu za kiuchumi, Kambi ya Upinzani inashauri Serikali za Mitaa zijengewe uwezo wa kiufundi wa kuandaa na kutekeleza Mipango mikubwa ya Maendeleo ya Kiuchumi ya Wilaya (*District Economic Development Master Plan*) ambayo itazingatia namna ya kutumia moja kwa moja rasilimali na fursa zilizopo katika maeneo yao kukuza uchumi wao na kujiletea maendeleo, bila kuingiliwa moja kwa moja na kwa kiasi kikubwa na na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango kama hii inaweza kuweka malengo mbalimbali kwa maendeleo ya wilaya kulingana na hali halisi ya maeneo husika, mathalan kutengeneza ajira zisizopungua 2,000 kwa mwaka ili kulifanya Taifa liwe na ajira nyingi na zilizosambaa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunapendekeza kuandaliwe mashindano maalum ya kila mwaka ya kupima uwezo wa kila Halmashauri ndani ya mkoa husika wa kuibua vyanzo vya uwekezaji vinavyopimika, vinavyotekelzeza na vyenye tija kwa maendeleo ya watu wa eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji wakuu katika wilaya zinazofanya vizuri watambuliwe kimkoa na zoezi hilo la ushindani kwa Halmashauri zinazofanya vizuri liende hadi ngazi ya Taifa na zawadi au tuzo mbalimbali zitolewe kwa wahusika ili kuchochea ari ya ubunifu na uwajibikaji kwa maendeleo ya haraka ya wananchi. Halmashauri zitakazoshindwa, nazo ziwe zikipewa stahiki zao za kushindwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunaamini kuwa changamoto hizi za uandaaji na utekelezaji wa mipango ya kina ya maendeleo ya wilaya pamoja na ushindani wa Halmashauri, vitasaidia kuondoa dhana iliyojenjeka kwa watendaji wa ngazi za mikoa na wilaya kukaa mkao wa kupokea fedha kutoka Serikali Kuu na kuzitumia tu bila kufikiria kuwa nao wana wajibu mkubwa wa kuziongoza Halmashauri na Mikoa yao kupata mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema kwenye Bajeti mbadala ya fedha tutaendelea kusisitiza kuwa kipaumbele chetu cha muhimu ni kuwezesha ukuaji wa sekta za uzalishaji na hasa ukuaji wa uchumi wa vijijini (*rural growth*). Kambi ya Upinzani inakichukulia kipaumbele hiki kama tiba halisi ya kuwaondolea umaskini Watanzania waishio vijijini kwa kuwa asilimia kubwa ya Watanzania wanaoishi vijijini maisha yao yanaendeshwa na shughuli zinazohusiana na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutimiza azma ya kuinua maisha yao, miundombinu ya barabara na umeme itachochea ujenzi na ukuaji wa viwanda vidogo vidogo vya kuongeza thamani za bidhaa zizalishwazo vijijini, ni dhahiri pia asasi za fedha zitaenda zenyewe na pia itasaidia kupunguza uhamiaji wa kutoka vijijini kwenda mijini (*rural urban migration*) kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kwa njia hii tutafanikiwa kuondoa umaskini uliokithiri na pia kuondoa nchi yetu kwenye hatari ya kuwa Taifa la wachuuzi. Pendekeso kubwa katika kuchochaea ukuaji wa uchumi wa vijijini ni la kupeleka vijijini shilingi bilioni 450 kila mwaka kwa miaka mitano mfululizo katika sekta za barabara za vijijini, umeme vijijini na maji vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jukumu pia la viongozi wa Halmashauri kushirikiana kikamilifu na sekta binafsi katika nyanja mbalimbali ili kuchochaea uwekezaji wa kutosha na wa moja kwa moja wa miradi ya maendeleo katika ngazi hizo za chini, bila kutegemea Serikali Kuu kwa kila jambo kubwa kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhamishia Makao Makuu Dodoma. Itakumbukwa kwamba mwaka 1973 Serikali ilifanya uamuzi wa kuhamishia Makao Makuu ya nchi kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma chini ya Programu ya Ustawishaji Makao makuu. Aidha, maandalizi ya mpango kabambe wa kuwezesha uhamiaji huo yalikamilishwa, kupata idhini na programu kuanza kutekelezwa rasmi mwaka 1976.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ikiwa ni miaka takribani 38 tangu kuitishwa kwa uamuzi huo na maandalizi hayo, bado sehemu kubwa ya Serikali ipo Dar es Salaam na leo ni miaka 38 tangu uamuzi huu ufikiwe, asilimia 80 ya Serikali bado iko Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Serikali iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Bunge inaonyesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2011/2012, inaonyesha kuwa kwenye

Kasma 6351, Serikali imeomba kiasi cha shilingi bilioni nne kwa ajili ya kujenga Ofisi ya Waziri Mkuu Dar es Salaam na makazi ya Waziri Mkuu Dodoma. Wakati huo huo mionganini mwa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu yaliyopo kwenye mgawanyo wa kazi kwa mujibu wa *instrument* ya Disemba 17, 2010, ni kusimamia na kuhakikisha kuwa Makao Makuu yanahamia Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa pia Kambi ya Upinzani tunaihoji Serikali, iweje pawe na mpango wa Serikali kuhamia Dodoma, ilihali wakati huo huo Serikali inaomba kutengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Waziri Mkuu jijini Dar es Salaam, Mtaa wa Luthuli. Kwa hali hii, inazidi kuonyesha kuwa Serikali yenyele iliyoamua kuhamia Dodoma haina dhamira ya dhati ya kufanya hivyo na ndio maana miaka 38 imepita bila mpango huo kufanikiwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema ikazingatiwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Mamlaka ya Ustawishaji wa Mji wa Dodoma ilitengewa Bajeti ya shilingi bilioni 1.6 lakini hadi kufikia mwezi Aprili, 2011, mamlaka hiyo ilikuwa imepokea shilingi milioni 150 tu. Huu ni ushahidi ulio dhahiri kabisa unaoashiria kuwa Serikali haina dhamira ya kuhamia Dodoma, kwani Bunge limekuwa likiidhinisha fedha kwa ajili hiyo, lakini huwa hazitumiki kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamo wetu na ushauri wetu kuhusu mpango wa kuhamia Dodoma. Tunataka Dodoma uwe ni Mji Mkuu wa elimu Tanzania na Makao Makuu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tumeutafakari na kutathimini kwa kina mwenendo wa utekelezaji wa mpango wa Serikali kutaka kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi na tumejiridhisha kuwa Serikali haionyeshi jitihada za dhati za kuhakikisha jambo hilo linafanyika hivyo. Aidha, tunaamini Serikali imekosa ujasiri wa kukiri kushindwa kwa mpango huu kwa sababu mbalimbali ikiwamo kukosekana kwa utashi wa kisiasa kama ilivyokuwa kwa muasisi wa fikra hii hayati, Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa fedha nyingi za walipa kodi zilikwishatumika kujenga ofisi zote za Serikali katika jiji la Dar es Salaam; na kwa kuwa Ofisi za Serikali kama Ofisi ya Waziri Mkuu, bado zinaendelea kujengwa jijini Dar es Salaam; kwa hiyo, Kambi ya Upinzani haioni busara ya Serikali kutaka kutumia vibaya mabilioni ya fedha za wananchi kujenga Ofisi za Serikali mjini Dodoma wakati tayari ofisi hizo zilikwishajengwa jijini Dar es Salaam na zinaendelea kutumika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya kutumia vibaya fedha za walipa kodi kufanya kitu kile kile cha ujenzi wa majengo ya ofisi za Serikali ambayo tayari yamekwishajengwa Dar es Salaam; Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali iendelee kutenga fedha za kutosha katika kila Bajeti ya mwaka, kwa ajili kuufanya mji wa Dodoma kuwa Mji Mkuu wa Elimu (*Academic City*) na Makao Makuu ya Bunge (*Parliamentary City*); iachane na mpango wa Serikali kwa sababu mpango huu umeshindwa kwa miaka 38. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo letu la kuufanya Mji wa Dodoma kuwa *Parliamentary City* na *Academic City*, linazingatia ukweli kuwa tayari tuna jengo kubwa na eneo la kutosha la Bunge na tayari kuna Vyuo Vikuu, hivyo ni rahisi kuendelea kujenga shule za sekondari nyingi zaidi na Vyuo Vikuu vingi zaidi vyenye hadhi ya Kitaifa na Kimataifa na mji kuwa Makao Makuu ya Kielimu na Makao Makuu ya Bunge, bado uchumi wa mji unakuwa kwa kasi ya haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mji wa Dodoma kijiografia upo katikati ya nchi, basi utakuwa ni mji muafaka zaidi kwa wanafunzi kutoka pembe mbalimbali za nchi kuja kusoma kwenye shule za sekondari, vyuo vya ufundi na vyuo vikuu vingi tunavyopendekeza vijengwe Dodoma. Aidha, jiografia ya mji huu ya kuwa katikati ya nchi, itaendelea kuwa kiunganishi kizuri kwa wawakilishi wa wananchi (Wabunge) kuendelea kukutana hapa Dodoma kwa ajili ya kujadili na kupitisha maamuzi yetu ya Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010; daftari la kudumu la wapiga kura. Tume ya Taifa ya Uchaguzi (*NEC*) ndiyo yenye jukumu la kutunza daftari la wapiga kura Kikatiba na kisheria. Hata hivyo, katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 kulikuwa na mapungufu mengi yaliyosababisha watu wengi kushindwa kupiga kura kwa sababu mbalimbali ikiwemo daftari kuchelewa kufika katika vituo vya wapiga kura ili kuhakiki majina yao. Kulikuwa na makosa ya kiuchapaji ya majina ya wapiga kura na kukosekana kwa takwimu halisi za wapiga kura katika daftari. Mapungufu haya na mengine mengi yaliyojitokeza katika uchaguzi huo yanatosha kabisa kuonyesha kuwa uchaguzi huo haukuwa wa huru wala wa haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapungufu haya yamebainishwa pia na waangalizi mbalimbali wa uchaguzi wa ndani na wa nje kama vile timu ya Jumuiya ya Ulaya, timu ya Umoja wa Afrika , Timu ya SADC pamoja na waangalizi mbalimbali wa ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria zinazoratibu Uchaguzi. Uchaguzi Mkuu huwa unaratibiwa kwa kuzingatia Katiba iliyopo na Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985, Sheria ya Gharama za Uchaguzi 2010, Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (Uchaguzi) ya mwaka 1979 na Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 kulijitokeza tatizo la karatasi za kura kufutika mara baada ya zoezi la kura kumalizika. Itakumbukwa kuwa katika Bunge la Bajeti la mwaka 2010/2011 Waziri wa Sera, Uratibu na Bunge wakati huo Mheshimiwa Phillip Marmo, aliyekuwa Mbunge wa Mbulu alitoa tamko kwenye Bunge hili kuwa karatasi za kura zitachapishwa hapa nchini na Mpigachapa Mkuu wa Serikali lakini Mkurugenzi wa *NEC* akiwa kwenye kikao cha Tume na Vyama vya Siasa kilichofanyika Dar es Saalam, alipingana na tamko hilo akisema kuwa karatasi zitachapishwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inataka kupata taarifa, je, ni shirika au kampuni gani ilitumika kuchapisha karatasi za kura ambazo zilikuwa chini ya kiwango kiasi hicho hata kufanya karatasi hizo zifutike mapema kiasi hicho? Je, ni Mpigachapa Mkuu wa Serikali ndiye aliyechapisha karatasi hizo kama Bunge lilivyokuwa limetaarifiwa wakati ule? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 uligubikwa pia na matatizo mengine mbalimbali na haswa kubwa likiwa ni kucheleweshwa kutangazwa kwa matokeo kwenye Halimashauri mbalimbali hapa nchini na haswa kwenye Majimbo ya Uchaguzi kama vile Nyamagana, Ilemela, Arusha Mjini, Hai, Moshi Mjini, Ubungo, Kawe na kadhalika. Majimbo haya ni ya maeneo ya mjini na hivyo hoja kuwa miundombinu ilikuwa ni tatizo sio sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali ilifahamishe Taifa kwa majibu ya uhakika kuwa ni kitu gani kilipelekeea wasimamizi wa uchaguzi kucheleta kutangaza matokeo kwenye maeneo mbalimbali ya nchi na haswa kule ambako Vyama vya Upinzani na hususani CHADEMA walikuwa wameshinda chaguzi hizo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu Maafa. Idara hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni idara muhimu na pana sana japokuwa kuna udhaifu mkubwa unafanywa na watendaji na kuionyesha idara hii kuwa ni idara inayoendeshwa zaidi kwa misingi ya siasa katika kusimamia haki na matatizo/maafa yanayojitokeza katika Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa Idara hii kwa wananchi haupo tu kwenye suala la njaa bali ni katika maeneo mengine kama afya, mafuriko na wakati wa milipuko ya magojwa ambayo yanatakiwa kuratibiwa kwa karibu sana. Pamoja na majukumu haya ya ofisi hii muhimu, Kambi ya Upinzani inapenda kupata majibu kuhusu mfuko huu kwani kwenye maafa kama ya Gongo la Mboto na mafuriko ya Kilombero walijitokeza wadau mbalimbali ambao walichangia. Je, kuna utaratibu gani wa kuratibu michango hii ya wananchi pindi wanapochangia na taarifa ya michango hii huwa inawasilishwa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha idara hii, Kambi ya Upinzani inapendekeza hatua zifuatazo ziweze kuchukuliwa ili kuweza kukabiliana na majanga/maafa mbalimbali hapa nchini. Kwanza kuandaa mfumo wa awali wa kutahadharisha umma juu ya ujio wa majanga (*emergency alert system*) kwa kutumia vyombo na nyenzo mbalimbali ili kuepusha madhara makubwa kwa watu na mali zao.

Pili, kutunga sheria mpya ya ujenzi na kuweka viwango vya ujenzi viwe vyenye hadhi ya Kimataifa na haswa majengo marefu na tatu, kuhakikisha kuwa kwenye miji yote mikubwa mtandao wa mabomba ya maji ya dharura unawekwa ili kuweza kukabiliana na majanga ya moto pindi yanapotokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa kazi kubwa na ya muhimu ya idara hii imekuwa kugawa chakula kusaidia Wilaya mbalimbali pale zinapokumbwa na baa la njaa linalosababishwa na ukame, mafuriko na kadhalika. Ni vyema sasa sambamba na utoaji

wa misaada hii ya chakula, ukawepo mpango wa muda wa kati na mrefu wa kuhakikisha tatizo hili la chakula linakuwa historia. (*Makofi*)

Kambi ya Upinzani inapendekeza mfumo huu wa kuhakikisha upatikanaji wa chakula uende sambamba na utambuzi wa chanzo cha tatizo na mikakati ya kukabiliana nalo. Kila Halmashauri ya Wilaya iwe na utaratibu wake wa kuhifadhi chakula. Mkakati mmojawapo ni pamoja na kuwa na mipango ya kilimo cha umwagiliaji ili kukabiliana na tatizo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri vile vile kuwa, njaa inayosababishwa na kukosekana kwa mvua kwa msimu mmoja ni kielelezo tosha cha umaskini wa wananchi wetu. Ni ushuhuda wa kukosekana akiba ya fedha na chakula kwa wananchi wetu. Ni wajibu sasa wa Halmashauri zetu kuanza kufikiria mikakati ya kuongeza mapato kwa wananchi wake ili kuwawezesha kuwa na akiba ya chakula na fedha endapo mvua itakosekana msimu mmoja wasiathirike kwa kiasi kikubwa kwa ukosefu wa chakula. Ni vyema kujiwekea lengo hili na mkakati maalum ya utekelezaji, si rahisi ila inawezekana. Lazima tujipe ujasiri wa kulikabili tatizo hili bila woga. Tukiogopa, tutashindwa kabla ya kuanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi na mauaji ya raia. Kwa kipindi kirefu sasa imejitokeza tabia ya polisi kuua raia kwa kuwapiga risasi maeneo mbalimbali ya nchi yetu na hakuna hatua zozote ambazo zimekuwa zikichukuliwa na Serikali katika kuthibiti hali hiyo. Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ya mwaka 2010 imeonyesha kuwa kwa kipindi cha mwaka 2010 watu 52 walikufa wakiwa mikononi mwa polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya hivi punde juu ya hali ya haki za binadamu kwa mwaka 2010, kama ilivyotolewa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*LHRC*) inaonesha kuzorota sana kwa namna vyombo vya dola, Serikali, Mahakama na jamii zinavyojali na kulinda haki za binadamu. Matukio ya rushwa, ajali za barabarani, mauaji ya *albino*, mauaji kwa imani za uchawi, jamii kujichukulia sheria mkononi na mauaji chini ya ulinzi wa vyombo vya dola, haswa polisi yamekuwa yakiongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki nyingine zinazokiukwa sana ni pamoja na haki ya usawa mbele ya sheria, kutoharakishwa utoaji haki, haki ya kupata mawakili, haki ya kupata habari, uhuru dhidi ya mateso na uhuru wa kujieleza na kuandamana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauaji ya raia mikononi mwa polisi yameendelea kuongezeka kwa kasi ya kutisha sana kutoka matukio ya kuuawa watu watano mwaka 2008, watu 15 mwaka 2009 hadi watu 52 mwaka 2010. Kwa kasi hiyo hiyo, mwaka huu pekee, kwa miezi ya Januari hadi Mei, 2011, tayari watu tisa wameripotiwa kuuawa na polisi katika eneo moja tu la Nyamongo, Tarime na kushuhudia matukio ya unyama wa kutisha yakifanyanya na chombo cha dola kwa kutupa miili ya marehemu hao barabarani na kuitelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunataka hali hii ichukuliwe hatua na kuangaliwa kwa umakini mkubwa hasa ikizingatiwa kuwa mwaka huu pia kumefanyika mauaji ya raia watatu huko Arusha ambao walipigwa risasi na polisi kwa kile kilichodaiwa kuwa walitaka kuleta vurugu na uvunjaji amani. Wananchi wengine tisa wameshauawa Tarime, watatu Mbarali, wawili Kisarawe, Sumbawanga na mwingine Tabora. Kwa mujibu wa ripoti hiyo, matukio haya yameainishwa kama ifuatavyo:-

Kwanza, mnamo Januari 5, 2011 watu watatu ambao ni Denis Michael, Ismail Omary na Paul Njuguna Kaiyele waliuwawa na wengine 21 kuumizwa vibaya wakati wa maandamano mijini Arusha.

Pili, mnamo tarehe 16 Mei, 2011 polisi waliwaua watu watano katika eneo la Mgodi wa *North Mara* Wilayani Tarime unaomilikiwa na Kampuni ya *African Barrick Gold Mine* na kufanya idadi ya watu waliouliwa katika eneo hilo toka mwaka 2009 hadi Juni 2011 kuwa 34. Kama hiyo haitoshi, mnamo tarehe 9 Juni, 2011 kijana ajulikanaye kama Nyaitore, mkazi wa kijiji cha Nyangoto Wilayani Tarime alipigwa risasi ya bega na polisi wa mgodi na kulazwa hospitali ya Sungusungu.

Tatu, mwezi Mei, 2011 katika kijiji cha Namanga wilayani Nachingwea, askari wa wanyamaporis walimpiga risasi kwenye miguu yote Juma James (27) ambaye anaendelea na matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Nachingwea.

Nne, Mkoani Tabora wilayani Urambo mnamo tarehe 28 Mei, 2011 askari polisi walimuua Juma Saidi na kujeruhi wengine kadhaa katika kijiji cha Usinge. Tukio hilo lilitanguliwa na kipigo kwa Mwenyekiti wa kijiji cha Shela na wenzake mnamo tarehe 26 Mei, 2011 vitendo vilivyoofanywa na askari walioenda kukamata mifugo.

Tano, mnamo Aprili 2, 2011 mkazi wa kijiji cha Mwanza Buriga kata ya Kukirango wilaya ya Musoma vijijini Mwabia Zome (40) aliuawa kwa kupigwa risasi chini ya titi la kushoto na askari Magereza wa gereza la Kyabakari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, watu wengine wa umri kati ya miaka 25 - 30 walipigwa risasi tarehe 7 Machi, 2011, ambapo Sese Kabanzi, alifia njiani wakati akipelekwa hospitali na July Hamisi alikuwa papo hapo baada ya kupigwa risasi maeneo ya kifuani.

Saba, mnamo tarehe 5 Februari, 2011 askari wa wanyamaporis katika Hifadhi ya Selous wameripotiva kuuwa watu wawili na kujeruhi mmoja Wilayani Kisarawe Mkoani Pwani. Waliokufa ni Hamisi Boy na Mohamed Suta na anayeuguza majeraha ni Mohamed Kigwiso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuna ushahidi kuwa askari hawa wanashutumiwa kwa kuendeleza matukio ya ukatili dhidi ya wananchi wanaozunguka hifadhi hiyo kwa makusudi huku Jeshi la Polisi likishindwa kuwasaidia raia kulinda usalama wao. Wilayani Kisarawe askari hawa wanadaiwa kuwauwa na kuwatupa mtoni na kupelekea raia wafuatao waliwe na mamba ambao ni Ndugu Majengo, Mohamed Kibavu, Adamu

Feruzi, Semeni Abdala Kube, Hemed Kassim, Mzee Hussein, Ramadhani Mgeto na Bwana Mkala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha zaidi kuna matukio mengi ambapo ndugu za waathirika hao wa ukatili wamekuwa wakinyanyaswa pale wanapofutilia haki au uwajibikaji katika vyombo vya usalama. Aidha, matukio ya uchomaji moto miili ya marehemu, kulishwa mamba na kutupwa na kutelekezwa barabarani maiti ni matukio yanayotuingiza katika historia mpya ya kutojali haki za binadamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kipindi cha miezi mitano ya mwaka 2011 tayari Watanzania 21 wameuwawa kwa kupigwa risasi maeneo mbalimbali ya nchi yetu na wengine wengi kuumizwa kwa kupigwa risasi wakiwemo wanafunzi wa shule za Sekondari na Vyuo Vikuu mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ifanye mambo yafuatayo ili kukomesha mauaji haya:-

Kwanza, kulipa fidia stahili kwa mujibu wa sheria husika za nchi kwa ndugu na/au jamaa wa wale wote waliouawa kutokana na vitendo vya Jeshi la Polisi la Tanzania na kwa wale wote walioumizwa kwa namna yoyote ile na/au kuharibiwa mali zao kutokana na vitendo hivyo.

Pili, kuwachukulia hatua askari polisi, askari magereza na wale wa wanyamaporii ambao wamehusika katika mauaji haya kwani hali hii ikiachwa iendelee kama ilivyo sasa ni hatari kwa usalama wa Watanzania wote na italifanya Taifa letu kuingia kwenye rekodi mbaya ya kukiuka haki za binadamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, iundwe Tume huru ya Uchunguzi ya Kimahakama (*Judicial Commission of Inquiry*) itakayoundwa na Majaji wa Mahakama ya Rufani ya Tanzania iundwe ili kufanya uchunguzi huru. Tunapenda kusisitiza kuwa tunataka iundwe Tume ya Uchunguzi ya Kimahakama kwani hufanya kazi zake kwa uwazi na huruhusu wananchi kuhudhuria na/au kushiriki moja kwa moja katika kazi za Tume kama mashahidi na/au kwa kuhoji mashahidi wengine wanaotoa taarifa kwenye Tume hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa sheria ipo wazi kuwa kila mtu ambaye ana mpango wa kuwa na mkutano katika eneo la umma anatakiwa kutoa taarifa polisi saa 48 kabla ya kufanya tukio hilo; na pia polisi wakiona kunaweza kutokea tatizo wanawenza kuzuia mkutano huo kabla ya saa 24. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na hivyo polisi wamekuwa na tabia ya kuzuia mikutano ya hadhara hasa ya vyama vya upinzani bila hata kutoa taarifa kwa maandishi, sababu za kukataza mikutano hiyo na pia jambo hili hufanyika saa chache tu kabla ya kufanyika mkutano husika. Mara zote polisi wamekuwa wakitumia kile wanachokiita kuwa ni taarifa za kiintelijensia.

Kambi ya Upinzani, inaona kuwa jambo hili hufanywa makusudi na ni kinyume cha sheria ya vyama vya siasa na pia Katiba yetu ambayo imetoa haki ya kukusanyika. Ni jukumu la Jeshi la Polisi kuhakikisha kuwa kama kuna taarifa za uvunjifu wa amani kuchukua hatua kwa wale wote ambao wanahusika na mpango huo na sio kuzuia mikutano ya vyama vya siasa kuendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika siku za hivi karibuni limejitokeza wimbi la polisi kuwakamata wawakilishi wa wananchi na haswa Wabunge bila kuzingaitia kuwa kuna Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge ambayo inaelekeza utaratibu wa kufuatwa wakati wa kumkamata Mbunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inatambua na kulinda uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu katika Bunge na uhuru huo hautavunja wala kuhojiwa na chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano au katika Mahakama au mahali penginepo nje ya Bunge. Uhuru huu wa Kikatiba umetiliwa mkazo katika vifungu vya 5, 6 na 11 vya Sheria ya Kinga, Mamlaka na Haki za Bunge ya mwaka 1988 vinavyokataza Mbunge kukamatwa au kupewa amri ya kuhudhuria mahakamani wakati akiwa ndani ya eneo la Bunge au wakati Bunge limekutana bila kuwepo kwa kibali cha Spika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati sheria hii ikiwepo Wabunge wa Vyama vya Upinzani na hususani CHADEMA wamekuwa wakikamatwa, kunyanyaswa na kupigwa na polisi bila kujali kuwa kuna utaratibu wa kufuatwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwagine, Kambi ya Upinzani Bungeni imeshangazwa na unafiki na ubagizi wa wazi unaooneshwa na Jeshi la Polisi juu ya Wabunge wa Vyama vya Upinzani. Hii ni kwa sababu wakati Jeshi la Polisi limekuwa likiwakamata Wabunge wa Upinzani bila kuomba kibali chochote kwa Spika kama inavyotakiwa na Sheria ya Kinga, Mamlaka na Haki za Bunge kama ilivyotokea kwa Wabunge wa CHADEMA wakiwemo mimi mwenyewe Freeman Mbowe, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Godbless Lema, Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Meshack Opulukwa, Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa, Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum wa Chama cha Wananchi (*CUF*).(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati hali ikiwa hivyo kwa upande wa Wabunge wa CCM na ambao wanakabiliwa na tuhuma za makosa makubwa zaidi wamekuwa wanaombewa kibali cha Spika kabla ya kukamatwa. Kwa hili tuna ushahidi wa barua ya Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa wa Mwanza SP B.M. Wakulyamba kwa Katibu wa Bunge ya kumwomba Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani, Mbunge wa Busega, CCM ili akahojoive na Jeshi la Polisi kuhusu kutuhumiwa kuhusika kwake na njama za kutaka kumuua aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Busega Dkt. Raphael Masunga Chegeni. Barua hiyo ya tarehe 31 Mei, 2011 yenye kumbukumbu namba *MZR/CID/SCR/105/2011/4* ilinakiliwa kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza na Mkurugenzi wa Upelelezi wa Jinai, Makao Makuu ya Polisi *DCI* Robert Manumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Mbunge hata mmoja wa CHADEMA au chama kingine cha upinzani ambaye kwa taarifa zetu amewahi kuombewa kibali cha kukamatwa na polisi kama inavyoonekana kwa Wabunge wa CCM. Hii inadhirihisha upendeleo wa wazi wa Jeshi la Polisi kwa Wabunge wa CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaitaka Serikali kwenye hili ieleze wazi ni nini misingi ya Wabunge wa CCM kuombewa kibali ilhali wa Upinzani wakikamatwa bila taratibu hizo kufuatwa kwani hali hii sio nzuri kwa ustawi wa haki na demokrasia hapa nchini mwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ajali za barabarani kuongezeka kwa kasi sana katika miaka ya hivi karibuni na kusababisha vifo vya Watanzania wenzetu mamia kwa mamia. Serikali haijonesha nia ya dhati ya kukabiliana na tatizo la ajali barabarani lakini imebakia kutuma salamu mbalimbali za rambirambi pindi ajali zinapotokea. Kwa mujibu wa kitabu cha taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa kipindi cha mwaka 2010 jumla ya ajali 24,926 zilitokea na kusababisha vifo vya watu 3,687 na majeruhi 22,064.

Kambi ya Upinzani inaona kuwa itakuwa ni busara kwa Serikali kuangalia ni jinsi gani idara hii ya maafa itavyoweza kufanya uratibu kwa kushirikiana na idara zingine za Serikali katika kuhakikisha vifo vitokanavyo na ajali vinapungua au vinakwisha kabisa. Kwani kwa hali hii ya ajali na vifo vya Watanzania, hili nalo ni miongoni mwa maafa/majanga kwa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwezeshaji wananchi kiuchumi, mojawapo ya sababu ambazo Kambi ya Upinzani inaona kuwa ni kikwazo katika uwezeshaji na uwekezaji ni kutokufikiria kwa makini ongezeko la watu. Takwimu zinaonyesha kuwa ongezeko la watu ni asilimia 3% kwa mwaka, pia kuna hoja ya kuwa Tanzania inaendelea kuwa na kiwango kikubwa cha ukuaji wa miji. Kwa mujibu wa makadirio ya idadi ya watu yaliyotokana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002, Tanzania inakadiria kuwa na idadi ya watu wapataao 43,187,823 mwaka 2010, ambao kati ya hao watu 31,809,808 sawa na asilimia 73.7 wanaishi vijijini na watu 11,378,015 sawa na asilimia 26.3 wanaishi mijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa miji umekuwa na changamoto nyingi zinazohusu uwezeshaji wa wananchi kutokana na shughuli chache za uzalishaji wa viwandani ikilinganishwa na miaka ya nyuma na kama kungekuwa na mpango mahususi zingeweza kutoa ajira kwa wakazi wengi walioko mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasi ndogo ya uwekezaji katika kuwawezesha wananchi kupata ajira za kuajiriwa na kujiajiri wenye na hivyo kuwa na vipato duni visivyowawezesha kumudu mahitaji yao muhimu nayo imekua sababu ya msingi inayosababisha kuongezeka kwa tatizo la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona kuwa ili kukabiliana na tatizo hili ni lazima uwezeshaji na uwekezaji uanzie kwenye Halmashauri zenyewe kwa kuwa na kile ambacho tumekiita *District Economic Development Master Plan* ambapo

kila Wilaya itakuja na mpango utakaota ajira zisizopungua 2000 kila mwaka kwa ajili ya vijana wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia hii inaondoa ukiritimba wa kufikiri walionao watu, wanaodhani wao ndio wanaoweza kuwawezesha wananchi peke yao na hivyo kusababisha maafisa mipango na watendaji wengine walio katika ngazi za mikoa kuwa wategemezi kimawazo na hivyo kushindwa kubadilisha fursa zinazowazunguka kuwa kichocheo cha uwekezaji na hatimaye fursa za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu katika sera za nchi unaonyesha kuwa siyo kila mtu ana uwezo wa kushiriki kikamilifu katika kujenga uchumi. Kukua kwa uchumi kunaweza kuacha wananchi wengi nje kama sera madhubuti hazikuwekwa kuwezesha watu wengi kushiriki katika kujenga uchumi, kupata ajira na kuongeza kipato chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inarudia tena kusema kuwa uwezeshaji utakaoletea wananchi hasa wa vijijini tija ni kuwa na mchakato utakao washirikisha wananchi wote katika suala zima la uwezeshaji na mchakato huo kuwa na utashi wa kisiasa. Kwa maana nyingine ni kuzipa Halmashauri zetu uhuru wa kutengeneza mpango wake wa kiuchumi na kuutekeleza ikishirikiana na sekta binafsi na kwa kutumia fursa zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ni roho ya Taifa. Pamoja na Serikali kutangaza azma ya kuhakikisha Taifa linapata Katiba Mpya itakayokidhi mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kijamii baada ya miaka 50 ya Uhuru wetu, bado jambo hili limegubikwa na hofu kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema tukatumia fursa hii kutibu majeraha mbalimbali na kuweka mazingira ya kuepusha machafuko yasiyo lazima kwa kuwa na mfumo shirikishi na wa wazi wa mchakato wa upatikanaji wa Katiba Mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandamano ni haki ya Kikatiba ya raia, ni fursa ya amani ya raia ama kufikisha mbele ya umma, taasisi mbalimbali au Serikali hisia zao kuhusu jambo mahususi la kupongeza, kulaani au kunung'unika. Siku za karibuni, chama ninachokiongoza kimefanya maandamano sehemu kadhaa za nchi yetu yakiwa na malengo mahsusni ya kuhamasisha, kuamsha na kuushirikisha umma katika kutambua haki na wajibu wake. Aidha, maandamano haya yalikusudia kufikisha ujumbe maalum kwa Serikali ili hatua za makusudi na za haraka ziweze kuchukuliwa kuliepusha Taifa na mlipuko unaoweza kutokea iwapo waliopo madarakani watashindwa kuchukua hatua za makusudi na za haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na upotoshaji mkubwa wa dhamira ya maandamano haya kutumia vikundi mbalimbali vikiwemo vya dini, vyama vingine vya siasa vikiwemo vya upinzani na hata Bunge lako limekuwa sehemu ya kampeni chafu dhidi ya maandamano ya watu, jambo ambalo linakusudia kupandikiza chuki, uhasama na hata kupoka haki ya msingi sana ya raia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri vilevile hofu ya kupotea kwa amani imekuwepo tu pale vyombo nya dola hususan polisi wanapajaribu kuingilia haki hii na kuzuia maandamano bila sababu za msingi kama ilivyokua kule Arusha. Kuna ushahidi usio na mashaka kuwa maandamano mengine yote yamekuwa ya amani na kwa kiasi kikubwa yamesaidia kuondoa dukuduku mbalimbali za wananchi na hivyo kusaidia kuendeleza amani badala ya kuvuruga amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa kejeli dhidi ya maandamano yetu ikome. Kila chama kikajipime kukubalika kwake kwa wananchi badala ya kupoteza muda kuzungumzia maandamano ya amani ya CHADEMA na wananchi mbalimbali. Kama chama hakina hoja za kushirikisha wananchi au kina hofu ya kupata waandamanaji, kisitumie kisingizio cha amani kama nyenzo ya kuepusha aibu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafalsafa mashuhuri walisema; “Viongozi makini na wanaojiamini huratibu mabadiliko yasiyoziulika ya kijamii na hivyo kujihakikishia amani ilhali viongozi dhaifu na wasojiamini huzuia mabadiliko yasiyoziulika ya kijamii kwa kutumia nguvu na matokeo yake ni kujiingiza kwenye machafuko ambayo yangeweza kuepukika.” (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utawala wa Bunge. Katika jambo hili, naomba nieleze wazi kuwa hoja hii haina *reference* yoyote kwenye uongozi wa Spika wa Bunge letu leo, bali ni uhalisia ambao kipekee niliuzungumzia tangu Bunge la Nane, hali iliyopelekea kushtakiwa na Spika wa wakati huo kwenye Kamati ya Maadili ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge letu leo linakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizi zinakolezwa na ukweli kuwa wananchi sasa zaidi ya siku zote huko nyuma wanaelewa na kutambua umuhimu wa Bunge katika Taifa. Hali kadhalika, maamuzi yoyote ndani ya Bunge hupokewa kwa hisia tofauti na wananchi. Maamuzi na mienendo ya Bunge hakika ni nyenzo muhimu ya amani katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mfumo wa Vyama Vingi, ni rahisi hisia za wanachama wa chama kimoja kuamini hakitendewi haki kama Spika anatoka kwenye chama kingine. Kambi ya Upinzani inashauri sasa paanze kuwepo wazo la kuwa na Spika asiyetokana na chama chochote cha siasa na kama atachaguliwa kutoka miongoni mwa Wabunge, basi itabidi ajiuzulu nafasi yake ya Ubunge sambamba na nafasi zake zote ndani ya chama chake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu utasaidia kuondoa hofu inayotokana na hisia na utatoa fursa kwa wananchi wa jimbo analotoka Spika, kupata uwakilishi rasmi ndani ya Bunge. Aidha, itampa Spika nafasi ya kusimamia Bunge kwa kujiamini bila shinikizo la chama chochote na hata kuweka msingi muhimu wa amani na mshikamano wa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho ya sheria mbalimbali nchini. Pamoja na lengo zuri la kuanzishwa Tume ya Kurekebisha Sheria, lakini maboresho ya sheria mbalimbali yanaenda taratibu sana na kupoteza lengo mahususi. Kuna tatizo kubwa sana la idadi ya Mahakimu na majengo mengi ya Mahakama ni machache na mengine ni mabovu. (*Makofi*)

Pamoja na umuhimu wa taaluma ya sheria katika uendeshaji wa haki nchini bado haijapewa kipaumbele kwa sababu mpaka sasa wapo wahitimwengi sana wa taaluma ya sheria ambao wameshindwa kujiunga na Shule Kuu ya Sheria (*Law School of Tanzania*) kwa sababu wanatakiwa kujigharimia gharama zote za mafunzo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii mara zote imekuwa ikiimba wimbo wa uhaba wa Mahakimu, itueleze ina mpango gani wa kugharamia mafunzo haya ambayo ni muhimu ili kuwawezesha wahitimwengi wetu kupata mafunzo haya na hatimaye kuziba pengo la uhaba wa Mahakimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandamano Vyuo Vikuu na uhuru wa kitaaluma, wanafunzi wa Vyuo Vikuu hapa nchini wamekuwa wakiandamana kutokana na sababu mbalimbali. Sababu kubwa ni kutokana na Serikali kutowatendea haki kwa kucheleweshewa ama kunyima fedha zao za mikopo na za mafunzo kwa vitendo. Pindi wanafunzi hawa wanapogoma ama kuandamana wamekuwa wakipigwa na wengine kuumizwa na jeshi la polisi na baadhi yao kuishia kufukuzwa vyuoni na au kusimamishwa masomo kama ambavyo imetokea katika Vyuo Vikuu vya Dodoma, Dar es Salaam, Muhimbili, Chuo cha Ardhi na vinginevyo vingi hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya mwaka 2009 iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali namba 178 la tarehe 12 Juni, 2009 inayojulikana kama Kanuni ya Vyama vya Wanafunzi Vyuo Vikuu (*Universities Students Organization Regulations ,2009*) pamoja na mambo mengine kanuni hizo zimeelezea kwenye kifungu cha 14 juu ya haki za wanafunzi kufanya mambo yafuatayo; kukusanyika (*assemble*), kuandamana (*demonstrate*) na kutoa maoni yao (*express their opinion*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali yenyewe kutoa haki hizo kwa wanafunzi lakini la kusikitisha ni kuwa pindi wanafunzi hawa wanapokuwa wanaandamana kama njia ya kuweza kutoa maoni yao na kama ambavyo kanuni zimewapa haki hizo, bado Serikali kwa kutumia jeshi la polisi wamekuwa wakiwapiga vijana hawa na hata wengine kuumizwa vibaya kama ilivyotokea hapa Dodoma kitendo kilichopeleka mwanafunzi mmoja kulazwa kutokana na maumivu makali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya polisi kuwapiga wanafunzi sasa imeenda mpaka kufikia ngazi za shule za sekondari kwani ni hivi majuzi tu polisi waliwafyatulia risasi za moto wanafunzi wa shule ya sekondari ya Mbezi iliyopo jijini Dar es Salaam na kupelekea wanafunzi wengi kuumia vibaya na kulazwa katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ni ya hatari kwa vijana wetu kwani kama imefikia mahali pa kuwafyatulia risasi za moto wanafunzi ambao hawana silaha yoyote na Serikali imeendelea kukaa kimya bila kuchukua hatua zozote dhidi ya wanaofanya vitendo hivyo ni kitu ambacho hakikubaliki.

Kambi ya Upinzani, tunaitaka Serikali itoe maelezo kuhusiana na mambo yafuatayo:-

Kwanza ni hatua gani Serikali imechukua mpaka sasa dhidi ya wale wote ambao wanasababisha majeruhi kwa kuwapiga wanafunzi kinyume cha sheria kama ambavyo kanuni tajwa hapo juu zinawapa haki ya kuandamana?

Pili, je, ni kesi ngapi ambazo mpaka sasa zinawakibili wanafunzi wa vyuo na wa sekondari kwa kuandamana na zipo mahakama gani? Tatu, ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya wale wote ambao wanasababisha kutokea kwa migomo hii na nne, je, Ofisi ya Waziri Mkuu imechukua hatua gani dhidi ya utawala wa Chuo Kikuu cha Dodoma baada ya kuunda tume kuchunguza malalamiko ya wanafunzi dhidi ya Mkuu wa Utawala wa Chuo hicho na vingine vingi nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa ni haki ya Kikatiba ya wanafunzi kuandamana na kutoa maoni yao na kamwe hatutakaa kimya pindi haki za wanafunzi zinapokuwa zinavunjwa na vyombo vyta Serikali na vijana wetu wakiendelea kuumizwa. Aidha, napenda kuwakumbusha wanafunzi wetu wanaojenga ujasiri wa kuhoji bila kuvunja sheria maneno aliyosema Mwanafalsafa Gwiji Aristotle; “*The roots of education is bitter but the fruit is sweet.*” (*Makofi*)

Kambi ya Upinzani tutalisimamia tamko la ulimwengu la uhuru wa kitaaluma (*The Declaration on Academic Freedom and Social Responsibility of Academics*) ambalo Tanzania tulisaini tamko hilo mnamo tarehe 19 Aprili, 1990. Kwani tunaamini kuwa Taifa haliwezi kuendelea kamwe kama wanataaluma wake wananyanyaswa na kukosa uhuru wa kutoa maoni yao kwa uwazi na bila kipingamizi chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 tumeshuhudia Serikali ikiwa inavinyima vyombo mbalimbali vyta habari uhuru wake wa kupata na kutoa habari na haswa kwa kuwatumia maafisa waliopo Idara ya Habari Maelezo kuandika barua mbalimbali za vitisho kwa vyombo mbalimbali vyta habari na hata kufikia hatua ya kuvitishia vyombo hivyo kuwa kama vitaendela kutoa habari ambazo Serikali haitaki kuzisikia basi itachukua hatua ya kuvifungia vyombo hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kukabiliana na tishio hili, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali iwasilishe Muswada wa Sheria ya Vyombo vyta Habari ambao tayari wadau walishaupitia na kukubaliana na Serikali kuwa Muswada huo ungewasilishwa tangu mwaka 2008 ila mpaka leo bado tunaelezwa kuwa mchakato unaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nimshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. (*Makofî*)

Sasa nafikiri tuanze kazi ya mchango wa hotuba hii, kama nilivyosema mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Amos Makalla ajiandae sina uhakika sana na muda wangu kama utakuwa umenitosha vizuri tutampa nafasi Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema. Mheshimiwa Michael Laizer. (*Makofî*)

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba hii ya Waziri Mkuu na natanguliza kusema kwamba naunga mkono hotuba hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu machache; kwanza niwape pole Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wanaokaa kwenye kiti hicho kwa sababu kiti hicho kimekuwa kitimoto. Nimekaa hapa Bungeni kwa muda mrefu kidogo na tulipoanza Bunge la Vyama vingi wakati huo ndiyo nimeanza kuwa Mbunge, kwa hiyo, huu ni mwaka wa 16 tangu tuanze Bunge la vyama vingi lakini sijawahi kuona Bunge la aina hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wenyewe Wabunge tukidhalilisha hili Bunge haya uheshimiwa wetu hautakuwa na maana. Jambo muhimu hapa ni sisi wenyewe kuheshimiana ndani ya hili Bunge. Mheshimiwa Spika, alisema tusifanye Bunge kama soko au *the comedy*, lakini mimi nasema tunapeleka Bunge letu lifanane na kama mkutano mkuu wa walevi, ndiko tunakoelekea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie ndugu zangu Wabunge...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Laizer naomba uendelee kuchangia huku ukizingatia sana hoja ya kutunza kauli ambazo hazitaleta maudhi Bungeni. (*Makofî*)

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge lililopita hatukuwa na malumbano, lakini nakumbuka Mawaziri wengi sana wameachia ngazi bila malumbano kwa ajili ya hoja za Wabunge walioko katika Bunge hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee na mchango, kwanza nashukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, nawapongeza sana na nawashukuru mwaka juzi, Jimbo la Longido limekumbwa na ukame mkubwa sana, wananchi karibu wafe, watoto wafe kwa ajili ya njaa lakini Serikali imesimama imara na kuwalisha mpaka wako hai, nawashukuru na naishukuru Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukame bado unaendelea, naomba Serikali iendelee na nadhani kipindi hiki ni Wilaya nyingi sana ambazo hazina chakula, naiomba Serikali iwalishe watu wake. Jambo lingine naishukuru Serikali na nakumbuka Bunge la mwaka 2008/2009 na 2010 kwenye Bajeti ya miaka hiyo miwili, nilisimama Bungeni nikasema

umeme usipofika Longido sitagombea wala sitachukua fomu na nilitangaza kwa wananchi na nikatangaza hapa Bungeni kwa hiyo, Ubunge nimeweka rehani kwamba sitagombea kama umeme haufikishwi Longido na naishukuru Serikali kwa sababu imefikisha umeme Longido na ndiyo maana nimechukua fomu. Nimekwishawatangazia wananchi na hata hili Bunge ninaaga kwamba umeme usipofika Longido sichukui fomu, nashukuru kwa sababu umeme umefika Longido naomba sasa Serikali isambaze umeme katika Mji wa Longido na Mji wa Namanga. (*Makofi*)

Ombi langu lingine ni umeme kutoka Rombo kuja Kamwanga, Omolo na kuelekea Ngarenairobi. Wakati mmoja niligombana kidogo na Serikali pamoja na aliyekuwa Waziri wa Ujenzi wakati huo Mheshimiwa Basil Mramba kwamba umeme umeletwa kutoka Rombo, ikafika kilomita kumi ikaachwa isifike Longido, barabara ya lami ikatoka Rombo mpaka mpakani mwa Longido na Rombo, nikapata wasiwasi nikasema au lami hii imeweka kutenga wamasai na wachaga kwa sababu umefika mpakani ikaachwa, barabara ya lami imefika mpaka ikaachwa, naomba Serikali itoe usemi huo niliousema kwa kupeleka umeme kutoka Rombo mpaka Ngaro Nairobi - Sanya Juu kwa sababu hiyo ndiyo niliyoona kwamba itakuwa ni baadhi ya maeneo kuendelea na maeneo mengine kutoendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru Serikali na niipongeze kwa mambo yanayobezwa kwamba Serikali hii haijafanya kazi, nakumbuka na kila mmoja ni shahidi kwamba kwa kila Wilaya shule za msingi zimeongezeka, sekondari zimeongezeka, barabara zimejengwa, taasisi zingine zimejengwa, maji yamewekwa katika baadhi ya maeneo hata kama haijatosheleza, lakini sasa tunasema Serikali haijafanya kitu, wanafunzi waliopo sekondari, waliopo Vyuo Vikuu wameongezeka, fedha za kuwasomesha hao wanafunzi zimeongeza, tunasomewa kwenye Bajeti, Serikali imefanya mengi lakini haiwezekani zikawa zimetimia kwa wakati mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la maliasili, nchi yetu ni nchi tajiri sana, lakini hatutangazi maliasili tulizonazo, tunaomba tutangaze maliasili kwa sababu tuna *national parks* nyingi, vivutio vingi lakini Kenya wanatuzidi kwa ajili ya matangazo tu mpaka juzi wanatangaza kwamba ukitaka kwenda kwa Babu nenda Nairobi, kwa sababu kwa Babu ni kilomita 120 kutoka Nairobi, wametangaza mpaka Babu, wanamtangaza Babu ambaye yupo Tanzania. Kwa hiyo, naomba tuongeze fedha kwa ajili ya utalii na tufufue ndege zetu, ATC iweze kuleta watalii kwa sababu hatuwezi tukategemea ndege za Kenya au sehemu nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ningependa kulizungumzia kwa haraka ni suala la Halmashauri. Nakubaliana na kila Mbunge aliyesema kwamba fedha za Halmashauri hazitumiki vizuri, zinaliwa na wajanja hasa fedha za *DADPS*, hizo fedha ni fedha zinazoliwa, hazifanyi kazi, nenda kaangalie mradi wowote wa *DADPS* katika Wilaya yoyote, hasa niseme katika Wilaya yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mabwawa yaliyochimbwa kwa fedha za *DADPS*, hayafanani na mabwawa yaliyochimbwa na wananchi. Siku moja Mheshimiwa Aggrey Mwanri alikwenda kuweka jiwe la msingi katika bwawa moja na hilo hilo bwawa

Waziri wa Maji akaenda kulizindua. Bwawa lililochimbwa kwa shilingi milioni 640 halifanani na bwawa lililo karibu ambalo limechimbwa na wanakijiji kwa shilingi milioni 15. Waziri akakiri mwenyewe kwamba ni afadhali hili la wananchi kuliko hili lililochimbwa kwa shilingi milioni 640 na nasema TAMISEMI imezidiwa na kuelemewa na kazi nyingi kwa sababu shughuli zote zimekwenda TAMISEMI kama maji, elimu, sekondari, ujenzi na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali sasa itumie *secretariat* za Mikoa, iangalie Halmashauri zilizopo katika Mkoa wa Arusha na kuthibitisha kwamba fedha zilizokwenda katika kila Halmashauri zinafanya kazi. Tunaomba kwa sababu fedha zote zinazokwenda katika Halmashauri zetu, Mheshimiwa Augustino Mrema anafahamu na Kamati ya *LAAC* inafahamu, *CAG* amegundua upotevu mkubwa sana wa fedha za Halmashauri lakini Serikali inakaa kimya. Nilishukuru sana Waziri Mkuu kutuma Tume iliyokuja kukaa miezi miwili Longido, hiyo Tume ipelekwe katika kila Halmashauri kwa sababu utashangaa kijana anakuja kutoka Chuo Kikuu, anafika kwenye Halmashauri miezi miwili baadaye amejenga nyumba, hizo fedha ametoa wapi? Ada alikuwa analipiwa na Serikali, amekuja ameanza kujenga nyumba, kesho ana gari, Halmashauri inakufa na Serikali inakaa kimya. Kwa hiyo, napenda kusema kwamba fedha za Halmashauri ziangaliwe kwa sababu zinatumika vibaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni elimu. Katika Wilaya za vijijini yaani Wilaya zote za vijijini tumeachwa nyuma, litatoka tabaka kama la matajiri na maskini. Litatoka tabaka la watu wenye elimu na watu ambao hawana elimu, kwa sababu shule za vijijini ambazo tunaziita za Kata hazina maabara, hazina walimu na watoto waliofaulu sana ni wale wanaopata *division three*. Hata ukiangalia katika Vyuo Vikuu vingi ni wanafunzi wachache wanaotoka Longido, Simanjiro, Ngorongoro na kadhalika ni wachache. Kwa hiyo, tuangalie na Halmashauri zilizopo nyuma siyo za Umasaini tu, bali zote ziangaliwe ili ziweze kusaidiwa.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Laizer hiyo ni kengele ya pili, hujaunga mkono.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitangulia kuunga mkono hoja lakini nirudie tena kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Kwa sababu ni muhimu kabisa Bunge litambue umetamka nini katika hoja iliyo mbele yetu. Naomba nimuite Mheshimiwa Amos Makalla.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii ili kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Lakini kwanza kabisa nami nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mvomero kwa kuniamini na kukipa ushindi mkubwa kwa chama changu kwa nafasi ya Ubunge, Udiwani na Urais na mimi nataka niwahakikishie kwamba imani hiyo walionayo kwangu katika miaka mitano sitawaangusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri kwa hotuba nzuri ambayo imetoa mwelekeo wa shughuli ambazo zitafanyika katika mwaka wa fedha lakini lengo ni kuwaleta wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze katika hoja mbalimbali lakini kwanza nianze na suala zima la miundombinu na hasa barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali ikazanie kuongeza kasi ya ujenzi wa barabara ya kutoka Magole, Turiani, Mzia hadi Handeni. Hivi sasa ujenzi wa barabara hii unasuasua lakini Serikali iliahidi kwamba barabara hii itakamilika mwakani. Naomba sasa ahadi hiyo ya Serikali itekelezwe kwa vitendo kwa maana ya kutenga fedha nydingi na barabara hii ijengwe kwa kasi kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ujenzi wa barabara hii, lakini nataka nniombe Serikali izingatie fidia kwa wananchi kwa sababu ndiyo maendeleo tunayoyahitaji. Lakini wakati mwingine wananchi wanakuwa na haki ya kulipwa fidia mathalani katika ujenzi wa barabara ya Magole, Turiani, Mzia mpaka Handeni yapo maeneo ambayo wananchi wamefuatwa na barabara lakini Serikali inatamka kwamba haitawafidia wananchi, hii siyo haki! Kama barabara haikupita eneo hilo na imewafuata wananchi na hili naongelea kwani kuna wananchi wa Kichangani waliambiwa kwamba hawatalipwa. Lakini nashukuru kwamba Mkuu wa Mkoo katika kikao cha barabara alisitisha zoezi lile la kuwabomolea wananchi wale na naomba Waziri Mkuu kwani nakuamini, utasimamia haki kwa wananchi ambao wamefuatwa na barabara kwamba watalipwa fidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuzipandisha hadhi barabara. Huko vijijini zipo barabara ambazo kwa kweli zinatakiwa kuwa katika hadhi ya kimkoa na sisi tumekuwa tukipendekeza miaka nenda-rudi. Naomba iingie katika *record* kwamba na sisi Mvomero tunaziombea barabara za Sangasanga, Mzumbe, Mlali mpaka Nyandira ziwe barabara za Mkoo. Tukifikisha barabara za Mgeta na Nyandira huko kuna chanzo kikubwa sana cha uchumi na chakula chote kama matunda na mboga mboga tunazonunua Kariakoo zinatoka Tarafa ya Mgeta. Kwa hiyo, barabara hii ikikamilika itawasaidia sana wananchi. Lakini ziko barabara za Mhonda, Ubiri mpaka Kibati na Pemba zote hizo naziombea zipandishwe hadhi ya kimkoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo kero kubwa kwa *TANROADS* Mkoo wa Morogoro. Kuna barabara ya kutoka Sangasanga - Chuo Kikuu cha Mzumbe, pale wamekufa watu tisa, walemau wawili, watoto wanne na watu wazima, kwa sababu tu eti *TANROADS* hawana fedha za kujenga matuta. Ninazo barua hapa na ikibidi nitaziwasilisha. Wanasema Bajeti wameshaomba ni miaka miwili na wananchi wanaendelea kufa. Kama mbuga ya Mikumi tumeweza kuwaona tembo na nyani wanawekewa matuta ije watu wanaoendelea kufa? Kwa hiyo, naiomba sana Serikali hili iliangularie maana ukiingia tu kwenye mbuga za wanyama unaambiwa hapa unaingia eneo la mbuga za wanyama, kuna matuta na kadhalika. Kama wale ni wanyama leo itashindikana kwa binadamu jamani? Kwa hiyo, naomba sana Serikali iwe *serious* katika hili ili kuona kwamba inawasaidia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni umeme. Kwa muda mrefu sana Tarafa ya Mgeta tumekuwa tukiomba umeme, lakini nashukuru kwamba Serikali sasa imeanza kazi hii na imeahidi kwamba itakamilika mwakani mwezi Novemba. Basi naomba sana suala hili linakwenda kwa kasi ili tuone huko Mgeta nako wanapata umeme. Maeneo mengine katika Jimbo la Mvomero ambayo nishati ya umeme bado ni kitendawili, yapo maeneo mengi kama Melela, Doma, Kanga, Kibati na Pemba yote yanahitaji umeme na itasaidia sana wananchi wa Mvomero kupiga hatua kubwa ya maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni migogoro ya ardhi na makazi. Naomba nijikite katika eneo la migogoro ya ardhi na makazi hasa nikiongelea tatizo la kijiji cha Wami Sokoine. Wananchi wa Wami Sokoine kwa miaka nane wamekatazwa kujenga nyumba kwa kisingizio kwamba Makao Makuu ya Wilaya wanaendelea kupima eneo la Wami Sokoine. Ikumbukwe kwamba Kijiji cha Wami Sokoine hakikuwepo katika eneo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, wao walipewa ekari 3,000 ili kujenga Makao Makuu ya Wilaya, haikugusa kijiji hiki. Lakini Makao Makuu ya Wilaya imejengwa ekari 3,000 na sasa wamevamia viwanja katika Kijiji cha Wami Sokoine na wananchi wamekatazwa kwa miaka nane wasiweze kujenga, huu ni uonevu.

Naomba sana Serikali iingilie kati, Waziri Mkuu nimemuandikia barua na mimi nakuamini katika hili utanaisidia. Wananchi hawa naomba wapate haki, waanze kujenga lakini kama viwanja vinaanza kupimwa kwa nini unamuondoa yule mwanakijiji unamweka mtu wa kutoka Dar es Salaam? Kwa nini usimpe kipaumbele mtu wa pale kijijini? Lakini hapo hapo mwaka 2002 katika Baraza la Mawaziri na barua ninayo, waliamua kwamba wafugaji wa asili wa Wami Sokoine wapewe ekari 5,000 lakini mpaka sasa hawajapata. Wamegawa maeneo kila mahali, *Mtibwa Sugar* wamepewa eneo, Wami Luimbo wamepewa lakini ndugu zangu wa Wami Sokoine wafugaji wa asili hawajapewa. Mheshimiwa Waziri Mkuu nimekupa barua, mimi naamini utafutilia juu ya suala hili. Naomba watendewe haki, wasizungushwe tena na wakati ukijibu Mheshimiwa Waziri basi naomba majibu ili na wao wafurahi. (*Makof*)

Lakini ipo migogoro ya muda mrefu kati ya Kiwanda cha Mtibwa na Kijiji cha Kidudwe na vingine kuhusu eneo la Newland. Tunaomba eneo hili pia Serikali iingilie kati ili wananchi hawa wapatiwe haki yao. Hakuna ushahidi wa moja kwa moja unaoonyesha kwamba eneo la Newland lipo katika kiwanda cha Mtibwa, hapana! Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hiyo, mimi na hilo naomba ultolee ufanuzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu kitengo cha maafa. Nitumie fursa hii kuishukuru sana Ofisi ya Waziri Mkuu, kuanzia Waziri Mkuu mwenyewe na Mheshimiwa William Lukuvi kwa namna walivyoshughulikia maafa na mafuriko Wilaya ya Mvomero. Kwanza tulipata maafa Tarafa ya Mgeta Serikali ikaleta tani 80 za chakula, nawashukuru sana. Lakini pia miundombinu inahitajika kukarabatiwa, tunahitaji shilingi milioni 800 tayari Ofisi ya Waziri Mkuu ilishafahamishwa juu ya hilo, kama mlivyo fanya Kilombero naomba mfanye pia na Mvomero, madaraja yako katika hali mbaya.

Lakini pia wakati Wabunge wanachangia na kuishukuru Serikali juu ya chakula cha msaada, lakini kwa Wilaya ya Mvomero tulipata bahati tena, mwezi wa nne Serikali imetoa tani 86 za chakula. Katika tani 86 za chakula walitoa maelekezo kwamba tani 8.6 zigawiwe bure na tani 77.4 ziuzwe kwa wananchi lakini kwa bahati mbaya Waziri Mkuu nikutaarifu kwamba Mkuu wa Wilaya ya Mvomero uliyempa nafasi kwa kutumia siasa amesitisha kugawa chakula na mpaka sasa wananchi hawajapata chakula hicho na kwa nini hajagawa chakula hicho? Ni pale ambapo Kamati ya Maafa ilitufahamisha tarehe 29 Aprili, 2011 kwamba chakula hiki tani 8.6 zitagawiwa bure na hiki kingine kiuzwe.

Mimi kwa kuelewa matatizo ya wananchi wangu niliamua kununua kile chakula ili kigawiwe bure kwa wananchi wangu lakini Mkuu wa Wilaya amekasirika mpaka anawakomoa wananchi hajagawa chakula hicho, pamoja na mimi kuingiza fedha na kulipa tani 77.4 mpaka sasa ninavyoongea *DC* ameendelea kuwa na msimamo bila kuwapatia wananchi chakula, hii ni kuwakoma wananchi. Mtu huyu ndiye Mkuu wa Wilaya, aliyepewa madaraka ya kuwalea wananchi na kuwaongoza lakini anachekelea wananchi wanapata matatizo ya chakula, inanisikitisha sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

#### **MBUNGE FULANI:** Piga makofi huyo!

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala zima la kiwanda cha Mtibwa. Nilikuwa nasoma Taarifa ya Hali ya Uchumi, imeonyesha kwamba hatujaweza kuuza sukari nje ya nchi, zaidi tunakuwa na upungufu wa sukari na tunaagiza, tatizo ni nini?

Tatizo mojawapo ni kwamba kiwanda cha Mtibwa kinazalisha sukari kwa kiwango cha chini. Leo asubuhi tuliamiwa kwamba *capacity* ya kuzalisha sukari Mtibwa ni tani 50,000. Hatujawahi kufikia kwani kiwanda kinazalisha tani 40,000 kwa mwaka jana, miaka mingine tani 20,000 na mwaka huu wamekusidia kuzalisha tani 47,000. Lakini ni kwa nini wanazalisha chini ya kiwango? Ni kwamba mitambo imechakaa lakini wananchi pia wameanza kukata tamaa kwa sababu ya bei ndogo ya miwa wanayopewa.

Leo hii nimeambiwa kwamba imeongezeka kwa tani 10 itakuwa 42,000 wakati huo huo kiwanda cha Kilombero mkulima wa aina hiyo hiyo analipwa shilingi 56,000/= tofauti ya 14,000. Hivi hiyo ya Kilombero inalimwa Ulaya? Hii inawakatisha tamaa wananchi na wakulima. Naomba Serikali na Waziri Mkuu nimemuandikia barua na Waziri mhusika waingilie kati kuona kwamba matatizo ya Mtibwa sasa yanaisha katika miaka hii mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la elimu. Naomba sana Serikali ilitazame hili kwamba tunalo tatizo kubwa la upungufu wa walimu, madawati, nyumba za walimu, madarasa na takwimu zipo, naomba na nafurahi kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu imekiri kabisa kwamba kwa Wilaya ya Mvomero tu kuna upungufu wa madawati 9,698, nyumba za walimu ni upungufu wa 1,466, madarasa upungufu wa 776. Naomba Serikali katika mwaka huu wa fedha itenye fedha kuona kwamba tatizo hili linapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu afya na naomba sana kwani tuna tatizo kubwa la ukosefu wa dawa na wataalamu wa afya na Mvomero iangaliwe kwa jicho la huruma ni Wilaya mpya, tunahitaji hospitali ya Wilaya lakini pia na ujenzi wa zahanati kwa kila kijiji na vituo vya afya katika kila Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni mawasiliano. Wilaya ya Mvomero bado maeneo mengi hatuna mawasiliano, nashukuru sana Profesa Mbarawa ameniahidi kushughulikia suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

## KUHUSU UTARATIBU

**MWENYEKITI:** Kanuni ya ngapi? Naomba uisome.

**MHE. MOSES J. MACHALI :** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 67(1) inatuambia kwamba; “Mbunge anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno kuhusu utaratibu ambapo Mbunge yeoyote ambaye wakati huo atakuwa anasema atanyamaza na kukaa chini na Spika atamtaka Mbunge aliyedai utaratibu ataje Kanuni au sehemu ya Kanuni iliyokiukwa.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(1)(a) inatuambia kwamba; “Hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji aliyemaliza muda wake Mheshimiwa Amos Makalla, Mbunge wa Mvomero, ametoa taarifa ndani ya Bunge ambazo kimsingi kama kweli aliyyoyazungumza ni sahihi kuna kila sababu ya kumtafuta huyu DC ambaye anawanyima wananchi chakula na ikiwezekana akamatwe na kufikishwa kwenye vyombo vya kisheria. Kwa sababu kama tunaweza tukawa tunatoa taarifa ndani ya Bunge, mahali ambapo tunaangaliwa na Watanzania na Jumuiya mbalimbali za Kimataifa kwamba Ma-DC wanapewa vyakula ili kusudi waende wakawagawie wananchi halafu hawawapi, ina maana wanahalalisha wananchi wale wafe na kama tungekuwa katika nchi za Mashariki ya mbali inawezekana mtu huyu angenyongwa hata kwa risasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako juu ya hatua zitakazochukuliwa dhidi ya DC huyo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, nadhani umechukua tu *advantage* ya Kanuni hiyo kueleza tu *feelings* ulizozipata. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni alioitumia Mheshimiwa Mbunge wala haihusiani kabisa na kile alichokisema ndani ya Ukumbi wa Bunge. Kanuni hiyo ingekuwa na maana kubwa sana kama angekuwa anamtaka Mheshimiwa Amos Makalla athibitishe yale anayoyasema kama ni kweli na kabla hajamtaka Mheshimiwa Amos

Makalla athibitishe ilikuwa yeye aanze kwanza kueleza ukweli wa jambo hilo ambalo anahisi si la kweli ambalo limezungumzwa na Mbunge. Huo ndiyo ukweli wa Kanuni ambayo Mheshimiwa Mbunge ameizungumzia. (*Makofi*)

Sasa kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ameitumia Kanuni hiyo kwa ajili ya kusema tu fikra zile alizokuwa nazo baada ya kulisikia jambo hili basi mimi Mwongozo wangu utabaki kwamba ujumbe umefika kwa Serikali kwa maana ya Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa anatoa hoja kueleza kile alichokuwa nacho na kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni hoja hizi zote siku ya mwisho Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote waliopo kwenye ofisi yake wana kazi ya kueleza katika Bunge letu yale yaliyojiri wakati wa mjadala naamini kabisa watakuwa na nafasi ya kutoa maelezo na wanaamini kabisa watapata nafasi ya kufanya *consultation* na Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*)

Kwa hiyo, katika hilo hakuna Mwongozo kwenye kauli yako, *agenda* ilishafungwa kwa Mheshimiwa Mbunge kuchangia hoja hiyo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nitoe tangazo moja ambalo liko hapa mezani kwangu na limetoka kwa Ndugu Herman Berege Msaidizi wa Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika anasema yahusu tangazo la kuhusu hafla au tafrija ya siku ya Uhuru wa Canada. Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa na Balozi wa Canada nchini Tanzania Mheshimiwa Robert Orr katika tafrija ya kusherehekeea siku ya Uhuru wa Canada. Tafrija hiyo itafanyika kesho Ijumaa tarehe 24 Juni, 2011 katika viwanja vya VETA vilivyopo karibu na lango C la kuingilia ndani ya viwanja vya Bunge. Aidha, taarifa hii inaweka sawa ama kurekebisha tangazo lililotangazwa na Mheshimiwa Spika jana kuwa tafrija hiyo ingefanyika leo siku ya Alhamisi. Kwa hiyo, inafuta lile tangazo la leo shughuli hiyo itafanyika kesho. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hivyo, kutokana na heshima mliyopewa na Ubalozi wa Canada kwa kuamua kuja kufanya tafrija hii Dodoma mnaombwa wote kuhudhuria bila kukosa mara tu baada ya kuahirishwa Kikao cha Bunge kesho Ijumaa tarehe 24 Juni, 2011 kuanzia saa 1.45 usiku. Katika tafrija hiyo Mheshimiwa Spika amealikwa kuwa mgeni rasmi hivyo wote mnaombwa kuhudhuria. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naombaniwashukuru sana kwa shughuli za leo jioni, muda wetu umetutupa mkono lakini hata hivyo tumekamilisha shughuli ambazo tulitakiwa kuzianza leo. (*Makofi*)

(*Saa 1.43 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 24 Juni, 2011 saa tatu asubuhi*)

